**25 MEI. 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 25 Mei, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. AGNES M. MARWA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja

na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Marwa, Katibu tuendelee.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali yetu kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, aulize swali lake.

Na. 429

**Hitaji la kuongeza majengo Kituo cha Afya cha Matamba – Makete**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaongeza majengo katika Kituo cha Afya cha Matamba Wilayani Makete?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Deogratius John Ndejembi majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2022 Serikali ilitenga na kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya vinne vya Ipelele, Kitulo, Bulongwa na Lupalilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa vituo vya afya kwenye maeneo ya kimkakati ikiwemo kuongeza majengo ya Kituo cha Afya Matamba katika Halmashauri ya Wilaya ya Makete kadri ya fedha zitakavyopatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa sababu ndani ya kipindi cha muda mfupi cha miaka miwili amejenga vituo zaidi ya vinne vya afya ndani ya Wilaya ya Makete kitu ambacho kwa historia ya Wilaya ya Makete hakikuwepo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maswali yangu ya nyongeza ni haya swali la kwanza; kuna Kituo cha Afya Kitulo, Kituo cha Afya Bulongwa, Kituo cha Afya Lupalilo na sasa Kituo cha Afya Mbalache hivi vimejengwa, vimekamilika lakini havina vifaa tiba, ipi ni kauli ya Serikali ili vifaa tiba vianze kupelekwa hapa na wananchi wa maeneo yale waweze kuanza kupata huduma kwa ajili ya kuwasaidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kuna Kituo cha Afya cha Ipepo au kwa maana ya eneo la Ipepo, wananchi wale wameandaa tofali zaidi ya laki moja, wameandaa mawe kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuwasaidia wananchi wa Kata ya Ipepo ili waweze kuwa na kituo cha afya kwa sababu wanasafiri umbali wa zaidi ya kilomita 50 hadi 100 kwenda kufuata huduma ya afya kwenye Jimbo langu la Wilaya ya Makete? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la kwanza la Mheshimiwa Sanga la vifaa tiba, Serikali imetenga fedha katika mwaka wa fedha huu ambao tupo wa 2022/2023, shilingi milioni 450 kwa ajili ya kununua vifaa

tiba kwa vituo vya afya vilivyopo Wilayani Makete lakini vilevile kuna shilingi milioni 50 kwa ajili ya zahanati zilizokuwepo katika Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge na Wanamakete kwa ujumla kwamba kuna shilingi milioni 600 ambayo imetengwa kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024, kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwenye vituo hivi vya afya ambavyo Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan imejenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda katika swali lake la pili la lini Serikali itasaidia nguvu za wananchi pale kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ipepo katika Kata ya Ipepo kule Makete. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba inakuwa na vituo vya afya katika maeneo ya kimkakati na hivi Mheshimiwa Mbunge ameitaja hapa kwamba ipo kilomita 50 kutoka Makao Makuu ya Wilaya, basi nichukue nafasi hii kumwelekeza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Njombe kuhakikisha anafika katika eneo hili la Ipepo na kufanya tathmini na kuona kama kituo hiki cha afya kinastahili kupandishwa hadhi sasa kuwa kituo cha afya kamili na walete taarifa yake Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki cha afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi nimekuona, Mheshimiwa Minza, atafuata na Mheshimiwa Ester Bulaya, naomba maswali mafupi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kata ya Manolo, Halmashauri ya Lushoto wameshajenga Wodi ya Mama na Mtoto na wodi mbili za baba na za akinamama, lakini sasa wako katika ujenzi wa *theater*. Je, Serikali iko tayari kuunga mkono juhudi hizi za wananchi ili sasa tuweze kukipasisha kiwe kituo rasmi cha afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, nikijibu swali la la nyongeza Mheshimiwa Shangazi la Kituo cha Afya Manolo kule Wilayani Lushoto, Serikali itafanya tathimini katika ujenzi huu wa *theater* ya pale Manolo na kadri ya upatikanaji wa fedha tutahakikisha kwenye bajeti hii tunayoenda kutekeleza kama ipo tutapeleka fedha kuwasaidia wananchi hawa, lakini kama haipo tutatenga katika bajeti ya mwaka 2024/2025, ili kusapoti jitihada zile za wananchi pale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza nilimtaja, halafu Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Kata ya Mwandoya kuna kituo kikubwa sana cha afya ambacho kinahudumia zaidi ya watu 3,500, lakini kuna upungufu mkubwa sana wa majengo, hakuna jengo la mama na mtoto wala jengo la *x-ray*. Je, ni lini Serikali itajenga majengo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata huduma ya afya iliyo bora hasa Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan na ndiyo maana katika mwaka wa fedha uliopita ilitengwa bilioni 117 ya kuhakikisha kwamba tunajenga vituo vya afya vya kimkakati. Sasa tutaangalia kituo cha afya hiki cha Mwandoya ni namna gani tunaweza tukatafuta fedha kama Serikali ya kwenda kujenga majengo ya mama na mtoto. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Halmashauri ya Bunda inajenga hospitali yake kwenye Kata ya Bunda Stoo na tunatambua Serikali imeshatoa bilioni moja na zinahitajika zaidi ya bilioni tatu ili ile hospitali ikamilike. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa hizo pesa haraka ili hospitali ikamilike na wananchi wa Bunda wapate mahitaji sahihi na kwa karibu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Bulaya alivyokuwa ameshasema, Serikali imeanza kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kule Bunda na tutaangalia katika mwaka wa fedha unaokuja huu wa 2023/2024 ni shilingi ngapi imetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi huu wa Hospitali ya Wilaya na tutahakikisha kama Serikali tunapeleka fedha mara moja kuendelea na ujenzi huo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 430

**Ujenzi wa Vituo vya Afya kata za pembezoni - Tabora Mjini**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Afya kwenye Kata zilizopo pembezoni mwa Tabora Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango mkakati wa kujenga vituo vya afya katika kata za pembezoni Tabora ambapo katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali ilitenga Shilingi Milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Misha. Aidha, ujenzi wa Jengo la *OPD* na Maabara umekamilika na kituo hicho tayari kimesajiliwa na kimeanza kutoa huduma kwa wagonjwa

wa nje, ujenzi wa jengo la wazazi, jengo la upasuaji upo katika hatua za ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye maeneo ya kimkakati nchini yakiwemo maeneo ya pembezoni ikijumuisha maeneo ya Jimbo la Tabora Mjini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Serikali yanaonyesha kwamba hata hiki Kituo cha Afya kilichopo Misha bado hakijakalimika, hivyo wananchi kushindwa kuona thamani ya fedha za Serikali zinazokwenda maeneo hayo na matokeo yake ni kuweza kuwaambia Wakurugenzi wetu wa Halmashauri wamalizie wakati wanajua kabisa mapato yanayopatikana kwenye halmashauri zetu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha ili kumalizia kituo hiki ambacho kitasaidia wananchi wa Kata za Ikomwa, Kakola pamoja na Kabila? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Tabora Mjini ni moja kati ya Majimbo ambayo yana kata nyingi ambazo ziko mbali, watu wanatembea umbali mrefu mpaka kilomita 30 au 40 kufuata huduma za afya kwenye maeneo ya mjini. Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuangalia maeneo ambayo yana changamoto za huduma za afya ili kupunguza changamoto hizi hususani kwenye mikoa yetu ya pembezoni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, la kwanza hili la fedha za kumalizia. Ni kipaumbele cha Serikali kuhakikisha kwamba inamaliza vituo hivi vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nikiri hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba Kituo hiki cha Afya cha Misha kinahudumia Kata ya Uyui, Kalunde, Misha, Ikomwa na Kabila na hivyo basi Serikali itatafuta fedha na kuhakikisha zinakwenda mara moja kwa ajili ya kwenda kumalizia majengo haya ili huduma iweze kupatikana kwa wananchi wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili la changamoto hii. Ni kweli katika Manispaa ya Tabora kuna vituo vya afya vitatu ambavyo vimekamilika ambavyo vinatoa huduma kwa wananchi na hiki Kituo cha Misha kikikamilika kitakuwa ni kituo cha afya cha nne na tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati katika Manispaa ya Tabora ili kuhakikisha huduma ya afya inasogea karibu kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amsabi Mrimi, nimekuona.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tunaishukuru Serikali kwa ujenzi wa Kituo cha Afya Machwechwe pamoja na changamoto zingine ndogo ndogo nimewasilisha TAMISEMI mara kwa mara juu ya changamoto ya kukabiliana nayo ya gharama kubwa za vifaa vya ujenzi. Sasa je, ni lini Ofisi ya Rais, TAMISEMI watatuongezea fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kile Kituo cha Afya cha Machwechwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaangalia, tutakakaa na Mheshimiwa Amsabi Mrimi kuhakikisha tunaangalia katika mwaka wa fedha huu unaoenda kuanza wa 2023/2024, ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya kumalizia Kituo cha Afya cha Machwechwe kule Wilayani Serengeti na ikiwepo basi tutahakikisha fedha hizo zinaenda mara moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas Mbunda, nimekuona.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika mpango wa Serikali wa kujenga vituo vya afya vya kimakakati, Kata ya Utiri Halmashauri ya Mji wa Mbinga ni moja ya kata ambazo ziliainishwa kujenga kituo hicho. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki cha afya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hiki Kituo cha Afya cha Utiri, Wilayani Mbinga, kama nilivyosema hapo awali Serikali ilitenga zaidi ya bilioni 117 kwa ajili ya ukamilishaji wa vitu vya afya vya kimkakati hapa nchini. Tutaangalia kwamba kituo hiki kama kimetengewa fedha, basi fedha hizo ziweze kwenda mara moja na kuanza kufanya ujenzi ili kutoa huduma kwa wananchi wa Utiri na kama fedha hiyo haijatengwa tutahakikisha bajeti inayokuja nayo, tutakitengea fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo hiki.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Bunda Mjini.

Na. 431

**Kubainisha mipaka ya Kata ya Wariku-Bunda**

**MHE. ROBERT C. MABOTO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itabainisha mipaka ya Kata ya Wariku - Bunda Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert

Chacha Maboto, Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya mipaka kati ya Kata ya Wariku na kata za jirani katika Wilaya za Butiama na Musoma zilianza kutatuliwa kwa njia ya vikao kati ya Mkurugenzi wa Mji wa Bunda na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya ya Musoma na Butiama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya vikao hivyo, wataalam waliweza kuwakutanisha Viongozi wa Mitaa ya Kata ya Wariku na Vijiji vya Kata za Kyanyari (Butiama) na Suguti (Musoma Vijljini) na kutafasiri mpaka huu ardhini na kugundua kuwa sehemu ya Mto Wariku ulimeguka na kuacha njia yake ya asili kutokana na shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na suluhu ya kudumu, zitawekwa nguzo ndefu na pana *(pillarrs)* zinazoweza kuonekana na kila mwananchi. Kazi ya maandalizi ya nguzo hizo inaendelea na itakapokuwa tayari wataalam watarudi uwandani kwa ajili ya kuzisimika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Robert Chacha Maboto.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nina swali moja la nyongeza. Kutokana na tatizo hili kuwa kubwa katika Halmashauri ya Mji wa Bunda na hasa kwa sababu kuna kata tatu, nne Kata ya Bunda Stoo, Kata ya Kunzugu, Kata ya Balili na Kata ya Mcharo ambazo zimepakana na Hifadhi ya Mbuga ya Serengeti tatizo ni hili hili. Je, Serikali itakuwa tayari na yenyewe kuweka mipaka kwenye maeneo hayo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali kuhakikisha kwamba mipaka yote katika maeneo ya nchi yetu inatambulika vizuri na hizi kata tatu

alizozitaja ambazo zinapatikana na Hifadhi ya Serengeti. Kwanza, nitumie nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumwelekeza Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya hii na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama kufika katika kata hizi na kuangalia mipaka hii kama iko sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama iko sahihi, basi wahakikishe *pillar* zinazoenda kuwekwa kwenye kata ile ambayo nimetoka kuitaja kwenye majibu yangu ya msingi, basi wahakikishe wanaweka pia *pillars* katika mipaka hii kati ya kata hizi tatu za Bunda Mjini na Serengeti.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Athuman Almas Maige Mbunge wa Tabora Kaskazini.

Na. 432

**Hitaji la vyumba vya kuhifadhi *x–ray* na *ultrasound* Kituo cha Afya Upuge - Uyui**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga vyumba maalum vya kuweka mitambo ya *x–ray* na *ultra sound* katika Kituo cha Afya Upuge?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018, Serikali ilitenga Shilingi Milioni 500 kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Afya Upuge kwa kujenga jengo la wazazi, jengo la

maabara, jengo la kuhifadhia maiti, nyumba ya mtumishi na njia ya kupita wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika vituo vya afya nchini kwa kuendelea kujenga majengo ya kutolea huduma muhimu ikiwemo huduma za mionzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga vyumba maalum vya kuweka mitambo ya *X–Ray* na *Ultra Sound* katika Kituo cha Afya Upuge kadri fedha zitakavyopatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Athuman Almas Maige.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri hayo ya ndugu yangu Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali haijali kuona mashine zile zimekaa kwenye makasha ya kusafirishia kwa miaka saba kuwa zinaweza kuharibika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali ina ushauri gani juu ya wagonjwa wanaokaa kusubiri huduma za *x-ray* mashine na *ultrasound* ili kufanyiwa upasuaji, ukizingatia kuwa hata katika hospitali ya Wilaya iliyoko kilomita tano tu kutoka Upuge nako huduma hizi hazipatikani kwa sababu mtumiaji wa mashine hizo hayupo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Maige kama ifuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajali sana na ndiyo maana kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi fedha ilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo yaliyokuwapo mwanzo, lakini nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge ndani ya wiki hii

nitaomba mbele ya Bunge lako tukufu, niongozane naye na wataalam wa afya kufika katika Kituo cha Afya cha Upuge na kuona ni namna gani tunaweza kuchukua hatua kwa sababu haikubaliki miaka saba vifaa hivi vikakaa bila kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali lake la pili nirejee kwenye jibu langu la kwanza katika maswali yake ya nyongeza. Tutatatua changamoto hizi tukiwa *site* palepale na Mheshimiwa Maige, lakini nikiwa katika ziara hiyo kwa sababu kuna Mbunge mwingine wa Tabora ambaye alizungumzia basi tutatembelea pia Kituo cha Afya cha Misha kuhakikisha tuone changamoto zilizopo na kuhakikisha tunazitatua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Sima na Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka kujua tu ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya kukamilisha Kituo cha Afya cha Kisaki? Pia ikikupendeza Mheshimiwa Waziri wakati unaenda Tabora upitie Singida uzungumze na wananchi wa Singida pale Kisaki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Sima tutapokuwa tunaelekea Tabora basi tutahakikisha tunapita Manispaa ya Singida ili kuona kituo hiki cha Kisaki na tutafanya maamuzi tukiwa pale kadri ya bajeti itakavyoruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, nilikutaja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Kwa kuwa huduma ya *ultrasound* imekuwa na umuhimu wa kipekee kwa wakinamama wajawazito.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuweka huduma hiyo ya *ultrasound* katika vituo vya kliniki ya mama na mtoto? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni adhma ya Serikali hii ya awamu ya sita kuhakikisha kwamba inakuwa ina vifaatiba vya kisasa katika vituo vyetu vyote vya afya hapa nchini. Tutahakikisha kwamba kadri miaka inavyokwenda na bajeti inatakavyoruhusu tunatenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya *ultrasound* kwenye maeneo yenye wodi za mama na mtoto kama ambavyo Mheshimiwa Kisangi amezungumza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, nimekuona.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Swaya ni Kata ambayo iko pembezoni sana. Je, ni lini Serikali itaamua kujenga kituo cha afya maeneo yale katika Wilaya ya Rungwe?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakagenda kuhusu kata ya Swaya, ninatoa agizo kwa Mganga Mkuu wa Mkoa kuhakikisha anafika katika Kata hii na kufanya tathmini, kuona ni namna gani kama kuna zahanati pale basi iweze kuombewa kupandishwa hadhi na maombi hayo yaletwe Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili tuweze kuyachakata na baada yakipandishwa hadhi tutafutie fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha afya.

**MWNEYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ni lini Serikali itapeleka majokofu kwenye vyumba vya kuhifadhia maiti kwenye vituo vya afya vya Muriti na Bwisya Jimboni Ukerewe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya majokofu haya katika vituo vya afya kule Ukerewe alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge kadri ya upatikanaji wa fedha na tutaangalia katika bajeti hii tunayoenda kuitekeleza ya 2023/2024, kama imetengwa fedha tutahakikisha inafika mara moja kwa ajili ya kupunguza changamoto hii iliyopo katika Wilaya ya Ukerewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimshukuru Mheshimiwa Rais ametupa fedha za *x–ray* mashine 150,000,000 katika Kata ya Sirari ambayo inahudumia Bumera, Mwema, Susuni Sirari, Kanyange, Itiryo, Mbuguni, Pemba na Ganyange.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua *x–ray* mashine ipo pale hakuna ukaguzi wa mataalam wa mionzi na hakuna mtaalam, hawa wananchi wanapata shida. Nini kauli ya Serikali katika jambo hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hii *x–ray* iliyopo Kata ya Sirari pale, tuna timu ambayo ni ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI inayozunguka nchini kote kutoa mafunzo kwa wataalam wetu wa afya namna ya kutumia vifaa hivi vya kisasa. Sasa nitumie nafasi hii mbele ya Bunge lako tukufu kuelekeza timu ile iweze kufika Mkoani Mara na kufika Sirari kwa ajili ya kutoa mafunzo ili *x–ray* hii mashine iweze kuanza kutumika mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho timu hii ilikuwa Mkoa wa Simiyu, kwa hiyo siyo mbali kutoka Mkoa wa Simiyu na

kuweza kufika Sirari kwa ajili ya kutoa mafunzo haya ili wananchi waweze kupata huduma.

**MWENYEKITI:** Tunamaliza na Mheshimiwa Saashisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hospitali ya Wilaya ya Hai *x–ray* mashine ni ya muda mrefu sana na ni chakavu na imekuwa ikiharibika mara kwa mara.

Je, ni lini Serikali itatununulia *x–ray* mashine mpya kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Hai?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge amekuwa hili pia akilifuatilia sana la *x–ray* mashine Wilaya ya Hai, tutaangalia katika mwaka wa fedha huu 2023/2024 kama fedha imetengwa na kama haijatengwa basi tutaangalia katika mwaka wa fedha 2024/2025 kuhakikisha kwamba wananchi wa Hai wanapata *x–ray* mashine basi Serikali iweze kutenga fedha hizo katika 2024/2025.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Deogratius John Ndejembi kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, tunaanza na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba.

Na. 433

**Malalamiko ya ajira kada za afya na elimu**

**MHE. ISSA J MTEMVU** aliuliza: -

Je, nini mkakati wa kushughulikia malalamiko ya ajira za Kada ya Afya na Elimu kutolewa kwa waombaji wanaotoka baadhi ya maeneo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 2.1. 2 cha Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo la Pili la mwaka 2008 na Kanuni D.6 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 ikisomwa kwa pamoja na Kanuni 12(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, ajira kwa nafasi zilizo wazi katika Utumishi wa Umma hujazwa kwa ushindani wa wazi kwa kufanya usaili na kupata washindi katika nafasi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliarifu Bunge lako kuwa, Serikali haitoi ajira kwa kuzingatia maeneo. Waombaji wote wa kazi Serikalini huchukuliwa kuwa na haki sawa na hivyo wote hupimwa na kuchujwa kwa vigezo vinavyofanana bila upendeleo wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahimize Watanzania wote wenye sifa stahiki kutoka maeneo yote nchini wajitokeze kuomba nafasi za kazi pindi zitakapotangazwa na Mamlaka zinazoshughulikia ajira nchini ili waweze kushindana na waombaji wengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ningeomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa waombaji wengi wanasifa za kitaaluma za jumla zinazofanana kwa sababu wamesoma katika vyuo au shule za pamoja hapa nchini, lakini bado malalamiko yapo mengi kwa sababu hamna nafasi wanazopata katika ajira katika Wilaya kadhaa.

Je, Serikali sasa iko tayari kutoa orodha za kiwilaya wakati inatoa hizo ajira ili waonekane wale katika kila Wilaya waliopata nafasi?

Swali la pili, kwa kuwa hapa Bungeni Serikali ilisema mwezi wa pili kwamba wale wote sasa ambao wapo kwenye *database* waliofika katika hatua ya mahojiano au *oral* watapelekwa kwenye vituo au watapangiwa moja kwa moja katika vituo, lakini *practice* kwa sasa inaonesha si hivyo, kuna watu wanachomekwa chomekwa.

Je, Serikali iko tayari kutoa orodha ile ambayo iko kwenye *database* ili wananchi waweze kuona wanaopangiwa kwamba ni wale ambao wako kwenye orodha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA N AUTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtemvu, Mbunge wa Kibamba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba waombaji wengi wana sifa zinazofanana na kwa kweli wamesoma kwenye vyuo vyetu lakini changamoto tunayoipata hapa ni kwamba pamoja na sifa hizo lakini nafasi ni chache, kwa hivyo namna pekee ya kuweza kuwapata hawa wanaotakiwa, mathalani nafasi zinaweza zikatangazwa labda 200, waombaji wakawa 1,000, namna pekee ya kuwapata hawa 200 ni lazima tu

uwashindanishe. Sasa huo ushindani haumaanishi kwamba pengine wengine walisoma ni bora zaidi, ni kama mbio tu za *marathon,* lakini kimsingi tungetamani wote wanaoomba wapate lakini nafasi ni chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kutoa orodha au kuweka utaratibu wa mfumo wa kiwilaya na wenyewe bado tunaendelea kuutafakari kama nilivyosema kwenye majibu yangu wakati tunahitimisha bajeti yetu kwamba tutajitahidi ku – *design* mfumo ambao utawabaini waombaji na maeneo wanayotoka ili tuweze kutafuta hicho ambacho kilisemwa sana kwa sauti kubwa na Waheshimiwa Wabunge juu ya hisia za upendeleo wa kimaeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili tunaendelea kulifanyia kazi na mpaka sasa tumeunda timu inajaribu kuchakata tuone namna gani bora siyo jambo jepesi, ukilisema hivi kama jepesi lakini kiuhalisia ni ngumu kutengeneza mfumo utakaobaini maana yake hatufuati kabila. Kwa sababu mwingine anatokea mahala kulingana na asili alikokulia au anaomba akiwa yuko Dar es Salaam hatokei Kibakwe lakini anaomba yuko sehemu nyingine, je unamuwekaje? sasa hilo nalo tunaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba wale waliokwishafanya usaili na mfumo wetu wa usaili ni wa aina mbili, kwanza ni wa kuandika na mwingine ni usaili wa kuulizwa maswali ya papo kwa papo. Sasa wanapotokea watu wamefika kwenye hatua ya pili maana yake wamejitahidi kufanya vizuri na pale napo utampata wa kwanza mpaka wa mwisho lakini uhitaji pengine ni wachache wanaobaki ndiyo Mheshimiwa Mbunge anasema kuwepo na uwazi ili wajulikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie kwamba tutajitahidi sana kuweka uwazi huo ili wajulikane, ili wanapochukuliwa wao wenyewe wadhihirishe kwamba kweli alikuwa wa kadhaa na waliochukuliwa na yeye ameweza kupata fursa ili tuondoe haya manung'uniko.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amandus Julius.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa nchi yetu kwa sasa ina wahitimu kila kona, na kwa sasa kwa sababu mfumo ulioko wa kuomba ajira una changamoto na una manung'uniko mengi.

Je, Serikali iko tayari sasa kupitia mfumo huu wa sasa ili kupeleka kwenye kila Jimbo idadi sawa ambayo itakwenda kutibu sasa tatizo hili la manung'uniko ambalo kwa kweli kila kona lipo?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA N AUTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili halitofautiani nalile lililoulizwa na Mheshimiwa Mtemvu, tofauti ni kwamba Mheshimiwa Mtemvu kasema Wilaya lakini Mheshimiwa Mbunge kasema Jimbo. Kama nilivyosema tunaendelea kufanya utafiti kwa kutumia mifumo lakini na uhalisia wa jambo lenyewe kama tunaweza tukalitekeleza katika usahihi sana kinyume na utaratibu wa sasa wa kushindanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna upungufu kwenye kushindanisha au kama hakuna uwazi wa kutosha kwenye kushindanisha inaweza ikawa kazi nyepesi zaidi kushughulikia kuliko kutafuta mfumo utakaoweza kuja na majawabu haya. Hata hivyo, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba tutajitahidi kuandaa, tumeunda timu ambayo inaendelea kufanya utafiti hata sasa wako kazini watatuletea majawabu ya namna gani tunaweza kufanya yote mawili mfumo na uhalisia ili tuweze kuona manung'uniko haya yanakwisha kabisa.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda nilikuona.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi nimemsilikiza sana Mheshimiwa Waziri na nimemuelewa lakini nataka niiambie Serikali kwamba akina

Simbachawene kule Sikonge wako wengi tu na akina Lusinde na wakina Mpangala. Kwa hiyo, suala siyo kabila au asili ya mtu, suala ni anuani. Kwa nini anuani zile zisitumike kuweka wazi kwamba huyu anuani yake ni *P.O.Box* 8 – Sikonge, ukawa na watu labda 20 ambao umewaajiri kutoka Sikonge ukaonesha pale, kwa nini isiwe rahisi namna hiyo badala ya anavyofikiria ukabila na mambo mengine?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA N AUTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimesema kwenye jibu langu la msingi, nataka aniseme tu Mheshimiwa Kakunda alichokisema ni kwamba tuende kwenye anuani. Tukienda kwenye anuani pia kuna *confusion* bado, bado utaiona tu *confusion* kwa sababu utaichukua anuani, unataka kumchukua mtu aliyetoka kwenye Jimbo anakotoka Mheshimiwa Kakunda, lakini utatumia chuo alichosoma, utatumia mahali alikokulia, utatumia anuani alikoombea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *so* kuna mambo mengi ya kuyaangalia ndiyo maana tunasema huo mfumo tunaouangalia na ushahidi tunaoungojea wa kitaalamu na utafiti unaofanyika utatusaidia zaidi kuliko hapa sasa hivi nikisema tutafata utaratibu huu. Nadhani mtuachie Serikali tulifanyie kazi tunaweza tukaja na kitu kizuri zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsnate sana Mheshimiwa Goerge Boniface Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalumu, aulize swali lake.

Na. 434

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Tarafa za Kitumbeine na Engarenaibor**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Tarafa za Kitumbeine na Engarenaibor hususan kwenye migodi ya Rubi.?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali na Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Kitumbeine na Engarenaibor zipo katika Wilaya ya Longido, Mkoa wa Arusha, Tarafa hizi hazina vituo vya Polisi vinavyofanya kazi. Huduma za Polisi hutolewa kwenye kituo cha Polisi cha Wilaya ya Longido kilichopo kilometa 54 toka Kitumbeine na kilometa 35 toka Engarenaibor. Serikali inatambua juhudi za wananchi wa Tarafa hizo mbili kuanza kujenga vituo vya Polisi viwili kwa nguvu zao na kwa kuwashirikisha wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tarafa ya Kitumbeine jengo la Kituo cha Polisi limejengwa katika Kijiji cha Gelai Lumbwa, Kata ya Gelai Lumbwa lakini bado hawajaanza ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari. Katika Tarafa ya Engarenaibor wananchi wamejenga Kituo cha Polisi katika kijiji cha Mundarara, Kata ya Mundarara na ujenzi umefikia kwenye hatua ya *lintel.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawapongeza wananchi wa Tarafa ya Kitumbeine na Engarenaibor na itawaunga mkono katika kuchangia nguvu za wananchi ili kukamilisha ujenzi wa majengo hayo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 ili kutoa huduma za Polisi katika maeneo hayo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa tarafa ya Kitumbeine na Engarenaibor ziko mpakani pia zina rasilimali nyingi ikiwemo machimbo ya Rubi. Wananchi wa Mundarara kwa nguvu zao binafsi wamejitolea ardhi pia wamejenga Kituo cha Polisi hadi kufikia kwenye ngazi ya *lintel*.

Je, Serikali haioni haja sasa kuunga mkono wananchi hawa kwa kumalizia kituo hiki cha Polisi ili kulinda usalama wa raia na rasilimali zao? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tumetambua juhudi za wananchi wa tarafa ua Kitumbeine na Engarenaibor ndiyo maana kwenye jibu langu la msingi nimesema tutawaunga mkono katika bajeti ya mwaka 2023/2024. Labda niwe *more pragmatic* katika bajeti ijayo tutatenga fedha za kuunga juhudi tuweze kukamilisha jengo lililojengwa kwenye eneo hili. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, nimekuona.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nimehudumu kwenye Kamati hii miaka miwili na nusu, Jeshi letu la Polisi linakabiliwa sana na uchakavu wa muindombinu ya vituo vya Polisi pamoja na makazi ya Askari kote nchini ikiwemo Jimbo la Mbulu Mji Manyara.

Je, ni mkakati upi wa Serikali wa kuondoa tatizo la uchakavu wa majengo ya Askari kote nchini?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AMAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya vituo vya Polisi majengo yake ya vituo ni chakavu na nyumba za Askari ni chakavu. Kwa msingi huo Wizara

ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Polisi limeandaa mpango mkakakti wa miaka 10, kwa ajili ya kufanya ukarabati wa vituo vilivyochakaa na nyumba Askari zilizochakaa, kwa hivyo kama eneo lako Mheshimiwa Mbunge pia lina changamoto hii litafikiwa. Tunashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa majibu hayo. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda aulize swali lake.

Na.435

**Kuwawezesha wavuvi - Busanda**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawezesha Wavuvi ambao wameunda vikundi na kuanza ufugaji wa vizimba katika Jimbo la Busanda?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Maendelo ya Kilimo *(TADB)* inatekeleza mradi wa kutoa mikopo yenye masharti nafuu na isiyo na riba ya pembejeo za ufugaji samaki ikijumuisha vizimba, vifaranga vya samaki na chakula cha samaki kwa ajili ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba. Aidha, jumla ya wanufaika 3,154 wameainishwa kunufaika na mradi huo ikijumuishwa vikundi 93, kampuni 10, na watu binafsi 32. Kwa upande wa *Geita DC* vikundi vitatu vinatarajiwa kunufaika na program hiyo ikiwemo kikundi cha Tumaini chenye wanachama 10 kutoka Jimbo la Busanda. Vikundi hivi vitapatiwa mikopo ya pembejeo za ufugaji samaki

kwenye vizimba yenye thamani ya Shilingi milioni 69.4 kwa kila kikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa kutoa mikopo yenye masharti nafuu na isiyo na riba ya pembejeo za ufugaji samaki kwa kuwawezesha wafugaji samaki wenye vizimba 893. Hivyo, natoa wito kwa wafugaji samaki nchini wakiwemo wale wa Jimbo la Busanda kuendelea kuchangamkia fursa hii kwa kujiunga katika vikundi na kuanzisha vyama vya ushirika wa ufugaji samaki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tumaini Bryson Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali yanayoonesha kwamba kikundi kimoja Jimboni Busanda kitapata shilingi milioni 69.4 hivi, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Jimbo la Busanda katika maeneo ya Ziwa Viktoria yana vikundi vingine katika Kata ya Nyamwilolelwa, Kata ya Bukondo na Kata ya Nyachiluluma: Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba, inaweza kuongeza vikundi vinavyokopesheka kwenye maeneo hayo ili huduma hii iweze kuwasaidia wananchi wengi kwa ajili ya maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Nini mkakati wa Serikali kuhamasisha ufugaji wa samaki kwenye maeneo ambayo yako mbali na Ziwa Victoria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jambo la kwanza Mheshimiwa Mbunge amezungumzia kuhusu kuongeza idadi ya vikundi katika jimbo lake. Bahati nzuri katika mwaka wa fedha tutaongeza idadi

ya vikundi kufikia 893. Kwa hiyo, katika mwaka huu unaokuja basi na jimbo lake tutaongeza hivyo vikundi ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameviainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali kuhusu maeneo ambayo yako mbali na Ziwa Viktoria, ni kwamba, tumeanzisha programu maalum ya ufugaji wa samaki kwa njia ya mabwawa ambayo sasa hivi katika mwaka uliopita tulikuwa na mashamba darasa kumi. Kwa hiyo, matarajio yetu ni kwamba mwaka wa fedha unaokuja, tutafanya hivyo. Kwa hiyo, huo ndiyo mkakati wa sasa na tutaendelea kuhimiza. Mfano mzuri, hata hapa Chamwino tunafanya shamba darasa katika maeneo ambayo ni kame. Kwa hiyo, huo ni mkakati ambao upo na ni endelevu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Marwa na Mheshimiwa Aloyce Kamamba atafuatia. Naomba maswali yawe mafupi.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itatoa elimu kwa wavuvi wa Mkoa wa Mara na hasa wale waliounda vikundi kwa ajili ya ufugaji wa vizimba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Zoezi la kutoa elimu ni endelevu. Kwa kuwa, vikundi bado viko vingi, basi tutawatuma tena wataalamu wetu waende kuwasaidia wafugaji wa Ziwa Victoria katika Eneo la Mara ambalo Mheshimiwa Mbunge ameainisha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Aloyce Kamamba na Mheshimiwa Fatma Toufiq atafuatia. Naomba maswali yawe mafupi.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Buyungu, wapo wafugaji wa samaki ambao wapo katika vikundi, lakini wapo

wengine ambao ni mmoja mmoja, lakini wanapungukiwa maarifa na mtaji kwa ajili ya kuwawezesha kufuga kwa tija. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunawawezesha hawa wafugaji waweze kufuga kwa tija? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge. Mkakati wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni pamoja na kuwezesha vikundi mbalimbali vya wavuvi na wavuvi binafsi. Ndiyo maana ukiangalia katika mwaka huu wa fedha tumetoa fedha nyingi na tunaenda kutoa mikopo ya maboti. Kwa hiyo, waliwemo wavuvi wa Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, Buyungu kule na wenyewe tutawafikia. Kwa hiyo, tuwaondoe shaka kwenye hilo.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Fatma Toufiq aulize swali la nyongeza kwa ufupi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Nini mkakati wa Serikali wa kuhamasisha wanawake wengi zaidi wafuge kwa kutumia vizimba ili wawezekuepukana na umasikini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa ufupi, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jambo la kwanza, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inazingatia sana na imekuwa ikihimiza wanawake kujiunga katika ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba. Ndiyo maana sasa hivi katika kila programu ambayo tunaianzisha tumeweka pale *threshold* ambayo lazima kwenye kila program pawepo na wanawake wanaojiunga na shughuli hizo. Kwa hiyo, hiyo ni sehemu yetu na tutaendelea kuisimamia kuhakikisha kwamba wanawake wanaingia katika shughuli hizi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Chaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Munira.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika Wilaya ya Manyoni tuna kata tatu za Majiri, Maweni na Kijiji cha Kibumagwa ambako kuna uvuvi wa Samaki: Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba, tunaboresha uvuvi huu?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa ufupi Mheshimiwa Waziri. Umemwelewa vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Manyoni ambako na kwenyewe wanaendesha uvuvi wa samaki, anachotaka ni sisi kwenda kuboresha. Jukumu letu kubwa ni kwamba, moja, tutaendelea kuleta elimu pamoja na kuongeza vifaa vya kisasa kupitia hii mikopo ya masharti nafuu. Kwa hiyo, tutafika katika kila eneo ambalo watu wetu wanajishughulisha na hizi shughuli za uvuvi pamoja na mifugo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munira nilikutaja, halafu Mheshimiwa Tunza Malapo. Atamalizia Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda. Waheshimiwa naomba muulize maswali yenu kwa ufupi sana.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante; je, Serikali ina mkakati gani wa kuvisaidia vikundi ambavyo vilikuwa vimeathirika na kutumia nyavu za *wiring?*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vikundi ambavyo vimeathirika na matumizi ya hizo nyavu, kwanza Serikali siyo waumini wa nyavu

zile ambazo hazijaruhusiwa nchini. Pili, sasa hivi tumekuwa tukikaa na kampuni zinazotengeneza nyavu kuhakikisha kwamba wanatengeneza nyavu ambazo zime-*meet* kiwango ili kuondoa vurugu ambazo zimekuwa zikijitokeza na wavuvi wetu kupata hasara. Kwa hiyo, moja ya sehemu ya mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba, zana za kisasa zinapatikana kwa wavuvi wetu ili waweze kuvua kisasa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Tunza Malapo.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kule kwetu Mtwara wananchi wamehamasika kufuga majongoo Bahari kwenye vizimba, lakini tatizo kubwa ni vifaranga. Nataka kujua ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wafugaji wale wanapata vifaranga kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, amezungumzia suala la majongoo bahari ambayo ni moja ya bidhaa kubwa ambayo sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunaitangaza. Niwaondoe shaka wananchi wa ukanda ule. Sasa hivi moja ya mkakati wa Serikali, tunaanzisha kituo cha kuzalisha vifaranga katika Mkoa wa Mtwara ili kuhakikisha kwamba uzalishaji wake unakuwa wa haraka na kwa ukaribu zaidi. Kwa hiyo, huo ndiyo mkakati wa sasa na tunalifanya hilo kwa haraka iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe.

**MHE. KIRUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba katika ziwa inaonekana ni njia moja nzuri ya kusaidia kupumzisha ziwa kwa wavuvi kuvua katika ziwa. Nini mkakati wa Serikali kusaidia wavuvi katika Ziwa Tanganyika kupata vizimba vya kutosha vya ufugaji wa samaki?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Bahati nzuri Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda anajua kabisa mkakati wa Serikali sasa hivi, baada ya kuwekeza sana katika Ziwa Victoria sasa tutafanya hivyo katika Ziwa Tanganyika pamoja na Ziwa Rukwa na Ziwa Nyasa. Ziwa Tanganyika tumeshakaa na Wabunge wa eneo hilo, na mwaka wa fedha unaokuja, mpango wetu kwa asilimia kubwa utakuwa katika ziwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tumalizie na Mheshimiwa Kihenzile.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kule Mufindi Kusini kuna Mabwawa ya Nzivi, Ngwazi pamoja na Kihanga; na mabwawa mengine kama yale ya Ihoanza ambayo yanachimbwa. Changamoto kubwa ambayo ilikuwepo pale ni mambo mawili; suala la vifaranga takribani milioni tano na zana za uvuvi: Je, Serikali iko tayari kupeleka vifaranga takribani milioni tano pamoja na mikopo ya vifaa vya uvuvi vya kisasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Uzuri ni kwamba, jambo hili ambalo amelizungumza Mheshimiwa Kihenzile, alishafika mpaka ofisini kwetu na tulizungumzanaye mimi pamoja na Mheshimiwa Waziri na wataalamu wetu. Tulishamuahidi kwa sababu, kwa sasa tuna vifaranga kama milioni 15 na tuliahidi katika jimbo lake kupeleka *minimum* ya vifaranga milioni nne. Kwa hiyo, hilo lipo katika mpango, ikiwemo zana za kisasa kulingana na tutakavyovipata katika mwaka wa fedha unaokuja, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa David Ernest Silinde kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, aulize swali lake.

Na. 436

**Kutatua mgogoro kati ya wananchi na Hifadhi za Taifa**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua migogoro kati ya Wananchi na maeneo ya Hifadhi za Taifa ikiwemo Jimbo la Momba?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa inachukua hatua mbalimbali kutatua migogoro baina ya hifadhi na wananchi. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kufanya tathmini ya aina, chimbuko na namna ya kutatua migogoro husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)* inasimamia misitu minne ya hifadhi katika wilaya ya Momba. Misitu hii ni Isalalolunga, Isalalo, *Ivuna North* na *Ivuna South* ambayo kimsingi haina mgogoro na wananchi. Katika kuimarisha ulinzi na usimamizi wa hifadhi hizi, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na uharibifu zikiwemo kuweka alama za kudumu za mipaka, kutoa elimu ya uhifadhi kwa jamii, kuondoa wavamizi na kuchukua hatua za kisheria kwa wahalifu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimeyasikia majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nataka tu kumwambia kwamba, migogoro ipo kwa sababu wananchi wanachukuliwa wanawekwa ndani. Sisi hii tunai-*term* kama mgogoro. Maswali yangu mawili ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameshawahi kutuambia tulete maombi Wizarani. Tumeshaleta maombi: Ni lini maombi yetu yatajibiwa ili kuwapa wananchi kipande cha ardhi ili waendelee kuendesha shughuli zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, kama maombi haya yakitoka yatakuwa hapana, Serikali inachukua hatua gani kuendelea kuwasaidia wakulima hawa wapate maeneo ya kulima kwa sababu, ni Watanzania na hawana mahali pa kwenda ili kuendelea kulea watoto wao?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Condester, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa aliwahi kuleta maombi yake na haya maombi mchakato wake unaendelea. Ila kwenye upande wa matokeo ya haya maombi kwamba, yatakuwaje, inategemea sasa na maeneo ambayo sisi tunayaona kama ni ya muhimu, hususan kwenye maeneo ambayo tunatunza vyanzo vya maji na maeneo ambayo ni muhimu kwa kuhifadhiwa. Kwa hiyo, Serikali itafanya tathmini na itaangalia umuhimu wa maeneo haya kwa ajili ya kutunzwa na Serikali na yale ambayo tutaona tunaweza tukayaachia, basi wananchi wataweza kufaidika na maeneo ambayo tutaweza kuyaachia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, halafu Mheshimiwa Luhaga Mpina nimekuona.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya tarehe 22 Jumatatu, kumetokea vurugu na sintofahamu kubwa sana kati ya wananchi wa Kijiji cha Jangwani Eneo la Mto wa Mbu na Askari wa Uhifadhi wa Eneo la Ziwa Manyara na kusababisha mwananchi mmoja kufariki na wananchi kadhaa kujeruhiwa kwa risasi za moto: Je, ni kwa nini askari hawa wa uhifadhi wamekuwa wakitumia nguvu kubwa kukabiliana na hii migogoro kati ya wananchi na maeneo ya hifadhi kiasi kwamba, wananchi wanapoteza maisha na wengine wengi kujeruhiwa? Kwa nini kusiwe na njia nyingine mbadala kukabiliana na changamoto hizi?

**MWENYEKITI:** Swali moja tu Mheshimiwa Paresso. Jibu swali moja la kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nifafanue kidogo kwa ridhaa yako. Kwa kawaida wahifadhi wanakuwa kwenye maeneo yao ya kutekeleza majukumu yao ya kawaida ya kila siku. Mgogoro huu ulijitokeza katika ziwa Manyara ambapo askari walikuwa katika shughuli zao za doria na waliweza kukamata wahalifu watatu ambao walikuwa wamevamia katika hifadhi hiyo. Baada ya kukamatwa hawa wahalifu, basi…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mzungumze taratibu kama mnaongea mambo ya maana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya wahalifu hawa kukamatwa ili wafikishwe kwenye vyombo vya kisheria kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo, wavuvi zaidi ya 30 walijiunga kwa pamoja na wakaenda kuwavamia wale wahifadhi ambapo walikuwa katika maeneo yao ya doria ya kawaida. Kwa bahati nzuri walikuwa tayari wameshawafunga pingu wale wahalifu watatu, lakini wananchi walienda kuwashambulia hao askari. Katika kujiokoa, waliweza kuwaachia hao wahalifu wakakimbia na pingu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kusema hapa ni kwamba, suala linapofika kwenye vyombo vya sheria ama wahalifu wanapokutwa na hatia, basi tuache sheria ichukue mkondo wake; lakini inapofika wananchi wanaungana pamoja, wanalishambulia jeshi, jeshi lenyewe sasa linakuwa linaonekana halina nguvu. Kizuri zaidi na kwa kuwa, maelekezo ya Mheshimiwa Waziri yameshaelekeza kwamba tusitumie nguvu, hawa askari waliweza kukimbia na hawakuweza kufanya vurugu yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandamano hayo, ilisababisha askari kujumuika na wahifadhi ili kuwatawanya watu. Watu walikuwa wengi sana kwa sababu waliungana, ni wanavijiji wa maeneo yale waliwazingira na kufanya maandamano, na walikuwa wanavunja magari, wakikutana na gari wanafanya uhalifu. Kwa hiyo, katika vurugu zile ndiyo zilisababisha sasa huyo mwananchi kufikwa na maafa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba sana wananchi wajitahidi sana kuheshimu vyombo vya Dola vilivyopo kwa sababu, viko kisheria na vinatekeleza majukumu yaliyokasimiwa. Kizuri zaidi, hawa tumewakasimisha madaraka kulinda rasilimali za nchi. Kwa hiyo, tunapowashambulia, tunawapunguzia nguvu ya kulinda rasilimali zilizopo hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Kwa kuwa chanzo kikubwa cha migogoro ya wananchi na wanaoishi katika maeneo ya hifadhi na wahifadhi ni mipaka pamoja na alama zinazoonekana, lakini pia ni pamoja na kuzuia matumizi mseto katika maeneo ya *WMA* kinyume na mikataba iliyofungwa katika uanzishaji wa *WMA* hizo: Je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa kuondoa changamoto hizo ili kuwezesha wananchi kuishi kwa ushirikiano mwema na wahifadhi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kimsingi Serikali inatamani sana kuimaliza hii migogoro, lakini tunatambua kwamba mahitaji ya ardhi sasahivi ni makubwa, wananchi wanaendelea kuongezeka na kila mtu anatamani kumiliki ardhi. Ardhi iliyobaki ni ardhi iliyohifadhiwa ambayo ni inasimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na utalii. Kwa hiyo, kumekuwa na hizi changamoto za hapa na pale na mara nyingi wananchi wanasema ni migogoro, lakini sisi tunasema siyo migogoro kwa sababu, maeneo yana mipaka yake, yana ramani zake, yana *GN* zake. *GN* zipo na zinajulikana, isipokuwa pale ambapo kunakuwa na sintofahamu ya mpaka, tunaenda kuufafanua kwa kuweka vigingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kuwaomba wananchi kwamba sisi tunaendelea kuongezeka, lakini ardhi ni ile ile. Tuendelee kuheshimu haya maeneo kwa mustakabali mzima kabisa wa Serikali na kwa vizazi vinavyokuja. Tunatunza haya maeneo siyo kwa sababu tu yameangaliwa, tunatunza kwa sababu tunaendelea kuongezeka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali fupi la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Liwale ina *WMA* ya Magingo, lakini uanzishwaji wa *TANAPA,* ile Hifadhi ya Mwalimu Nyerere imeingia kwenye maeneo ya *WMA* ya Magingo katika Kitalu cha Nachengo, Kijiji cha Mpigamiti na Ndapata na Kimambi: Je, Serikali inachukua hatua gani kwenda kutatua migogoro hii iliyoletwa na uanzishwaji wa Hifadhi ya Mwalimu Nyerere?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaenda kuufafanua huo mpaka na kutafsiri mpaka ili *WMA* ziweze kufanya kazi zake na Hifadhi ya *TANAPA* iendelee na shughuli zake.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Francis Masanja kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, aulize swali lake.

Na. 437

**Ujenzi wa barabara ya Nangurukuru – Liwale**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Nangurukuru - Liwale?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Alfred Mwakibete, Naibu Waziri wa Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*, inaendelea na kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Nangurukuru hadi Liwale yenye urefu wa kilometa 230. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ipo katika hatua za mwisho. Katika mwaka wa fedha wa 2023/24, Serikali itaanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu ya kwanza, kuanzia Liwale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunujibu swali langu kwa ufupi na kwa malengo ambayo niliyakusudia. Ninapenda nishauri barabara hii ianze kujengwa toka Nangurukuru kuelekea Liwale kwa sababu itatengeneza muunganiko wa lami inayotoka Dar es Salaam – Kilwa Masoko pamoja na Mkoani Lindi kuelekea Liwale…

**MWENYEKITI:** Naomba uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** …na kugusa majimbo yote yalipo katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niulize maswali yangu mawili ya nyongeza.

**MWENYEKITI:** Kwa ufupi.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kupata kujua;

Je, katika awamu ya kwanza ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hii, itajengwa kilometa ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna barabara ya kutoka Njianne kwenda Kipatimu yenye urefu wa kilometa 50, imekuwa ikijengwa kwa urefu wa mita 700 mwaka 2021, mita 700 2022 na mita 600 2023;

Je, ni lini Serikali itakuja na mradi wa kimkakati ili iweze kujenga kwa urefu mrefu katika barabara hii?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa ufupi Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake wa karibu katika barabara hii. Lakini pia tumeupokea ushauri wake, kwamba ianze kujengwa kutoka Nangurukuru kwenda Liwale, naamini haya tutaweza kuyazungumza. Mkandarasi huyu mmoja anaweza akaanza upande wa Nangurukuru – Liwale ama Liwale – Nangurukuru, yote yanawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yake mawili ya nyongeza, la kwanza anataka kujua ni kilometa ngapi katika ujenzi huu utakaoanza Mwaka wa Fedha 2023/2024; ni kilometa 72 kati ya kilometa 230.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, anataka kujua barabara hii ya Tinga – Kipatimu, ni kweli kwamba barabara hii tumekuwa tukiijenga sisi kama *TANROADS* kidogokidogo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuijenga barabara hii hadi ukamilifu wake, na sasa tumetenga jumla ya takribani milioni 281.81 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii katika Mwaka wa Fedha ujao, 2023/2024, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kutokana na muda, tunamalizia na swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo.

Na. 438

**Ufunguzi wa Bandari ya Karema – Mpanda**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza: -

Je, lini Bandari ya Karema itafunguliwa na kuanza kufanya kazi kwa kuwa ujenzi umekamilika kwa asilimia 87?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania imeshakamilisha ujenzi wa Bandari ya Karema na huduma katika bandari hiyo zimeanza kutolewa rasmi kuanzia tarehe 1 Septemba, 2022 baada ya kufanyiwa uzinduzi na Mkuu wa Wilaya ya Ziwa Tanganyika. Bandari hiyo inahudumia abiria na shehena mbalimbali za ndani ya nchi na zile zinazosafirishwa kati ya Tanzania na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili bandari iweze kufanya kazi vizuri, inahitaji kuwa na barabara ya lami kutoka bandarini, lakini pia inahitaji kuwa na reli kwa ajili ya kubeba mizigo. Kwa kuwa barabara ya lami kutoka Karema kwenda Mpanda bado haijakamilika, na kwa kuwa Serikali bado haijajenga reli kutoka Karema kwenda Mpanda;

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kujenga reli pamoja na barabara ya lami ili kuwezesha kubeba mizigo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuwa na bandari ambayo haifanyi kazi, ambayo haina meli, ni sawa na kuwa na nyumba ambayo haikaliwi na mtu. Ziwa Tanganyika halina meli inayofanya kazi sasa hivi, MV. Liemba haifanyi kazi na MV. Mwongozo haifanyi kazi;

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inajenga meli ili ziweze kubeba mizigo kutoka Kongo na nchi za jirani?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Bandari yetu ya Karema inatakiwa ifungamanishwe na barabara kwa kiwango cha lami pamoja na reli. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika mwaka wa fedha ambao tunauanza wa 2023/2024, kati ya kilometa 112 zote zimekwisha tangazwa na itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuifungua bandari hii ya Karema – Ikola mpaka Kagwira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, anataka kujua meli katika Ziwa Tanganyika. Kama ambavyo tuliweza kuwasilisha bajeti yetu siku ya Jumatatu na Jumanne, tuliweza kutoa *commitment* kwamba kati ya Ziwa Tanganyika, meli tatu tunaendelea kuzikarabati, hususan Meli ya MT. Sangara inayobeba mafuta ambayo iko asilimi 90, pia kuna Meli ya MV. Liemba ambayo tayari mkataba wake tutasaini mwezi Juni, na MV. Mwongozo tumepata mkandarasi mshauri atakayeweza kuishauri Serikali namna gani ya kuifanya hii meli i-*balance* maana ilikuwa na shida ya *stability*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo pia tumetenga fedha kwa kutengeneza meli kubwa mbili, moja ya mizigo itakayobeba tani 3,500 na nyingine ni ya kubeba abiria 600 pamoja na tani 400 ambayo kwa ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Katavi, Rukwa na Kigoma, mlisema ikiwezekana ziwe mbili, na sisi Serikali tukasema tunakwenda kulifanyia kazi hili. Kwa hiyo hii ni mipango na tunakwenda kufanya katika mwaka wa fedha ujao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fredy Mwakibete, Naibu Waziri wa Uchukuzi, kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu kwa siku ya leo yameishia hapo, na sasa ni wakati wa matangazo.

Naanza na matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; kwanza wageni waliopo Jukwaa la Mheshimiwa Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula (Mb), ambaye ni Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi; wa kwanza ni *Engineer* Anthony Sanga, Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, karibu sana Katibu Mkuu wetu. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Nathaniel Nhonge, Kamishna wa Ardhi, karibu sana Kamishna katika Bunge letu. *(Makofi)*

Kuna Ndugu Hamad Abdallah, Mkurugenzi Mkuu *National Housing Corporation,* karibu sana. *(Makofi)*

Tuna Dkt. Sophia Kongela, Mwenyekiti wa Bodi ya *National Housing,* karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna Profesa Wakuru Magigi, Mkurugenzi Mkuu *NLUPC;* karibu sana Mkurugenzi katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna Dkt. Fred Msemwa, Mkurugenzi Mkuu *Utumishi Housing – WHC,* karibu sana. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Deogratius Kalimenze, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Makazi, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Hamdouny Mansour, Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Evelyne Mugasha, Mthamini Mkuu wa Serikali; karibu sana Mthamini Mkuu wetu wa Serikali. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Lukas Mwaisaka, Msajili wa Bodi ya Mipango Miji, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna Ndugu yetu *Chief* Daudi Babu Mrindoko ambaye ni Mwenyekiti wa Wazazi Kilimanjaro, karibu sana Mwenyekiti wetu wa Wazazi kutoka Mkoa wa Kilimanjaro kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Pia tuna viongozi wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Ilemela wakiongozwa na Mjumbe wa *NEC,* Ndugu Elen Bogohe, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna Mapadre watano kutoka Mwanza Jimbo Kuu wakiongozwa na Fr. John Kasembo, karibuni sana Mapadre wetu kutoka huko Mwanza. *(Makofi)*

Pia tuna viongozi watano wa Dini ya Kiislam wakiongozwa na Sheikh Fadhili Salum Ndumiwe, mwakilishi wa Sheikh wa Mkoa, karibu sana Masheikh wetu. *(Makofi)*

Pia tuna wageni watano ambao ni familia ya Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ambao ni watoto wake wakiongozwa Ndugu David Mabula, wale pale, karibu sana watoto wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wafuatao sasa ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tuna wageni 90 wa Mheshimiwa Deogratius Ndejembi (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao ni Makatibu Wenezi wa Kata, Wenyeviti na Makatibu wa Jumuiya za Chama, karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Tuna wageni 47 wa Mheshimiwa Aloyce Kamamba ambao ni wanafunzi wa Vyuo vya Dodoma kutoka Jiji la Dodoma, karibuni sana wanafunzi wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna wageni 33 wa Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda ambao ni viongozi wa CCM kutoka Kigoma Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni 30 wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi ambao ni walimu wakuu wa shule za msingi kutoka Kilosa, Mkoa wa Morogoro, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 37 wa Mheshimiwa Jonas Zeeland ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Sekondari *Sokoine Memorial* kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Luhaga Mpina kutoka Wilaya ya Meatu, Mkoa wa Simiyu, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni watano wa Mheshimiwa Furaha Matondo ambao ni wanafunzi wa *Bihawana Boys* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, tuna wanafunzi 72 na walimu 11 kutoka Shule ya Msingi Kingdom ya Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, ambao ni kaka na dada zake wakiongozwa na Ndugu Richard Abdalla Lubala. Hawa wako kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika kule, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo ya wageni, tuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge ambaye anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Nishati itaendesha semina kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki *(East African Crude Oil Pipeline)*. Semina hii itafanyika leo, siku ya Alhamisi, tarehe 25 Mei, 2023 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa, wote mnakaribishwa.

Lakini pia tuna tangazo la pili kutoka kwa Katibu wa Bunge, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa Kamati ya Uongozi ilikutana tarehe 23 Mei, 2023 na kufanya marekebisho ya ratiba ya Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge unaoendelea. Marekebisho hayo yanahusu shughuli za nyongeza zilizowasilishwa na Serikali ili kufanyiwa kazi katika kipindi cha majumuisho ya bajeti tarehe 8 – 14 Juni, 2023. Ratiba yenye mabadiliko imeshatumwa kwenye vishkwambi vyenu. Kwa hiyo, wote mnaombwa mpitie vishkwambi na kuona ratiba mpya.

Lakini pia kuna tangazo lingine ambalo linatoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania.

Mheshimiwa Spika anaombwa kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wanawake wa *TWPG* kuwa tarehe 26 Mei, 2023 mara baada ya kusitisha kikao cha Bunge saa saba mchana kutakuwa na mafunzo ya Wabunge wote wanawake. Mafunzo hayo yameandaliwa na Wizara ya Madini na yatafanyika katika Ukumbi wa Hazina uliopo Jengo la *Treasury House*. Naomba kuwasilisha tangazo hilo na Waheshimiwa Wabunge wanawake wote msisahau tangazo hilo.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mwongozo, Mheshimiwa Kakunda.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nina heshima kubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Liwale. Wakati Mheshimiwa Kuchauka anauliza maswali yake hapa, na hii imekuwa ni mara ya tatu au ya nne, anakitaja Kijiji kimoja kinaitwa Mpigamiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jina la kijiji hiki pamoja na kwamba inawezekana kimesajiliwa kihalali, lakini tafsiri ya baadhi ya Wabunge, na hata huko nje kwenye jamii, inakuwa siyo nzuri sana.

Je, hivi Bunge lako tukufu na Kiti chako hakiwezi kutoa mwongozo kwa Serikali wabadilishe jina la hicho kijiji?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kakunda kwa kuomba mwongozo huo. Naomba tutulie Waheshimiwa Wabunge. Tanzania ina majina mengi sana ya vijiji, hata ukienda kule Zanzibar utakuta majina ya tofauti kabisa ambayo hayaendani na Lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

Kwa hiyo naamini Serikali wanayajua hayo, lakini kutokana na utamaduni wetu na jinsi ambavyo majina yamepangwa basi wao Serikali wanaweza kuona nini cha kufanya. Lakini majina

yapo miaka na miaka na yanatokana na historia ya nchi yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadiro ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, karibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumaliza hotuba yake mtampigia makofi zaidi. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03), naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lipokee na kujadili taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka 2022/23. Naomba pia Bunge lako tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo mawili kwa mwaka 2023/24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano wa 11 wa Bunge la 12 ambalo ni mahsusi kwa ajili ya kujadili Mpango na Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, ninaomba kutumia fursa hii kipekee kumshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini kuendelea kusimamia majukumu ya Sekta hii muhimu ya Ardhi. Nimuahidi na kumhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba, imani aliyoionesha kwangu nitaendelea kuitafsiri kwa vitendo kwa kuhakikisha masuala muhimu yanayohusu ustawi na uendelevu wa sekta hii yanasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, napenda kutumia pia fursa hii kuwapongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Isdor Mpango, Makamu wa Rais; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu na Mbunge wa Ruangwa, kwa uongozi wao mahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia kwa miongozo, maelekezo na ushirikiano wao walioonesha katika kutekeleza majukumu ninayoongeza katika sekta hii. Katika kipindi cha miaka miwili wameleta mageuzi katika mifumo ya utoaji huduma, kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji, kuimarisha sekta ya milki na miradi mikubwa ya kuendeleza sekta ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza wewe binafsi na nampongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo Mwenyekiti wa Bunge na Mbunge wa Babati Vijijini, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini kwa kuongoza shughuli za Bunge kwa umahiri na umakini mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pia pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndugu, jamaa, marafiki wa Jimbo la Amani kwa kuondokewa na Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na ndugu Najma Murtaza Giga kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati. Wizara inaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu ya usimamizi wa Sekta ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri na Viongozi wengine walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika mabadiliko ya kiutendaji yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni. Pia, nampongeza Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhandisi Anthony Damian Sanga kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu na Bi. Lucy Dominico Kabyemera kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa uchambuzi makini na ushauri iliyoutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara - Fungu 48 na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi - Fungu 03 kwa mwaka 2023/2024. Wizara inalihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara itaendelea kuzingatia maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati katika kuboresha utendaji ili kuongeza tija katika utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM, Taifa kwa kura nyingi walizoniwezesha kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa. Nawashukuru viongozi wa CCM kwa miongozo, ushauri na maelekezo mbalimbali wanayonipatia. Nitahakikisha natekeleza

kuhakikisha Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 kwa ufanisi mkubwa. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Ilemela kwa ushirikiano walionipatia wakati wa kutimiza majukumu yangu kama mwakilishi na leo hapa Bungeni wapo nadhani wataingia baadaye wako Ukumbi wa Msekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, naishukuru familia yangu kwa kuwa karibu nami na kunitia moyo katika shughuli ninazozifanya. Kadhalika, nawashukuru viongozi wa dini madhehebu yote ambao tumekuwa tukifanya nao kazi kwa karibu na kwa muda wote wamekuwa wakiniombea dua na sala ili niweze kufanya kazi yangu vizuri. Nawashukuru wale wote ambao wameweza kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya mwaka 2023/2024. Bajeti hii imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026); Mikataba; Itifaki; Mipango na Makubaliano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa; Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Sekta ya Ardhi na Kitaifa; na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mwaka 2022/2023 na malengo ya mwaka 2023/2024; matumizi; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 105.5. Aidha, Wizara ilipata nyongeza ya bajeti ya shilingi bilioni 69.8 ikiwa ni fedha za ndani za Maendeleo na kulipa madeni. Ongezeko hilo limefanya bajeti ya Wizara kufikia shilingi bilioni 175.3. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 147.7, kati ya bajeti ya shilingi bilioni 175.3 sawa na asilimia 84.2 katika bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni 21.5 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)* ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia 64 ya bajeti, shilingi bilioni 32.8 ni mishahara ya watumishi sawa na asilimia 74.0 ya bajeti ya mshahara; na shilingi bilioni 93.3 ni fedha za maendeleo sawa na asilimia 96.1 ya bajeti yote ya miradi ya maendeleo. Jedwali Na.1 limeainisha hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara kupitia Fungu Namba 48 ilipanga kukusanya shilingi bilioni 250.1 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ya Sekta ya Ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara imekusanya Shilingi Bilioni 132.9 sawa na asilimia 53.2 na imeainishwa katika Jedwali Na.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia lengo la makusanyo, Wizara inaendelea kuboresha kumbukumbu na mifumo ya TEHAMA iliyopo ili iweze kutuma ujumbe kwa njia ya simu. Maboresho hayo yamewezesha kutuma ujumbe mfupi wa kuwakumbusha walipa kodi wote nchini ardhi wamiliki wapatao 202,563 katika kipindi cha Februari - Mei, 2023. Utaratibu huu ni endelevu na utaendelea kukumbushwa kwa wale wote ambao wametoa taarifa zao sahihi. Aidha, Wizara imetumia taarifa za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 iliyofanya pia kuhusisha kumbukumbu za wamiliki katika kutambua vipande 524,131 katika maeneo yasiyopangwa na kuviingiza kwenye kanzidata kwa lengo la kuongeza wigo wa makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga mazingira rafiki ya kuwezesha wananchi kuitikia wito wa kulipa kodi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa msamaha kwa wale wote waliokuwa wakidaiwa madeni ya msingi pamoja na riba. Alitoa msamaha wa riba kuanzia Julai, 2022 hadi Aprili 2023. Kupitia Msamaha huo jumla ya shilingi bilioni 38 zimekusanywa kama deni la msingi na bilioni 27 kama msamaha wa riba na hizo zimekusanywa kutoka kwa watu wapatao 15,986.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo

ameweza kutoa nafuu kwa walipa kodi wote ambao wametumia fursa hii vizuri na ametoa kwa muda mrefu muda wa miezi kumi kuweza kusamehe riba hiyo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu bilioni 27 alizozisamehe ni wazi zimekwenda kusaidia jamii yetu katika shughuli zingine za kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara imeweka lengo la kukusanya Shilingi Bilioni 300 kwa kupitia mikakati iliyojiwekea, ikiwemo kuhuisha na kutunza kumbukumbu za wamiliki wa ardhi katika mfumo wa kielektroniki ili kurahisisha utumaji wa ankara kwa kutumia simu za viganjani; kuimarisha miundombinu ya TEHAMA; kutoa elimu; kuhuisha viwango vya ukadiriaji kodi; na kuhamasisha halmashauri na sekta binafsi kuendelea kupima maeneo mapya ili kuongeza wigo wa makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe rai kwa mashirika na taasisi zote, ni vizuri wakaweza kuchukua hati zao katika maeneo wanayoyamiliki kwa sababu changamoto imeonekana ni kubwa katika maeneo mengi yanayomilikiwa na taasisi ambayo kwa sehemu kubwa wanakuwa hawatambui mipaka yao, hawajachukua hati, wengine, wanaishi kwa mazoea. Niombe sasa nitoe rai kupitia Bunge lako, wamiliki wote wa ardhi nchini waweze kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati kama sehemu ya mchango wa maendeleo ya Taifa letu, lakini pia kuepuka usumbufu unaoweza kuchukuliwa hatua za kisheria kwa ukiukaji wa sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara au Serikali haipendi kuona mwananchi yeyote anasumbuliwa ama kunyang'anywa mali yake. Kwa hiyo ni vizuri tunapoitikia wito wa Serikali wa kulipa kodi kwa wakati ili ziweze kutumika kodi hizo katika shughuli za kimaendeleo. Wote tunatambua ardhi ni Wizara wezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapato na Matumizi ya Fungu Na.03; katika mwaka 2022/2023, Tume ya Matumizi ya Ardhi iliidhinishiwa shilingi bilioni 8.9. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Tume imepokea jumla ya shilingi bilioni 5.97, kati ya shilingi bilioni 8.9 ya bajeti yake ambayo ni sawa na 67.4% ya bajeti. Kati ya

fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 1.1 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na 70.6% ya bajeti; shilingi bilioni 1.95 ni Mishahara, sawa na 98.8%; na shilingi 2.97 ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi wa Maendeleo, sawa na 50%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala wa ardhi; kwa mujibu wa Ibara ya 74A ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaelekeza kuhusu kuhakikisha ardhi yote nchini inapangwa, kupimwa na kumilikishwa kwa wananchi kwa manufaa ya kiuchumi na kijamii. Kwa kuzingatia maelekezo haya katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara iliahidi kuandaa Hatimiliki 500,000, Hatimiliki za Hati Kimila 520,000 na hati za sehemu ya Jengo 1,000. Aidha, Wizara iliahidi kusajili miamala ya hatimiliki na Nyaraka za Kisheria 100,000 na kutoa Vyeti vya Ardhi katika vijiji 10. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara imeandaa na kusajili Hatimiliki 76,746 sawa na asilimia 15.3 ya lengo na jumla ya Hati za Hakimiliki za Kimila 51,762 zimetolewa sawa na asilimia 10 ya lengo. Jedwali Na.3 linaonesha. Hatimiliki hizi zimeleta tija kiuchumi kwa wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 15 Mei, 2023, mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 60.1 imetolewa na Taasisi za fedha kwa kutumia Hati za Hakimiliki za Kimila kwa jumla ya wananchi 1,382 katika Wilaya za Mbozi, Iringa, Babati, Bariadi, Arumeru, Mbarali, Manyoni, Kilombero, Bagamoyo, Mbinga na Tandahimba. Napenda kuwahakikishia wananchi na Taasisi za Fedha kuwa Hati za Hakimiliki za Kimila ni nyaraka halali za kisheria na hivyo, nasisitiza waendelee kuzitumia kwa manufaa ya kiuchumi. Napenda kuwahakikishia wananchi na taasisi za fedha kuwa hati za hatimiliki za Kimila ni nyaraka halali kisheria na hivyo nasisitiza waendelee kuzitumia kwa manufaa yao kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara haikuweza pia kufikia malengo kutokana na uandaaji wa hatimiliki za kimila kutokana na baadhi ya watu pengine kupuuzia na kutotaka kumilikishwa wakififikiri ya kwamba hati za hatimiliki za kimila hazina faida, lakini kama nilivyosema mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 60.1 zimeweza kutolewa na mabenki kwa kutumia hizo hati za kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa usalama za Milki nao pia unaendelea kufanyika katika halmashauri zetu wakati wa mradi wa KKK katika mamlaka za upangaji, wananchi wengi pia wameweza kujitokeza lakini hawakukamilisha taratibu katika suala zima la kumilikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara itaandaa na kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila 520,000, Hatimiliki 500,000 na Hati za Sehemu ya Jengo 1,000. Vilevile, Wizara inatarajia kusajili miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za kisheria 100,000. Wizara inatarajia pia kufikia malengo haya kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Milki za Ardhi, Programu ya Kupanga na Kupima halimaarufu kama KKK na Mradi wa Kuboresha Miundombinu ya Upimaji na Ramani kwa kushirikisha wadau wa sekta binafsi, kuimarisha mifumo ya TEHAMA ambayo itarahisisha utoaji wa Hatimilki na kupitia upya viwango vya tozo na ada za umilikishaji ili kuleta unafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili Wizara imejipanga vyema tutakwenda kuangalia upya tozo zile ambazo wananchi wanatozwa kwa ajili ya umilikishaji kwa sababu wengi wamekuwa wakilalamikia kwamba pengine gharama ni kubwa, wanashindwa kumilikishwa. Kama Serikali tunakwenda kupitia upya na kuweza kuona ni namna gani na mchakato tayari umekwishaanza nadhani Wabunge wanaweza wakapata taarifa mapema zaidi kadri tunavyozidi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu rai ya kwamba wananchi wajitokeze kwa wingi waombe kumilikishwa. Pia kupitia mfumo unaokwenda kuboreshwa tunakwenda pia kufanya kazi kubwa ya kuingiza katika mfumo na kuepusha miliki pandikizi ambazo zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ya uwekezaji; Wizara kupitia Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi imesimamia, imeidhinisha maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 vikao vinne vya Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji wa Ardhi vilikaa na vilipokea na kupitisha maombi 135 ya ardhi

yaliyowasilishwa yenye ukubwa wa hekta 29,820.4 zilizoombwa kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje**.** Jedwali Na.5 linaonesha waombaji wote na namna walivyopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji huu una mtaji wa thamani ya dola za Marekani milioni 3.4 sawa na shilingi Trilioni 7.8 za Tanzania. Katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea kuratibu ugawaji na usimamizi wa maeneo ya ardhi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili tupende tena kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameifungua nchi na kufanya wawekezaji sasa wawe huru kuja katika nchi yetu na kuweza kuomba maeneo kwa ajili ya uwekezaji. Tuna imani wawekezaji wote hawa ambao wamepewa ardhi hiyo watakwenda kuwekeza kwa wakati pasipo kukiuka masharti ya uendelezaji. Kwa sababu dhamira ya Mheshimiwa Rais ni njema kuhakikisha wawekezaji wa ndani na nje wanakuja kuwekeza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kuhuisha kumbukumbu na kuziingiza katika Mifumo ya TEHAMA ili kuwezesha utoaji wa huduma kwa urahisi na kwa muda mfupi. Aidha, uhakiki unafanyika kwa kutumia taarifa zilizokusanywa katika zoezi la anuani za makazi na sensa ya watu na makazi pamoja na kumbukumbu za viwanja husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kuishukuru Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kwa kubuni mfumo wa *NaPA (National Physical Addressing System)* ambao umewezesha upatikanaji wa taarifa zinazotumika katika kurahisisha pia uhuishaji wa kumbukumbu za wamiliki wa ardhi. Mfumo huo utasaidia ukusanyaji na ufuatiliaji wa kodi ya pango la ardhi kwa kutumia majira nukta na usimamizi wa uendelezaji wa miji katika maeneo yetu. Tunaipongeza sana Wizara ya Habari kwa kazi kubwa ambayo imefanya hata wale ambao hawakuwa wamejitokeza kwa ajili ya kutambulika kwenye Wizara wanaanza kutambulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi 15 Mei, 2023, Wizara imehuisha

kumbukumbu za wamiliki wa ardhi 635,833 kati ya 500,000 zilizopangwa kuhuishwa kwa mwaka 2023, ambayo ni sawa na asilimia 127 ya lengo. Zoezi hili linatekelezwa kwa kutumia wataalam kutoka Serikalini na wataalam wa kuajiriwa wa muda mfupi. Tunao vijana mahiri kabisa 26 ambao wamefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza sana kwa uzalendo wao lakini kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya na wameweza kuisaidia sana Wizara kupata taarifa zingine muhimu ambazo pengine hazikuweza kupatikana kwa wakati, lakini pia kuongeza wigo mpana wa walipakodi ambao hawakuwepo katika wigo na wamewezeshwa pia kupitia zoezi la sensa na lile la utambuzi wa makazi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea na zoezi hili la kuhuisha kumbukumbu za ardhi hadi kuhakikisha wote wanafikiwa. Nitoe rai kwa wamilki wa ardhi wote nchini ili uweze kupata taarifa zako na kumbukumbu sahihi, tunaomba unapotoa taarifa zako hakikisha unatoa namba yako ya simu ambayo inaweza kufikika wakati wote wa wewe kutaka kupata hoja au kupata taarifa ambazo zinatunzwa na Wizara au kupata taarifa zozote zinazohusiana na salama ya milki yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa migogoro ya ardhi kiutawala; katika kutekeleza Ibara ya 74(i) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kinachotuelekeza kutatua migogoro, Wizara imeendelea kushughulikia migogoro ya ardhi kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo Madawati ya Kushughulikia Malalamiko, Kliniki za Ardhi ambazo zilikuwa zikifanyika katika mikoa yote, Kamati Maalum ya Wataalam ambazo zimekuwa zikiundwa kwenda kufanya kazi katika halmashauri zetu na ziara za viongozi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara imeendelea kupanga matumizi ya ardhi na kutoa elimu kwa umma kuhusu umiliki. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 migogoro 2,684 imeshughulikiwa kiutawala. Jedwali Na.6 linaonesha orodha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika Wizara imeendelea kuhuisha rejista ya migogoro katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Wilaya na katika Halmashauri ili kuwa na taarifa sahihi za migogoro ambayo imetatuliwa na kumalizika na ile inayoendelea. Hii tunaifanya hivyo ili kukwepa kile ambacho kinafanyika kila mabadiliko ya viongozi yanapobadilika, mgogoro hata kama ulikuwa umekwishapatiwa ufumbuzi unaanza upya. Kwa hiyo, tumeelekeza Halmashauri zote nchini katika kila Wilaya kuhakikisha zinatunza rejista za migogoro kadri mtu anavyoingia, kumwandika jina lake, kuweka kumbukumbu ya namba yake ya simu na namna walivyotatua mgogoro wake na pale wanapokuwa wanakamilisha wanaonesha katika *register* zao kwamba mgogoro huu umekwisha ili kuepusha kukaa unajirudia rusia mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara itaendelea kushugulikia migogoro ya ardhi kadri itakavyokuwa inajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa migogoro ya ardhi katika Jiji la Dodoma na Dar es Salaam. Wizara yangu kwa kushirikiana na mamlaka zingine za Serikali iliunda Kamati ya wataalam kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi hususani katika Mikoa yenye migogoro mingi ikiwemo Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jiji la Dodoma, jumla ya migogoro 815 ilipokelewa, ambapo migogoro 429 sawa na asilimia 52.6 ilipatiwa ufumbuzi wa migogoro hiyo, na migogoro 386 inaendelea kushughulikiwa. Vyanzo vya migogoro imebainika kuwa ni milki pandikizi, madai ya fidia, wananchi kutoridhika na upimaji shirikishi, uwepo wa watumishi wengi wa kujitolea waliokosa uratibu na usimamizi wa karibu kwa uzingatio hafifu wa sheria na taratibu zinazoongoza Sekta ya Ardhi na ukosefu wa maadili kwa baadhi ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunashugulikia mgogoro wa Dodoma tumekuta kuna vibarua zaidi ya 126 hawana mikataba na wanafanya kazi za Halmashauri, watu hao walikuwa

wamekabidhiwa miradi, wanashugulikia miradi hawalipwi posho na Halmashauri. Sasa tujiulize watu hao, huna mkataba na Halmashauri, hulipwi posho na unasimamia mradi na hao ndiyo wamekuwa chanzo kikubwa cha migogoro na wamekuwa wakitumika kama *middle men* kwenye shughuli hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechukua hatua ya kuwaondosha wote na tunafanya uchambuzi na yeyote atakayetaka kuingia kama kibarua siyo Dodoma tu bali Halmashauri zote, tunatoa rai wazingatie taratibu. Wakurugenzi katika maeneo yale wazingatie sheria, kanuni na taratibu za kuwaweka vibarua katika maeneo ya kazi ili kuepusha migogoro inayojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mapendekezo hayo ya kumaliza migogoro Wizara pia iliamua kuchukua hatua ya haraka kama nilivyosema kuwaondoa. Katika mwaka 2023/2024, Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali itaendelea na utaratibu wa kutatua migogoro katika Mikoa yenye migogoro mingi ikiwemo Mikoa ya Arusha, Mwanza, Mbeya na Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa migogoro katika vijiji 975; Kamati ya Mawaziri Nane wa Kisekta inayokuwa inaratibu utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri hususani migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975 nchini, inaendelea kusimamia utekelezaji wa uamuzi huo katika Mikoa mbalimbali. Hadi Tarehe 15 Mei, 2023, Kamati ya Mawaziri Nane imefanya ziara kwenye mikoa yote 26, kazi zilizotekelezwa na Kamati hiyo ni pamoja na kutoa matamko kuhusu uamuzi wa Baraza la Mawaziri, kufanya vikao na viongozi wa ngazi mbalimbali na kuweka mikakati ya utekelezaji katika ngazi ya Mkoa na kwa kushirikiana na timu ya wataalam ambazo zimekuwa zikifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila baada ya ziara ya Kamati ya Mawaziri Nane wa Kisekta maelekezo yote yaliachwa chini ya Mkuu wa Mkoa. Wakuu wote wa Mikoa nchini wana maelekezo hayo na watakiwa kukamilisha taratibu ambazo tumewaelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako tukufu nitoe shukrani za dhati kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ndugu yangu Mheshimiwa Homera, Mkuu wa Mkoa wa Mara Ndugu yangu Mheshimiwa Mzee na Mkuu wa Kilimanjaro Ndugu yangu Babu ambao wamefanya kazi yao vizuri na kukamilisha. Serikali inashukuru na inawataka Wakuu wa Mikoa mingine wakamilishe kazi zao ili utaratibu mwingine wa kukamilisha kazi ya kuwamegea wananchi sehem, ambayo Mheshimiwa Raisameridhia wapate iweze kufanyika kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazoendelea kutekelezwa na timu ya wataalam wa kisekta wakiongozwa na Wakuu wetu wa Mikoa ni pamoja na kubainisha maeneo yatakapangwa na kutolewa kwa wananchi, kutafsiri mipaka ya baadhi ya hifadhi na kuweka alama za kudumu na zinazoonekana ardhini, kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji vinavyopakana na Hifadhi za Taifa na kufanya tathmini na uthamini kwa wananchi watakaopisha shughuli za uhifadhi kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako hili ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambae kwa moyo wa dhati kabisa, pamoja na kwamba tunatambua wapo watu ambao waliingia katika maeneo yale kinyume na utaratibu, lakini wapo ambao ambao wako kisheria kwa maana ya vijiji vimesajiliwa. Hata hivyo Mheshimiwa Rais, ameridhia hata wale ambao waliingia kinyume na taratibu ameweza kumega hekari 2,385,316 na imetolewa kwa wananchi ili kuwaondolea adha kwa ajili ya maeneo ambayo pengine walikuwa wakiyamiliki kinyume na utaratibu lakini bado ameridhia wapewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeenda mbali zaidi ametoa kifuta machozi na ameahidi kutoa kifuta machozi kwa watu hawa. Siyo wote watakaopata ni baadhi katika maeneo mbalimbali kutegemeana na uhalisia wake. Kwa hiyo watu wasije wakalichukulia kwamba sasa kila mhalifu aliyeingia katika eneo lisilo lake kwanza kwa utaratibu ni jinai, anatakiwa kushtakiwa kwa jinai. Hata hivyo bado Mheshimiwa Rais ameridhia watu hao

kuweza kupewa kifuta jasho ili waweze kuanza maisha mengine. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake huo wa busara ambao ameamua kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa mgogoro wa mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha unaotokana na Tangazo la Serikali Na. 28 la mwaka 2008 uliogusa Wilaya za Mbarali na Chunya ambao unaendelea chini ya uratibu wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Kazi ya marekebisho ya mpaka uwandani imekamilika ambapo alama 671 za kudumu zinazoonekana kiurahisi, zimewekwa katika eneo lenye urefu wa kilometa 344 na mkuza ambao tayari umekwishawekwa wa kilometa 177 umechongwa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, marekebisho ya Tangazo la Serikali Na. 28 liko katika hatua za mwisho wakati wowote litatangazwa ili wananchi sasa waweze kujua mipaka yao iko wapi. Pamoja na kusubiri tangazo jipya litakalotoka baada ya kuwa tumefuta *GN*. 28 bado ninawataka wananchi wawe wavumilivu, wastahimilivu lakini kazi ya Uwandani kuweka *beacon* umekamilika na Mkuza wa kutenganisha maeneo ambayo ni ya hifadhi na wananchi umewekwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaombe sana wananchi katika maeneo ambayo Serikali imeweza kufanya kazi yake imekwisha weka mipaka na imeweka Mkuza kutenganisha wasiingie kwenye maeneo yale. Kwanza, kuingia kule ni jinai, licha ya hivyo wanakiuka hata ule utaratibu na ridhaa ambayo Mheshimiwa Rais, amewapa katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza zoezi hilo jumla ya ekari 850 kati ya 1,500 zilizopakana katika vijiji vya Uhambule, Chamoto, Nyamakuyu, Iheha, Nyakadete, Mapogoro, Nyakazombe na Miyombweni zilizotengwa kwa ajili ya makazi ya wananchi watakaopisha katika eneo hilo. Mipango ya Matumizi katika maeneo hayo imeandaliwa katika Vijiji 15 kati ya 23 vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Kazi ya uthamini kwa ajili ya fidia imefanyika kwa wananchi 4,072 katika vijiji vinne vya Kilambo, Iyala, Masundasi na Msanga kati ya vijiji vitano ambavyo

vinatakiwa kupisha. Kazi hiyo inaendelea katika Kijiji cha Luhanga pia chenye vitongoji 15 kati ya 38 vilivyopo katika vijiji 16 Wilayani Mbarali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Wabunge na wataalam wote walioshiriki katika utekelezaji wa zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya; katika mwaka 2022/2023 Wizara imefanikiwa kuongeza Mabaraza 12 na hivyo kufanya Mabaraza 92 kati ya Mabaraza 139 yaliyoanzishwa. Kuanzishwa kwa Mabaraza haya kumeleta nafuu ya usafiri na gharama kwa wananchi katika kufuata huduma mbali waliyokuwa wanafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 mashauri 23,412 kati ya 33,250 sawa na asilimia 70 ya lengo yalitolewa maamuzi na mashauri 15,710 yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, katika mwaka 2022/2023, Wizara inatarajia kufungua Mabaraza mapya 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthamini wa mali; katika mwaka 2022/2023, Wizara iliapanga kuratibu uandaaji na uidhinishaji wa taarifa za uthamini 54,000 ambazo kati ya hizo, uthamini wa kawaida 20,000 na taarifa za wafidiwa 34,000 na kushughulikia migogoro 30 ya uthamini wa fidia. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini 62,211 sawa na asilimia 113 ya lengo ambapo kati ya taarifa hizo, uthamini wa kawaida 21,272 na taarifa za fidia 39,939. Aidha, migogoro 20 ya fidia imepokelewa na kushughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023, Wizara iliahidi kuboresha kanzidata ya viwango vya thamani ya ardhi ya mazao na kuhuisha viwango vya kodi ya ardhi nchini ili kuhakikisha uthamini unafanyika kwa kuzingatia bei halisi ya soko na hivyo kuwezesha ulipaji wa fidia stahiki, kupunguza malalamiko kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili limekuwa na malalamiko

mengi na pengine wananchi wanashindwa kutambua thamani ya ardhi haiwezi kulingana. Iliyopo Dodoma Mjini haiwezi kuwa sawa na Bahi na iliyoko Bahi Mjini haiwezi kuwa sawa na kule Mayamaya. Kwa hiyo, kila eneo linakuwa na thamani yake katika ardhi lakini wananchi wetu wamekuwa hawaelewi. Ukimpa thamani anaona kama ameonewa analinganisha thamani yake ya kijijini na mjini. Serikali sikivu imeona ni vema kupitia upya thamani hizi na toka mwezi wa nne 2023 tutatumia viwango vipya ambavyo vimehuishwa kulingana na hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine Serikali pia inakuwa rahimu kiasi kuweza kuangalia hata kama thamani ya pale iko chini lakini bado tumeweza kuongea na wananchi na kuweza kutoa thamani walau ya kumwezesha mwananchi kupata shughuli ya kufanyia pesa hiyo. Wizara itahakikisha viwango hivi vinatumika kwa usahihi kwa kuzingatia sheria na taratibu za uthamini ili kuhakikisha wananchi wanalipwa fidia stahiki inayoendana na bei ya soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe rai kwa taasisi zote, ziwe za umma, ziwe za binafsi kwa wale wote wanaotaka kutwaa ardhi ni marufuku kuchukua ardhi ya mtu kama haujatenga fedha kuweza kumlipa. Kwa sababu tulishapitisha sheria hapa, ndani ya miezi sita haujamlipa tunaanza ku–*charge* riba ya bei soko sawasawa na Benki, ikifika miaka miwili hujamlipa mwananchi yule yuko na uhuru wa kuendelea na eneo lake na ukilitaka utaanza kufanya uthamini upya. Kwa hiyo, niombe sana wale wawekezaji na watu wengine wanaotaka kutwaa ardhi hakikisha umejiweka sawa kuwa na pesa, tusingependa kama Serikali kuendelea kulaumiwa na wananchi kwamba hawajalipwa fidia zao.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Wizara imeshiriki na kuratibu mazoezi mbalimbali ya uthamini kwa ajili ya fidia kwa wananchi wanaopisha miradi mbalimbali ya Serikali pamoja na wananchi wanaopisha maeneo ya hifadhi. Jedwali Na.7 linanesha.

Mheshimiwa Mwenyekiri, katika mwaka 2023/2024, Wizara

itaratibu na kusimamia uandaaji wa taarifa za uthamini 54,000, kati ya hizo, uthamini wa kawaida 20,000 na uthamini wa fidia wa fidia 34,000. Vilevile, Wizara itaendelea kushughulikia malalamiko yatakayotokana na uthamini wa fidia, na kuendelea kuratibu utekelezaji wa mazoezi mbalimbali ya uthamini yanayoendelea nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya TEHAMA katika sekta ya ardhi kama ilivyoelekezwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 74 (b), 2020. Kwa kuzingatia maelekezo hayo Wizara inaendelea kukamilisha maboresho ya Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System – ILMIS)* kwa kutumia watalaam wa ndani. Aidha, pamoja na maboresho yanayoendelea, mfumo huu umeendelea kutumika katika kutoa hati za kielektroniki katika Jiji la Dodoma na Mkoa wa Dar es Salaam. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 jumla ya hati za kielektroniki 23,150 zimetolewa kupitia mfumo huo na kufanya hati zote za kielektroniki kufikia 55,550.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya bajeti ya Mwaka 2022/2023, Wizara iliahidi kujenga, kusimika na kuimarisha miundombinu wezeshi ya TEHAMA kwa awamu katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri nchini na kukarabati mtandao kiambo katika ofisi za ardhi za Halmashauri 47 zikiwemo Makao Makuu ya Mikoa ya Iringa, Lindi, Mwanza na Mbeya. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara imekamilisha kujenga miundombinu wezeshi katika ofisi za ardhi za Halmashauri ya Chalinze, Chamwino na Mkuranga. Vilevile, Wizara imekamilisha kujenga mtandao kiambo (*Local Area Network*) katika ofisi za ardhi za Mikoa ya Iringa, Lindi, Mwanza na Mbeya na kuiunganisha na Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi (*National Land Information Centre*). Aidha, Wizara inakamilisha usimikaji wa mtandao kiambo katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri 14

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024, Wizara inatarajia kusimika na kusambaza miundombinu ya mtandao kiambo katika ofisi za ardhi za Mikoa 26 na Halmashauri 132 na hivyo kuwezesha kukamilisha usambazaji wa mfumo wa *ILMIS* katika Halmashauri zote. nchini. Vilevile, katika mwaka 2023/2024,

Wizara itaanzisha wavuti ya wateja ambapo wananchi watapata huduma kupitia wavuti hiyo na kutolazimika kwenda ofisi za ardhi. Kupitia huduma hii, mwananchi atakuwa na uwezo wa kufuatilia kila hatua ya maombi yake anayoomba kwa ajili ya kumiliki ardhi kupitia simu yake ya kiganjani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mageuzi makubwa ambayo tunaendelea kumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambae ameona changamoto katika Wizara na anaendelea kuiwezesha tutoke katika analogia tuingie katika dijitali na kuwezesha wananchi kuweza kupata taarifa zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubadilishaji wa michoro ya rmipango ya ramani na upimaji wa nyaraka za umiliki kutoka anaolgia kuingia katika Digitali. Mwaka 2022/2023 iliahidi kubadilisha taarifa za ardhi kutoka mfumo wa analogia kwebda kidigitali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 michoro ipatayo 30,812 yenye jumla ya viwanja 7,241,686 na ramani za upimaji 112,297 zenye jumla ya viwanja 2,385,114 zimebadilishwa katika Mikoa yote 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kukuthibitishia katika ubadilishaji wa ramani pamoja na ramani zile za ardhi tumekamilisha katika Mikoa yote 26 kwa asilimia 100. Vilevile, nyaraka za Hati na Majalada 524,131 yamebadilishwa kwa asilimia 100 katika ofisi za ardhi za Mikoa 15 ikiwemo Kagera, Geita, Rukwa, Katavi, Songwe, Tabora, Dodoma, Singida, Shinyanga, Mbeya, Njombe, Kigoma, Iringa, Simiyu na Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024, Wizara itaendelea na zoezi la ubadilishaji wa taarifa za ardhi kutoka mfumo wa analojia kwenda kidigitali kwa nyaraka za Hati na majalada 1,647,326 katika ofisi za ardhi za mikoa 11 nchini ikiwemo Mkoa wa Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Mtwara, Arusha, Pwani, Lindi, Mara, Morogoro, Ruvuma, Tanga na baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upanganji wa miji na maendeleo ya makazi. Wizara katika mwaka 2022/23, iliahidi kuendelea

kushirikiana na Mamlaka za Upangaji katika kuandaa na kutekeleza mpango kabambe katika Mikoa yetu, hii ikiwa ni mwitikio wa Ibara ya 74(a) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 15 Mei, 2023, mpango kabambe mmoja wa Manispaa ya Moshi umekamilika na kuidhinishwa. Rasimu za Mipango Kabambe miwili ya miji ya Mafinga na Bagamoyo inaendelea lakini pia katika Manispaa ya Kahama na Mji wa Chalinze ipo katika hatua za awali. Aidha, katika kipindi hicho Wizara inafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2023 Wizara itaendelea kushirikiana na mamalaka za upangaji katika kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa mipango hiyo kabambe. Kumekuwa na changamoto kubwa mipango inaandaliwa halafu haitekelezwi, mabadiliko ya matumizi ya ardhi yanatoka bila sababu za msingi na hivyo kuifanya miji yetu ionekane ni miji isiyopendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa mamlaka za upangaji nchini kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuandaa mipango kabambe ili kufanya miji yao iende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka zetu zimekuwa zikikiuka taratibu za mipango kabambe na kwa mwaka huu wa fedha tunaoendelea nao, maombi 300 yaliwasilishwa, lakini mabadiliko yamefanyika katika maombi 611 sawa na asilimia 204. Hii inaonesha ni kwa jinsi gani hakuna nidhamu katika kusimamia mipango ambayo wanajiwekea wao wenyewe katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatoa maelekezo katika Ofisi zote za ardhi mikoa kufanya ukaguzi na kubaini maeneo yote yaliyobadilishwa matumizi kinyume na utaratibu ili kuchukua hatua za kisheria kwa wahusika ikiwemo kuwatoza faini ya kisheria ili mambo haya yasijirudie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuandaa miji endelevu ya baadaye, tunaandaa mwongozo kwa ajili ya kuboresha vijiji vyetu ili viweze kukua sawa sawa na namna ambavyo inatarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uratibu wa Sekta ya Nyumba, mwaka 2022, Wizara ilipanga kuwezesha kuboreshwa kwa mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya nyumba za wananchi kupitia *Tanzania Mortgage Refinance Company* na hadi tunavyoongea jumla ya benki 32 zimehusika katika kutoa mikopo na jumla ya Shilingi bilioni 26.4 zimetoka katika ujenzi kwa ajili ya watu hawa waliofaidika na mkopo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023/2024 bado tutaendelea na zoezi hilo na tunategemea kufanya kazi iliyo nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sensa ya Majengo, Ibara ya 74(d) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2022/2023 tuliahidi kufanya zoezi la Sensa ambalo limekamilika na kama nilivyosema awali limekamilika vizuri. Kwetu kama Wizara ya Ardhi, limetuoa takwimu mbalimbali ambazo katika taarifa yangu tutakwenda kuzisoma, ziko zimeainishwa kwenye kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na muda naomba niseme zoezi la upimaji na uandaaji wa ramani ambalo linaendelea, bado tunafanya kazi katika hatua kulingana na mahitaji katika maeneo yetu. Nitoe tu taarifa njema kwa Watanzania kwamba Wizara itaanza hatua ya awali ya kujenga ujenzi wa vituo 22 vya upimaji ambavyo vitakwenda kurahisisha zoezi la upimaji kuwa la muda mfupi Zaidi. Jedwali Na. 10 (a) linaonesha. Pia tutasimika pia alama za msingi 276, Jedwali Na. 10(b) linaonesha. Tukishapata ramani zetu, tutaondokana na kununua ramani kutoka maeneo mengine, pia zitaturahisishia kupata ramani za msingi ambazo zitakwenda kurahisisha zoezi la upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maendeleo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Shilingi bilioni 50 alizotupa, lakini niseme tu, matumizi ya pesa hizi

katika baadhi ya Halmashauri imekuwa siyo nzuri, wengi wamepewa mikopo na hawajaweza kurejesha. Ukiangalia katika majedwali ambayo tumeyaweka, tumeanisha Halmashauri zote ambazo zinadaiwa. Nitoe rai, watu waweze kurudisha mikopo hiyo ili Halmashauri nyingine ziweze kupewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza halmashauri ambazo zimekamilisha mkopo wao; Manispaa ya Morogoro, Manispaa ya Ilemera, Mji wa Tunduma, Mji wa Bariadi, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Meru, Geita na Mbozi. Hawa wote wamekamilisha malipo ya mkopo waliopewa. Waliotoa nusu ni Babati, Sumbawanga, Kishapu, Musoma Mjini, Ifakara, Manispaa ya Shinyanga, Shinyanga *DC*, Chalinze na kwingineko. Wale ambao sijawataja hapa, wako wameorodheshwa, wanadaiwa na hawajaweza kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi wa uboreshaji wa usalama wa milki ambao upo katika vishikwambi vyetu na niseme tu, tumepata mkopo wa *US Dollar* milioni 150, sawa na Shilingi bilioni 345. Mkopo huo utakwenda kufanya kazi za uimarishaji makazi yasiyopangwa, uboreshaji wa miundombinu, usimamizi, kujenga Ofisi za Mikoa yote, usimikaji na usambazaji wa mfumo, ubadilishaji wa nyaraka na utoaji wa vitendea kazi. Taarifa hii inapatikana ukurasa wa 61 hadi 62.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu utakwenda kufanyika katika mikoa iliyopangwa yote 25 itakuwepo, na tunakwenda kutoa hati kama ambavyo zinaonekana kwenye taarifa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa muda, naomba niende eneo lingine katika suala zima la *National Housing* ambayo nayo iko chini ya Wizara. Naomba taarifa yangu yote ichukuliwe kwenye taarifa sahihi ya kumbukumbu za Bunge. Nakimbizana na muda. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameendelea kuliwezesha Shirika letu la Nyumba kuweza kuendelea na miradi

ambayo ilikuwa imelala. Kwa muda mfupi ametoa Shilingi bilioni 173.9 kuridhia Shirika la Nyumba liweze kuendelea na kazi ambazo amekuwa akizifanya. Wote ni mashahidi, tumeona miradi ya *Morocco Square* ilikuwa imesimama, ukamilishaji wake sasa ni asilimia 100, kuna mradi wa Kawe *7/11,* kuna miradi mingine ambayo tumeanzisha *Plot No. 300* nao ulikuwa haujakamilika, lakini tuna *Samia Housing Scheme* ambayo imeanza na utekelezaji wake unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu shirika hili ni shirika pekee ambalo liko kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na pia katika suala zima la uwekezaji. Hapa tunapozungumza, tayari tulizindua sera ya ubia ambapo Shirika la Nyumba linakwenda kuingia ubia na mashirika zaidi ya 20 kwa ajili ya kuweza kufanya uendelezaji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tuseme tu ya kwamba miradi hiyo ambayo inakwenda kufanyika, ina gharama kubwa kiasi kwamba tunakwenda kubadilisha kabisa sura ya nchi yetu hasa katika maeneo ya uwekezaji ambao unakwenda kuwekeza. Pia ukiangalia mradi wa *Samia Housing Scheme* ambao unagharimu Shilingi bilioni 466, utakwenda kuanza na utakwenda kukamilisha nyumba 560 ambazo zimeshaanza katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kule Kawe na zinaendelea kujengwa, na pia itakwenda katika maeneo mengine kama ambavyo tumekuwa tukiendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia shirika hili limekuwa likifanya kandarasi mbalimbali. Hapa tunapoongea, tayari lina miradi katika Wizara zetu nane, ambapo limekuwa likijenga yale majengo ya Wizara. Katika majengo hayo yanayojengwa ni pamoja na Wizara ya Nishati; Madini; Habari; Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Utamaduni, Sanaa na Michezo; na Mambo ya Ndani. Hizo ni Wizara ambazo wanaendelea nazo. Pia wameweza kujenga jengo la Ofisi ya Wakala wa Huduma kwa ununuzi Serikalini kwa maana ya *GPSA* katika Mkoa wa Pwani, Dodoma Simiyu na Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeweza pia kuwekeza katika Kituo cha Biashara cha *Tanzanite* katika miji ya Mererani, Simanjiro Mkoa wa Manyara, mradi ambao utagharimu Shilingi bilioni 5.49**.** Mradi huu ulianza Mei, 2022 na umefikia asilimia 70. Nadhani unakwenda kubadilisha kabisa hali ya pale na mauzo ya madini yetu ambayo ni Fahari ya Tanzania yatakwenda kuwa katika maeneo mazuri. Ujenzi huu ulianza Aprili na utakamilika Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Mipango, ibara ya 74 (b) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaelekeza kuweza kupanga mpango wa matumizi bora ya ardhi. Tume yetu ya Mipango inaendelea kuratibu na kusimamia halmshauri zetu katika maeneo mbalimbali. Pia nayo imekuwa ikifanya kazi nzuri katika maeneo hayo. Imefaya kazi katika maeneo ya Nsimbo, Katavi, Ngorongoro, Arusha na Kigoma ambao wamemaliza suala zima la mpango matumizi ya ardhi. Jumla ya mipango ya matumizi 306 sawa na asilimia 153 imekamilika. Jedwali Na. 14 linaonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 maeneo yenye ukubwa wa hekta 231,321 yametengwa kwa ajili ya malisho na hekta 191,110 hifadhi ya misitu na mengine yanasomeka katika jedwali Na. 15, naomba Waheshimiwa Wabunge mweze kuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe rai kwa halmashauri zote zote nchini kutoa kipaumbele katika kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa sababu hii ni kazi ya msingi ya halmashauri zetu kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Na. 8. Pia Sheria ya Vijiji inawapa mamlaka halmashauri zetu kuweza kupanga mpango wa matumizi ya ardhi zao. Tunavyo vyuo vyetu na bodi za wataalamu vyuo vya ardhi Tabora pamoja na Morogoro vimeendelea na kazi zake zikisimamiwa na bodi za wataalamu ambazo zipo. Taarifa zake ziko ukurasa wa 91 hadi 93.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nitoe shukrani za dhati na kutambua mchango wa viongozi wenzangu; Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Waziri na kwa Wabunge. Kwa

namna ya pekee namshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Namshukuru Katibu Mkuu Anthony Sanga; Naibu Katibu Mkuu, Lucy Kabyemera; Kamishna wa Ardhi, Nathaniel Mathew Nhonge; pamoja na Wakurugenzi wote kwa idara zote bila kuwataja mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wadau wote wa sekta ya ardhi ambao tulikuwa tukishirikaiananao, wakiwemo Benki ya Dunia, Benki *ya EXIM* ya Korea, *UN-HABITAT*, *Shelter Afrique*, *African Union Comission,* Benki ya Maendeleo ya Afrika, taasisi za fedha, Asasi za kiraia, mashirika yasiyo ya kiserikali, wananchi na watu wengine kwa mchango wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye makadirio sasa ya matumizi ya mwaka 2023/2024; naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi mishahara shilingi bilioni 43.4; matumizi mengineyo, shilingi bilioni 37.6; jumla ndogo shilingi bilioni 81.04. Matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 14; fedha za nje, Shilingi bilioni 68; jumla ndogo, shilingi bilioni 84.126. Jumla ya matumizi ni shilingi 163,169,880,000. Jumla ya matumizi ya kawaida pamoja na maendeleo ni shilingi 163,169,840,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango ya Matumizi, Wizara inaomba kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya shilingi bilioni 8.2 katika mgawanyo ufuatao: Matumizi kwa maana ya mishahara, shilingi bilioni 2.4; matumizi mengineyo, shilingi bilioni mbili; mapato ya Serikali ni shilingi milioni 18; fedha za ndani kwenye matumizi ya maendeleo ni shilingi bilioni 3.4. Jumla ndogo, shilingi bilioni 3.4. Ukichukua jumla ya pamoja ni shilingi 8,202,628,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla kuu ya fedha zinazoombwa kwa Wizara, Fungu Namba 48 na Fungu Namba 3 ili Bunge liweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi bilioni 171,372,508,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara www.lands.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana wewe binafsi pamoja na Wabunge wote kwa muda wenu ambao mmeweza kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

### UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**). Naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2022/23. Naomba pia Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo mawili kwa mwaka 2023/24.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa **11** wa Bunge la **12** ambalo ni mahsusi kwa ajili ya kujadili Mpango na Bajeti ya Serikali. Aidha, kwa heshima na taadhima naomba kutumia fursa hii kipekee kumshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuendelea kusimamia majukumu ya Sekta hii muhimu ya

Ardhi. Nimuahidi na kumhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba, imani aliyoionesha kwangu nitaendelea kuitafsiri kwa vitendo kwa kuhakikisha masuala muhimu yanayohusu ustawi na uendelevu wa Sekta hii yanasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri ambao katika kipindi cha miaka miwili umeleta mageuzi katika mifumo ya utoaji huduma, kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji, kuimarisha Sekta ya Milki na miradi mikubwa ya kuendeleza Sekta ya Ardhi.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwapongeza Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Ruangwa kwa uongozi wao mahiri. Nawashukuru kwa miongozo, maelekezo na ushirikiano wanaonipa unaoniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza Sekta hii muhimu. Aidha, nampongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake mahiri na jitihada za dhati katika kusimamia uchumi, maslahi na ustawi wa wananchi.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nakupongeza wewe binafsi na Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza shughuli za Bunge kwa umahiri na umakini. Vilevile, nawapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile Mbunge wa Mufindi Kusini kwa kuchaguliwa kuwa wenyeviti wa Bunge. Tunawaombea Mwenyezi Mungu awajalie afya njema na hekima katika utekelezaji wa majukumu yao.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na Mhe. Mussa Hassan Mussa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani-Zanzibar. Pia, natoa pole kwa familia, ndugu, jamaa,

marafiki na wananchi wa jimbo la Amani kwa kuondokewa na mpendwa wao. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema, Amina.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile natoa pole kwa watanzania wenzetu walioathirika na majanga mbalimbali ikiwemo ajali ya ndege katika ziwa Victoria iliyotokea tarehe 6 Novemba, 2022, ajali za barabarani na mafuriko. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuepushe na majanga hayo.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza Mhe.Timotheo Paul Mzava (Mb.), kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.), kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati. Wizara inaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu ya usimamizi wa Sekta ya Ardhi kwa ustawi na maendeleo ya nchi yetu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nawapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri na Viongozi wengine walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika mabadiliko ya kiutendaji yaliyofanywa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Angela Jasmin Kairuki (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Namtakia kheri katika utekelezaji wa majukumu ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kupitia Ofisi anayoisimamia. Pia, nampongeza Mhe. Abdul Yussuf Maalim kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Amani.

10. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuwapongeza Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb.), kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhandisi Anthony Damian Sanga kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu na Bi. Lucy Dominico Kabyemera kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua fursa hii kumpongeza

Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba yake nzuri ya Bajeti ambayo imetoa utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2022/23, pamoja na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2023/24. Kama Waziri mwenye dhamana ya Ardhi naahidi kusimamia kikamilifu utekelezaji wa maelekezo yote yanayohusu Sekta ya Ardhi.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa uchambuzi makini na ushauri iliyoutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu **48)** na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03)** kwa mwaka 2023/24. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara itaendelea kuzingatia maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati katika kuboresha utendaji kazi na hivyo kuongeza tija katika utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kwa kura nyingi zilizopelekea kuchaguliwa kwangu kuwa mjumbe wa NEC, pia nawashukuru viongozi wa Chama cha Mapinduzi kwa miongozo, ushauri na maelekezo mbalimbali wanayonipatia kuhakikisha Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 inatekelezwa kwa ufanisi. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Ilemela kwa ushirikiano wanaonipa wakati nikitimiza majukumu yangu kama mwakilishi wao hapa Bungeni. Kipekee kabisa, naishukuru sana familia yangu kwa kuwa karibu nami na kuendelea kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu. Pia, nawashukuru viongozi wa dini kwa sala na dua ambazo zinanipa nguvu katika kutekeleza majukumu yangu.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/24. Bajeti hii imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa

Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); Mikataba; Itifaki; Mipango na Makubaliano mbalimbali ya kikanda na kimataifa; Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Sekta ya Ardhi na Kitaifa; na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

**Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2022/23 na Malengo ya Mwaka 2023/24.**

Matumizi

15. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **bilioni 105.5.** Kati ya fedha hizo, shilingi **bilioni 33.9** zilikuwa kwa ajili ya kuwezesha Matumizi Mengineyo (OC); shilingi **bilioni 44.4** kwa ajili ya Mishahara ya watumishi (PE); na shilingi **bilioni 27.2** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za Miradi ya Maendeleo shilingi **bilioni 14** ilikuwa ni fedha za ndani na shilingi **bilioni 13.2** fedha za nje. Aidha, katika mwaka 2022/23, Wizara iliongezewa bajeti ya shilingi **bilioni 69.8** ikiwa ni fedha za ndani za Maendeleo na kulipa madeni. Ongezeko hilo limefanya bajeti ya Wizara kufikia shilingi **bilioni 175.3.**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara imepokea jumla ya shilingi **bilioni 147.7** kati ya bajeti ya shilingi **bilioni 175.3** sawa na asilimia **84.2** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi **bilioni 21.5** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia **64** ya bajeti ya OC; shilingi **bilioni 32.8** ni mishahara ya watumishi sawa na asilimia **74** ya bajeti ya mshahara; na shilingi **bilioni 93.3** ni fedha za maendeleo sawa na **asilimia 96.1** ya bajeti yote ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo fedha za ndani zilizopokelewa ni shilingi **bilioni 80.3** sawa na asilimia **95.7** na shilingi **bilioni 13** sawa na asilimia **98.9** ya fedha za nje za maendeleo ***(Jedwali Na. 1).***

Ukusanyaji wa Maduhuli

17. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara kupitia Fungu **48** ilipanga kukusanya shilingi bilioni **250.1** kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ya Sekta ya Ardhi. Hadi kufikia tarehe 15

Mei, 2023, Wizara imekusanya shilingi bilioni **132.9** sawa na asilimia **53.2** ya lengo ***(Jedwali Na.2)*.**

18. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia lengo la makusanyo, Wizara inaendelea kuboresha kumbukumbu na mifumo ya TEHAMA iliyopo ili iweze kutuma ujumbe kwa njia ya simu. Maboresho hayo yamewezesha kutuma ujumbe mfupi wa kuwakumbusha kulipa kodi ya pango la ardhi wamiliki **202,563** katika kipindi cha Februari-Mei, 2023 na utaratibu huu ni endelevu. Aidha, Wizara imetumia taarifa za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 kuhuisha kumbukumbu za wamiliki na pia kutambua vipande vya ardhi **524,131** katika maeneo yasiyopangwa na kuviingiza kwenye kanzidata kwa lengo la kuongeza wigo wa makusanyo. Vilevile, Wizara itaendelea kutumia Kanuni za Msamaha wa Riba ya Malimbikizo ya Kodi ya Pango la Ardhi za mwaka 2022, Tangazo la Serikali Na.537B pale inapolazimu, kutoa elimu na kuhamasisha wamiliki wa ardhi kulipa kodi kwa wakati.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa muda mrefu baadhi ya wamiliki wa ardhi wamekuwa wakishindwa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati na hivyo kulimbikiza madeni na riba. Katika kujenga mazingira rafiki ya kuwezesha wananchi kuitikia wito wa kulipa kodi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa msamaha wa kulipa deni la msingi bila riba kwa kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Aprili 2023. Msamaha huo umewezesha kulipwa kwa deni la msingi la kiasi cha shilingi bilioni **38.** Aidha, Jumla ya wamiliki **15,986** wamesamehewa kiasi cha shilingi bilioni **27.**

20. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2023/24, Wizara imeweka lengo la kukusanya shilingi **bilioni 300**. Ili kufikia lengo hili Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa mikakati iliyojiwekea ikiwemo kuhuisha na kutunza kumbukumbu za wamiliki wa ardhi katika mfumo wa kielektroniki ili kurahisisha utumaji wa ankara kwa kutumia simu za viganjani; kuimarisha miundombinu ya TEHAMA; kutoa elimu ya mlipa kodi; kuhuisha viwango vya ukadiriaji kodi; na kuhamasisha Halmashauri na Sekta binafsi kuendelea kupima maeneo mapya ili kuongeza wigo wa makusanyo. ***Natoa rai kwa wamiliki wote wa ardhi nchini kulipa kodi ya pango la ardhi kwa***

***wakati kama sehemu ya mchango wa maendeleo ya Taifa letu lakini pia kuepuka usumbufu endapo watachukuliwa hatua za kisheria kwa ukiukaji wa sheria, kanuni na taratibu.***

Mapato na Matumizi ya Fungu Na.03

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Tume ya Matumizi ya Ardhi iliidhinishiwa jumla ya shilingi **bilioni 8.9.** Kati ya fedha hizo Shilingi **bilioni 1.98** ni Mishahara ya watumishi (PE); shilingi **1.5** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC); na shilingi **bilioni 5.4** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ambazo ni fedha za ndani.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Tume imepokea jumla ya shilingi **bilioni 5.97** kati ya bajeti ya shilingi **bilioni 8.9** sawa na **67.4%** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi **bilioni 1.1** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) sawa na **70.6%** ya bajeti; shilingi **1.95** ni Mishahara sawa na **98.8%**; na shilingi **2.97** ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Maendeleo sawa na **55.0%.**

Ukusanyaji wa Maduhuli Kupitia Fungu 03

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imeendelea kukusanya maduhuli kutoka katika vyanzo mbalimbali. Katika mwaka 2022/23, Wizara kupitia Tume ilipanga kukusanya shilingi milioni **6** kutokana na kodi ya pango la nyumba zake zilizopo Tabora. Hadi, kufikia Machi, 2023 shilingi milioni **13.2** sawa na **asilimia 220** zimekusanywa kutoka kwenye chanzo hicho. Mapato hayo yako juu ikilinganishwa na malengo kwa sababu yamejumuisha madeni ya kipindi cha nyuma.

**UTAWALA WA ARDHI**

24. ***Mheshimiwa Spika***, ardhi ni moja ya rasilimali muhimu ya uzalishaji na utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi. Hata hivyo, ardhi haiongezeki lakini mahitaji yake yanaendelea kuongezeka, hivyo kuwa na uhitaji wa usimamizi na udhibiti ili kuwa na matumizi endelevu. Usimamizi na utoaji huduma za ardhi unazingatia sera,

sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya kisekta na kitaifa.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** usimamizi wa ardhi unajumuisha uandaaji na usajili wa Hatimiliki za ardhi, usimamizi wa masharti ya umilikishaji, ugawaji wa ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi, usimamizi wa ardhi ya uwekezaji, uhuishaji wa kumbukumbu za ardhi na uthamini wa ardhi.

Uandaaji na Usajili wa Hatimiliki za ardhi

26. ***Mheshimiwa Spika,*** *kwa mujibu wa Ibara ya 74(a) ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza kuhusu kuhakikisha ardhi yote inapangwa, kupimwa na kumilikishwa kwa wananchi kwa manufaa ya kiuchumi na kijamii.* Kwa kuzingatia maelekezo haya katika mwaka 2022/23, Wizara imeendelea kuandaa na kusajili Hatimiliki na Hati za Hakimiliki za Kimila kwa wananchi na taasisi na kutoa Vyeti vya Kijiji. Umuhimu wa Hatimiliki za ardhi ni kuongeza usalama wa milki na kuwezesha kupunguza migogoro ya ardhi. Vilevile, Hatimiliki zinaweza kutumika kama dhamana kwenye Taasisi za Fedha na Vyombo vya Kisheria. Mathalan, hadi tarehe 15 Mei, 2023 mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni **60.1** imetolewa na Taasisi za fedha kwa kutumia Hati za Hakimiliki za Kimila **1,382** katika Wilaya za Mbozi, Iringa, Babati, Bariadi, Arumeru, Mbarali, Manyoni, Kilombero, Bagamoyo, Mbinga na Tandahimba. Napenda kuwahakikishia wananchi na Taasisi za fedha kuwa Hati za Hakimiliki za Kimila ni nyaraka halali za kisheria hivyo, nasisitiza waendelee kuzitumia kwa manufaa ya kiuchumi.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2022/23, iliahidi kuandaa Hatimiliki **500,000,** Hati za Hakimiliki za Kimila **520,000** na Hati za Sehemu ya Jengo **1,000.** Aidha, Wizara iliahidi kusajili miamala ya hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **100,000** na kutoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **100**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara imeandaa na kusajili Hatimiliki **76,746** sawa na **asilimia 15.3** ya lengo. Pia, jumla ya Hati za Hakimiliki za Kimila **51,762** zimetolewa sawa na **asilimia 10** ya lengo.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji,

jumla ya vyeti **67** vimeandaliwa sawa na **asilimia 67** ya lengo, Hati za Sehemu ya Jengo **300** sawa na **asilimia 30** ya lengo na miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **92,124** sawa na **asilimia 92.1** ya lengo zimesajiliwa ***(Jedwali Na.3).***



*Waziri wa Ardhi Mhe. Dkt Angeline Mabula akimkabidhi mwananchi wa Msomera wilayani Handeni mkoa wa Tanga Hatimiliki ya Kimila.*

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara haikuweza kufikia malengo katika uandaaji na usajili wa Hatimiliki na Hati za Hakimiliki za Kimila kutokana na kuchelewa kuanza kwa mradi wa Uboreshaji wa usalama wa Milki za Ardhi, kutokamilika kwa wakati miradi ya KKK katika mamlaka za upangaji, wananchi wengi kutokamilisha ulipaji wa gharama za umilikishaji na changamoto ya mifumo ya TEHAMA.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara itaandaa na kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila **520,000**, Hatimiliki **500,000** na Hati za Sehemu ya Jengo **1,000**. Vilevile, Wizara itasajili miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za kisheria **100,000.** Wizara inatarajia kufanikisha malengo haya kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Milki za Ardhi, Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK), na Mradi wa Kuboresha Miundombinu ya Upimaji na Ramani kwa kushirikisha wadau wa

sekta binafsi, kuimarisha mifumo ya TEHAMA ambayo itarahisisha utoaji wa Hatimilki na kupitia upya viwango vya tozo na ada za umilikishaji ili kuleta unafuu kwa wananchi.

Usimamizi wa Masharti ya Umiliki

31. ***Mheshimiwa Spika,*** umilikishaji wa ardhi unahusisha utoaji wa hatimiliki unaoambatana na masharti ya umiliki yakiwemo sharti la uendelezaji, ulipaji kodi ya pango la ardhi, utunzaji wa mazingira na utunzaji wa mipaka ya eneo. Pamoja na masharti hayo, Wizara imeimarisha zaidi sharti la utunzaji mazingira kwa kuongeza kipengele kinachomtaka kila mmiliki kupanda miti kwa lengo la kuunga mkono jitihada za Serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



*Waziri wa Ardhi Mhe. Dkt Angeline Mabula akiwa katika picha ya pamoja na wananchi wa Msomera wilayani Handeni mkoa wa Tanga alipowakabidhi Hatimiliki ya Kimila pamoja na mti ikiwa ni juhudi za kuhamasisha utunzaji na uhifadhi mazingira*

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuchukua hatua kwa wamiliki wa ardhi ambao wamebainika kukiuka masharti ya milki walizopewa. Lengo la hatua hiyo ni kuhakikisha ardhi inaendelezwa na kutumika kwa mujibu wa mipango iliyoandaliwa na vilevile inachangia ipasavyo kwenye uchumi wa Taifa. Napenda kuchukua nafasi hii kuwaasa wamiliki wa ardhi

kuzingatia masharti ya umiliki waliyopewa ili kuepuka milki zao kubatilishwa kwa kuwa imebainika pia kuwa mashamba na viwanja visivyoendelezwa vimekuwa ni chanzo cha migogoro mingi ya ardhi.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kukagua milki za mashamba **230** ili kubaini uzingatiwaji wa masharti ya umiliki. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, jumla ya mashamba **216** yalikaguliwa na kubainika kuwa hayajaendelezwa na hatua za ufutaji milki zimenza kuchukuliwa kwa mashamba **49** na uchambuzi wa hatua za kuchukua kwa mashamba **167** unaendelea (***Jedwali Na. 4***). Katika mwaka 2023/24, Wizara itakagua mashamba **230** ili kubaini uzingatiwaji wa masharti ya umiliki.

Usimamizi wa Ardhi ya Uwekezaji

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi inasimamia uidhinishaji wa maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Vikao vinne (**4**) vya Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji wa Ardhi vilipokea na kupitisha maombi **135** ya ardhi yaliyowasilishwa yenye ukubwa wa hekta **29,820.4** zilizoombwa kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ***(Jedwali Na. 5***). Uwekezaji huu una mtaji wa thamani ya dola za Marekani milioni **3.4** sawa na shilingi Trilioni **7.8** za Tanzania. Katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kuratibu ugawaji na usimamizi wa maeneo ya ardhi ya uwekezaji.

Uhuishaji wa Kumbukumbu za Ardhi

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa taarifa sahihi za wamiliki wa ardhi, Wizara inaendelea kuhuisha kumbukumbu na kuziingiza katika Mifumo ya TEHAMA ili kuwezesha utoaji wa huduma kwa urahisi, usahihi na kwa muda mfupi. Uhuishaji huo unahusisha uhakiki wa taarifa za namba za simu za wamiliki, uoanishaji wa namba za NIDA, ukubwa wa viwanja, matumizi na mahali vilipo. Aidha, uhakiki unafanyika kwa kutumia taarifa zilizokusanywa katika zoezi la anuani za makazi na sensa ya watu na makazi pamoja na

kumbukumbu za viwanja husika. Aidha, naishukuru Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kwa kubuni mfumo wa NaPA (National Physical Addressing System) ambao umewezesha kupatikana kwa taarifa zinazotumika katika kurahisisha uhuishaji wa kumbukumbu za wamiliki wa ardhi. Mfumo huo utasaidia ukusanyaji na ufuatiliaji wa kodi ya pango la ardhi kwa kutumia majira ya nukta na usimamizi wa uendelezaji wa miji.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi 15 Mei 2023 Wizara imehuisha kumbukumbu za wamiliki wa ardhi **635,833** kati ya **500,000** zilizopangwa kuhuishwa kufikia Juni 2023 sawa na **asilimia 127** ya lengo. Zoezi hili linatekelezwa kwa kutumia wataalam kutoka Serikalini na wataalam wa muda **26**. **Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza kwa kazi kubwa na ya kizalendo ambayo imewezesha uchakataji kidigitali wa taarifa hizo.** Katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea na zoezi la kuhuisha kumbukumbu za ardhi**.**





*Wataalamu wakifanya kazi ya uhuishaji kumbukumbu za wamiliki wa ardhi jijini Dodoma*

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Kiutawala**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** *Ibara ya 74(i) ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza kuhusu kuimarisha usimamizi wa utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini kwa kuchukua hatua stahiki ikiwemo kuboresha shughuli za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya*. Katika kutekeleza agizo hili, Wizara imeendelea kushughulikia migogoro ya ardhi kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo madawati ya kushughulikia malalamiko, kliniki za ardhi, Kamati Maalum ya Wataalam wa Wizara na ziara za viongozi

katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali Wizara imeendelea kupanga matumizi ya ardhi na kutoa elimu kwa umma kuhusu umiliki na madhara ya migogoro ya ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 migogoro **2,684** imeshughulikiwa kiutawala **(*Jedwali Na. 6*).** Aidha, Wizara imeendelea kuhuisha rejista za migogoro katika ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri ili kuwa na taarifa za migogoro iliyopatiwa ufumbuzi na ambayo inaendelea na utatuzi wake. Katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kushughulikia migogoro ya ardhi kadri itakavyokuwa ikijitokeza.

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika Jiji la Dodoma

38. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua changamoto za migogoro iliyopo nchini, Wizara yangu kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali iliunda Kamati ya wataalam kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi hususani katika Mikoa yenye migogoro mingi kwa awamu. Katika awamu ya kwanza, Kamati hiyo imeshughulikia migogoro ya ardhi katika Mkoa wa Dar es Salaam na Jiji la Dodoma. Kwa Mkoa wa Dar es Salaam, jumla ya migogoro **386** ilipokelewa ambapo migogoro **201** sawa na asilimia **52** ilipatiwa ufumbuzi na hatua za utatuzi wa migogoro **186** iliyosalia zinaendelea.

39. **Mheshimiwa Spika,** kwa Jiji la Dodoma, jumla ya migogoro **815** ilipokelewa ambapo migogoro **429** sawa na asilimia **52.6** ilipatiwa ufumbuzi na migogoro **386** inaendelea kushughulikiwa. Vyanzo vya migogoro iliyobainika hasa kwa Jiji la Dodoma ni pamoja na uwepo wa milki pandikizi, madai ya fidia, wananchi kutoridhika na upimaji shirikishi, uwepo wa watumishi wengi wa kujitolea waliokosa uratibu na usimamizi wa karibu na uzingatiaji hafifu wa sheria na taratibu zinazoongoza Sekta ya Ardhi na ukosefu wa maadili kwa baadhi ya watumishi.



*Waziri wa Ardhi Mhe. Dkt Angeline Mabula akizungumza na wananchi wa Ndachi Mnadani jijini Dodoma alipokwenda kusikiliza changamoto za ardhi.*

40. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za Wilaya na Mkoa itaweka mpango wa pamoja wa kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya kumaliza migogoro iliyopo na kuweka mikakati ya kutozalisha migogoro mipya. Sambamba na hatua hiyo, Wizara iliamua kuchukua hatua za haraka kwa kuwaondoa watumishi wote wa muda katika Jiji la Dodoma ili kudhibiti migogoro iliyokuwa inaendelea kuzalishwa. Aidha, katika mwaka 2023/24, Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali itaendelea na utaratibu wa kutatua migogoro katika mikoa yenye migogoro mingi ikiwemo Mikoa ya Arusha, Mwanza, Mbeya na Morogoro.

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika Vijiji 975

41. ***Mheshimiwa Spika***, Kamati ya Mawaziri wa Kisekta inayoratibu utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusu migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji **975** nchini inaendelea kusimamia utekelezaji wa uamuzi huo katika mikoa mbalimbali. Hadi tarehe 15 Mei, 2023, Kamati ya Mawaziri imefanya ziara kwenye mikoa yote **26**. Kazi zilizotekelezwa na Kamati hiyo ni pamoja na kutoa matamko kuhusu uamuzi wa Baraza la Mawaziri, kufanya vikao na viongozi wa ngazi mbalimbali na kuweka mikakati ya utekelezaji katika ngazi ya mkoa kwa kushirikiana na timu ya wataalam wa kisekta.

42. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zinazoendelea kutekelezwa na timu ya wataalam wa kisekta wakiongozwa na Wakuu wa Mikoa ni pamoja na kubainisha maeneo yatakayomegwa na kutolewa kwa wananchi; kutafsiri mipaka ya baadhi ya hifadhi na kuweka alama za kudumu na zinazoonekana ardhini; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji vinavyopakana na Hifadhi za Taifa; na kufanya tathmini na uthamini kwa wananchi watakaopisha shughuli za uhifadhi kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Serengeti (Ghuba ya Speke).



*Mikutano ya utatuzi wa migogoro ya vijiji 975 ikiendelea uwandani, Wilayani Mbarali, Mkoani Mbeya.*

43. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza maamuzi ya Serikali, ardhi yenye ukubwa wa ekari **2,385,316** imetolewa kwa wananchi baada ya kumegwa au kufutwa kwa baadhi ya maeneo ya Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Hifadhi za Misitu**.** Maeneo hayo yanaendelea kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi ili yaweze kutumika kwa ajili ya shughuli za makazi, kiuchumi na kijamii.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** utatuzi wa mgogoro wa mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha unaotokana na Tangazo la Serikali Na. 28 la mwaka 2008 (GN 28) unaogusa Wilaya za Mbarali na Chunya unaendelea chini ya uratibu wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 kazi ya marekebisho ya mpaka uwandani imekamilika ambapo alama **671** za kudumu

zinazoonekana kirahisi zimewekwa katika eneo lenye urefu wa kilomita **344** na mkuza wenye urefu wa kilomita **177** umechongwa**.** Aidha, marekebisho ya Tangazo la Serikali (GN 28) yako katika hatua za ukamilishaji.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza zoezi hilo jumla ya ekari **854** kati ya **1,500** zimepatikana katika vijiji vya Uhambule, Chamoto, Nyamakuyu, Iheha, Nyakadete, Mapogoro, Nyakazombe na Miyombweni kwa ajili ya makazi ya wananchi watakaopisha maeneo ya hifadhi; Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeandaliwa katika Vijiji **15** kati ya **23** vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa ya Ruaha; kazi ya uthamini kwa ajili ya fidia imefanyika kwa wananchi **4,072** katika vijiji vinne (**4**) vya Kilambo, Iyala, Masundasi na Msanga kati ya vijiji vitano (**5**) na kazi hiyo inaendelea katika Kijiji cha Luhanga na vitongoji **15** kati ya **38** vilivyopo katika vijiji **16** Wilayani Mbarali. **Napenda kutoa msisitizo kwa Wakuu wa Mikoa husika na timu za wataalam kuhakikisha kazi hii inakamilika bila kuzua taharuki kwa wananchi.**

Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

46. ***Mheshimiwa Spika,*** mojawapo ya jukumu la Wizara ni kutatua migogoro ya ardhi kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kuongeza idadi ya Mabaraza yanayotoa huduma ambapo hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Mabaraza mapya **12** yameanza kutoa huduma na hivyo kuwa na jumla ya Mabaraza **92** yanayotoa huduma kati ya Mabaraza **139** yaliyoanzishwa na hivyo kuongeza wigo na idadi ya mashauri yaliyoshughulikiwa. Aidha, kuanzishwa kwa mabaraza hayo kumepunguza muda wa kusafiri na gharama kwa wananchi katika maeneo husika.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara ilipanga kushughulikia na kutoa maamuzi ya mashauri **33,250**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 mashauri **23,412** sawa na **asilimia 70** ya lengo yalitolewa maamuzi na mashauri **15,710** yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, katika mwaka 2023/24, Wizara inatarajia kufungua mabaraza mapya **47** na kushughulikia mashauri **33,250**. Katika kuhakikisha jukumu hilo linatekelezwa kikamilifu, ***napenda***

***kutoa rai kwa Mikoa na Wilaya kuendelea kutoa kipaumbele katika upatikanaji wa majengo kwa ajili ya kuanzisha mabaraza hayo.***




*Naibu Waziri wa Ardhi, Mhe. Geophrey Pinda akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wananchi mara baada ya kuzindua Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Mlele, Katavi.*

48. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kukamilisha ujenzi na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa kusimamia mashauri katika Mabaraza *(Intergrated Land cases management System)*. Mfumo huo utarahisisha utendaji kazi wa Mabaraza katika kutunza kumbukumbu za mashauri; kufungua mashauri mapya; kufuatilia mwenendo wa mashauri; utendaji kazi wa watumishi; na upatikanaji wa nakala za hukumu kwa njia ya mtandao. Wizara imekamilisha ujenzi wa mfumo huo ambao kwa sasa upo katika hatua za majaribio kabla ya kuanza kutumika rasmi.

49. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inatambua umuhimu wa kuongeza ufanisi katika kus-hughulikia migogoro ya ardhi nchini ili kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kujiletea maendeleo. Hivyo, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Serikali imeunda timu ya wataalamu ambayo inaendelea kufanyia kazi mapendekezo mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge na wadau muhimu kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi

na usimamizi wa vyombo na mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini.

**UTHAMINI WA MALI**

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma za uthamini kwa ajili ya madhumuni mbalimbali ikiwemo kuiwezesha Serikali na Taasisi nyingine katika ulipaji wa fidia, ukadiriaji tozo na kodi za Serikali, uhamisho wa milki, mizania ya hesabu, dhamana, rehani na mirathi. Katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kuratibu uandaaji na uidhinishaji wa taarifa za uthamini **54,000** ambazo kati ya hizo, uthamini wa kawaida **20,000** na taarifa za wafidiwa **34,000** na kushughulikia migogoro **30** ya uthamini wa fidia. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini **61,211** sawa na asilimia **113** ya lengo ambapo kati ya taarifa hizo, uthamini wa kawaida **21,272** na taarifa za wafidiwa **39,939.** Aidha, migogoro **20** ya fidia imepokelewa na kushughulikiwa.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** viwango vya thamani ya ardhi na mazao ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa mazoezi mbalimbali ya uthamini wa fidia na thamini nyingine kwa madhumuni mbalimbali. Kwa vipindi tofauti Wizara imekuwa ikihuisha jedwali la viwango vya thamani ya ardhi na mazao. Katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kuboresha kanzidata ya viwango vya thamani ya ardhí, mazao na kuhuisha viwango vya kodi ya ardhí nchini. Hatua hii ililenga kuhakikisha uthamini unafanyika kwa kuzingatia bei halisi ya soko na hivyo kuwezesha ulipaji wa fidia stahiki, kupunguza malalamiko kutoka kwa wananchi na kuiwezesha Serikali kupata kodi stahiki. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa viwango vya thamani ya ardhi na mazao vimehuishwa na vimeanza kutumika kuanzia mwezi Aprili, 2023. Wizara itahakikisha viwango hivi vinatumika kwa usahihi na kwa kuzingatia sheria na taratibu za uthamini ili kuhakikisha wananchi wanalipwa fidia stahiki inayoendana na bei ya soko.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara imeendelea kushiriki katika kuhakikisha azma ya Serikali ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati inafanikiwa. Katika kipindi tajwa, Wizara imeshiriki na kuratibu mazoezi mbalimbali ya uthamini kwa

ajili ya fidia kwa wananchi wanaopisha miradi mbalimbali ya Serikali pamoja na wananchi wanaopisha maeneo ya hifadhi ***(Jedwali Na.7)*. Natoa rai kwa maeneo ambayo uthamini umekamilika, kampuni zinazohusika zilipe fidia kwa wakati ili kuepuka usumbufu kwa wananchi. Kampuni hizo ni Mgodi wa Barrick North Mara Tarime, TANESCO na TRC katika Mradi wa Reli ya Kisasa, Kabanga Nickel-Ngara, Nyati Mineral Sands Ltd-Kigamboni na SOTTA Mining Corporation Ltd-Nyanzaga Sengerema.**



*Mthamini Mkuu wa Serikali (wa nne kulia) akikagua zoezi la uthamini wa Fidia kupisha Mgodi wa Kabanga Nickel, Ngara Kagera.*



*Wataalam katika zoezi la uthamini katika Mradi wa SGR Lot IV (kutoka Tabora kwenda Isaka)*

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara itaratibu na kusimamia uandaaji wa taarifa za uthamini **54,000,** kati ya hizo, uthamini wa kawaida **20,000** na uthamini wa fidia wenye wafidiwa **34,000**. Vilevile, Wizara itaendelea kushughulikia malalamiko yatokanayo na uthamini wa fidia, na kuendelea kuratibu utekelezaji wa mazoezi mbalimbali ya uthamini wa fidia katika miradi inayotekelezwa na Serikali.

**HUDUMA ZA TEHAMA**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutumia mifumo ya TEHAMA iliyopo katika kutunza kumbukumbu, kuzichakata na kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo utoaji hati za kieletroniki na ulipaji kodi ya pango la ardhi. Hata hivyo mifumo iliyopo haikidhi mahitaji ya sasa. Kutokana na umuhimu wa matumizi ya TEHAMA katika sekta ya Ardhi, *Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 katika Ibara ya 74(b) inaelekeza kuhusu kuweka Mfumo Unganishi wa Kielektroniki wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi katika mikoa na halmashauri zote nchini;* Hivyo, ili kufanikisha azma hiyo, katika mwaka 2022/23 Wizara inakamilisha maboresho ya Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System* – ILMIS) kwa kutumia watalaam wa ndani. Aidha, pamoja na maboresho yanayoendelea, mfumo huu umeendelea kutumika katika kutoa hati za kielektroniki katika Jiji la Dodoma na Mkoa wa Dar es Salaam ambapo hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 hati za kielektroniki **23,150** zimetolewa kupitia mfumo huo na kufanya hati zote za kielektroniki zilizotolewa kuwa **55,550.** Sambamba na uboreshaji na usimikaji wa mfumo wa ILMIS, Wizara itajenga uwezo kwa watumiaji wa mfumo katika ngazi ya Wizara, Mkoa na Halmashauri. Mafunzo yatahusisha matumizi ya mfumo, huduma kwa wateja pamoja na maadili katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA.



*Waziri wa Ardhi Mhe. Dkt Angeline Mabula akimkabidhi mmoja wa wananchi wa Kigamboni jijini Dar es Salaam Hatimiliki za kielektroniki.*

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya bajeti ya Mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kujenga, kusimika na kuimarisha miundombinu wezeshi ya TEHAMA kwa awamu katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri nchini na kukarabati mtandao kiambo katika ofisi za ardhi za halmashauri **47** zikiwemo makao makuu ya mikoa ya Iringa, Lindi, Mwanza na Mbeya. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara imekamilisha kujenga miundombinu wezeshi katika ofisi za ardhi za halmashauri za Wilaya ya Chalinze, Chamwino na Mkuranga. Vilevile, Wizara imekamilisha kujenga mtandao kiambo (*Local Area Network*) katika ofisi za ardhi za mikoa ya Iringa, Lindi, Mwanza na Mbeya na kuiunganisha na Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi (*National Land Information Centre*-NLIC). Aidha, Wizara inakamilisha usimikaji wa mtandao kiambo katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri **44**.



*Bi. Mwajuma Mohammed (kushoto)akipokea hati ya kielektroniki kutoka kwa Afisa Msajili Msaidizi wa hati Bi. Christina Sanga alipotembelea banda la Wizara wakati wa maonyesho ya Wiki ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.*

56. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/2024, Wizara inatarajia kusimika na kusambaza miundombinu ya mtandao kiambo katika ofisi za ardhi za mikoa **26** na halmashauri **132** na hivyo kuwezesha kukamilisha usambazaji wa mfumo wa ILMIS katika halmashauri zote nchini. Usimikaji wa miundombinu hiyo utawezesha matumizi ya mfumo wa ILMIS kwenye halmashauri hizo. Vilevile katika mwaka 2023/2024, Wizara itaanzisha wavuti ya wateja (*self-service portal*) ambapo mwananchi atapata huduma kupitia wavuti hiyo bila kulazimika kwenda ofisi za ardhi ili kupatiwa huduma na hivyo kupunguza gharama na muda wa kutafuta huduma. Hatua hii inatarajia kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za ardhi. Kupitia huduma hii, mwananchi atakuwa na uwezo wa kufuatilia kila hatua ya maombi kwa njia ya simu ama huduma ya mtandao.

**Ubadilishaji wa Michoro ya Mipangomiji, Ramani za Upimaji na Nyaraka za Umiliki kutoka Analogia kwenda Digitali**

57. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha kunakuwepo na taarifa sahihi za ardhi ambazo zitatumika katika Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi - ILMIS pamoja na kurahisisha muunganiko wa mifumo mingine, Wizara katika mwaka 2022/23, iliahidi kubadilisha taarifa za ardhi kutoka mfumo wa analogia kwenda kidigitali.

Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 michoro ya mipangomiji **30,812** yenye jumla ya viwanja **7,241,686** na ramani za upimaji **112,297** zenye jumla ya viwanja **2,385,114** zimebadilishwa katika mikoa yote **26**. Vilevile, nyaraka za Hati na majalada **524,131** yamebadilishwa kwa **asilimia 100** katika ofisi za ardhi za mikoa **15** ya Kagera, Geita, Rukwa, Katavi, Songwe, Tabora, Dodoma, Singida, Shinyanga, Mbeya, Njombe, Kigoma, Iringa, Simiyu na Manyara.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea na zoezi la ubadilishaji wa taarifa za ardhi kutoka mfumo wa analojia kwenda kidigitali kwa nyaraka za Hati na majalada **1,647,326** katika ofisi za ardhi za mikoa **11** ya Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Mtwara, Arusha, Pwani, Lindi, Mara, Morogoro, Ruvuma,Tanga na mamlaka za Serikali za Mitaa.

**UPANGAJI MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa majukumu ya Wizara ni kuratibu na kusimamia upangaji wa miji na uendelezaji makazi ambayo yanajumuisha utangazaji wa maeneo yaliyoiva kwa upangaji, uandaaji wa mipango ya jumla na Mipango kina, udhibiti wa uendelezaji miji na vijiji, urasimishaji makazi na uratibu wa uendelezaji nyumba. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Miradi na Programu mbalimbali za kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali.

Utangazaji wa Maeneo ya Upangaji Miji

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kutangaza maeneo ya vijiji yanayoiva na kuwa na sifa ya kupangwa na kuendelezwa kimji kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji Sura 355. Aidha, eneo lolote linaweza kutangazwa kuwa la upangaji maalum iwapo lina sifa za kipekee au muhimu za kiuchumi, kimaendeleo au kimazingira. Wizara hutangaza maeneo yenye sifa hizi baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwenye Mamlaka za Upangaji.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi

kuendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji kutambua, kupokea mapendekezo na kutangaza maeneo yaliyoiva kimji. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 jumla ya maeneo **228** yalipokelewa kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Kati ya hayo **90** yalikuwa ni maeneo mapya na **138** maeneo ya urasimishaji. Kati ya maeneo mapya **90,** maeneo **71** yametangazwa na **19** yako katika hatua za mwisho za kutangazwa. Kwa upande wa urasimishaji, maeneo **76** yametangazwa na **62** yapo katika hatua za mwisho za kutangazwa ***(Jedwali Na. 8 ).*** **Nazisisitiza Mamlaka za Upangaji kuendelea kuwasilisha mapendekezo ya maeneo yaliyoiva kimji ili yaweze kutangazwa kuwa maeneo ya upangaji.**

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha udhibiti wa ukuaji holela wa vijiji vinavyochipukia kuwa miji, Wizara imesambaza Mwongozo wa Upangaji na Ujenzi wa Nyumba Bora Vijijini ulioboreshwa kwa lugha ya picha kurahisisha utekelezaji wake katika vijiji. Mwongozo huo utasaidia kuongoza utengaji wa maeneo ya huduma za jamii na za kiuchumi katika vijiji na kuboresha upangaji wa vijiji na hatimaye kuwa na miji iliyopangika vizuri, endelevu na nyumba bora.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Halmashauri za vijiji pamoja na majukumu mengine zitakuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa Mwongozo na utungaji wa Sheria Ndogo za kulinda mipango na kuhakikisha zinazingatiwa. Ili kujenga uelewa wa mwongozo huo, Wizara imeanza kutoa elimu kwa umma kupitia viongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri katika mikoa ya Mbeya, Morogoro, Geita, Mwanza na Dodoma na kazi hiyo inaendelea katika mikoa mingine. Kazi ya kusambaza na kutoa elimu kuhusu mwongozo huo inatarajiwa kukamilika katika mwaka 2023/2024.

Uandaaji wa Mipango Kabambe

64. ***Mheshimiwa Spika,*** ukuaji na uendelezaji wa miji huongozwa na Mipango Kabambe inayoainisha matumizi mbalimbali ya ardhi katika miji nchini. Mipango hiyo ni dira ya utoaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi, kijamii pamoja na usalama wa miji na watu wake. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara katika mwaka

2022/23, iliahidi kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji katika uandaaji na utekelezaji wa Mipango Kabambe kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo na kwa kuzingatia *Ibara ya 74(a) ya Ilani ya CCM inayoelekeza kuhusu kusimamia na kuratibu uandaaji na ukamilishaji wa Mipango Kabambe (Master Plans) ya miji mbalimbali nchini.*




*Waziri wa Ardhi Mhe. Dkt Angeline Mabula akimkabidhi Nakala ya Mpango Kabambe Meya wa jiji la Mbeya Mstahiki Dourmohamed Issa alipokwenda kuuzindua rasmi.*

65. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi tarehe 15 Mei, 2023, Mpango Kabambe mmoja **(1)** wa Manispaa ya Moshi umekamilika na kuidhinishwa. Rasimu za Mipango Kabambe miwili **(2)** ya miji ya Mafinga na Bagamoyo ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji na Mipango Kabambe ya Manispaa ya Kahama na Mji wa Chalinze ipo katika hatua za awali za utayarishwaji. Aidha, katika kipindi hicho Wizara imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mipango katika Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya, na Manispaa za Morogoro, Lindi, Mtwara Mikindani na Songea. Ufuatiliaji huo ulibaini changamoto za utekelezaji kwa baadhi ya halmashauri kuandaa mipangokina na utoaji wa vibali vya ujenzi inayokinzana na Mipango Kabambe. Kufuatia changamoto hizo, Wizara imezielekeza halmashauri kuzingatia Mipango Kabambe iliyoandaliwa wakati wa usanifu wa mipangokina na utoaji wa vibali vya ujenzi.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea

kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Mipango Kabambe katika Halmashauri sita **(6)** za Majiji ya Tanga na Arusha, Manispaa ya Moshi na Miji ya Korogwe, Kibaha na Babati. Vilevile Wizara itafuatilia utayarishaji wa Mipango Kabambe minne **(4)** na kuratibu uandaaji wa Mipango kabambe sita **(6)** katika Halmashauri za miji ya Kasulu, Masasi, Bunda, Mbinga, Nzega na Mbozi. ***Natoa rai na kuzihimiza Mamlaka za Upangaji nchini kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji, utekelezaji na udhibiti uendelezaji miji ili kuwezesha miji yetu kusanifiwa na kuendelezwa kwa kuzingatia Mipango Kabambe.***

Uandaaji wa Mipangokina

67. ***Mheshimiwa Spika*** Wizara ina jukumu la kuratibu uandaaji wa mipangokina ambayo huandaliwa kwa lengo la kuelekeza ukuaji, uboreshaji wa makazi, hifadhi ya mazingira, kuondoa ukinzani wa matumizi ya ardhi na kutoa uhakika wa upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo ya uwekezaji na huduma za jamii.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara ilipanga kuidhinisha michoro ya mipangokina **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2023, michoro ya Mipangokina **2,827** yenye viwanja **393,978** sawa na asilimia **141** ya lengo imeidhinishwa. Katika mwaka 2023/24, Wizara inatarajia kuidhinisha mipangokina **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini.

Urasimishaji Makazi

69. ***Mheshimiwa Spika,*** *Ibara ya 74(d) ya Ilani ya CCM inaelekeza kuhusu kuimarisha utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kurasimisha Makazi katika mikoa 26 nchini ikiwa ni pamoja na kuwezesha ujenzi wa miji ya kisasa na kuandaa Mipango Kabambe sita (6) ya miji ya Mpanda, Njombe, Mirerani, Chato, Ifakara na Kahama;* Hivyo kwa kuzingatia maelekezo haya, Wizara inaendelea na utekelezaji wa Programu ya miaka kumi ya Kurasimisha Makazi na Kuzuia Makazi yasiyopangwa mijini (2013–

2023). Lengo la programu hii ni kuimarisha usalama wa milki na kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya miundombinu na huduma za kijamii kwa njia shirikishi. Kupitia Programu hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na Sekta Binafsi imeendelea kuboresha makazi ya wananchi wanaoishi katika maeneo yasiyopangwa. Katika mwaka 2022/23, Wizara ilipanga kurasimisha makazi **300,000**. Hadi tarehe 15 Mei, 2023, jumla ya makazi **190,768** sawa na asilimia **64** yamerasimishwa katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, idadi ya makazi yaliyopangwa katika maeneo ya urasimishaji tangu kuanza kwa utekelezaji wa Programu yamefikia vipande **2,389,179** katika mitaa **2,020** **(*Jedwali Na.* 9)**.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara itarasimisha vipande vya ardhi **500,000** pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Programu ya Kurasimisha Makazi na Kudhibiti Makazi Yasiyopangwa Mijini kwa lengo la kubaini mafanikio, changamoto zilizojitokeza na matarajio ya baadae. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na Sekta Binafsi itaendelea kufanya uhamasishaji kwa wananchi ambao bado makazi yao hayajarasimishwa ili kukamilisha zoezi hilo. **Nawasisitiza wananchi ambao makazi yao hayajarasimishwa kuhakikisha kuwa maeneo yao yanarasimishwa.**

Mabadiliko ya Matumizi ya Ardhi

71. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kumekuwepo na ongezeko kubwa la ukuaji wa miji na kusababisha hitaji kubwa la kubadilisha matumizi ya ardhi ili kukidhi mahitaji. Wizara imekuwa ikiidhinisha maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka katika Halmashauri mbalimbali nchini. Katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kuratibu uidhinishaji wa maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi ambapo hadi tarehe 15 Mei, 2023, jumla ya maombi **611** sawa na **asilimia 204** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi yaliidhinishwa. Ongezeko hilo linatokana na sababu mbalimbali ikiwemo ongezeko la shughuli za kiuchumi baada ya Serikali kuhamia Dodoma na miradi ya kimkakati.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa maelekezo kwa Ofisi za ardhi za Mikoa na Halmashauri kufanya ukaguzi ili kubainisha maeneo yote yaliyobadilishwa matumizi kinyume cha utaratibu na kuchukua hatua za kisheria kwa wahusika ikiwemo kutoza asilimia **2** ya thamani ya maendelezo yaliyofanyika kinyume cha utaratibu.

Usimamizi na Uratibu wa Sekta ya Nyumba

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kusimamia na kuratibu uendelezaji wa nyumba nchini. Uendelezaji wa nyumba hufanywa na watu binafsi, taasisi za umma na binafsi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma za uendelezaji nyumba nchini. Huduma hizo ni pamoja na upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, ubunifu wa nyumba za gharama nafuu na utoaji wa mikopo ya nyumba kwa watumishi wa Serikali.

Mikopo ya ujenzi wa nyumba

74. ***Mheshimiwa Spika,*** mikopo ya ujenzi wa nyumba ni muhimu katika kuwezesha upatikanaji wa makazi bora kwa wananchi kwa gharama nafuu. Katika mwaka 2022/23, Wizara ilipanga kuwezesha kuboreshwa kwa mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kupitia *Tanzania Mortgage Refinance Company (TMRC)*. Hadi tarehe 15 Mei, 2023, Serikali kupitia TMRC imewezesha taasisi za fedha **32** kutoa mikopo yenye riba nafuu kiasi cha shilingi **bilioni 26.34** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kutumia fursa za kupata mikopo ya ujenzi wa nyumba kutoka katika taasisi za fedha ambazo zinapokea fedha Serikalini kupitia TMRC.

Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu upatikanaji wa mikopo kwa watumishi inayotolewa kupitia Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa watumishi wa Serikali. Mfuko huo unalenga kuongeza upatikanaji wa makazi bora kwa watumishi wa Serikali.

Katika mwaka 2022/23, Wizara imeendelea kuratibu upatikaji wa mikopo kwa watumishi kulingana na taratibu zilizowekwa. Hadi tarehe 15 Mei, 2023 watumishi **49** waliokidhi vigezo wamepatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi **milioni 606.83** kati ya watumishi **99** waliotimiza masharti ya mkopo. Katika mwaka 2023/24, mfuko umepanga kukopesha watumishi **100.**

Ushirikiano na Taasisi za Kimataifa Katika Uendelezaji wa Makazi

76. ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imeendelea kuwa na ushirikiano na taasisi za kimataifa katika masuala ya makazi. Kwa muktadha huo, Wizara inaratibu ushirikiano huo na taasisi mbalimbali ikiwemo Shirika la Makazi Duniani (*UN-Habitat*) na Taasisi ya *Shelter Afrique*. Ushirikiano huo pamoja na kuongeza mahusiano ya kidiplomasia baina ya nchi yetu na nchi zingine duniani katika usimamizi na uendelezaji wa miji umekuwa ni jukwaa la kuelezea mafanikio ya nchi yetu katika kutekeleza Ajenda Mpya ya Miji na kupata uzoefu kutoka nchi nyingine.



*Waziri wa Ardhi Mhe. Dkt Angeline Mabula pamoja na Mawaziri wenzake na viongozi wa Shelter Afrique wakiwa katika picha ya pamoja na Makamu wa Rais wa Zimbabwe Mhe. Constantino Chiwenga (aliyekaa katikati) katika mkutano wa Shelter Afrique uliofanyika Victoria Falls Zimbabwe.*

77. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Wizara iliratibu na kushiriki katika maadhimisho ya Siku ya Makazi Duniani yaliyofanyika tarehe 03 Oktoba 2022 Jijini Dodoma. Pia, ilishiriki

katika mikutano mitatu (3) ya kimataifa ikiwemo Mkutano Mkuu wa **41** wa Makazi Barani Afrika uliofanyika *Victoria Falls* nchini Zimbabwe mwezi Julai 2022 ambao ulihusisha Mawaziri wenye dhamana ya makazi ulioandaliwa na Taasisi ya *Shelter Afrique*. Vilevile, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Kikanda uliohusu masuala ya Ajenda Mpya ya Miji Duniani uliohusisha Wakurugenzi wa Maendeleo ya Makazi kutoka nchi za SADC uliofanyika nchini Afrika ya Kusini mwezi Machi, 2023 na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa **42** wa Shirika la Makazi Afrika uliofanyika Jijini Abuja Mwezi Mei, 2023.



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi Bi. Lucy Kabyemera akiwa katika mkutano wa Shelter Afrique jijini Abuja Nigeria*

78. ***Mheshimiwa Spika***, manufaa ya jumla yaliyopatikana ni kuendelea kukua kwa mahusiano ya kidiplomasia na nchi nyingine, kupata uzoefu kutoka nchi nyingine kuhusu namna zinavyokabiliana na changamoto za makazi mijini hususan ujenzi holela. Manufaa mengine yaliyopatikana kwa upande wa *Shelter Afrique* ni Tanzania kupata mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa taasisi za umma na sekta binafsi zinazojishughulisha na uendelezaji milki. Katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu ushirikiano huu ili kuboresha mahusiano ya kimataifa na kulinda diplomasia ya nchi yetu na nchi zingine katika masuala yahusuyo Sekta ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Sensa ya Majengo ya Mwaka 2022

79. ***Mheshimiwa Spika,*** *Ibara ya 74(d) ya Ilani ya CCM inaelekeza Serikali kuanzisha kanzidata ya nyumba pamoja na kuimarisha mahusiano kati ya wamiliki wa nyumba na wapangaji nchini*, kwa kuzingatia matakwa hayo katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kushiriki katika zoezi la kitaifa la Sensa ya Watu na Makazi ambalo lilihusisha pia ukusanyaji wa taarifa za majengo nchini. Madhumuni ya zoezi hilo yalikuwa ni pamoja na kupata takwimu za majengo zitakazoiwezesha Serikali kufanya mapitio na kuboresha sera, sheria, kanuni, programu na mipango mbalimbali ya kitaifa na kimataifa pamoja na uboreshaji wa huduma za kijamii na matumizi bora ya ardhi. Aidha kupitia zoezi hilo, Wizara imeweza kupata taarifa ambazo zitaiwezesha kupata kanzidata ya majengo nchini.

80. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba zoezi hilo limefanyika kwa mafanikio makubwa. Hivyo nichukue fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ambao walifanya kazi kwa juhudi katika kuhakikisha kuwa Sensa ya Majengo inatekelezwa kama ilivyopangwa.

81. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kazi ya kuchakata taarifa zilizotokana na matokeo ya sensa ngazi ya Taifa imekamilika ambapo imebainishwa kuwa Tanzania Bara ina majengo **13,907,951** kati ya hayo majengo **4,132,438** sawa na asilimia **29.7** yapo mijini na majengo **9,775,513** sawa na asilimia **70.3** yapo vijijini. Kati ya majengo hayo, majengo **12,717,893** sawa na asilimia **91.4** ni ya makazi, majengo **470,476** sawa na asilimia **3.4** ni ya makazi na biashara na majengo **719,582** sawa na asilimia **5.2** ni majengo ya matumizi mengineyo.

82. ***Mheshimiwa Spika***, kati ya majengo yote, majengo ya kawaida ni **13,152,298** sawa na asilimia **94.4**, ya ghorofa ni **61,258** sawa na asilimia **0.4** na majengo **694,395** sawa na asilimia **5** ni majengo yaliyo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Matokeo haya yana mchango chanya katika kuiwezesha Wizara kupitia upya na kuboresha sera, miongozo na mikakati ya usimamizi wa ardhi na uendelezaji makazi mijini na vijijini kwani uwepo wa majengo

mengi yasiyo ya ghorofa unaashiria kuwa majengo mengi yanajengwa kwa mtawanyiko hivyo kusababisha athari katika utoaji wa huduma za msingi kama vile afya, elimu, barabara, maji, umeme na upatikanaji wa maeneo ya umma na kupunguza maeneo ya hifadhi za misitu, ardhi ya malisho na ardhi inayofaa kwa kilimo.

Usimamizi wa Milki Kuu

83. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ina jukumu la kusimamia uendelezaji wa milki kuu nchini. Usimamizi huo unahusisha pamoja na mambo mengine masuala ya majengo, mawakala wa milki/madalali, waendelezaji wa milki, taasisi binafsi za fedha zinazojishughulisha na uendelezaji milki pamoja na uratibu wa taasisi za uendelezaji wa milki za kitaifa na kimataifa.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara iliandaa kikao cha wadau wa sekta ya milki nchini kutoka taasisi za uendelezaji wa milki za kitaifa na kimataifa. Lengo la kikao hicho lilikuwa ni kufanya` tathmini ya hali ya sasa ya milki na kubainisha changamoto na kuweka mikakati ya pamoja ya uendelezaji wa sekta ya milki nchini. Kikao hiki kimefungua fursa na kuwezesha kampuni mbalimbali kuwasilisha maombi ya kuwekeza katika ujenzi wa makazi ya gharama nafuu kwa kutumia teknolojia mbalimbali. Hadi tarehe 15 Mei, 2023 kampuni mbalimbali za ndani na nje ya nchi zimeonyesha nia ya kuwekeza katika sekta ya milki.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uendelezaji Milki nchini imeendelea kukua kwa kasi na kuvutia uwekezaji mkubwa kwenye eneo la uwekezaji, soko la fedha (mitaji) na wadau wengine muhimu kwenye Sekta. Pamoja na kuendelea kukua kwa Sekta hiyo, zimekuwepo changamoto mbalimbali kati ya wamiliki wa nyumba na watumiaji wa nyumba (wapangaji au wanunuzi). Moja ya changamoto iliyobainishwa na wadau wa sekta ya milki ni usimamizi hafifu wa gharama za upangishaji, uboreshaji wa makazi, usimamizi wa nyumba kwa wamiliki na ukarabati wa majengo ya biashara na upangishaji nchini.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/24, Wizara inatarajia kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa wadau wote muhimu kwenye Sekta ya Milki kuhusu umuhimu wa kutumia kampuni na wataalam wenye ueledi kwenye eneo hilo kwa ajili ya kusimamia Sekta ya Milki ili kuwezesha wamiliki wa majengo nchini na wapangaji kuwa na utaratibu mahsusi wa kupata nyumba kwa matumizi mbalimbali. Aidha, utaratibu huu utaiwezesha Serikali kusimamia vizuri Sekta hii na kuboresha mazingira ya kufanya biashara katika Sekta ya Nyumba nchini. Aidha, Wizara itaratibu ukamilishaji wa rasimu za sheria ya maendeleo ya milki na kanuni zake na kuandaa kanzidata ya mawakala wa milki nchini.

**UPIMAJI ARDHI NA UANDAAJI RAMANI**

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu upimaji wa ardhi, upimaji wa mipaka ya kitaifa na kimataifa, kutafsiri matangazo ya Serikali ardhini kuhusu mipaka ya kiutawala, pamoja na uandaaji wa ramani kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Wizara pia inatoa miongozo ya upimaji na ramani kulingana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji.

Uwekaji Alama za Msingi za Upimaji Ardhi

88. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupunguza muda na gharama za upimaji ardhi nchini, Wizara imekuwa ikiongeza alama za msingi za upimaji zinazotumika pamoja na mambo mengine kurahisisha upimaji wa ardhi na urasimishaji. Katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kusimika alama mpya za msingi **100** katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 alama za msingi za upimaji **106** zilisimikwa katika mikoa ya Dodoma (**13**), Pwani (**27**), Iringa (**13**), Mbeya (**28**), Tanga (**9**), Manyara (**4**), Singida (**3**), Kagera (**3**), Geita (**2**) na Tabora (**4**) na hivyo kuwa na jumla ya alama za upimaji **1,041** nchini.



*Wataalam wakiweka alama za msingi za upimaji ardhi*

89. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika maeneo mengi nchini alama za msingi za upimaji zimewekwa katika umbali wa kilometa **40** kutoka alama moja kwenda nyingine. Hali hii husababisha kuongezeka kwa gharama za upimaji na muda mrefu wa upimaji. Ili kukabiliana na changamoto hii, Wizara imeendelea kusimika alama hizi ili kupunguza wastani wa umbali wa sasa hadi kufikia kilometa **20** kati ya alama moja na nyingine.

90. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Wizara itaanza hatua za awali kwa ajili ya ujenzi wa vituo **22** vya upimaji (Continuously Operating Reference Station- CORS) vinavyofanya kazi muda wote yaani mchana na usiku katika makao makuu ya mikoa **22 *(Jedwali Na. 10***) na pia itasimika alama mpya za msingi **267** katika Halmashauri **25** za mikoa **10 *(Jedwali Na. 11)***.

Upimaji wa Ardhi

91. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba unaofanywa na Mamlaka za Upangaji pamoja na sekta binafsi. Katika mwaka 2022/23, Wizara kwa kushirikiana na wadau zikiwemo mamlaka za upangaji ilipanga kuratibu upimaji na uidhinishaji wa ramani za viwanja na mashamba **500,000**. Hadi tarehe 15 Mei, 2023, viwanja

**314,977** na mashamba **2,564** yalipimwa na kuidhinishwa na kutunzwa kwenye kanzidata ya Wizara sawa na asilimia **63** ya lengo ***(Jedwali Na.12).*** Katika mwaka 2023/24, Wizara itasimamia upimaji na uidhinishwaji wa viwanja **500,000** na mashamba **500**.



*Wataalam wakiendelea na kazi ya upimaji wa mashamba wilayani Rungwe*

Tafsiri na Uhakiki wa Mipaka ya Kiutawala na Hifadhi

92. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kutafsiri Matangazo ya Serikali (GN) ya mipaka ya utawala na hifadhi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara za kisekta, na Mamlaka mbalimbali ili kutatua changamoto za mipaka. Tafsiri hizo zimewezesha kutatua migogoro ya mipaka baina ya vijiji, wilaya na mikoa na kati ya vijiji na hifadhi.



*Waziri wa Ardhi Mhe. Dkt Angeline Mabula (wa tatu kulia)*

*akikagua mipaka ya kiutawala na hifadhi wilayani Tarime mkoa wa Mara.Kulia kwake na Waziri wa OR-TAMISEMI na kushoto ni Naibu Waziri Maliasili na Utalii.*

93. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi tarehe 15 Mei, 2023, Matangazo ya Serikali (GN) sita (**6**) ambayo ni Tangazo moja (**1**) la Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na matangazo matano (**5**) ya mipaka ya Mapori ya akiba ya Kilombero, Pollolleti, Makere, Uvinza na Ruhuhu-Rutikila yametafsiriwa, kuhakikiwa na kubainishwa mipaka yake. Manufaa yanayotokana na tafsiri ya Matangazo ya Selikali na kubainishwa kwa mipaka ni kupata taarifa sahihi za uwandani kwa ajili ya matumizi ya Taasisi mbalimbali, kuondoa migogoro miongoni mwa makundi mbalimbali ya watumiaji wa ardhi pamoja na kuchochea shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**MAPITIO YA SERA NA SHERIA**

94. ***Mheshimiwa Spika,*** *Ibara ya 74(h) ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza kuhusu kufanya mapitio na kuhuisha sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya usimamizi na utawala wa ardhi*; katika kuhakikisha kwamba Sheria na Kanuni za Sekta ya Ardhi zinaboreshwa ili ziakisi mahitaji ya sasa, Wizara imeendelea kufanya marekebisho ya sheria na kanuni zinazosimamia utekelezaji wa shughuli za Sekta ya Ardhi.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia kutolewa kwa msamaha wa riba ya malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara imefanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2022 ili kuwezesha utoaji wa msamaha huo sambamba na kutunga Kanuni za utekelezaji wake. Lengo la msamaha huo ni kuwaondolea wananchi mzigo wa kulipa malimbikizo ya riba.

96. ***Mheshimiwa Spika***, Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 ilikuwa na mapungufu katika suala la uteuzi na nidhamu ya madalali wanaotekeleza hukumu na amri za Mabaraza. Sheria hiyo haikuweka utaratibu na sifa za kuweza kuwa dalali na udhibiti wa nidhamu hivyo, kusababisha baadhi ya

madalali kufanya udanganyifu katika kukamata na kuuza mali, kukwepa kulipa kodi na  tozo za Serikali na pia kuhifadhi fedha za mauzo katika akaunti binafsi. Kutokana na mapungufu hayo, Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments*)] Na. 3 ya mwaka 2021 iliweka sharti la kutungwa kwa Kanuni mpya za Uteuzi na Nidhamu ya Madalali wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

97. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka 2022/23, Wizara imetunga Kanuni za Uteuzi, Malipo na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka za mwaka 2023 ambazo zimeanza kutekelezwa baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na.**172** la tarehe 17 Machi, 2023. Kanuni hizo pamoja na masuala mengine zinalenga kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara na Mahakama ya Tanzania katika kusimamia nidhamu na maadili ya Madalali; kuweka masharti na sifa za kusajiliwa, kuweka utaratibu wa kudhibiti fedha za wadaawa na kuwezesha ulipaji wa ada na tozo za Serikali kutoka kwenye kampuni za udalali.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 na kuendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali za Sekta ya Ardhi kwa lengo la kuziboresha. Vilevile, Wizara itakamilisha taratibu za utungaji sheria mpya ya Chuo cha Ardhi pamoja na Sheria ya Upimaji Ardhi.

## MIRADI YA MAENDELEO

Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi

99. ***Mheshimiwa Spika,*** *Ibara ya 74(f) ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza pamoja na mambo mengine kuanzisha miradi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi.* Katika kutekeleza maelekezo haya, mwaka 2021/22 Serikali ilizikopesha Halmashauri **57**, Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa, Vyuo vitatu vya Ardhi vya Tabora, Morogoro na Chuo Kikuu cha Ardhi kiasi cha shilingi **bilioni 50** ambapo utekelezaji wake uliendelea mwaka

2022/23. Pia, katika mwaka 2022/23 Wizara ilipokea Kiasi cha shilingi **bilioni 10.6** kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, kazi zilizotekelezwa ni upimaji wa viwanja **116,499** na mashamba **401** sawa na asilimia **39** ya lengo la viwanja **300.** Upimaji huo unafanya jumla ya viwanja vilivyopimwa kupitia fedha za mkopo wa Shilingi **bilioni 50** kuwa viwanja **232,723.**



*Waziri wa Ardhi Mhe. Dkt Angeline Mabula akizungumza wakati kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii ilipotembelea mradi wa KKK Arumeru Arusha. Kushoto ni Naibu Waziri Mh. Geophrey Pinda.*

100. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha fedha zilizotolewa zinarejeshwa, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango imeendelea na uratibu na ufuatiliaji marejesho ya fedha hizo katika Halmashauri **57** na Taasisi zilizopatiwa fedha hizo. Kupitia ufuatiliaji huo, Halmashauri **48** zimerejesha jumla ya shilingi **bilioni 17.2** ambapo Halmashauri tisa (**9**) na Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa zimerejesha kwa asilimia **100**, Halmashauri **40** na vyuo vya Ardhi zimerejesha sehemu ya fedha na Halmashauri **8** hazijarejesha kabisa.



*Waziri wa Ardhi Mhe. Dkt Angeline Mabula akioneshwa eneo la mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi eneo la Mto Mkavu na Likong'o katika manispaa ya Lindi.*

101. ***Mheshimiwa Spika,*** nazipongeza Halmashauri za Jiji la Mwanza, Manispaa za Morogoro na Ilemela; Miji ya Tunduma na Bariadi; Halmashauri za Wilaya za Moshi, Meru, Geita, na Mbozi kwa kukamilisha marejesho ya fedha za mkopo. Hata hivyo, Halmashauri za Wilaya za Sumbawanga, Babati, Kishapu, Musoma, Mji wa Ifakara, Manispaa ya Shinyanga, Shinyanga DC na Chalinze DC hazijarejesha kabisa fedha za walizokopeshwa kutekeleza miradi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi (***Jedwali Na.13 A, B, C na D).*** Aidha **Natoa wito kwa Taasisi na Halmashauri ambazo hazijakamilisha marejesho kurejesha fedha hizo ndani ya muda uliowekwa na Serikali ili kuziwezesha Halmashauri nyingine kunufaika na fedha hizo kwa utaratibu endelevu.**

102. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi itaendelea kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi **300,000** kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji pamoja na Sekta Binafsi. Vilevile, itaendelea kupanga na kupima maeneo yanayozunguka miradi ya kimkakati (SGR, EACOP, JNHPP); na itaandaa mipangokina mitano (**5**) ya uendelezaji upya wa maeneo ya visiwa na fukwe

kwa ajili ya uwekezaji pamoja na maeneo chakavu (dilapidated areas) katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Arusha.

Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP)

103. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi unatekelezwa na Serikali kwa Mkopo toka Benki ya Dunia wa Dola za Kimarekani **milioni 150** sawa na shilingi za kitanzania **bilioni 345.** Utekelezaji wa mradi huu umeanza rasmi mwaka 2022/2023 na utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2022/23 – 2026/27). Mradi umelenga kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Ardhi nchini zikiwemo:

(i) Upungufu wa miundombinu ya upimaji uliopo katika sekta ambapo kwa kipindi kirefu zimesababisha kasi ndogo ya upangaji na upimaji wa ardhi katika maeneo ya mijini na vijijini. Mathalani, Wizara inahitaji angalau vituo **72** vya upimaji ambapo kwa sasa kuna vituo vitatu (**3**) nchi nzima ambavyo ni vichache ikilinganishwa na mahitaji.

(ii) Upungufu wa miundombinu ya mfumo wa kielektroniki unaoweza kukidhi mahitaji ya utoaji wa huduma za Ardhi; mathalani mfumo wa kielekroniki MOLIS V3 uliopo katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hauwezi kuunganisha kwa pamoja taarifa za kijiografia (taarifa za ramani na michoro ya mipango miji) na taarifa zisizo za kijiografia (nyaraka za umiliki wa ardhi). Hivyo kutokuwa na muunganiko huu kumesababisha huduma za ardhi kushindwa kutolewa kwa haraka na kwa gharama nafuu.

(iii) Uwepo wa makazi yasiyopangwa ambayo hayatambuliwi, yasiyowanufaisha wananchi kiuchumi na kukosa usalama wa miliki za ardhi mijini na vijijini.

(iv) Upungufu wa majengo ya ofisi za mikoa za ardhi kutokana na Wizara kupanua wigo wa utoaji huduma kutoka kwenye kanda kwenda kila mkoa.

(v) Kasi ndogo ya utoaji wa huduma kwa watumishi kwa kuzingatia teknolojia mpya zilizopo na upungufu wa vitendea kazi yakiwemo magari.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutatua changamoto hizi, Mradi utatekeleza yafuatayo:

i. Urasimishaji wa makazi yasiyopangwa katika mitaa **559**, uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya sita (**6**) na Vijiji **500,** kuandaa Mipangokina ya vitovu vya vijiji **250** na kuhakiki mipaka ya vijiji **500.** Matokeo ya urasimishaji na upangaji wa vijiji utawezesha Hati za Hakimiliki ya Kimila **500,000** kutolewa na Leseni za makazi na Hatimiliki **2,000,000** kutolewa kupitia urasimishaji wa makazi. Nyaraka hizi zitaweza kuwanufaisha na kuwasaidia wananchi kuwa na usalama wa miliki, kudhamini mikopo na huduma nyingine kutoka taasisi mbalimbali;

ii. Uboreshaji wa miundombinu ya usimamizi wa ardhi ambao utahusisha kujenga vituo vya upimaji **22** katika mikoa **22** na alama za upimaji **400** nchini. Vituo na alama hizo zitawezesha kuongeza ufanisi katika upimaji wa ardhi kwa kupunguza muda na gharama za upangaji na upimaji;

iii. Kujenga ofisi za ardhi za mikoa **25** na kukarabati ofisi za ardhi zilizopo katika majengo ya Halmashauri **41**;

iv. Usimikaji, usambazaji na ufungaji wa mfumo unganishi wa kielektroniki (ILMIS) kwenye mikoa **25** na Halmashauri **41** nchini;

v. Ubadilishaji wa majalada yote ya umiliki kutoka analogia kwenda digitali; na

vi. Utoaji wa vitendea kazi ikiwemo magari, na kuwajengea uwezo watumishi ili kuimarisha utendaji.

**Utekelezaji wa mradi katika mwaka 2022/23 na malengo ya mwaka 2023/24**

105. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara ilipanga kuanza kujenga majengo ya Ofisi za Ardhi za Mikoa **25**; kuboresha mfumo wa ILMIS; kutoa Hatimiliki **500,000** katika Halmashauri **23**; kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila **200,000** katika Vijiji **200** na kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **200** katika Wilaya sita (**6**) na kutoa Leseni za Makazi **250,000**. Katika utekelezaji wa kazi hizi, Wizara ilitarajia kutoa ajira za muda mfupi **2,300** na vibarua **4,200**.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, usanifu wa majengo ya ofisi za ardhi za mikoa **25** nchini umefanyika na zabuni imetangazwa na usimikaji wa alama za msingi za upimaji **67** umefanyika ili kuwezesha upimaji wa ardhi na utoaji wa Hatimiliki katika maeneo hayo.

107. ***Mheshimiwa Spika,*** majaribio ya namna bora ya kuongeza kasi ya zoezi la urasimishaji kwa lengo la kutoa hatimiliki yanafanyika katika Jiji la Dodoma katika mitaa mitatu (**3**) ya Bihawana kata ya Mbabala; Mapinduzi B kata ya Ng'ongh'ona; na Mkwawa kata ya Mpunguzi. Maeneo ya mitaa hiyo yametambuliwa na michoro ya mipangomiji imeandaliwa. Njia mbalimbali zinafanyiwa majaribio ambapo njia itakayoonesha ufanisi itatumika katika maeneo mengine ya mradi. Katika utekelezaji wa kazi za mradi ajira za muda mfupi **1,200** zilipatikana.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, uandaaji wa Mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya sita (**6**) za Chamwino, Longido, Maswa, Mbinga, Mufindi na Songwe imefikia **asilimia 90**. Aidha, Hati za Hakimiliki za Kimila **3,584** zimeandaliwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.

109. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi itapima mipaka ya vijiji **200,** kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na mipangokina ya vijiji **200**; itaandaa na kuidhinisha Hati za Hakimiliki za Kimila **200,000**; kukarabati ofisi za ardhi za Halmashauri **41**. Aidha, makazi

**500,000** yatarasimishwa katika Halmashauri **23**, Vituo **22** vya alama za upimaji vitaanza kujengwa na alama **276** za upimaji zitasimikwa. Vilevile, kumbukumbu za ardhi **1,647,330** zitabadilishwa kutoka analojia kwenda digitali; Mfumo Unganishi wa Kumbukumbu za ardhi (ILMIS) utasimikwa katika Halmashauri **132** na kujenga kumbi za mihadhara nne (**4**) katika Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro.

Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani (Land Data Infrastructure- LDI)

110. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Serikali iliahidi kuanza utekelezaji wa mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani wenye thamani ya dola za kimarekani milioni **65**. Lengo la mradi huu ni kuweka miundombinu ya upimaji na ramani ambayo itaongeza kasi ya upangaji, upimaji ardhi na uandaaji wa ramani kwa matumizi mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mkataba wa mkopo wa kutekeleza mradi ulisainiwa mwezi Novemba, 2022 kati ya Serikali ya Korea Kusini kupitia Benki ya EXIM ya nchini humo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maandalizi ya awali ya utekelezaji wa mradi yameanza kwa kutangaza zabuni ya kumpata Mshauri Mwelekezi (*Project Consultant*) atakayesimamia mradi huo. Utekelezaji wa mradi utaanza rasmi katika mwaka 2023/24.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na mradi wa LDI, Wizara inaanzisha kituo kitakacho tumika kuwajengea watumishi uwezo, maarifa, ubunifu na matumizi ya teknolojia mpya ya mifumo ya kumbukumbu za ardhi, na menejimenti ya taarifa za kijiografia kwa ujumla**.** Kituo hicho kitakuwa na jukumu la kutoa mafunzo mahsusi kwa wataalamu wa teknolojia ya mifumo ya kumbukumbu za ardhi na taarifa za kijiografia ili kukidhi mahitaji yaliyopo na yanayotarajiwa baadae. Kituo hicho kitaongeza uwezo wa wataalamu wetu kutekeleza miradi mikubwa ya ardhi na hivyo kuokoa matumizi makubwa ya fedha za kigeni zinazotumika kuajiri wakandarasi kutoka nje ya nchi.

Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa

112. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha mipaka ya kimataifa kwa kuongeza alama, kuzipima, kuboresha zilizoharibika, kuandaa ramani za mipaka na kuandaa mikataba ya mipaka. Katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kuendelea na uimarishaji wa mipaka ya nchi kavu yenye jumla ya urefu wa kilometa **210,** (Tanzania na Kenya kilometa **110** na Tanzania na Burundi kilomita **100)** kwa kushirikiana na Serikali za nchi hizo. Hadi tarehe 15 Mei, 2023, ukaguzi wa kipande cha mpaka kutoka Namanga hadi Tarakea chenye urefu wa kilomita **110** umekamilika na kazi ya uimarishaji wa mpaka uwandani inaendelea. Aidha, kipande cha mpaka chenye urefu wa kilomita **110** cha kutoka Ziwa Natroni hadi Namanga kimeimarishwa kwa kuongeza alama za mipaka zinazoonekana. Katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea na uimarishaji wa sehemu ya mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya yenye urefu wa kilomita **80** pamoja na mpaka wa Tanzania na Burundi wenye urefu wa kilomita **100.**




*Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Geofrey Pinda (wa nne kushoto) akiwa na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi Malisilia na Utalii walipotembelea mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la Namanga mkoani Arusha.*



*Muonekano wa mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la Motemorabu Tarime mkoa wa Mara*

Ushiriki wa Wizara katika Miradi ya Kimkakati Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta

113. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani jijini Tanga. Hadi tarehe 15 Mei, 2023, Wizara imekamilisha upimaji wa maeneo kwa ajili ya vituo saba vya kusukuma mafuta ghafi vilivyopo Kikagate (Muleba), Lubeho (Mbogwe), Nanga (Igunga), Misindo (Singida), Kimana (Kiteto), Sindeni (Handeni) na Chongoleani (Tanga) pamoja na kupima barabara (access roads) za kufika kwenye vituo hivyo zenye jumla ya kilomita **34.7**. Katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kushiriki katika kuwezesha utekelezaji wa miradi ya kimkakati kadri itakavyohitajika.

**Uandaaji wa Mpango Kabambe wa Jiji la Kibiashara na Uwekezaji la Kwala Mkoani Pwani**

114. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inatekeleza mpango wa Kuanzisha, Kupanga na Kuendeleza Jiji la Kibiashara na Uwekezaji katika eneo la Kwala, mkoani Pwani. Katika kufanikisha Mpango huo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine za Kisekta imeshiriki katika uandaaji wa Mpango Kabambe wa Jiji hilo.



*Muonekano wa eneo la Bandari Kavu Kwala mkoani Pwani*



*Eneo la Bandari Kavu Kwala mkoani Pwani*

115. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango Kabambe huo unahusisha eneo lenye ukubwa wa hekta **181,130** linalojumuisha vijiji **30** vya Halmashauri za Wilaya za Kibaha **(16),** Chalinze **(9)** na Kisarawe **(5)**. Uanzishwaji wa Jiji hilo unalenga kupata eneo kubwa zaidi la uwekezaji wa viwanda na shughuli nyingine za kiuchumi na pia kupunguza msongamano wa shughuli mbalimbali za kiuchumi katika Jiji la Dar es Salaam ikiwemo bandari ya Dar es Salaam. Kazi ya kuandaa Mpango huo inaendelea.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** *Ibara ya 74(a) ya Ilani CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 imeelekeza kupanga matumizi bora ya ardhi katika shoroba tatu ambazo ni ushoroba wa SGR, Bomba la Mafuta (EACOP) na Mradi wa uzalishaji wa Umeme wa Mwalimu Nyerere (JNHPP)*. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara kupitia Tume imeendelea kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwenye maeneo ya miradi hiyo. Kwa mwaka 2022/23, Wizara kupitia Tume ilipanga kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **75** katika maeneo yenye Miradi ya Kimkakati. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, jumla ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **75** katika Halmashauri za Wilaya sita (**6**) za Kilosa (**13**), Rufiji

(**20**), Mkalama (**4**), Kondoa (**6**), Bahi (**10)** na Ngorongoro (**22**) imeandaliwa. Aidha, katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Tume itaendelea kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi katika maeneo yenye Miradi ya Kimkakati.

**Shughuli za Uthamini katika Miradi ya Kimkakati**

117. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha azma ya Serikali ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati inafikiwa, Wizara imeendelea kushiriki katika kuratibu mazoezi mbalimbali ya uthamini kwa ajili ya fidia ya wananchi wanaopisha Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR). Katika mwaka 2022/23, Wizara imeratibu utekelezaji wa mazoezi ya uthamini wa mali za Wananchi wanaopisha mradi wa reli ya kisasa awamu ya tatu, nne na tano (SGR Lot III, IV & V) ***Jedwali Na. 14.***

**TAASISI NA BODI ZILIZO CHINI YA WIZARA**
**Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)**

118. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia shughuli za Shirika la Nyumba la Taifa ambalo lina jukumu la ujenzi wa majengo ya makazi, ofisi na biashara. Majukumu ya Shirika yanatekelezwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wake wa Miaka 10 (2015/16 – 2024/25) ambao unalenga kukamilisha miradi ya Shirika iliyo katika hatua mbalimbali; kufanya ukarabati wa majengo ya Shirika; kujenga majengo ya biashara na nyumba za gharama nafuu katika maeneo mbalimbali; kuendeleza Miji ya Pembezoni *(Satellite Towns);* na kutekeleza miradi ya ukandarasi.

Ujenzi wa Nyumba

119. ***Mheshimiwa Spika,*** *Ibara ya 75(i) ya Ilani ya CCM inaelekeza kuhusu kuboresha na kuimarisha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ili litekeleze miradi kwa tija na kujenga nyumba, majengo ya Serikali na majengo ya biashara kwa gharama nafuu katika maeneo mbalimbali nchini;* katika mwaka 2022/23, Shirika lilipanga kukamilisha miradi ya *Morocco Square, Kawe 711, Golden Premium Residence na PLOT 300 Regent Estate* iliyopo Jijini Dar es Salaam iliyokuwa imesimama tangu mwaka 2018 kutokana

na sababu mbalimbali ikiwemo ukosefu wa fedha. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iliruhusu Shirika kukopa shilingi **bilioni 173.9** ambapo hadi sasa Shirika limekopa shilingi **bilioni 44.7** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, mradi wa *Morocco Square* umekamilika kwa asilimia **100**; Miradi ya *Kawe 711 na Golden Premium Residence* mazungumzo kati ya Shirika na wakandarasi yanaendelea ili kazi iweze kuendelea na Mradi wa *PLOT 300 Regent Estate* haukutekelezwa kutokana na fedha iliyokuwa imetengwa kuhamishiwa katika mradi wa nyumba za gharama nafuu wa *Samia Housing Scheme* uliopo Kawe.



*Mradi wa Morocco Square uliopo kawe jijini Dar es Salaam unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)*

120. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na ukamilishaji wa miradi iliyokuwa imesimama kwa muda mrefu, Shirika pia liliahidi kukamilisha ujenzi wa nyumba **101** katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino na nyumba **303** katika Jiji la Dodoma eneo la Iyumbu kwa ajili ya kupangisha na kuuza ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa nyumba **1,000** Jijini Dodoma. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi tarehe 15 Mei, 2023, ujenzi wa nyumba **100** na jengo la maduka katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino umekamilika na ujenzi wa nyumba **300** na majengo matatu (**3**) ya huduma za kijamii katika Jiji la Dodoma (Iyumbu) umekamilika.



*Mradi wa ujenzi wa nyumba eneo la Chamwino Dodoma*

**Mradi wa ujenzi wa nyumba unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)**

121. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na utekelezaji wa miradi ya nyumba za gharama ya kati, Shirika lilibuni mradi wa nyumba **5000** za gharama nafuu wa *Samia Housing Scheme* zitakazojengwa kwa awamu katika mikoa mbalimbali nchini kwa gharama ya shilingi **bilioni 466.** Kwa kuanzia, Shirika lilianzisha ujenzi wa nyumba **560** Kawe Jijini Dar es Salaam. Aidha, utekelezaji umefikia asilimia **15** na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2023/2024.

122. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Shirika lilipanga kuendelea na utekelezaji wa miradi ya biashara katika maeneo mbalimbali ya Bukoba, Mwanza, Dodoma, Kahama, Morogoro, Masasi na Lindi. Hadi tarehe 15 Mei, 2023, ujenzi wa majengo ya biashara katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama umeanza na mradi wa maduka Jijini Mwanza umekamilika.

Miradi ya Ukandarasi

123. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23, Shirika limeendelea na utekelezaji wa miradi ya ukandarasi ikiwemo ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara nane (**8**) Jijini Dodoma katika Mji wa Serikali Mtumba. Wizara zinazohusika ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Nishati; Madini; Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mifugo na Uvuvi; Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Utamaduni Sanaa na Michezo na Mambo ya Ndani ya Nchi ambapo miradi hiyo imefikia wastani wa asilimia

**60**. Aidha, ujenzi wa Jengo la Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unaendelea na umefikia asilimia **56** na upanuzi wa jengo la Kitengo cha Moyo cha Jakaya Kikwete (JKCI) umefikia wastani wa asilimia **67.**



*Utekelezaji wa miradi ya ukandarasi katika eneo la Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma*

124. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika pia linatekeleza miradi minne (**4**) ya ukandarasi wa ujenzi wa Ofisi za Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) katika Mikoa ya Pwani, Dodoma, Simiyu na Songwe yenye thamani ya shilingi **bilioni 2.8** ambayo imefikia wastani wa **asilimia 95.** Aidha, Shirika linatekeleza mradi wa Serikali wa ujenzi wa jengo la Kituo cha Biashara Tanzanite (*Tanzanite Trade Center)* katika mji wa Mirerani Wilaya ya Simanjiro Mkoa wa Manyara ambao utagharimu shilingi **bilioni 5.49.** Mradi huu ulianza kutekelezwa Mei, 2022 na umefikia **asilimia 70**. Vilevile, Shirika linatekeleza mradi wa ujenzi wa jengo moja la wagonjwa wa nje (OPD) katika Hospitali ya Ligula mkoani Mtwara. Ujenzi huo ulianza mwezi Aprili, 2022 na utakamilika mwezi Juni, 2023 kwa gharama yashilingi **bilioni 2.7.**

Usanifu na Usimamizi wa Miradi ya ujenzi

125. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika linaendelea na usimamizi wa miradi mbalimbali ya kimkakati ya Serikali ikiwemo ile ya ujenzi wa majengo **8** ya Ofisi katika mji wa Serikali eneo la Mtumba, Usanifu na Usimamizi wa soko la Kariakoo na jengo la Ofisi ya Wizara ya Fedha na Mipango awamu ya pili eneo la Mtumba umekamilika

na ujenzi unaendelea. Aidha, Usimamizi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira Awamu ya Pili ujenzi umefikia **asilimia 60** na usanifu wa jengo la Kituo cha Biashara Tanzanite (*Tanzanite Trade Center)* eneo la Mirerani Manyara umefikia **asilimia 85**.

### Utekelezaji wa Sera ya Ubia ya Shirika

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika lilizindua sera yake ya ubia iliyoboreshwa, tarehe 16 Novemba, 2022. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, miradi **24** ya ubia yenye thamani ya Shilingi **bilioni 340** imepitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika. Hatua inayoendelea ni uandaaji wa mikataba ya ubia, upitishwaji wa mikataba husika na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na utiaji saini wa mikataba hiyo ili kuanza ujenzi.

### Ukusanyaji wa Mapato

127. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Shirika lilipanga kukusanya shilingi **bilioni 268.03** kutokana na vyanzo mbalimbali ikiwemo shilingi **bilioni 97.5** za kodi ya pango na shilingi **bilioni 170.53** kutoka katika vyanzo vingine. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Shirika limekusanya jumla ya shilingi **bilioni 190** sawa na asilimia **71** ya lengo la kukusanya **bilioni 268.03**. Kati ya hizo, **bilioni 103** ni makusanyo ya kodi ya pango na **bilioni 87** ni mapato yanayotokana na mauzo ya nyumba na miradi ya ukandarasi. Ukusanyaji wa mapato ya Shirika unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo wadaiwa sugu wa kodi ya pango kutokulipa kodi kwa wakati na wanunuzi wa nyumba kutokukamilisha malipo yao kwa wakati. **Natoa rai kwa wadaiwa wote kulipa madeni yao kwa wakati ili kuliwezesha Shirika kuendelea kutoa huduma bora kwa watanzania wengine.**

### Ukarabati wa Nyumba

128. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na utekelezaji wa miradi ya ujenzi, Shirika limeendelea kuboresha nyumba zake kwa kuzifanyia ukarabati katika mikoa mbalimbali nchini. Katika mwaka 2022/23, Shirika lilitenga shilingi **bilioni 8** kwa ajili ya ukarabati wa majengo **200** yenye nyumba **2,000** katika mikoa ya Kilimanjaro, Shinyanga,

Arusha, Mwanza, Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam na Katavi. Hadi tarehe 15 Mei, 2023, shilingi **bilioni 6** zimetumika kukarabati majengo **153** yenye nyumba **1,500.**

129. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Shirika limepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

(i) Kukamilisha miradi mikubwa iliyosimama ya Kawe 711 na Golden Premier Residence Jijini Dar es Salaam;

(ii) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Samia Housing Scheme (SHS) wa ujenzi wa nyumba **560** katika eneo la Kawe;

(iii) Kuendelea na ujenzi wa nyumba **500** katika Jiji la Dodoma maeneo ya Ndejengwa, Iyumbu na Medeli;

(iv) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya biashara katika miji mbalimbali ikiwemo Bukoba, Tabora, Dodoma, Iringa, Kahama, Morogoro, Masasi na Lindi;

(v) Kuendelea kutekeleza Sera ya Ubia kwa kuishirikisha Sekta Binafsi katika uwekezaji na uendelezaji wa majengo ya biashara na makazi;

(vi) Kuendelea kutekeleza Mpango wa miaka mitano wa ukarabati wa nyumba za Shirika (2022-2027);

(vii) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya ukandarasi ikiwemo ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Wizara nane (**8**) Jijini Dodoma, ujenzi wa Jengo la Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ujenzi wa majengo manne (4) ya Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA), ujenzi wa jengo la Kituo cha Biashara ya Madini ya TANZANITE Mirerani na ujenzi wa Jengo la Kitengo cha Moyo cha Jakaya Kikwete (JKCI);

(viii) Kukarabati majengo **250** yenye takribani nyumba **2,500** katika mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Tabora, Arusha,

Kigoma, Morogoro, Lindi, Tanga, Mbeya, Mwanza, Singida na Kagera; na

(ix) Kutekeleza miradi mingine itakayojitokeza.

Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

130. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu ina jukumu la kusimamia shughuli za Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Tume hii ina jukumu la kuandaa, kuratibu, kuwezesha na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini ikiwemo pia kufanya tafiti. Utekelezaji wa majukumu hayo unazingatia Sheria ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi, Sura Na.116, Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Taifa (2013-2033) na Mpango Mkakati wa Tume (2021/22-2025/26).

131. ***Mheshimiwa Spika,*** mipango ya matumizi ya ardhi huwezesha utengaji wa maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo makazi, kilimo, nyanda za malisho, hifadhi ya misitu, miundombinu, huduma za jamii, mapitio ya wanyamapori na ardhi ya akiba kwa ajili ya uwekezaji na ukuaji wa Miji na Vijiji. Mipango hii pia huwezesha utatuzi wa migogoro ya ardhi, utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila, kulinda ikolojia, mazingira, mabadiliko ya Tabianchi na kuchangia kuboresha uzalishaji wenye tija katika kukuza pato la wananchi na Taifa kwa ujumla.

Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi

132. ***Mheshimiwa Spika,*** *Ibara ya 74(b) ya Ilani ya CCM inaelekeza kuhusu kupanga matumizi bora ya ardhi katika wilaya 54 zenye miradi ya kimkakati pamoja na vijiji 4,131 vilivyopo katika maeneo ya mipakani mwa nchi;* katika mwaka 2022/23, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilipanga kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya nne **(4)** na vijiji **200** katika Halmashauri mbalimbali nchini. Mipango hii huandaliwa kwa njia shirikishi na kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na wadau wa kimkakati.



*Waziri wa Ardhi Mhe. Dkt Angeline Mabula akimkabidhi mwananchi wa Serengeti mkoa wa Mara kitabu cha Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi.*

133. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imewezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Halmashauri za Wilaya tatu **(3)** za Nsimbo (Katavi), Ngorongoro (Arusha) na Kigoma (Kigoma). Aidha, jumla ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **306** sawa na **153%** ya lengo, imeandaliwa katika Halmashauri za Wilaya **31** nchini *(**Jedwali Na. 15**)*. Mipango hii inafanya kuwa na jumla ya vijiji **2,860** vyenye mipango ya matumizi ya ardhi kati ya vijiji **12,318** vilivyopo nchini.



*Wananchi wa Kijiji cha Oloipiri kilichopo Wilaya ya Ngorongoro Mkoani Arusha wakiwa kwenye Mkutano Mkuu wa kijiji kwa ajili ya kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya kijiji chao.*

134. ***Mheshimiwa Spika,*** mipango ya matumizi ya Ardhi iliyoandaliwa imewezesha utengaji wa maeneo ya matumizi ya

ardhi katika Vijiji na Halmashauri za Wilaya mbalimbali nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, maeneo yenye ukubwa wa hekta **231,321** yametengwa kwa ajili ya malisho, hekta **199,110** hifadhi za misitu, hekta **23,215** misitu ya uvunaji, hekta **61,135** makazi, hekta **199,591** kilimo na makazi, hekta **312,842** kilimo, hekta **49,059** uwekezaji, hekta **7,681** huduma za jamii, hekta **7,569** miundombinu, hekta **72,574** hifadhi ya vyanzo vya maji, hekta **11,378** ardhi ya jumla, hekta **2,572** ardhi ya akiba na matumizi mengine ni hekta **152,582 *(Jedwali Na.16).***

135. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi itaendelea kuandaa, kuwezesha, kuratibu na kusimamia mipango ya matumizi ya Ardhi ya Wilaya tano (**5**) na vijiji **410** ambapo mipango ya Wilaya tano (**5**) na vijiji **210** itaandaliwa kupitia fedha za ndani za maendeleo na mipango ya vijiji **200** itaandaliwa kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP). Pamoja na jitihada za Wizara kupitia Tume katika utekelezaji wa jukumu hili ***natoa rai kwa Halmashauri za Wilaya zote nchini kutoa kipaumbele katika kutenga Fedha za uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi.***

Uandaaji wa Mipangokina ya Vitovu vya Vijiji na mashamba

136. ***Mheshimiwa Spika,*** *Ibara ya 74(c) ya Ilani ya CCM inaelekeza kuhusu kuandaa mipango kina ya matumizi ya ardhi ili kutekeleza usimamizi wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya kilimo, makazi na malisho katika vijiji 874*. Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeendelea kuwezesha uandaaji wa Mipangokina ya maeneo yaliyotengwa katika Vijiji mbalimbali nchini. Kwa mwaka 2022/23, jumla ya mipangokina **14** ya vitovu vya vijiji na mashamba imeandaliwa katika Halmashauri za Wilaya mbalimbali nchini. Mipangokina hiyo imewezesha uwekaji wa miundombinu na huduma za jamii, utoaji wa Hati za hakimilki za kimila **7,515** katika vijiji nane **(8)** vya Halmashauri za Wilaya za Nzega (Buduba na Seki), Kondoa (Haubi na Mafai), Mkalama (Munguli), Handeni (Msomera) na Chalinze katika vijiji vya Pongwe Mnazi na Pongwe Kiona **(Jedwali Na.17).**

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi itaendelea kuwezesha uandaaji wa mipangokina katika maeneo yanayotengwa kwa matumizi mbalimbali ili kuwezesha uboreshaji wa huduma za jamii na miundombinu, makazi, uzalishaji na utoaji wa Hati za Hakimilki za Kimila na hivyo kuwezesha miliki salama kwa wananchi nchini.

Uwezeshaji wa Mamlaka za Upangaji

138. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, imeendelea kuziwezesha Mamlaka za Upangaji kwa kutoa mafunzo kwa timu shirikishi za upangaji katika Halmashauri za Wilaya na Vijiji pamoja na elimu kwa umma. Elimu inayotolewa inahusu Sheria za Ardhi, Miongozo na Taratibu za uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi, usuluhishi wa migogoro, uhifadhi wa mazingira, wanyamapori, vyanzo vya maji na uzingatiaji wa mipango na mabadiliko ya tabianchi.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilizijengea uwezo Mamlaka za Upangaji katika uandaaji na usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa wajumbe **248** katika Halmashauri za Wilaya **31;** Wajumbe **6,120** wa Halmashauri za Vijiji **306**; Wajumbe **2,448** wa Kamati za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi za Vijiji **306;** na Wajumbe **2,142** wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji **306**.



*Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Usimamizi ya Mipango ya Matumizi ya kijiji cha Lumage Wilayani Makete wakihakiki mipaka ya kijiji chao na kuandaa ramani ya msingi kupitia picha ya anga (satellite image)*

140. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Mipango ya Matumizi ya Ardhi kupitia njia mbalimbali ikiwemo vipindi **28** vya Runinga, Makala, Tovuti na mitandao ya kijamii. Aidha, Tume iliendesha mikutano mbalimbali uwandani yenye lengo la kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi na sheria mbali mbali. Katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Tume itaendelea kuziwezesha Mamlaka za Upangaji na kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria za Ardhi, miongozo na taratibu za upangaji, usimamizi na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini.

Uhuishaji wa Mipaka ya Vijiji

141. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, imewezesha uhuishaji wa mipaka ya kiutawala ya vijiji **98** vilivyopo katika Wilaya **14** za Meatu **(12),** Ngorongoro **(36),** Kilosa **(8),** Sumbawanga **(4),** Kondoa **(2),** Wanging'ombe **(2),** Iringa **(2),** Tanganyika **(2)**, Mpimbwe **(3),** Bahi **(4),** Rufiji **(8),** Mkalama **(2)**, Itilima **(10)** na Busega **(3**) (***Jedwali Na. 18****)*. Vilevile, Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **34** vimetolewa katika Halmashauri za Wilaya mbili **(2)** za Handeni (**1)** na Ngorongoro (**33**). Katika mwaka 2023/24, Tume itaendelea kuwezesha uhuishaji wa mipaka ya vijiji vilivyogawanyika kutoka kwenye vijiji mama, kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kutoa vyeti vya ardhi ya kijiji na kuimarisha mipaka ya kiutawala.

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Katika Vijiji

142. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeendelea kutatua migogoro ya kiutawala ya ardhi katika vijiji mbalimbali nchini. Migogoro hii kwa kiasi kikubwa inatokana na uelewa mdogo wa mipaka ya kiutawala, ushindani katika utumiaji wa rasilimali ardhi, uanzishwaji wa vijiji vipya ndani ya vijiji mama, uvamizi wa maeneo ya hifadhi na muingiliano wa matumizi ya ardhi kinzani. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Tume imewezesha utatuzi wa migogoro ya ardhi ya vijiji **75** vilivyopo katika Wilaya za

Ngorongoro (**23**), Kilosa (**8**), Sumbawanga (**4**), Kondoa (**4**), Mufindi (**2**), Tanganyika (**2**), Bahi (**3**) Rufiji (**8**), Mpimbwe (**3**) na Mkalama (**2**), Meatu (**11**), Itilima (**2**) na Busega (**3**). ***(Jedwali Na. 18).***



*Wajumbe wa Halmashauri ya Vijiji vya Darajani na Msagali wakifukia jiwe la mpaka (Beacon) mara baada ya kutatua mgogoro wa mpaka wa vijiji vyao wakati wa zoezi la uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji hivyo.*

**Utafiti**

143. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeendelea kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ardhi na upangaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Katika mwaka 2022/23, Tume ilipanga kufanya tafiti mbili (**2**) zinazohusiana na usimamizi na uzingatiaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika Halmashauri mbalimbali nchini. Tafiti hizi husaidia kujenga uelewa kwa wadau na kuhuisha Sheria na Miongozo mbalimbali ndani ya Sekta ya Ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Tume imefanya utafiti unaohusu usimamizi na changamoto zinazokabili uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Utafiti huo umefanyika katika vijiji **24** vilivyopo katika Halmashauri za Wilaya tatu (**3**) za Chamwino, Rufiji na Mbarali, ambapo kati ya hivyo, vijiji **12** Mipango ya Matumizi ya Ardhi imekwisha muda wake na vijiji **12** Mipango yake inaendelea kutekelezwa.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa mabadiliko ya uongozi katika vijiji na kukosekana kwa mfumo rasmi wa makabidhiano ya uongozi kuwa ni chanzo cha athari hasi katika usimamizi na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya vijiji. Aidha, utunzaji hafifu wa kumbukumbu

na kukosekana kwa ramani za Mipango katika Ofisi za halmashauri za Vijiji umebainika kuathiri usimamizi wa Mipango hii wakati wa mabadiliko ya uongozi. Vilevile, Mamlaka za Upangaji kutotenga fedha kwa ajili ya kuendelea kutoa elimu ya usimamizi na utawala wa ardhi baada ya kuandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi imebainika kusababisha changamoto ya utekelezaji na usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini. Katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Tume itafanya tafiti mbili (**2**) zinazohusu matumizi ya ardhi na Maendeleo ya Vijiji katika Halmashauri mbalimbali nchini na kusambaza matokeo kwa wadau.

Uimarishaji wa mfumo wa Taarifa na utunzaji wa kumbukumbu za Mipango ya Matumizi ya Ardhi

145. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeendelea kuboresha na kusimamia Mfumo wa Taarifa na Utunzaji wa Kumbukumbu za Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUIS). Mfumo huu unawezesha kuhifadhi kumbukumbu za Mipango ya Matumizi ya Ardhi katika ngazi ya Taifa, Kanda, Mkoa, Wilaya na Vijiji. Vilevile, mfumo unawezesha kufanya ufuatiliaji, tathmini, utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila na upatikanaji wa taarifa za Mipango ya matumizi ya ardhi kwa urahisi.

146. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2022/23, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilipanga kuhifadhi Mipango ya Matumizi ya Ardhi **800** pamoja na kuendelea kuboresha mfumo huu. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, jumla ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **656** imehifadhiwa kwenye mfumo. Aidha, maboresho ya mfumo yanaendelea ili kuwezesha uandaaji na uhifadhi wa taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi mbalimbali za upangaji. Katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Tume itaendelea kuhifadhi katika mfumo taarifa za Mipango ya Matumizi ya ardhi ya Vijiji **810** na Wilaya **10**.

Bodi za Wataalam

147. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pamoja na majukumu mengine ina jukumu la kusimamia taasisi zilizo chini ya Wizara zikiwemo Bodi

za Wataalam wa Sekta ya Ardhi. Bodi hizo ni Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Usajili wa Wathamini na Baraza la Taifa la Wapima Ardhi. Majukumu ya Bodi hizi yanajumuisha kusajili wataalam wa sekta na kampuni za kitaalam, kusimamia weledi na maadili ya kitaaluma.

Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji

148. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, wataalam **25** na kampuni sita (**6**) za Mipangomiji zimesajiliwa, hivyo kuwa na jumla ya wataalam **472** na kampuni **91** zilizosajiliwa. Bodi imefanya ufuatiliaji wa utendaji kazi na uzingatiaji Sheria za Mipangomiji katika Mikoa ya Mbeya, Manyara, Tabora, Simiyu na Mara, na kufanya ukaguzi wa jumla ya michoro ya mipangomiji **620** pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam katika Ofisi za Ardhi za Mikoa hiyo. Katika mwaka 2023/24, Bodi itaendelea kusajili wataalam na kampuni za mipangomiji zitakazokidhi vigezo ili kuimarisha utendaji kazi. Aidha, usimamizi na ufuatiliaji wa utendaji kazi na uzingatiaji wa sheria za mipangomiji utaendelea kufanyika ili kuimarisha ustawi wa sekta ya mipangomiji.




*Waziri wa Ardhi Mhe. Dkt Angeline Mabula akifungua Mkutano Mkuu wa mwaka wa Wataalam wa Mipangomiji jijini Dodoma.*

Bodi ya Usajili wa Wathamini

149. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/23, Bodi ya Usajili wa Wathamini imesajili wathamini wa ngazi ya kudumu **53**, ngazi ya awali **41**, Wathamini Wasaidizi **29**, Kampuni za Uthamini **11** na

hivyo kufanya Wathamini wa ngazi ya kudumu kufikia **291**, Wathamini wa ngazi ya awali **704**, Wathamini Wasaidizi **86** na Kampuni za Uthamini **63**.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imefanya ukaguzi wa kampuni tano (**5**) ambapo baada ya ukaguzi huo kampuni mbili (**2**) zimetozwa faini na kampuni moja (**1**) imepewa onyo kutokana na kukiuka maadili ya kitaaluma. Vilevile, ukaguzi umefanyika kwa Wathamini ambapo baada ya ukaguzi huo, imesitisha leseni ya mthamini mmoja (**1**) kwa muda wa miezi sita (**6**) na kumuweka chini ya uangalizi maalum wa miaka mitatu (**3**) mthamini mmoja (**1**) kutokana na kukiuka maadili ya kitaaluma. Aidha, Bodi imeendesha semina ya mafunzo kwa wathamini na mafunzo ya usajili wa kudumu kwa Wathamini wa ngazi ya awali **117**. Katika mwaka 2023/24, Bodi itaendelea kusimamia shughuli za uthamini sambamba na kampuni zilizosajiliwa kwa kazi hiyo.

Baraza la Taifa la Wapima Ardhi

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Taifa la Wapima Ardhi linasimamia taaluma ya Upimaji Ardhi nchini. Katika mwaka 2022/23, Baraza lilitoa usajili kwa Wapima Ardhi **33** kati ya **63** walioomba na hivyo kufanya jumla ya wapima waliosajiliwa kuwa **719**. Aidha, Baraza lilitoa Leseni za upimaji ardhi kwa Kampuni za Upimaji Ardhi **20** na kufanya Kampuni zenye Leseni za Upimaji Ardhi kuwa **95**.

Vyuo vya Ardhi Morogoro na Tabora

152. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia mafunzo ya taaluma za Sekta ya Ardhi ngazi ya kati katika vyuo vya Ardhi Morogoro (ARIMO) na Tabora (ARITA). Vyuo hivyo vinafundisha fani za Mipangomiji, Upimaji ardhi, urasimu ramani, ubunifu na uchapishaji, usimamizi wa ardhi, uthamini na usajili. Katika Mwaka 2022/2023, Wizara kupitia vyuo hivyo iliahidi kudahili wanafunzi **2,300** (ARITA **1,600** na ARIMO **700**). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa jumla ya wanafunzi **2,045** walidahiliwa ambapo Chuo cha Ardhi Tabora kilidahili wanafunzi **1,361** kati ya hao wanaume ni **785** na wanawake **576** na Chuo cha Ardhi Morogoro kilidahili

wanafunzi **495** ambapo **331** ni wanaume na **164** ni wanawake. Katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia vyuo hivyo itadahili wanafunzi **2,045** (ARITA **1,580** na ARIMO **495**).



*Naibu Waziri wa Ardhi Mhe. Geofrey Pinda akijaribu ufanisi wa kifaa cha kupimia wakati wa mahafali ya Chuo cha Ardhi Morogoro*




*Waziri wa Ardhi Mhe. Dkt Angeline Mabula akiweka jiwe la msingi wakati akizindua jengo la madarasa katika Chuo cha Ardhi Tabora.*

**MASUALA MTAMBUKA**

Ushirikiano baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar

153. ***Mheshimiwa Spika,*** kama ambavyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza mara kwa mara umuhimu wa kuboresha ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Tanzania Bara na Wizara ya

Ardhi na Maendeleo ya Maakazi Zanzibar zimekuwa zikitekeleza maelekezo hayo ili kuimarisha Muungano na kuleta manufaa yenye tija kwa wananchi wa pande zote za Muungano na Taifa letu kwa ujumla.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maelekezo ya Mhe. Rais kwa vitendo, wizara hizi mbili zimeingia makubaliano ya maeneo ya ushirikiano ambayo ni kukusanya, kuchakata na kubadilishana taarifa za ardhi baharini; kubadilishana uzoefu kwenye maendeleo na matumizi ya mifumo ya habari na teknolojia kwa sekta ya ardhi; kushirikiana kitaalamu na kubadilishana uzoefu katika kuendeleza mfumo wa usimamizi na maendeleo ya sekta ya milki kuu ambayo inajumuisha makazi na nyumba; kuweka utaratibu wa mafunzo, kubadilishana uzoefu, ujuzi na utendaji mzuri ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha wafanyakazi/kubadilishana wataalam wa sekta ya ardhi; kubadilishana uzoefu katika kuandaa na kutekeleza Sera, Sheria na miongozo mbalimbali ya Sekta ya Ardhi; kushirikiana na kubadilishana uzoefu katika utafiti na maendeleo katika sekta ya ardhi; kushirikiana katika utekelezaji wa miradi ya pamoja kwa madhumuni ya kujenga uwezo; kushirikiana na kubadilishana uzoefu juu ya utatuzi wa migogoro ya ardhi; kushirikiana na kubadilishana uzoefu katika usimamizi na maendeleo ya miji mikongwe; na kushirikiana katika nyanja nyingine kadri itakavyoonekana inafaa.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa, Katibu Mkuu kutoka SMZ, Naibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi pamoja na Wataalamu wa pande zote mbili za SMT na SMZ katika kufanikisha ushirikiano huu. Ni matarajio yangu kuwa ushirikiano huu utaendelea hasa kwa kutekeleza kwa vitendo makubalino yaliyofikiwa kwa pamoja.



*Mawaziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi (SMT) na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi wa Zanzibar wakishuhudia utiaji saini wa hati za makubaliano ya ushirikiano baina ya Wizara hizo mbili Jijini Dodoma*.

**Utawala na Rasilimali Watu.**

156. ***Mheshimiwa Spika,*** Utawala na Rasilimali Watu ni sehemu muhimu katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara ina jumla ya watumishi **2,307**. Aidha, katika kipindi hicho, watumishi **380** walipandishwa madaraja na **33** walibadilishwa kada. Kwa kuzingatia muundo na majukumu ya Wizara, idadi halisi ya mahitaji ya watumishi ni **5,028** na hivyo kuwa na upungufu wa watumishi **2,723 *(Jedwali Na. 19)***. Katika kukabiliana na upungufu huo Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais -Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kupatiwa watumishi kwa idadi inayokidhi mahitaji. Aidha, katika mwaka 2023/2024, Wizara inatarajia kupata vibali vya ajira mpya **76,** kupandisha vyeo **346** na kubadilishwa kada watumishi **15**.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara imeendelea kusimamia uadilifu katika utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi nchini. Hatua muhimu zilizochukuliwa ni pamoja na kuboresha mifumo ya TEHAMA, kuendesha vikao vya Kamati ya Kudhibiti Uadilifu kwa ajili ya kujadili na kuishauri Wizara kuhusu masuala ya uadilifu katika utendaji kazi. Aidha, kupitia Kamati za nidhamu, jumla ya watumishi ishirini na saba (**27**) wamechukuliwa

hatua za kinidhamu kwa ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma ambapo watumishi **12** wamefukuzwa kazi, watumishi nane **(8)** wameshushwa ngazi ya mishahara, watumishi wawili **(2)** wamepewa onyo na watumishi watano **(5)** wameshushwa cheo.

158. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha usimamizi na utendaji wa Sekta ya Ardhi, katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Sekta ya Ardhi (*Land Sector Governance Framework*) ambao unalenga kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika usimamizi na utoaji huduma. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kupitia Mshauri Mwelekezi, inafanya tathmini ya hali halisi, kubaini changamoto zilizopo na kupendekeza mfumo sahihi na endelevu utakaokidhi mahitaji ya usimamizi wa Sekta ya Ardhi nchini.

159. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Mshauri Mwelekezi amekamilisha na kuwasilisha taarifa ya tathmini ya awali ya hali halisi na changamoto zinazoikabili Sekta ya Ardhi ikiwa ni pamoja na kupata maoni ya Wizara. Kwa sasa Mshauri Mwelekezi anaendelea na kazi ya kukamilisha Mfumo ambao unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2023/24.

Mafunzo kwa Watumishi

160. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwezesha watumishi kushiriki katika mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa lengo la kuhakikisha wanakuwa na weledi katika utoaji wa huduma. Katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kuwezesha watumishi kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa kuzingatia mahitaji na Mpango wa Mafunzo wa Wizara. Hadi kufikia 15 Mei, 2023, Wizara imewezesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi **290.** Aidha, katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kuwezesha mafunzo kwa watumishi kwa kuzingatia Mpango wa Mafunzo wa Wizara.

Habari na Elimu kwa Umma

161. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuzingatia umuhimu

wa kutoa elimu kwa umma kuhusu shughuli na masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Ardhi. Kwa mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya Sekta ya Ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara iliandaa na kusambaza nakala **18,900** za vipeperushi vyenye jumbe za kuelimisha umma kuhusu huduma zinazotolewa na Sekta ya Ardhi na nakala **5,200** za machapisho, na elimu kwa umma kupitia mikutano ya hadhara **24**. Aidha, Makala za magazeti **413**, vipindi **396** vya redio, **378** vya luninga na mitandao ya kijamii **1,862**, viliandaliwa na kutangazwa. Taarifa hizo pia zilitolewa katika mitandao ya Wizara ambayo ni Tovuti, *Instagram* na chaneli ya *Youtube*. Vilevile, elimu kwa umma imetolewa kupitia maonesho mbalimbali kitaifa na kimataifa.

162. *Mheshimiwa Spika,* Kwa mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo mbalimbali vya habari, mitandao ya kijamii, mikutano ya hadhara na maonesho mbalimbali.

**SHUKRANI**

163. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kwa umuhimu wa pekee kutambua mchango wa viongozi wenzangu katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Ninamshukuru Naibu Waziri, Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb.), kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Damian Sanga, Naibu Katibu Mkuu Bi. Lucy Dominico Kabyemela, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Taifa la Nyumba Bw. Hamad Abdallah Hamad, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Prof. Wakuru Magigi Maseka, Kamishna wa Ardhi Bw. Nathaniel Mathew Nhonge, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo pamoja na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

164. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, napenda kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Ardhi wanaojumuisha Mamlaka za Serikali za Mitaa, sekta binafsi, Bodi za Kitaaluma, Kamati za Ugawaji Ardhi, washirika wa maendeleo wakiwemo Benki ya Dunia, Benki ya

EXIM ya Korea Kusini, UN-HABITAT, TMRC, *Shelter Afrique*, *African Union Comission,* Benki ya Maendeleo Afrika, taasisi za fedha za ndani, Asasi za kiraia, mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu. Wizara inatambua na kuthamini michango yao katika Sekta ya Ardhi inayolenga maslahi mapana ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

**HITIMISHO**

165. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa maendeleo ya Sekta ya Ardhi kwa: -

i. Kuwekeza zaidi katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji huduma na upatikanaji wa taarifa za ardhi;

ii. Kuweka mazingira rafiki ya upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji;

iii. Kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi;

iv. Kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi;

v. Kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa maduhuli ya serikali yatokanayo na Sekta ya Ardhi ikiwa ni pamoja na matumizi ya teknolojia rahisi ya mawasiliano ya simu za mkononi; na

vi. Kuimarisha mipaka ya kimataifa.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2023/24**

166. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kama ifuatavyo: -

**Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

| | MAPATO | SHILINGI |
|---|---|---|
| A | **Mapato ya Serikali** | **300,000,000,000.00** |
| | **MATUMIZI** | |
| B | **Matumizi ya Kawaida:** | |
| | Mishahara (PE) | 43,428,651,000.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 37,614,584,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **81,043,235,000.00** |
| C | **Matumizi ya Maendeleo:** | |
| | Fedha za Ndani | 14,006,000,000.00 |
| | Fedha za Nje | 68,120,645,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **82,126,645,000.00** |
| | **JUMLA MATUMIZI (B+C)** | **163,169,880,000.00** |

Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Fungu **48** ni shilingi **163,169,880,000**.

**Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03)**

**Sura ya Bajeti ya Tume kwa mwaka 2023/24**

167. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, Tume inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni **8.2** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Maendeleo kama inavyoonekana katika Jedwali lifuatalo: -

**Fungu 03: Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.**

| AINA | AINA YA MATUMIZI | SHILINGI |
|---|---|---|
| A | **Mapato** | |
| | **Mapato ya Serikali** | **18,000,000** |
| B | **Matumizi ya Kawaida;** | |
| | Mishahara (PE) | 2,498,904,000 |
| | Matumizi Mengineyo | 2,293,724,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **4,792,628,000** |
| C | **Matumizi ya Maendeleo** | |
| | Fedha za ndani | 3,410,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **3,410,000,000** |
| **JUMLA KUU (B+C)** | | **8,202,628,000** |

168. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla kuu ya fedha zinazoombwa na Wizara (Fungu **48** na Fungu **03**) ili Bunge liweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi **171,372,508,000.00**.

169. ***Mheshimiwa Spika***, hotuba yangu imeambatana na majedwali yanayoainisha kwa ufasaha takwimu zinazohusiana na shughuli zilizotekelezwa na Wizara. Aidha, hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni *www.lands.go.tz*.

170. ***Mheshimiwa Spika,*** nakushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Angeline Mabula. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii. Karibu sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu 48 na Fungu 03, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, majukumu ya Kamati kuhusiana na uchambuzi wa bajeti ya Wizara au taasisi

inazozisimamia ikiwemo bajeti ya Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, yameelezwa kwa kina katika kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utayarishaji wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Naomba taarifa yote iingie kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na namna Kamati ilivyotekeleza Majukumu yake, masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, yanazitaka Kamati zote za kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazozisimamia na kufanya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti hayo ya kikanuni, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ilitekeleza wajibu huo kuanzia tarehe 24 – 28 Machi, 2023 kwa kufanya uchambuzi wa kina wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Uchambuzi huo ulihusu kutathmini utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wake kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo inahusisha mafungu mawili; Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

(a) Ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2022/2023;

(b) Utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha fedha 2022/2023;

(c) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(d) Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kufikia Februari, 2023; na

(e) Utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) ziliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya Shilingi bilioni 29.06 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ambazo ni fedha za ndani pamoja na nje. Katika ukaguzi uliofanywa na Kamati, Kamati ilifanikiwa kutembea katika mikoa mitatu ambayo ni Mkoa wa Manyara, Arusha na Kilimanjaro ili kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo, mafanikio na changamoto ili hatimaye kamati iweze kulishauri kikamilifu Bunge lako Tukufu juu ya hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa fedha. Mradi namba moja ni Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha – KKK (Mradi Na. 2326) katika Shamba la Valeska. Mradi huu unatekelezwa kwa utaratibu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutoa mikopo ya fedha isiyo na riba kwa halmashauri nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara iliidhinishiwa na Bunge kiasi cha Shilingi 5,358,166,155.56 kwa ajili ya kutekeleza mradi huu kwenye halmashauri mbalimbali nchini. Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi wa KKK katika Shamba la Valeska lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Mkoani Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Meru ilipatiwa na Wizara mkopo usio na riba wa Shilingi bilioni 1.65 ambao ulitumika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika shamba la Valeska lenye ukubwa wa ekari 4087. Awali shamba hilo lilikuwa likimilikiwa na Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Arusha *(ACU)*. Utekelezaji wa mradi huu umekamilika na

Halmashauri ya Wilaya ya Meru inatarajia kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 8.5. Baada ya kutoa fedha za mkopo Shilingi bilioni 1.65 na gharama nyingine za mradi, halmashauri inatarajia kupata faida ya Shilingi bilioni sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi Na. 2 ni Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka Kimataifa, mradi namba 2324. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara iliidhinishiwa Shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya uimarishaji wa mipaka ya kimataifa kati ya Tanzania na Kenya, hususan eneo la Namanga. Kwa ujumla mpaka wa Kenya na Tanzania unakadiriwa kuwa na urefu wa Kilomita 818, ambapo kilomita 758 ni eneo la nchi kavu na kilomita 60 ni eneo la maji. Kazi hii inafanyika kwa awamu. Hadi Februari, 2023 Shilingi milioni 669 zilikuwa zimeshatumika kwa ajili ya kuimarisha kilomita 348 kutokea Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na hali ya uimarishaji wa mpaka na usalama katika eneo hilo. Hata hivyo, hairidhishwi na kasi ndogo ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni, Ushauri na Mapendekezo kuhusu miradi;-

(1) Wananchi waelimishwe na kuhimizwa kulipa gharama za viwanja na mashamba yanayopimwa kupitia mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha;

(2) Halmashauri nchini zihamasishwe kutumia mapato yanayotokana na mradi wa KKK kurejesha mikopo wizarani na kuendeleza mradi huo katika maeneo mengine;

(3) Serikali iongeze bajeti inayotengwa kwa ajili ya uimarishaji wa mipaka ya kimataifa ili kukamilisha utekelezaji wa mradi huo; na

(4) Serikali itengeneze miundombinu ya barabara katika maeneo ya mipaka ili kuwezesha usafirishaji wa vifaa na utekelezaji wa kazi kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya ukusanyaji wa maduhuli kufikia Februari, 2023, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) ilikadiria kukusanya Shilingi bilioni 250 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 106 sawa na asilimia 42.55 ya makadirio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi hicho Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi milioni 706 kutoka katika vyanzo vyake. Hadi Februari, 2023 Tume ilikuwa imefanikiwa kukusanya shilingi milioni 881.5 sawa na asilimia 124.86 ya makadirio. Kielelezo namba mbili kinaonesha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Fungu 48 hauridhishi kwa kuwa uko chini ya malengo ambayo yalikuwa yamekusudiwa. Katika kipindi hicho cha miezi nane tangu kuanza kwa mwaka wa fedha, Wizara ilitakiwa kuwa imefikia wastani wa asilimia 66.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume hali ya ukusanyaji wa maduhuli ilikuwa ni nzuri. Tume ilivuka lengo lililowekwa kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha kwa kukusanya kwa asilimia 124.86. Kamati inapongeza tume kwa hatua hii ya ukusanyaji wa maduhuli na kutoa maoni kwamba, tume ipitie upya makadirio yanayowekwa ili kuhakikisha kuwa yanakuwa na uhalisia katika makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa fedha mpaka Februari, 2023; katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu 48 iliidhinishiwa shilingi bilioni 105.9 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 78 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 73.9 ya fedha yote iliyoidhinishwa Bunge lako. Aidha, Wizara ilitengewa shilingi bilioni 27.6 sawa na asilimia 26.1 ya fedha yote kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo fedha za ndani ni shilingi bilioni 14.5 na fedha za nje ni shilingi bilioni 13.1. Hadi Februari, 2023

Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 53.5 sawa na asilimia 50.5 ya fedha iliyoidhinishwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 26.2 ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 59.1 na shilingi bilioni 16.79 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 49.5 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu Namba 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Fungu Namba 03 iliidhinishiwa Shilingi bilioni 4.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 3.45 sawa na asilimia 71 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 1.4 sawa na asilimia 28 ni kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo Kamati; Taarifa ya Kamati kuhusu Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na mambo mengine, ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo kumi na tano ili yaweze kuzingatiwa na kutekelezwa na Wizara kwa lengo la kuboresha na kuongeza tija katika utendaji wa Sekta ya Ardhi. Katika kikao cha Kamati na Wizara kilichofanyika tarehe 24 Machi, 2023 Kamati ilibaini kwamba, Wizara imejitahidi kutekeleza sehemu kubwa ya maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Hata hivyo, bado kulikuwa na maeneo yanayoendelea kufanyiwa kazi na mengine yalikuwa hayajafanyiwa kazi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilichambua na kujadili Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

a) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

b) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

c) Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa; na

d) Mambo muhimu yanayogusa Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu 48 inakadaria kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 300. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio haya yameongezeka kwa shilingi bilioni 59.9 sawa na asilimia 19.95 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha unaokwisha. Aidha, uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kwamba Wizara imekuwa ikikusanya kwa wastani wa asilimia 42 katika kipindi cha miaka miwili ya fedha iliyopita (2021/2022, 2022/2023). Kutokana na mwenendo huo Kamati haioni uwezekano wa kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa na Wizara. Kamati inashauri Wizara ishughulikie changamoto zinazosababisha ikusanye kwa kiwango cha chini kabla ya kuongeza makadirio ili kuwa na uhalisia katika makusanyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imekadiria kukusanya jumla ya shilingi milioni 718. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, makadirio hayo yameongezeka kwa shilingi milioni 12 sawa na asilimia 1.69 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka fedha uliopita. Kamati inaipongeza Tume kwa kuongeza makadirio ya makusanyo hasa ikizingatiwa kwamba, katika mwaka huu wa fedha ilivuka malengo yake. Hata hivyo, ni ushauri wa Kamati kwamba Tume ipitie kikamilifu kanzi *data* yake na kuainisha madeni yaliyolimbikizwa ili iweze kukusanya na kufikia ongezeko hilo la asilimia 1.69. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makadirio ya matumizi kwa mwaka 2023/2024; Fungu Namba 48, Wizara ya Ardhi, Nyumba na

Maendeleo ya Makazi; ili kutekeleza malengo na vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu 48, inakadiria kutumia shilingi bilioni 163 ambazo zinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 81 sawa na asilimia 49.66 ya bajeti yote na shilingi bilioni 82 sawa na asilimia 50.34 ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 43 sawa na asilimia 53.59 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 37.6 sawa na asilimia 46.41 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha Bajeti ya Wizara (Fungu 48) kwa Mwaka wa Fedha unaokwisha na kubaini kwamba, Bajeti ya Wizara imeongezeka kwa asilimia 54.73 kutoka shilingi bilioni 105 kwa mwaka wa fedha unaokwisha hadi kufikia shilingi bilioni 163.2 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Wizara hii muhimu katika maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi; ili kutekeleza malengo na vipaumbele vyake Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03), inakadiria kutumia shilingi bilioni 6.2 ambazo zinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida shilingi 4.7 sawa na asilimia 76.25 ya bajeti yote na shilingi bilioni 1.4 sawa na asilimia 22.75 ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha bajeti ya Fungu 03 kwa mwaka wa fedha uliokwishwa na kubaini kwamba, Bajeti ya Tume imeongezeka kwa asilimia 27.42 kutoka shilingi 4.8 kwa mwaka wa fedha unaokwisha. Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Tume ambayo imekuwa ikifanya kazi nzuri licha ya bajeti ndogo inayotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha hakukuwa na ongezeko lolote kwenye fedha za maendeleo katika bajeti ya Tume wakati mahitaji halisi ni shilingi bilioni 20.65 katika mwaka wa fedha ujao. Kamati inasikitishwa na hali hii kwani licha ya ushauri uliotolewa katika mwaka wa fedha uliopita, kwamba chombo hiki muhimu

kiongezewe fedha za maendeleo ili kiweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu hakuna ongezeko lililowekwa. Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali iongeze fedha za maendeleo kwa ajili ya Tume hii ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwa ni pamoja na kupima na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu yanayogusa sekta ya ardhi; wakati wa kujadili mpango wa bajeti wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024, mambo kadhaa yanayogusa sekta ya ardhi yalijadiliwa. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na yafuatayo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Mradi wa Kuboresha Usalama wa Miliki za Ardhi *(LTIP)*. Mradi huu ni sehemu ya juhudi za Serikali zinazolenga kuondoa changamoto zinazoikabili sekta ya ardhi nchini yenye maeneo mengi ambayo hayajapimwa. Mradi unatekelezwa kwa miaka mitano kwa mkopo wa shilingi bilioni 350 kutoka Benki ya Dunia na utatekelezwa katika halmashauri 41 ambazo ni sawa na asilimia 22.28 ya halmashauri 184 zilizopo nchini. Hii inaashiria kwamba, mradi utagusa eneo ambalo ni chini ya robo ya eneo la nchi nzima. Mradi huu una maeneo manne kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; ni kuimarisha usalama wa taarifa za miliki za ardhi kwa kuandaa hati za kimila, leseni za makazi na leseni za miji, ununuzi wa magari, vifaa na vitendea kazi na kupima vijiji 500 kwa wastani wa vijiji 100 kwa mwaka. Idadi ambayo imeongezeka kutoka 250 vya awali baada ya juhudi na ushauri wa Kamati kwamba idadi hiyo iongezwe. Gharama ya eneo hilo la kwanza ni shilingi bilioni 167.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili la mradi ni ujenzi wa mfumo wa kuhifadhi taarifa za miliki za ardhi kwa kukarabati na kuweka samani katika ofisi za ardhi za wilaya na mikoa na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya mfumo, kwa gharama ya shilingi bilioni 76.93.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni ujenzi wa ofisi za ardhi za mikoa 25, ukarabati wa ofisi za ardhi za wilaya 40,

kusimika vifaa vya mfumo wa *ILMIS* na eneo hili litagharimu shilingi bilioni 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la nne na la mwisho la mradi huu ni uendeshaji, uratibu na dharura kwa gharama ya shilingi bilioni 46.86. Mgawanyo wa fedha katika maeneo hayo ni shilingi bilioni 2.4 (uendeshaji), shilingi bilioni 29.46 (uratibu) na shilingi bilioni 17.41 (dharura).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mchanganuo wa utekelezaji wa mradi huo, fedha nyingi zimeelekezwa kwenye maeneo ambayo kwa mtazamo wa Kamati hayana tija ya moja kwa moja na utatuzi wa changamoto za maeneo mengi ya ardhi kutopimwa. Kwa mfano, fedha iliyowekwa kwenye kupima na kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi kwenye vijiji hivyo 500 haizidi shilingi bilioni 10, wakati fedha ya uratibu, uendeshaji na dharura ni shilingi bilioni 46.68. Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ipitie upya mpango wa matumizi wa fedha za mradi huo na kufanya maboresho yatakayowezesha fedha zaidi zielekezwe katika mpango wa matumizi bora ya ardhi na kuimarisha mfumo wa *ILMIS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo Kamati iliangalia kama maeneo mahususi inayogusa sekta ya ardhi ni utatuzi wa migogoro nchini. Kumekuwa na migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji vinavyozunguka maeneo ya baadhi ya hifadhi nchini. Migogoro hiyo imekuwa chanzo cha uvunjifu wa amani na kusababisha madhara kwa wananchi na mali zao kwa upande mmoja na uharibifu wa mazingira ya hifadhi kwa upande mwingine. Kamati inatambua na kupongeza juhudi za Serikali ambazo ni pamoja na kuundwa kwa Kamati Maalum ya Mawaziri Nane wa Kisekta kwa lengo la kushughulikia utatuzi wa changamoto hiyo kwa vijiji 975. Hata hivyo utendaji wa Kamati hiyo umekuwa ukikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na malalamiko kutoka kwa wananchi na wawakilishi wao kwamba, hawashirikishwi kikamilifu katika utekelezaji wa maazimio ya Serikali kuhusiana na utatuzi wa migogoro iliyobainika katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kwamba, Kamati ya Mawaziri nane inapokwenda kwa wananchi kwa lengo la kutoa mrejesho wa Maazimio ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro iliyobainika, ihakikishe wananchi na wawakilishi wao wanashirikishwa kikamilifu. Aidha, taarifa ya utendaji wa Kamati hiyo iwasilishwe Bungeni ili Bunge lako Tukufu lipate fursa ya kuijadili na kuishauri Serikali juu ya namna bora ya kupata utatuzi wa kudumu kuhusiana na migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo yanayopakana na hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa; Shirika la Nyumba la Taifa ni taasisi ya umma ambayo ilianzishwa kwa lengo la kuchangia upatikanaji wa hitaji la makazi kwa Watanzania. Aidha, utendaji wa taasisi hii ni muhimu katika mipango ya matumizi bora ya ardhi nchini kupitia uendelezaji wa Sekta ya Nyumba na Makazi. Shirika hili limekuwa likitekeleza wajibu huo kama sehemu ya majukumu yake kupitia uanzishwaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba za kuuza na kupangisha. Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuruhusu na kuwezesha shirika hili kuzindua Sera mpya ya Ubia ambayo imefungua milango kwa sekta binafsi kushirikiana na shirika hilo katika uendelezaji wa sekta ya nyumba na makazi nchini. Utekelezaji wa sera hii utalisaidia shirika kuongeza uwezo wa kifedha na ujuzi na hivyo kuendeleza maeneo yake ambayo hayajaendelezwa ili kupata faida zaidi na kuongeza ukwasi kwa shirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali iendelee kuboresha mazingira ya shirika hili na shirika hili liendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kutekeleza na kukamilisha miradi yake kwa wakati na hivyo kudhibiti ongezeko la gharama za miradi. Aidha, shirika liwezeshwe kukwamua miradi ambayo utekelezaji wake umekwama kwa muda mrefu kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo za kifedha, pamoja na kuangalia uwezekano wa kulipa shirika hili nafuu ya kikodi ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka

huu wa fedha na uchambuzi wa kina kuhusu taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 na taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa Fungu 48 na Fungu 03. Naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kutotolewa kwa wakati kwa fedha za miradi ya mendeleo kunaathiri utekelezaji wa miradi hiyo hasa ikizingatiwa kuwa gharama za vitu zinapanda na kusababisha gharama za mradi kuongezeka. Kamati inashauri Serikali kutoa fedha kwa wakati na kwa kiwango stahiki ili kuiwezesha Wizara kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa ufanisi hasa ikizingatiwa kuwa utekelezaji wa miradi hiyo unategemea zaidi fedha za ndani kuliko fedha za wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo ya maduhuli katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 kunaathiri malengo ya makusanyo na kupunguza ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Wizara. Katika kipindi hicho makadirio yalikuwa shilingi bilioni 250 lakini ni asilimia 42 tu ndiyo ilikusanywa. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo: -

a) Kuweka maoteo yenye uhalisia na yanayoweza kufikiwa kwa wakati uliopangwa.

b) Kubuni mbinu mpya za makusanyo, ikiwa ni pamoja na kuongeza vyanzo vipya vya mapato, kuboresha mfumo wa makusanyo, kutoa elimu ya mlipa kodi na kurahisisha mfumo wa makusanyo kwa kuwawezesha wananchi kulipa pango la ardhi kupitia simu za viganjani.

c) Kusimamia kwa kina Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi ambao una lengo la kuongeza makusanyo ili kuweza kufikia matarajio,

d) Kutafuta mbinu ya kuongeza makusanyo katika ofisi za ardhi za mikoa. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023

mikoa imekusanya chini ya asilimia 50 ya lengo na mingine ikionesha udhaifu zaidi. Aidha, kila ofisi ya ardhi ya mkoa iandae mchanganuo utakaonesha kwa kina makadirio na makusanyo halisi ya pango la ardhi pamoja na maduhuli mengine katika mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; taasisi, mashirika ya umma na wananchi kutolipa kodi ya pango la ardhi na maduhuli yatokanayo na ardhi kunaathiri kwa kiwango kikubwa makusanyo yatokanayo na sekta ya ardhi. Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Kuhuisha taarifa katika kanzi *data* za taasisi na wamiliki wa viwanja, kuainisha wadaiwa sugu na kuwapa ukomo wa muda wa kulipa madeni yao ili wawajibike ipasavyo.

b) Kubuni mbinu mahususi za kuleta mwamko wa ulipaji kodi kwa wananchi na taasisi kwa ujumla. Hii ni pamoja na kutoa elimu ya mlipa kodi, kuboresha mfumo wa makusanyo wa mapato na kurahisisha zoezi la ulipaji kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne; halmashauri kutobakiwa na asilimia 30 ya makusanyo *(retention)* kumeathiri utendaji kazi wa halmashauri. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali ipitie maamuzi yake ili kufikiria upya namna ya kuziwezesha halmashauri kubakiza sehemu ya makusanyo yao ili kuziwezesha kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano; upungufu wa rasilimali fedha na vitendea kazi katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi umesababisha Mradi wa Kupanga Kupima na Kumilikisha kutotekelezwa kwa kasi na kuzifikia halmashauri nyingi nchini, jambo linalochangia ongezeko la makazi holela. Serikali iharakishe mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Ardhi na Nyumba ili kuongeza raslimali fedha kwa ajili ya programu ya KKK na hivyo kuwezesha halmashauri kutokomeza makazi holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu Namba 03 – Tume ya Taifa Mipango na Matumizi ya Ardhi; Kamati imebaini kutokuongezeka kwa fedha ya maendeleo iliyotengwa kwa ajili ya Tume kwa mwaka wa fedha 2023/2024 jambo hili linaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwani chombo hiki ni chombo muhimu. Kamati ilitarajia mabadiliko ya ongezeko la makadirio ya bajeti ya maendeleo kwa shilingi bilioni nne kutoka pale ilipokuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 na kupelekea makadirio ya 2023/2024 kufikia kiasi cha shilingi 5,410,000,000. Kamati inashauri ifuatavyo: -

a) Serikali iongeze fedha za maendeleo kwa Tume katika mwaka wa fedha 2023/2024 ili kukiwezesha chombo hiki muhimu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

b) Serikali ihakikishe inatimiza makubaliano yanayofikiwa baina yake na Bunge ili kutokwamisha utendaji wa taasisi zake. Mfano, kutoipatia Tume ongezeko la shilingi bilioni nne zilizoahidiwa ni kutokutimiza makubaliano baina ya Serikali na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; upungufu wa rasilimali watu unadhoofisha utendaji kazi wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Kamati inashauri Serikali ikamilishe kushughulikia ikama za watumishi 79 wanaohitajika ili kuongeza kasi ya utendaji wa Tume. Aidha, Serikali iiwezeshe Tume kupata vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; malimbikizo ya madeni ya kodi za nyumba na ardhi kutokana na mikataba iliyopitwa na wakati yameathiri makusanyo ya maduhuli na kupunguza ufanisi wa majukumu ya Tume. Kamati inashauri Serikali kuhuisha mikataba ili kuwasaidia wadaiwa kulipa madeni yao kwa wakati na hivyo kuisaidia Tume kukusanya kulingana na matarajio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne; Tume iongeze wigo wa kuhamasisha wadau wa kimkakati kushiriki katika kuchangia shughuli za upangaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini kwa lengo la kuinua makusanyo na maduhuli yatokanayo na sekta ya

ardhi na kuongeza kasi ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kumpongeza Mheshimiwa Spika, kukupongeza wewe binafsi, kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wengine wa Bunge kwa namna ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa weledi na umakini mkubwa na kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii hadi kukamilika kwa taarifa hii. Kwa umuhimu wake, ningetamani kuwatambua Wajumbe wote wa Kamati, lakini kwa kuzingatia muda ninaomba majina yao yote yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama yalivyoorodheshwa kwenye taarifa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula (Mb) na Naibu Waziri, Mheshimiwa Geofrey Mizengo Pinda, Mbunge kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Niwashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Sanga, akisaidiana na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Lucy Kabyemera, kwa ushirikiano na mchango wao kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, kwa namna ya kipekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc,* kwa kuongoza vyema uratibu wa

shughuli za Kamati za Bunge kwa ujumla. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndugu Chacha Nyakega na Ndugu Haika Mtui wakisaidiwa na Ndugu Pauline Mavunde kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuhakikisha maandalizi ya taarifa hii yana kamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba niliombe Bunge lako tukufu lipokee na kujadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 202**3**1**,** naomba nitumie fursa hii adhimu kukushukuru kwa kunipatia fursa ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48 na Fungu 03), kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Aidha, majukumu ya Kamati kuhusiana na uchambuzi wa bajeti ya Wizara au taasisi inazozisimamia ikiwemo bajeti ya Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, yameelezwa kwa kina katika kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023.

**Mheshimiwa Spika**, utayarishaji wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 kama ifuatavyo:-

a) Sehemu ya Kwanza ambayo inatoa utangulizi wa jumla na maelezo kuhusu msingi na muundo wa taarifa;

b) Sehemu ya Pili ambayo inaeleza kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na namna Wizara ilivyotekeleza ushauri na mapendekezo ya Kamati;

c) Sehemu ya Tatu inachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

d) Sehemu ya Nne inafafanua kuhusu mambo ambayo Kamati iliyobaini, ushauri na mapendekezo yake kwa Wizara na Serikali kwa ujumla; na

e) Sehemu ya Tano ambayo ni ya mwisho inahusu hitimisho la taarifa, ikijumuisha shukrani na kutoa hoja kwa Bunge lako Tukufu.

### 1.1 Namna Kamati ilivyotekeleza Majukumu yake

**Mheshimiwa Spika**, masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 yanazitaka Kamati zote za kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazozisimamia na kufanya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Kwa kuzingatia masharti hayo ya kikanuni, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ilitekeleza wajibu huo tarehe 24 – 28 Machi, 2023 kwa kufanya uchambuzi wa kina wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Uchambuzi huo ulihusu kutathmini utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA UZINGATIAJI WA USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo inahusisha mafungu mawili (**Fungu 48** - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na **Fungu 03 -** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi) kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

a) Ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2022/2023;

b) Utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha fedha 2022/2023;

c) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

d) Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kufikia Februari, 2023; na

e) Utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati;

## 2.1 Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa fedhaMheshimiwa Spika.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) ziliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 29,057,322,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ambazo ni fedha za ndani na nje.

Aidha, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023[1], kabla ya kuanza uchambuzi wa bajeti, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi iliyotengewa fedha na kutekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ziara ya Kamati ilihusisha mikoa mitatu (3) ambayo ni Manyara, Arusha na Kilimanjaro ili kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo, mafanikio na changamoto ili hatimaye Kamati iweze kulishauri kikamilifu Bunge lako Tukufu juu ya hatua za kuchukuliwa.

### 2.1.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi iliyotengewa fedha

(a) **Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha – KKK (Mradi Na. 2326) katika Shamba la Valeska.**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa kwa utaratibu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutoa mikopo ya fedha isiyo na riba kwa halmashauri nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara iliidhinishiwa na Bunge kiasi cha **Shilingi 5,358,166,155.56** kwa ajili ya kutekeleza mradi huu kwenye halmashauri mbalimbali nchini. Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi wa **KKK** katika Shamba la **Valeska** lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Mkoani Arusha.

Halmashauri ya Wilaya ya Meru ilipatiwa na Wizara mkopo usio na riba wa **Shilingi 1,655,000,000/=** ambao ulitumika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika shamba la Valeska lenye ukubwa wa ekari 4087. Awali shamba hilo lilikuwa mali ya Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Arusha (Arusha Cooperative Union Ltd – ACU) kabla ya umiliki wake kufutwa na mwaka, 2018 na shamba hilo kukabidhiwa Halmashauri ya Wilaya ya Meru.

Mkopo huo ulitumika kupanga, kupima, kufungua baadhi ya miundombinu ya barabara na kumilikisha kwa mujibu wa mwongozo wa KKK. Aidha, shilingi 394,010,000/= ilitumika kulipa fidia kwa Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Arusha**.** Aidha, utekelezaji wa mradi umewezesha ekari 1500 kutengwa kwa ajili ya wananchi wa vijiji vitatu vya Kwaugoro, Valeska na Maroroni, ekari 1028 kwa ajili ya kilimo na ekari 1559 kwa ajli ya makazi, biashara, viwanda vidogo na huduma nyingine za kijamii.

**Mhesimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu umekamilika na Halmashauri ya Wilaya ya Meru inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi 8,466,795,725/=.** Baada ya kutoa fedha za mkopo shilingi **1,655,000/=** na gharama nyingine za mradi **shilingi 598,231,950/=** faida halisi itakayopatikana ni **shilingi 6,213,563,775**. Faida hiyo ni sawa na asilimia 375.44 ikilinganishwa na gharama zilizotumika.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Kamati inatembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu tayari Halmashauri ya Wilaya ya Meru ilikuwa imekusanya **Shilingi 2,364,112,379/=** ambazo zimeiwezesha kurejesha mkopo wote na kuelekeza fedha iliyosalia kutekeleza mradi wa KKK katika maeneo mengine ya Halmashauri. Aidha, licha ya mradi huu kupata mafanikio hayo, kumekuwa na kasi ndogo ya ulipaji wa gharama za viwanja na mashamba kwa wananchi walionufaika.

(a) **Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka Kimataifa Na 2324**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara iliidhinishiwa **Shilingi 2,495,830,550/=** kwa ajili ya uimarishaji wa mipaka ya kimataifa kati ya Tanzania na Kenya, hususani eneo la Namanga. Kwa ujumla mpaka wa Kenya na Tanzania unakadiriwa kuwa na urefu wa Kilomita 818, ambapo kilomita 758 ni eneo la nchi kavu na kilomita 60 ni eneo la maji.

Kazi hii inafanyika kwa awamu na hadi Februari, 2023 S**hilingi 669,063,600/=** zilikuwa zimetumika kwa ajili ya kuimarisha kilomita 348 kutokea Ziwa Victoria. Kilimomita hizo ni sawa na asilimia **48** ya zoezi zima kwa eneo la mpaka wa Tanzania na Kenya, upande

wa Namanga**.** Kamati imeridhishwa na hali ya uimarishaji wa mpaka na usalama katika eneo hilo. Hata hivyo, hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi huu, kutokana na changamoto zifuatazo:-

i. Ufinyu wa Bajeti unaosababisha fedha kutengwa kidogo na kutolewa kwa awamu na hivyo kuchelewesha kazi;

ii. Ukosefu wa miundombinu ya barabara maeneo ya mipakani ambao unakwamisha usafirishaji wa vifaa na kuathiri utekelezaji wa kazi;

iii. Uharibifu wa alama za mipaka kutokana na shughuli za kilimo kwa wananchi wa pande zote;


iv. Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu umuhimu wa mipaka jambo linalosababisha migogoro kutokana na muingiliano wa shughuli baina ya watumiaji wa ardhi maeneo ya mipakani.

### 2.1.2 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi

**Mheshimiwa Spika**, tathmini ya Kamati kuhusiana na utekelezaji wa miradi inaonesha kwamba kuna mafanikio makubwa hasa kwa mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ambao utaiwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Meru kupata faida inayofikia asilimia 375.4. Tazama kielelezo **Na.01**

Aidha, kwa upande mwingine utekelezaji wa mradi wa uimarishaji wa mipaka ya kimataifa, hasa mpaka wa Tanzania na Kenya, upande wa Namanga unaenda kwa kasi ndogo kutokana na ufinyu wa bajeti.

**Kielelezo Na. 01: Utekelezaji wa Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha**
**– Halmashauri ya Wilaya ya Meru**




**Chanzo:** Taarifa ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Usanifu wa Kamati

### 2.1.3 Maoni, Ushauri na Mapendekezo kuhusu miradi

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia ziara ya ukaguzi wa miradi na yote yaliyobainika, Kamati inatoa maoni na mapendekezo yafuatayo:-

i. Wananchi waelimishwe na kuhimizwa kulipa

ii. gharama za viwanja na mashamba yanayopimwa kupitia mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha (KKK);

iii. Halmashauri nchini zihamasishwe kutumia mapato yanayotokana na mradi wa KKK kurejesha mikopo wizarani na kuendeleza mradi huo katika maeneo mengine;

iv. Halmashauri zilizokopeshwa fedha kwa ajili ya mradi wa KKK ziige mfano kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Meru ambayo imelipa mkopo wote na kutumia faida kuendeleza mradi katika maeneo mengine;

v. Serikali iongeze bajeti inayotengwa kwa ajili ya uimarishaji wa mipaka ya kimataifa ili kukamilisha utekelezaji wa mradi huo;

vi. Serikali itengeneze miundombinu ya barabara katika maeneo ya mipakani ili kuwezesha usafirishaji wa vifaa na utekelezaji wa kazi kikamilifu; na

vii. Wananchi waelimishwe kuhusu umuhimu wa kulinda alama za mpaka kwa kuepuka kuendesha shughuli za kilimo na kijamii.

2.2 **Utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Vipaumbele vya Serikali kwa ujumla unazingatia maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) mwaka 2021/22 – 2025/26 na maelekezo mengine.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ina dhamana ya kusimamia sekta ya ardhi ambayo ni raslimali muhimu kwa maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla. Kwa mantiki hiyo, usimamizi sahihi wa sekta hii utawezesha kuzingatiwa kwa malengo ya yaliyowekwa na Katiba yetu Ibara ya 8 (1) (b) ya kuhakikisha ustawi wa wananchi[2].

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba, bado sekta ya ardhi inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na kasi ndogo ya kupanga, kupima na kumilikisha, upimaji na uandaaji wa hati za umiliki wa maeneo, uwezo mdogo wa taasisi za ardhi kuhudumia wananchi, kasi ndogo ya uendelezaji wa makazi, na utatuzi utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Changamoto hizo zinakwamisha kufikiwa kwa malengo ya ilani ya Uchaguzi ya CCM inayoitaka Serikali kupima asilimia 50 ya vijiji vyote ifikapo mwaka 2025. Ni maoni ya Kamati kwamba,

changamoto hizo zitatuliwe ili kuiwezesha sekta hii muhimu kutoa mchango unaokidhi matarajio ya wananchi na hivyo kuboresha ustawi wao.

### 2.3 Hali ya ukusanyaji wa maduhuli kufikia Februari, 2023

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi **(Fungu 48)** ilikadiria kukusanya **shilingi 250,000,000,000/=** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya **shilingi 106,430,859,714/=** sawa na **asilimia 42.55** ya makadirio.

Aidha, katika kipindi hicho Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, (Fungu 03) ilikadiria kukusanya **shilingi 706,000,000/=** kutoka katika vyanzo vyake. Hadi kufikia Februari, 2023 Tume ilikuwa imefanikiwa kukusanya **shilingi 881,531,015/=** sawa na **asilimia 124.86** ya makadirio. **Kielelezo Na.02** kinaonesha makusanyo ya maduhuli kwa mafungu hayo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Fungu 48 hauridhishi ukusanyaji uko chini ya malengo yaliyowekwa na Wizara. Katika kipindi hicho cha miezi nane tangu kuanza kwa mwaka wa fedha, Wizara ilitakiwa kuwa imefikia wastani wa **asilimia 66.6.**

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa makusanyo hafifu yanatokana na madeni mengi ya ardhi na pango la ardhi ambayo Wizara inadai kutoka kwa wananchi pamoja na taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma. Aidha, kasi ndogo ya kurejesha fedha za mkopo wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha na udhaifu katika ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi na maduhuli yatokanayo na ardhi katika ofisi za ardhi za baadhi ya mikoa nchini. Mfano mikoa ya Simiyu na Rukwa ilikusanya kwa asilimia 19 tu ya lengo, kiwango ambacho ni cha chini sana. **Kamati inashauri Wizara kuzisimamia kikamilifu ofisi za ardhi za mikoa ili kuhakikisha zinaongeza umakini katika makusanyo sambamba na kuweka makadirio halisi ya makusanyo. Aidha, Wizara iboreshe mifumo ya ukusanyaji wa maduhuli kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Tume (Fungu 03) hali ya ukusanyaji wa maduhuli ilikuwa nzuri. Tume ilivuka lengo lililowekwa kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha kwa kukusanya kwa **asilimia 124.86**. Kamati inapongeza hatua hii ya ukusanyaji wa maduhuli na kutoa maoni kwamba, Tume ipitie upya makadirio yanayowekwa ili kuhakikisha kuna uhalisia wa makusanyo.

**Kielelezo Na. 02 Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2023**

| Fungu | Makadirio | Makusanyo | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **Fungu 48 (Wizara)** | 250,100,000,000 | 106,430,859,714 | 42.55 |
| **Fungu 03 (Tume)** | 706,000,000 | 881,531,015 | 124.86 |

**Chanzo: Randama ya Wizara & Tume 2023 na Usanifu wa Kamati**

**2.4 Hali ya upatikanaji wa fedha kufikia Februari, 2023**

**(a) Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**
**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (**Fungu 48)** iliidhinishiwa **Shilingi 105,949,770,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo **shilingi 78,302,448,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 73.9** ya fedha yote iliyoidhinishwa na **shilingi 33,918,651,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **shilingi 44,383,797,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara (PE).

Aidha, Wizara ilitengewa **shilingi 27,647,322,000/=** sawa na **asilimia 26.1** ya fedha yote kwa ajili ya miradi ya maendeleo kati ya fedha hizo fedha za ndani ni **shilingi 14,500,000,000/**= na fedha za nje ni **shilingi 13,147,322,000/=**.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2023 Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 53,533,004,601/=** sawa na **asilimia 50.5** ya fedha iliyoidhinishwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kati ya fedha zilizopokelewa **shilingi 26,219,595,076/=** ni kwa ajili ya mishahara sawa na **asilimia 59.1** na **shilingi 16,785,297,220/**= ni

kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na **asilimia 49.5** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

Aidha, katika fedha hizo **shilingi 10,528,112,303/=** ni kwa ajili ya maendeleo sawa na **asilimia 38.1** ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo. Fedha hizo zinajumuisha fedha za ndani s**hilingi 7,244,972,303/=** sawa na **asilimia 50** ya fedha za ndani na fedha za nje **shilingi 3,283,140,000/=** ambazo ni sawa na **asilimia 25.0** ya fedha za nje zilizotengwa. Kamati imebaini kwamba fedha za nje zilipatikana kwa kiwango cha chini sana (25%) na hairidhishwi na hali hiyo kwani inaathiri utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa. **Kielelezo Na. 03 kinafafanua zaidi**.

**Kielelezo Na.3: Upatikanaji wa fedha hadi Februari, 2023 (Fungu 48)**

| Matumizi | Kilichoidhinishwa | | Kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **OC** | 33,918,651,000 | | 16,785,297,220 | 49.4 |
| **Mishahara** | 44,383,797,000 | | 26,219,595,076 | 59.1 |
| **Maendeleo** | **Ndani** | 14,500,000,000 | 7,244,927,303 | 50.0 |
| | **Nje** | 13,147,322,000 | 3,283,140,000 | 25.0 |
| | **Jumla** | 27,647,322,000 | 10,528,112,303 | 38.0 |
| **Jumla Kuu** | 105,949,770,000.00 | | 53,533,004,601 | 50.5 |

**Chanzo**: Randama ya Wizara mwaka 2023 na Usanifu wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni **asilimia 54.9**. **Wastani** huu uko chini ya lengo ikilinganishwa na matarajio katika kipindi hicho cha bajeti ambayo ni **asilimia 66.6** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kamati inasikitishwa na mwenendo huu kwani haioni uwezekano wa Wizara kupokea kikamilifu kiasi cha fedha kilichobaki kabla ya kukamilika kwa mwaka huu wa bajeti.

**(b) Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) iliidhinishiwa

**Shilingi 4,867,704,000/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi 3,457,644,000/=** sawa na **asilimia 71.03** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 1,410,000,000/=** sawa na **asilimia 28.97** ni kwa ajili ya maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida **shilingi 1,977,882,000/=** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na **shilingi 1,479,822,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2023 Tume ilikuwa imepokea **shilingi 3,056,289,450/=** sawa na **asilimia 62.59** ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa. **Uchambuzi** wa Kamati ulibaini kwamba, kati ya fedha zilizopokelewa **shilingi 1,344,576,000/=** ni kwa ajili ya mishahara sawa na **asilimia 67.98** na **shilingi 736,715,950/**= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na **asilimia 49.78** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge. Aidha, katika fedha hizo **shilingi 974,997,500** ni kwa ajili ya maendeleo sawa na **asilimia 69.15** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) kwa fungu hili hauridhishi kwani ni **asilimia 49** tu. Kiasi hiki ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotakiwa kutolewa katika kipindi hicho. Hali hii inaleta mashaka kwani matumizi mengineyo ndiko kuna fedha za kuendeshea ofisi na kulipia huduma za lazima. K**ielelezo Na. 04** kinafafanua zaidi kuhusu upatikani wa fedha kwa Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

**Kielelezo Na.04 Upatikanaji wa fedha hadi Februari, 2023 (Fungu 03)**

| Matumizi | Kilichoidhinishwa | Kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **OC** | 1,479,822,000 | 736,715,950 | 49.78 |
| **Mishahara** | 1,977,882,000 | 1,344,576,000 | 67.98 |
| **Maendeleo** | 1,410,000,000 | 974,997,500 | 69.15 |
| **JUMLA** | 4,867,704,000 | 3,056,289,450 | 62.79 |

**Chanzo**: Randama ya Tume mwaka 2023 na Usanifu wa Kamati.

## 2.5 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo Kamati

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na mambo mengine, ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kumi na tano (**15)** ili yaweze kuzingatiwa na kutekelezwa na Wizara kwa lengo la kuboresha na kuongeza tija katika utendaji wa sekta ya ardhi.

Katika kikao cha Kamati na Wizara kilichofanyika tarehe 24 Machi, 2023 Kamati ilibaini kwamba, Wizara imejitahidi kutekeleza sehemu kubwa ya maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Hata hivyo, bado kulikuwa na maeneo yanayoendelea kufanyiwa kazi na mengine yalikuwa hayajafanyiwa kazi kabisa.

Miongoni mwa maoni yaliyotekelezwa ni pamoja na Serikali kuandaa mfumo mahsusi wa kuwakumbusha wateja kulipa kodi ya pango la ardhi kwa kutumia simu ili kuongeza ari ya kulipa kodi na kufikia lengo la makusanyo. Tayari Wizara imebadilisha taarifa za ardhi kuwa za kieletroniki kupitia zoezi la kubadili taarifa (data conversion)kwa kutumia taarifa za anuani za makazi na taarifa za sensa ili kuhuisha kumbukumbu za wamiliki wa ardhi nchini na tayari wamiliki wameanza kupata jumbe za kuwakumbusha kulipa kodi ya ardhi kwa wakati.

Aidha, kwa upande wa maoni ambayo hayakutekelezwa, ni pamoja na lile lililoitaka Serikali kutenga bajeti itakayokidhi mahitaji halisi ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ikiwa ni pamoja na kuiongezea **Shilingi 4,000,000,000**/= ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Hili halikufanyika licha Serikali kupitia Waziri wa Fedha kuahidi kutoa kiasi hicho kwa Tume katika mwaka huu wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihitaji ufafanuzi wa kina na majibu ya Wizara yalionesha nia njema ya Serikali kuendelea kutekeleza maoni ya Kamati. Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, **utekelezaji wa Ushauri, maoni na mapendekezo hayo ufanyike kikamilifu ili kuboresha utendaji wa sekta ya ardhi ambayo inagusa maisha ya kila mtanzania, lakini pia ni miongoni mwa**

**maeneo ambayo Serikali iliyopo madarakani iliahidi kupitia Ilani ya CCM ya mwaka 2020 kuyafanyia kazi ili kuondoa changamoto zilizopo.**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilichambua na kujadili Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.
Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-
a) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024;
b) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;
c) Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa; na
d) Mambo muhimu yanayogusa sekta ya ardhi.

### 3.1 Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024

(a) **Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48)**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara (Fungu 48) imekadaria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 300,000,000,000/=.** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio haya yameongezeka kwa **shilingi 59,900,000,000/=** sawa na **asilimia 19.95 i**kilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2022/2023 ambayo yalikuwa **shilingi 250,100,000,000/=** kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.5.**

Kamati ina mashaka kuhusiana na ongezeko hili kutokana na ukweli kwamba, hali ya ukusanyaji wa maduhuli kwa Wizara hairidhishi kwani hadi Februari, 2023 Wizara ilikuwa imekusanya kwa asilimia 42 tu, hivyo kuna mashaka iwapo lengo litafikiwa kabla ya mwaka wa bajeti kukamilika.

Aidha, uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kwamba Wizara imekuwa ikikusanya kwa wastani wa asilimia 42 katika kipindi cha miaka miwili ya fedha iliyopita (2021/2022 na 2022/2023). **Kutokana na mwenendo huu Kamati haioni uwezekano wa kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa na Wizara. Kamati inashauri Wizara ishughulikie changamoto zinazosababisha ikusanye kwa kiwango cha chini kabla ya kuongeza makadirio ili kuwa na uhalisia katika makusanyo.**

**(b) Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03)**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imekadiria kukusanya jumla ya **shilingi 718,000,000/=.** Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, makadirio hayo yameongezeka kwa **shilingi 12,000,000/=** sawa na **asilimia 1.69** ikilinganishwa na makadirio ya mwaka fedha 2022/2023, kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 05 cha taarifa hii.

Kamati inaipongeza Tume kwa kuongeza makadirio ya makusanyo hasa ikizingatiwa kwamba, katika mwaka huu wa fedha ilivuka malengo yake. Hata hivyo, ni ushauri wa Kamati kwamba Tume ipitie kikamilifu kanzi data yake na kuainisha madeni yaliyolimbikizwa ili iweze kukusanya na kufikia ongezeko hilo la asilimia 1.69 katika mwaka wa fedha ujao.

**Kielelezo Na. 05: Ulinganishio wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli 2022/2023 na 2023/2024**

| FUNGU | 2022/2023 | 2023/2024 | Ongezeko/ Punguzo | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Wizara (48)** | 250,100,000,000 | 300,000,000,0 00 | 49,900,000,000 | 19.95 |
| **Tume (03)** | 706,000,000 | 718,000,000 | 12,000,000 | 1.69 |

**Chanzo: Randama za Wizara na Tume na Usanifu wa Kamati**

### 3.2 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2023/2024

(a) **Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu-48)**

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza malengo na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48), inakadiria kutumia **Shilingi 163,169,880,000/=** ambazo zinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida **shilingi 81,043,235,000/=** sawa na **asilimia 49.66** ya bajeti yote, na **shilingi 82,126,645,000/=** sawa na **asilimia 50.34** ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Katika fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 43,428,651,000/=** sawa na **asilimia 53.59** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na **shilingi 37,614,584,000/=** sawa na **asilimia 46.41** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC)**.** Aidha, katika fedha za maendeleo **shilingi 14,006,000,000/=** sawa na **asilimia 17.05** ni fedha za ndani na **Shilingi 68,120,645,000/=** sawa na **asilimia 82.95** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha bajeti ya Wizara - Fungu 48 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 na kubaini kwamba, Bajeti ya Wizara imeongezeka kwa asilimia 54.73 kutoka **Shilingi 105,455,770,000/**= mwaka 2022/2023 hadi kufikia **Shilingi 163,169,880,000/=** mwaka 2023/2024. Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Wizara hii muhimu katika maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kuwa, ongezeko kubwa liko katika fedha za maendeleo (**asilimia 200)** ikilinganishwa na fedha zilizotengwa kwenye eneo hilo katika mwaka huu wa fedha. Aidha, fedha za nje zimeongezeka kwa **asilimia 418.13** ikilinganishwa na fedha za nje katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Eneo lingine ambalo bajeti imeongezeka ni kwenye matumizi mengineyo (OC) kwa **asilimia 10.89.** Vilevile, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, fedha za mishahara (PE) zimepungua kwa **asilimia 2.2** ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa mwaka 2022/2023 kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.6**.

**Kielelezo Na.6: Ulinganisho wa Bajeti 2022/2023 na 2023/2024**

| **Mwaka** | **Matumizi ya Kawaida** | | **Maendeleo** | |
|---|---|---|---|---|
| | PE | OC | Ndani | Nje |
| 2022/23 | 44,383,797,000 | 33,918,651,000 | 14,006,000,000 | 13,147,322,000 |
| 2023/24 | 43,428,651,000 | 37,614,584,000 | 14,006,000,000 | 68,120,645,000 |
| Ongezeko/Punguzo | 955,146000 | 3,695,933,000 | 0 | 54,973,323,00 |
| Asilimia - % | -2.2% | 10.89 | 0 | 418.133 |

*Chanzo: Taarifa za Wizara na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji kuhusu ongezeko la fedha za maendeleo kutoka nje, wakati hakuna uhakika wa kuzipata kutokana na ukweli kwamba, katika mwaka huu wa fedha hadi kufikia Februari, 2023 wakati Kamati inapokea taarifa, fedha hizo zilikuwa zimepatikana kwa **asilimia 25** tu**.** Hata hivyo, Kamati ilihakikishiwa kuwa fedha hizo zitapatikana kabla ya kukamilika kwa mwaka huu wa fedha.

(b) **Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu -03)**

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza malengo na vipaumbele vyake Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03), inakadiria kutumia **Shilingi 6,202,628,000/=** ambazo zinajumuisha fedha za matumizi ya kawaida **shilingi 4,729,628,000/=** sawa na **asilimia 76.25** ya bajeti yote, na **shilingi 1,410,000,000/=** sawa na **asilimia 22.75** ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Katika fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 2,498,904,000/=** sawa na **asilimia 52.14** ni kwa ajili ya mishahara (PE) na **shilingi 2,293,724,000/=** sawa na **asilimia 47.86** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC)**.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha bajeti ya Fungu 03 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 na kubaini kwamba, Bajeti ya Tume imeongezeka kwa **asilimia 27.42** kutoka **Shilingi 4,867,704,000/=** mwaka 2022/2023 hadi kufikia **Shilingi 6,202,628,000/=** mwaka 2023/2024. **Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya**

**Tume ambayo imekuwa ikifanya kazi nzuri licha ya bajeti ndogo inayotengwa.**

Uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini ongezeko liko kwenye matumizi ya kawaida kwa **asilimia 38.6** ikilinganishwa na fedha zilizotengwa kwenye eneo hilo katika mwaka wa fedha unaoisha. Aidha, ongezeko hilo limeathiri upande mishahara kwa **asilimia 26.34** na upande wa matumizi mengine kwa **asilimia 55** ikilinganishwa na fedha zilizotengwa katika maeneo hayo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha hakukuwa na ongezeko lolote kwenye fedha za maendeleo katika bajeti ya Tume, wakati mahitaji halisi ni **shilingi bilioni 20.65** katika mwaka ujao wa fedha. Kamati inasikitishwa na hali hii kwani licha ya ushauri uliotolewa katika mwaka wa fedha uliopita kwamba, chombo hiki muhimu kiongezewe fedha za maendeleo ili kiweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu hakuna lolote ambalo limekuwa likifanyika. Kamati ilitarajia kwamba, Tume ingetengewa angalau kuanzia **Shilingi Bilioni 5.41** (**Shilingi 1,410,000,000/=** zilizotengwa mwaka 2022/23 ikijumuishwa na kiasi cha **shiliingi 4,000,000,000/=** ambazo ziliahidiwa kuongezwa wakati wa majadiliano baina ya Kamati ya Uongozi, Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha), ingawa bado kiwango hicho kiko chini ikilinganishwa na mahitaji halisi.

Hali hii inachangia kukwamisha chombo hiki kufikia malengo ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwa idadi ya vijiji inayotakiwa kwa mwaka. **Kielelezo Na. 07** kinabainisha ulinganisho wa bajeti ya Tume.

Kwa ujumla bajeti ya tume kwa ajili ya maendeleo haikidhi mahitaji sambamba na matakwa ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020 – 2025 inayoelekeza uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa Vijiji 4031 hadi kufikia 2025.

Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali iongeze fedha za maendeleo kwa ajili ya Tume hii ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwa ni pamoja na kupima na kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi hapa nchini

**Kielelezo Na.7: Ulinganisho wa Bajeti 2022/2023 na 2023/2024 Mwaka**

| Mwaka | Matumizi ya Kawaida | | Maendeleo |
|---|---|---|---|
| | PE | OC | |
| 2022/23 | 1,977,882,000 | 1,479,822,000 | 1,410,000,000 |
| 2023/24 | 2,498,904,000 | 2,293,724,000 | 1,410,000,000 |
| Ongezeko/Punguzo | 521,022, 000 | 813,902,000 | - |
| Asilimia -% | 26.34% | 55 | - |

*Chanzo: Taarifa za Tume na usanifu wa Kamati*

**3.3 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulijielekeza pia kwenye ulinganisho wa bajeti ya Wizara ya ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na bajeti ya Taifa. Ulinganisho huo uliangalia bajeti ya Wizara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 na mwaka wa fedha 2023/2024 dhidi ya bajeti ya Taifa katika kipindi hicho. Matokeo ya uchambuzi wa Kamati umebaini mambo kama ifuatavyo:-

a) Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi dhidi ya Bajeti ya Taifa imeongezeka kutoka asilimia **0.26 hadi asilimia 0.36.**

b) Bajeti ya Matumizi Mengineyo imeshuka kutoka **asilimia 0.75** hadi **asilimia 0.67.**

c) Bajeti ya mishahara ilipungua kutoka asilimia 0.46 hadi kufikia asilimia 0.40

d) Bajeti ya Maendeleo kutokana na fedha za ndani haikuwa na mabadiliko kwani ilisalia katika kiwango cha **asilimia 0.12** katika vipindi hivyo.

e) Kumekuwa na ongezeko kubwa katika bajeti ya maendeleo kutokana na fedha za nje kutoka asilimia 0.39 hadi asilimia 2.08

**Kielelezo Na. 8: Bajeti ya Wizara (Fungu 48) dhidi ya Bajeti ya Taifa**

| BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2022/2023 NA 2023/2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI YA ARDHI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 4,493,500,000.00 | 33,918,651,000.00 | 0.75 |
| **MISHAHARA** | 9,740,800,000.00 | 44,383,797,000.00 | 0.46 |
| **MAENDELEO NDANI** | 12,122,100,000,000.00 | 14,006,000,000.00 | 0.12 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,399,200,000,000.00 | 13,147,322,000.00 | 0.39 |
| **DENI LA SERIKALI** | 11,308,400,000,000.00 | | - |
| **JUMLA** | 41,064,000,000,000.00 | 105,455,770,000.00 | 0.26 |
| **BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2023/2024** | | | |
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI YA ARDHI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 5,578,433,000,000 | 37,614,584,000.00 | 0.67 |
| **MISHAHARA** | 10,882,126,000,000 | 43,428,651,000 | 0.40 |
| **MAENDELEO NDANI** | 11,873,900,000,000 | 14,006,000,000.00 | 0.12 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,282,100,000,000 | 68,120,645,000.00 | 2.08 |
| **DENI LA SERIKALI** | 12,771,500,000,000 | 0 | - |
| **JUMLA** | **44,388,059,000,000.00** | **163,169,880,000.00** | **0.37** |

*Chanzo: Taarifa ya Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023, Randama ya Wizara ya Ardhi 2022/2023*

### 3.4 Mambo muhimu yanayogusa sekta ya ardhi

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kujadili mpango wa bajeti wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024, mambo kadhaa yanayogusa sekta ya ardhi yalijadiliwa. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na:-

#### 3.4.1 Mradi wa Kuboresha Usalama wa Miliki za Ardhi (LTIP)

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ni sehemu ya juhudi za Serikali zinazolenga kuondoa changamoto zinazoikabili sekta ya ardhi

nchini yenye maeneo mengi ambayo hayajapimwa. Mradi utatekelezwa kwa miaka mitano kwa mkopo **wa shilingi bilioni 350** kutoka Benki ya Dunia na utatekelezwa katika halmashauri 41 ambazo ni sawa na asilimia 22.28 ya halmashauri 184 zilizopo nchini. Hii inaashiria kwamba, mradi utagusa eneo ambalo ni chini ya robo ya eneo la nchi nzima. Mradi huu una maeneo manne yafuatayo:-

i. Kuimarisha usalama wa taarifa za miliki za ardhi kwa kuandaa hati za kimila, leseni za makazi na leseni za mijini, ununuzi wa magari, vifaa na vitendea kazi na kupima vijiji 500 (wastani wa vijiji 100 kwa mwaka) idadi ambayo imeongezeka kutoka 250 vya awali baada ya juhudi na ushauri wa Kamati kwamba idadi ya vijiji iongezeke. Gharama ya eneo hili ni **Shilingi bilioni 167.1;**

ii. Ujenzi wa mfumo wa kuhifadhi taarifa za miliki za ardhi kwa kukarabati na kuweka samani katika ofisi za ardhi za wilaya na mikoa na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya mfumo, kwa gharama ya **shilingi bilioni 76.93;**

iii. Ujenzi wa ofisi za ardhi za mikoa 25, ukarabati wa ofisi za ardhi za wilaya 40, kusimika vifaa vya mfumo wa ILMIS ili kuuwezesha kufanya kazi kikamilifu, kuboresha ofisi za mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya na kujenga uelewa kwa wadau na taasisi zinazosimamia ardhi. Eneo hili litagharimu **shilingi bilioni 55;** na

iv. Uendeshaji, uratibu na dharura kwa gharama ya **shilingi bilioni 46.86.** Mgawanyo wa fedha katika maeneo hayo ni **shilingi bilioni 2.4 (**uendeshaji), **shilingi bilioni 29.46** (uratibu) na **shilingi bilioni 17.41** (dharura).

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa mchanganuo wa utekelezaji wa mradi huo, fedha nyingi zimeelekezwa kwenye maeneo ambayo kwa mtazamo wa Kamati hayana tija ya moja kwa moja na utatuzi wa changamoto za maeneo mengi ya ardhi kutopimwa. Kwa mfano fedha iliyoelekezwa kwenye kupima na kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi kwenye vijiji hivyo 500

haizidi shilingi **bilioni 10**, wakati fedha ya uratibu, uendeshaji na dharura ni **shilingi bilioni 46.68**.

Ni ushauri wa Kamati kwamba, Serikali ipitie upya mpango wa matumizi wa fedha za mradi huo na kufanya maboresho yatakayowezesha fedha zaidi zielekezwe katika mpango wa matumizi bora ya ardhi na kuimarisha mfumo wa ILMIS.

**3.4.2 Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi nchini**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji vinavyozunguka maeneo ya baadhi ya hifadhi nchini. Migogoro hiyo imekuwa chanzo cha uvunjifu wa amani na kusababisha madhara kwa wananchi na mali zao kwa upande mmoja, na uharibifu wa mazingira ya hifadhi kwa upande mwingine.

Kamati inatambua na kupongeza juhudi za Serikali ambazo ni pamoja na kuundwa kwa Kamati Maalum ya Mawaziri nane wa kisekta kwa lengo la kushughulikia utatuzi wa changamoto hiyo kwa vijiji 975. Hata hivyo utendaji wa Kamati hiyo umekuwa ukikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na malalamiko kutoka kwa wananchi na wawakilishi wao kwamba, hawashirikishwi kikamilifu katika utekelezaji wa maazimio ya Serikali kuhusiana na utatuzi wa migogoro iliyobainika katika maeneo yao.

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kwamba, Kamati ya Mawaziri nane inapokwenda kwa wananchi kwa lengo la kutoa mrejesho wa Maazimio ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na utatuzi wa migogoro iliyobainika, ihakikishe wananchi na wawakilishi wao wanashirikishwa kikamilifu.

Aidha taarifa ya utendaji wa kamati hiyo iwasilishwe Bungeni ili Bunge lako tukufu lipate fursa ya kuijadili na kuishauri Serikali juu ya namna bora ya kupata utatuzi wa kudumu kuhusiana na migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye maeneo yanayopakana na hifadhi.

### 3.4.3 Shirika la Nyumba la Taifa

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ni taasisi ya umma ambayo ilianzishwa kwa lengo la kuchangia upatikanaji wa hitaji la makazi kwa watanzania. Aidha, utendaji wa taasisi hii ni muhimu katika mipango ya matumizi bora ya ardhi nchini kupitia uendelezaji wa sekta ya nyumba na makazi. Shirika hili limekuwa likitekeleza wajibu huo kama sehemu ya majukumu yake kupitia uanzishwaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba za kuuza na kupangisha.

Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuruhusu na kuwezesha Shirika hili kuzindua Sera mpya ya Ubia ambayo imefungua milango kwa sekta binafsi kushirikiana na shirika hilo katika uendelezaji wa sekta ya nyumba na makazi nchini. Utekelezaji wa sera hii utalisaidia shirika kuongeza uwezo wa kifedha na ujuzi na hivyo kuendeleza maeneo yake ambayo hayajaendelezwa ili kupata faida zaidi na kuongeza ukwasi kwa shirika.

Kamati inaishauri Serikali iendelee kuboresha mazingira ya NHC ili shirika hili liendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kutekeleza na kukamilisha miradi yake kwa wakati na hivyo kudhibiti ongezeko la gharama za miradi. Aidha, shirika liwezeshwe kukwamua miradi ambayo utekelezaji wake umekwama kwa muda mrefu kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo za kifedha, pamoja na kuangalia uwezekano wa kulipa shirika hili nafuu za kikodi. Ni matumaini ya Kamati kwamba, iwapo haya yatafanyika shirika litaweza kujiendesha kwa mafanikio.

### 3.4.4 Changamoto ya Upimaji wa Ardhi katika Jiji la Dodoma

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusiana na upimaji shirikishi wa ardhi katika Jiji la Dodoma kutokana na zoezi hilo kutoshirikisha wamiliki wa ardhi ipasavyo, jambo ambalo limesababisha migogoro kati ya waliouziwa maeneo baada ya upimaji na wamiki wa awali. Suala hili linakwamisha makundi hayo kuendelea na taratibu za kupata hati za umiliki na Serikali kukosa mapato stahiki.

Aidha, yapo pia malalamiko ya umilikishaji wa kipande kimoja cha ardhi kwa zaidi ya mmiliki mmoja (double allocation). Kamati inatambua kwamba, changamoto hii ipo pia katika maeneo mengine hapa nchini.

Kamati inaishauri Serikali kutafuta ufumbuzi wa malalamiko hayo ili kuondoa migogoro ya ardhi iliyojitokeza katika eneo hilo na maeneo mengine na hivyo kuleta maelewano baina ya wananchi waliouziwa baada ya zoezi la upimaji na wamiliki wa awali.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka huu wa fedha, uchambuzi wa kina kuhusu taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 na taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ninaomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

### 4.1 Fungu 48 – Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi

i. Kutotolewa kwa wakati kwa fedha za miradi ya mendeleo kunaathiri utekelezaji wa miradi hiyo hasa ikizingatiwa kuwa gharama za vitu zinapanda na kusababisha gharama za mradi kuongezeka. Kamati inashauri Serikali kutoa fedha kwa wakati na kwa kiwango stahiki ili kuiwezesha Wizara kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa ufanisi hasa ikizingatiwa kuwa utekelezaji wa miradi hiyo unategemea zaidi fedha za ndani kuliko fedha za wafadhili ambazo hupatikana kwa kusuasua.

ii. Kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo ya maduhuli katika mwaka wa fedha 2022/2023 kunaathiri malengo ya makusanyo na kupunguza ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Wizara. Katika kipindi hicho makadirio yalikuwa shilingi bilioni 250, lakini ni asilimia

42 tu ndiyo ilikusanywa. Katika Mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imeweka makadirio ya kukusanya Bilioni 300, ambayo ni ya juu zaidi kuliko mwaka 2022/2023 ambayo hayakufikiwa. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo:-

a) Kuweka maoteo yenye uhalisia na yanayoweza kufikiwa kwa wakati uliopangwa.

b) Kubuni mbinu mpya za makusanyo, ikiwa ni pamoja na kuongeza vyanzo vipya vya mapato, kuboresha mfumo wa makusanyo, kutoa elimu ya mlipa kodi, na kurahisisha mfumo wa makusanyo kwa kuwawezesha wananchi kulipa pango la ardhi kupitia simu za viganjani.

c) Kusimamia kwa kina mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi ambao una lengo la kuongeza makusanyo ili kuweza kufikia matarajio,

d) Kutafuta mbinu ya kuongeza makusanyo katika ofisi za ardhi za mikoa. Katika mwaka wa fedha 2022/23 mikoa mingi imekusanya chini ya asilimia 50 ya lengo na mingine ikionesha udhaifu zaidi. Aidha, kila ofisi ya ardhi ya mkoa iandae mchanganuo utakaonesha kwa kina makadirio na makusanyo halisi ya pango la ardhi pamoja na maduhuli mengine katika mwaka wa fedha.

iii. Taasisi, Mashirika ya Umma na wananchi kutolipa kodi ya pango la ardhi na maduhuli yatokanayo na ardhi kunaathiri kwa kiwango kikubwa makusanyo yatokanayo na sekta ya ardhi. Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Kuhuisha taarifa katika kanzi data (data base) za taasisi na wamiliki wa viwanja, kuainisha wadaiwa sugu na kuwapa ukomo wa muda wa kulipa madeni yao ili wawajibike ipasavyo;

b) Kubuni mbinu mahususi za kuleta muamko wa ulipaji kodi kwa wananchi na Taasisi kwa ujumla. Hii ni pamoja na kutoa elimu ya mlipa kodi, kuboresha mfumo wa makusanyo na kurahisisha

zoezi la ulipaji kodi kwa njia ya simu za viganjani sambamba na kuwakumbusha wananchi madeni kupitia simu za viganjani,

iv. Halmashauri kutobakiwa na asilimia 30 ya makusanyo *(retention)* kumeathiri utendaji kazi wa Halmashauri. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali ipitie maamuzi yake ili kufikiria upya namna ya kuziwezesha Halmashauri kubakiza sehemu ya makusanyo yao ili kuziwezesha kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kwa wakati.

v. Upungufu wa rasilimali fedha na vitendea kazi katika Wizara ya Ardhi kwa Mwaka 2022/2023 umesababisha mradi wa Kupanga Kupima na Kumilikisha (KKK) kutotekelezwa kwa kasi na kuzifikia halmashauri nyingi nchini, jambo linalochangia ongezeko la makazi holela. Serikali iharakishe mchakato wa kuanzisha mfuko wa maendeleo ya sekta ya ardhi na nyumba ili kuongeza raslimali fedha kwa ajili ya programu ya KKK na hivyo kuwezesha Halmashauri kutokomeza makazi holela.

vi. Kasi ndogo ya ulipaji wa gharama za mashamba na viwanja kwa wananchi waliopewa viwanja na mashamba katika Programu ya Kupima, Kupanga na Kumilikisha (KKK) kunasababisha Halmashauri kushindwa kukusanya mapato ipasavyo na kuweza kurejesha mikopo kwa wakati. Kamati inashauri Serikali ihamasishe Halmashauri kuhimiza wananchi kulipa gharama za upimaji wa mashamba na viwanja kwa wakati. Aidha Wizara itoe muda wa ukomo kwa wananchi ambao hawajalipia gharama hizo na iwapo watashindwa warejeshe mashamba na viwanja kwa Halmashauri husika ili yagawiwe kwa wananchi watakaoweza kulipia kwa wakati.

vii. Gharama kubwa za kutengeneza huduma za maendeleo kama miundombinu, maji na umeme katika miradi ya KKK zinasababisha gharama za mradi kuwa za juu na kusababisha wananchi wengi kushindwa kulipa kwa wakati. Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maji, na Wizara ya Nishati ione namna bora ya kupeleka huduma za maendeleokatika maeneo ya miradi hiyo ili

kupunguza gharama na hivyo kuwawezesha wananchi kupata viwanja na mashamba kwa gharama nafuu.

viii. Ufinyu wa bajeti unaosababisha kutolewa fedha kidogo kwa ajili ya Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka Kitaifa unadhoofisha kasi ya uwekaji wa alama za mipaka baina ya nchi yetu na nchi jirani. Kamati inashauri Serikali kutoa fedha za kutosha katika mradi huu ili kuuwesha kutekelezwa kwa kasi.

ix. Ukosefu wa miundombinu ya kutosha katika maeneo ya mipakani kunasababisha Wizara kushindwa kusafirisha vifaa na kuchelewesha utekelezaji wa kazi ya uimarishaji wa alama za mipaka kwa wakati. Kamati inashauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha ili kujenga barabara za mipakani kwa lengo la kuwezesha zoezi la uimarishaji wa alama za mipaka na kuimarisha shughuli za ulinzi na usalama katika mipaka yetu.

x. Uelewa mdogo wa wananchi waishio mipakani unasababisha kuongezeka kwa migogoro ya ardhi baina yao na kuchelewesha shughuli za maendeleo. Kamati inashauri wizara kutoa elimu kwa wananchi waishio mipakani ili kupunguza migogoro na kusogeza huduma za maendeleo kama maji, barabara n.k

xi. Uvamizi wa maeneo ya mipakani unaofanywa na wananchi umesababisha wananchi kujenga makazi ya kudumu na kuendesha shughuli za kilimo na hivyo kuharibu alama za mipaka. Kamati inashauri Serikali kupitia kuzipitia sheria za mipaka na kuzisimamia kikamilifu ili kuhakikisha wananchi wanazitekeleza ili kuwezesha usalama wa mipaka yetu na nchi jirani.

xii. Changamoto za kimfumo zinazoukabili mfumo unganishi wa taarifa za ardhi wa kielektroniki (ILMIS), zinachelewesha upatikanaji wa hati miliki za kielektroniki na kupunguza mapato yatokanayo na umiliki wa ardhi nchini. Kamati inashauri Serikali kuangalia upya mfumo wa ILMIS wa awali wa Dar es Salaam na Mfumo mpya wa Dodoma ili kuleta tija ya uanzishaji wa mifumo hiyo.

## 4.2 Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

i. Kamati imebaini kutokuongezeka kwa fedha ya maendeleo iliyotengwa kwa ajili ya Tume kwa mwaka 2022/23 na 2023/24 kunaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa chomho hiki. Kamati ilitarajia mabadiliko ya ongezeko la makadirio ya bajeti ya maendeleo kwa shilingi 4,000,000,000 kutoka pale ilipokuwa katika mwaka wa fedha 2022/23 na kupelekea makadirio ya 2023/24 kufikia kiasi cha shilingi 5,410,000,000. Kamati inashauri ifuatavyo:-

a) Serikali iongeze fedha za maendeleo kwa Tume katika mwaka wa fedha 2023/2024 ili kukiwezesha chombo hiki kutekeleza kazi zake kwa ufanisi.

b) Serikali ihakikishe inatimiza makubaliano yanayofikiwa baina yake na Bunge ili kutokwamisha utendaji wa taasisi zake.
Mfano kutoipatia Tume ongezeko la shilingi 4,000,000,000/= zilizoahidiwa ni kutokutimiza makubaliano baina ya Serikali na Bunge.

ii. Upungufu wa rasilimali watu unadhoofisha utendaji kazi wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Kamati inashauri Serikali ikamilishe kushughulikia Ikama za watumishi 79 wanaohitajika ili kuongeza kasi ya utendaji wa tume. Aidha Serikali iiwezeshe tume kupata vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

iii. Malimbikizo ya madeni ya kodi za nyumba na ardhi kutokana na mikataba iliyopitwa na wakati yameathiri makusanyo ya maduhuli na kupunguza ufanisi wa majukumu ya Tume. Kamati inashauri Serikali kuhuisha mikataba ili kuwasaidia wadaiwa kulipa madeni yao kwa wakati na hivyo kuisaidia Tume kukusanya kulingana na matarajio.

iv. Tume iongeze wigo wa kuhamasisha wadau wa kimkakati kushiriki katika kuchangia shughuli za upangaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini kwa lengo la kuinua makusanyo ya maduhuli yatokanayo na sekta ya ardhi na kuongeza kasi ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa namna ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa weledi na umakini mkubwa na kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya wizara hii hadi kukamilika kwa taarifa hii. Kwa umuhimu wake, ningetamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kuwataja kwa majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Wajumbe ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Muntazar Giga, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Shaabani Omar Shekilindi, Mb
4. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb
5. Mhe. Innocent Seba Bilakwate, Mb
6. Mhe. Ester Lukago Midimu, Mb
7. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
8. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb
9. Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb
10. Mhe. Neema William Mgaya, Mb
11. Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb
12. Mhe.Nancy Hassan Nyarusi, Mb
13. Mhe. Festo Richard Sanga , Mb
14. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb
15. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
16. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb
17. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb
18. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
19. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb

20. Mhe. Munira Mustafa Khatib, Mb
21. Mhe. Dkt. Florence G. Samizi,Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Dkt. Angeline Sylvester Mabula (Mb), na Naibu Waziri, Mhe. Geofrey Mizengo Pinda (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa kwa kamati ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Sanga, akisaidiana na Naibu Katibu Mkuu Ndg Lucy Kabyemera, kwa ushirikiano na mchango wao kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

Mwisho lakini si kwa umuhimu, kwa namna ya pekee nammshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, ndc, kwa kuongoza vyema uratibu wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Chacha Nyakega na Ndg. Haika Mtui wakisaidiwa na Ndg. Pauline Mavunde, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuhakikisha maandalizi ya taarifa hii yanakamilika kwa wakati.
Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha.

Timotheo Paul Mnzava, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**
25 Mei, 2023

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava kwa kuwasilisha Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza uchangiaji naomba nitoe matangazo tena ya wageni ambao wameingia tena hapa katika Bunge letu.

Kwanza wageni waliopo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao wako kwenye Jukwaa hilo la Spika wadau wa Sekta ya Ardhi ambao ni wawakilishi wa kampeni za upangaji, upimaji ardhi na uendelezaji milki. Wageni wa Mheshimiwa Mabula hao wamekaa upande ule kule. Karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa Mikoa, bado hawajaingia. Kuna Wasajili Wasaidizi wa Mabaraza wa Kanda, nao bado hawajaingia. Watumishi nane wa Idara ya Ardhi Manispaa ya Ilemela wakiongozwa na Ndugu Esau Mwakatumbula, wale pale; karibuni sana watumishi wa Idara ya Ardhi kule Ilemela. *(Makofi)*

Tuna Viongozi wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya ya Ilemela wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Ndugu Yusuph Bujiku, karibuni sana wageni wetu wa Halmashauri Kuu ya CCM kutoka Ilemela. *(Makofi)*

Wageni wote wa Mheshimiwa Angeline Mabula na wa Wizara ya Ardhi wanaweza kusimama kwa pamoja kama wapo wengine. Basi karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Waziri wetu wa Ardhi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Wageni 10 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Viongozi na wanafunzi wanaosoma katika Chuo cha Elimu ya Biashara

*(CBE)* kutoka Matawi ya Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya na Mwanza. Wale pale, karibuni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati, Ndugu Liberata Stanslaus kutoka Bukoba Mjini; hajaingia bado. Hapana yupo, haya karibu. *(Makofi)*

Kuna wageni 10 wa Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma, Wachungaji kutoka Hanang' Mkoa wa Manyara, wale pale, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Samweli. *(Makofi)*

Wageni 20 wa Mheshimiwa Mussa Sima ambao ni viongozi wa CCM Wilaya ya Singida Mjini na Wenyeviti wa CCM Kata kutoka Singida. Wale pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna mgeni wa Mheshimiwa Sylvia Sigula kutoka Jijini Dar es Salaam, yule kule juu, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Zaytun Swai, wawakilishi waliokuwa wafanyakazi wa *Kiliflora* kutoka Arusha; karibuni sana wageni wetu wote ambao mmeingia muda huu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza sasa michango kwa Wizara hii ya Ardhi. Nitaanza na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuata Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Kwa niaba ya Wananchi wa Tarime Vijijini, Wananchi wa Tarime na Wananchi wa Mkoa wa Mara tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupeleka shangwe kubwa katika Mkoa wa Mara, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Mungu ambariki sana aendelee kuwa na sikio la kusikia kilio cha wanyonge na hasa kutoka Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara ya Ardhi ina changamoto nyingi na niwe mkweli, mimi ni miongoni mwa watu ambao wana migogoro mingi yaani kule Mkoa wa Mara lakini na mikoa mingine. Kwa hiyo la kwanza nimwombe Mheshimiwa Waziri awe na ngozi ngumu katika eneo hili. Ameshikilia kura za Chama cha Mapinduzi, ameshikilia kura za Mheshimiwa Rais, ameshikilia kura za sisi Wabunge kurudi hapa Dodoma kuendelea kukalia kwenye viti hivi. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri ni lazima ajipange vizuri katika eneo hili. Huo ndiyo ukweli wa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba yetu ya Mwaka 1977, Toleo la Mwaka 2005 Ibara ya 8 naomba ninukuu Ibara ya 8(1).

"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hiyo:-

(a) wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata mamlaka na madaraka yake toka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii;

(b) lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi;

(c) Serikali itawajibika kwa wananchi;

(d) wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hii ibara kuonyesha kwamba kitendo cha kutotatua migogoro vizuri ya ardhi kinawakwaza wananchi walio wengi na hao wananchi wanaipenda Serikali yao. Maendeleo yote ambayo yanafanyika na Mheshimiwa Mama Samia ni kwa ajili ya wananchi. Mheshimiwa Waziri katika eneo hili, lazima ibara ya 8 hii niliyosoma izingatiwe sana. Maana yake katika mipango yote ya Serikali ya ardhi lazima tuangalie haki za watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika maeneo mengi kule Tarime, Wizara ya Ardhi ndiyo inamiliki Mthamini Mkuu wa Ardhi. Akishafanya tathmini ya ardhi, wanawasiliana na Wizara ya Madini, halafu mgodi unaambiwa kwamba ulipe. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, kitendo cha watu wa Tarime maeneo ya mgodi chini ya ardhi kuna dhahabu, wanalipwa ekari moja shilingi milioni tano, bei ambayo hata ukienda mtaani Tarime huwezi kununua ardhi ekari moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hicho kinafanya tufikirie zaidi, kwa nini eneo ambalo chini kuna dhahabu unalipa ekari moja shilingi milioni tano sawasawa na ardhi ambayo unaweza kufidia ujenge choo au ujenge zahanati? Wizara haioni kuna sababu ya msingi sana kuangalia viwango vipya vya bei ya ardhi na hivyo ndiyo vinapelekea migogogro mingi kwa sababu wananchi wanajua ukishatoa ardhi yetu unaenda kuchimba dhahabu au vito vingine na unapata fedha nyingi zaidi. Hili ni vizuri pia likaangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile migogoro ya ardhi, Waheshimiwa Wabunge nataka nishauri, ukisikiliza vizuri Hotuba ya Kamati yetu wanasema fedha zilizotengwa kwenda kutatua migogoro ni kidogo ukilinganisha na fedha ambayo imepelekwa kwenda kulipana posho, *allowance,* mafuta na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwashawishi Waheshimiwa Wabunge, katika eneo hilo Mheshimiwa Waziri lazima atuambie tubadilishe sisi hapa ndiyo Watanzania. Fedha nyingi iende kutatua migogoro ili uchaguzi ujao Chama Cha Mapinduzi kisiadhibiwe ili uchaguzi wa Mama Samia 2025 tupate ushindi wa kishindo. Hatuwezi kushinda vizuri uchaguzi kama watu wanaenda kwenye uchaguzi na vinyongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna taarifa, Kamati ilimwita Mheshimiwa Waziri na Mwenyekiti hapo yupo, wametusomea Waheshimiwa Wabunge, tusome Taarifa ya Kamati, tuunge mkono Waziri atueleze, kwa nini aliamua kupanga fedha kidogo ya kwenda kutatua migogoro kwenye majimbo yetu na fedha

nyingi kwenye safari na posho? Hilo ni muhimu sana tukaambizana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hii migogoro kwa mfano kule kwangu, leo tunapozungumza ukizungumza habari ya Komarela, Kewanja na Nyamichere, Mthamini Mkuu wa Serikali ameenda ametoa notisi kwamba watu eneo hili msiendeleze, halafu baada ya muda fulani anaambiwa kwamba usilipe. Wakati fulani wanafanya tathmini ambayo wanalalamikiana. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri akijipanga vizuri maana yake kwangu na Wabunge wengine migogoro ya fidia itakwisha. Kwa sababu watu wake ndiyo wanafanya kazi ya uthamini katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina migogoro ya ardhi ile ya Komarela na mgodi, nina mgogoro wa ardhi Mheshimiwa Waziri wa siku nyingi kwa Korutambe na Remagwe, nina mgogoro wa ardhi pale Kebweye na Kyoruba, nina mgogoro wa ardhi Mwito na Msege, nina mgogoro wa ardhi Mwito na Gibaso, nina migogoro mingi ambayo hii inapelekea amani isiwepo na watu wanapoteza imani. Mheshimiwa Waziri anayo kazi hiyo, Mheshimiwa Rais amempa kipande muhimu kweli kweli, awe mpole apokee maoni, awe *humble,* asikilize na atatue migogoro na timu yake aiambie kwamba kule kuna wananchi ambao lazima wasikilizwe vizuri ili kuondoa changamoto tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri, katika utatuzi wa migogoro wamesema kamati hapa, tunajua kuna Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, lakini vile vile tuna Sheria ya Fidia ya Ardhi ya mwaka 2016 na Kanuni zake za mwaka 2018, lakini ushirikishwaji. Wasiende kusoma *document* kama zilivyo kwa wananchi wa kawaida, wanawaamrisha. Waende kwenye vijiji, waite Viongozi wa Vijiji, Wabunge na Madiwani watushirikishe tuwape maoni. Tukienda kutatua mgogoro hatumwachii Waziri peke yake, tunataka mgogoro ukitatulika, Serikali inufaike na wananchi wanufaike na amani itawale na maendeleo yapatikane katika eneo husika, tusiamrishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Kamati kwamba jambo hili wameliona na ndicho kilichofanyika katika maeneo mengi sana, lakini pia kamati imeomba kwa kuwa na mimi naunga mkono, Taarifa hiyo ya Mawaziri nane ije hapa Bungeni, kila mtu aone eneo lake walipitia wapi, *GN* inasema nini, tusome tuweze kuwashauri. Hatuwezi kuwa Wabunge tena sehemu ya kulalamika, wakati sisi ndiyo wasemaji kwa niaba ya Watanzania ambao walituamini kuja hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri, walipokuja Tarime kule, msoma ramani wake alisema ile *GN* ya mwaka 1968 ina ramani *(surveyed map)* ya mwaka 1968. Wakasema hii ramani kwa haraka haraka tumeacha kwenye gari, tukienda kwenye mkutano tutawapa. Inaombwa tangu siku ile mpaka juzi, mpaka jana, mpaka leo haipo. Tunahitaji Tarime pale kwenye ile migogoro ya ardhi tupate *GN* ile tunayo ya mwaka 1968, tupate ramani, *(surveyed map)* ya mwaka 1968 mjadala uanzie hapo ili kuweza kuondoa mzizi wa fitina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mapendekezo hapa kwa Mheshimiwa Waziri. Migogoro ya ardhi iliyopo, ukienda Nanyumbu kuna mgogoro, ukienda Kiteto kuna mgogoro, ukienda sijui wapi kuna mgogoro. Mkoa wa Mara kuna mgogoro wa ardhi pale Rorya, Serengeti, Bunda pale Nyatwali, Tarime Mjini na Vijijini. Hii migogoro huu ni Mkoa mmoja wa Mara. Sina taarifa nzuri ya mikoa mingine. Nataka nimwombe tena Mheshimiwa Waziri, shemeji yangu, mke wangu ni Msukuma, Waziri mwenye nguvu kubwa tunaomba sasa aonyeshe Udaktari wako kwenye kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatamani tunapoenda kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa atumalizie migogoro ya ardhi kwa watu wetu. Tunatamani uchaguzi wa mwakani tusihukumiwe kwa sababu ya migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuombe pia kwenye kiti hicho, ni vizuri Wabunge tusome Ripoti ya Kamati hii, tuisimamie Serikali, tuishauri vizuri. Mheshimiwa Rais ameshampa dhamana Mheshimiwa Angeline Mabula kutatua migogoro ya ardhi.

Naomba Mheshimiwa Waziri avae kiatu kimtoshe afanye kazi ya kutatua migogoro hii. Tumechoka kulalamikiana na kuja kulia katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja hasa Ripoti ya Kamati ije Bungeni tujadili ili Watanzania wapate amani ya kwao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Waitara. Nilimtaja Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, atafuata Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mheshimiwa Mohamed Monni na Mheshimiwa Halima Mdee wajiandae.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata fursa. Nami niungane na kaka yangu Mwita Waitara kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Tunaona nia ya dhati kabisa ya Mheshimiwa Rais wetu kuhakikisha kwamba anamaliza suala la migogoro ya ardhi ndani ya Taifa hili. Nia hiyo tunaona tafsiri nzuri kabisa ya Mheshimiwa Rais, hataki migogoro ya ardhi ndani ya Taifa, lakini tatizo linakuja kwa wasaidizi wake huku chini kwenye tafsiri ya nia njema ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tarehe 18 mwezi wa kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika pale Mbarali. Alifika pale Kapunga, Mbarali na Mheshimiwa Waziri alikuwepo Mama yangu Dkt. Angeline Mabula. Aliona kiu ya Wanambarali kutaka kujua hatma ya mgogoro huu. Wanambarali walijitokeza kwa wingi pamoja na shughuli za shamba hawakwenda ili wasikilize Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alituambia kati ya migogoro ya vijiji 34 ambavyo tumedumu navyo Mbarali kwa miaka 15, vijiji 29 vitarudi kwa wananchi na vijiji vitano vitabaki kwenye hifadhi. Sasa kinachoendelea kule Mbarali tunaona watu wa *TANAPA* wanaendelea kuweka *beacon* kila mahali. Hata vile vijiji ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu alitamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mama yangu Mheshimiwa Angeline, kesho anavyokuja kufanya majumuisho hapa, tunachotaka sisi Wanambarali na Wanambarali wamesema kesho watakuwa kwenye *TV* watashika kalamu na karatasi wajue kijiji kwa kijiji, vipi vijiji hivyo 29 ambavyo vinabaki kwa wananchi na vijiji vitano vipi ambavyo vitabaki hifadhini? Kesho tutamsikiliza mama yangu, la sivyo kesho, nitaondoka na shilingi ya Mama yangu mpendwa, asipotutajia vijiji hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ni salamu za Wanambarali, kesho tunamsubiri mama yangu Mheshimiwa Waziri hapo, atuambie kwa majina kijiji kwa kijiji na vinavyoondoka ni vipi na vinavyobaki ni vipi?

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi? Mheshimiwa.

**TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Anachokizungumza Mheshimiwa Bahati ni sahihi kabisa. Licha ya nia njema ya Serikali ya kutatua mgogoro ambao uko Mbarali, kumekuwa na changamoto ya uwekaji *beacon* kiholela kwenye maeneo ambayo wananchi wanafahamu kabisa Serikali iliwazuia. Kwa hiyo ni vyema Serikali ikaenda kuangalia, kinachozungumzwa hapa Bungeni na kinachofanyika nje, ni vitu viwili tofauti. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili kaka yangu Festo naye ni muhanga kwa sababu Mbarali na Makete ni watu wale wale wanaingiliana. Kwa hiyo anaijua vizuri hii historia ya kule Mbarali. Namshukuru sana *my brother. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, inasikitisha sana kuona kwamba mpaka sasa hivi 25% tu ya ardhi ya Tanzania

ndiyo imepimwa. Hii migogoro tunayoimba kila siku humu Bungeni ni kwa sababu tunaenda pole pole sana kwenye kupima ardhi ya Taifa hili. Hivi kwa mfano, kweli tangu tumepata uhuru, leo hii tumepima 25% tu ya ardhi, tunahitaji miaka 180 kumaliza kupima nchi hii, kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo sawa, teknolojia zimekua. Ujuzi wetu umeongezeka, kwa nini hawapimi ardhi? Watu wanashindwa kuendelea, leo hama hapa, ondoka hapa, yaani fujo tu, kwa sababu hawapimi ardhi. Wapime ardhi ya Taifa hili tuondokane na migogoro ya kila kukicha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wanawekeza watu hapa, walime, kesho ondokeni hapa nenda hapa, wamekaa miaka 70, wamezika babu, vijukuu, kesho ondokeni hapa, tunakuwaje hivyo? *Why*? Kwa nini hatupimi ardhi yetu na wanaangalia kabisa taarifa za Mtakwimu wa Serikali. Sasa hivi…

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**TAARIFA**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka nimpe taarifa dada yangu Bahati kwamba anachosema ni kwamba itatuchukua muda mrefu kupima ardhi. Leo mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji vyetu, mfano, Wilaya ya Ikungi, katika vijiji vilivyopo 101, *it's only* vijiji vitano tu ndiyo vina mpango wa matumizi bora ya ardhi. Kwa hiyo tusitegemee kwamba bila kupima tutamaliza migogoro. Kwa hiyo migogoro itaendelea, dawa ni kupima ardhi ya nchi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazipokea taarifa zote, ni kweli kabisa hatuko *serious* kwenye upimaji wa ardhi ya Taifa letu na hatuwezi kumaliza migogoro ya Taifa hili

kama hatupimi ardhi. Kwanza tunawarudisha watu nyuma kimaendeleo kila siku, leo watu wanalima hapa, kesho ondoka hapa nenda hapa, hatuwezi kuendelea kama Taifa. *(Makofi)*

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba ule mradi ambao Mheshimiwa Waziri ameuzungumza hapa ndiyo una lengo la kwenda kutayarisha miundombinu ya teknolojia bora ya upimaji ili tukimaliza kuutekeleza ule mradi, sasa itakuwa ni rahisi kwa kuweka miundombinu bora ya upimaji na tutakwenda kwa haraka zaidi katika upimaji, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bahati unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei hiyo taarifa, yaani kweli leo hii ukaende kupima vitu vya hivyo? Hapana, siipokei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima Wizara iwe *serious* na tuone kwenye mikakati yao wako *serious* kupima ardhi ya Taifa hili. Hivi wenzenu kila siku ni migogoro, kila siku ni migogoro. Mama yangu atakwenda kule, wapime ardhi, matatizo yote haya yatakuwa hamna. Kwa kweli tunaomba wapime ardhi ya nchi hii. Mipango yao hiyo haionyeshi kama kuna uthabiti kabisa na wana malengo la kweli la kutaka kupima ardhi ya nchi hii. Kwa kweli mama yangu Mheshimiwa Waziri ili na apumue, wapime ardhi ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata fursa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo. Nilimtaja Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mheshimiwa Monni na Mheshimiwa Halima wajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati najiandaa asubuhi ya leo kuja kuchangia Wizara hii wezeshi kwa sekta zote za uzalishaji nchini, nilimwomba Roho Mtakatifu anipe hekima, maarifa na busara ili niweze kuwatendea haki Watanzania wote wa nchi hii siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020/2025, nimekuja na hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati anahutubia Bunge. Wakati najianda kuchangia, labda nieleze maeneo nitakayopita, eneo la kwanza ni kuhusu mradi, matumizi ya fedha za mradi wa bilioni 345 ambazo ni mkopo wa Benki ya Dunia, mkopo ambao kila Mtanzania atalipa, mimi nitalipa, wananchi wa Mlimba watalipa na wananchi wa Mlimba wameniambia katika hili hapana, wengine mkikubalia sawa lakini wananchi wa Mlimba wamesema hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni migogoro ya ardhi, eneo lingine ni usimamizi wa watumishi wa sekta ya ardhi na mwisho nitahubiri kidogo injili. Nianze na mradi wa bilioni 345 mkopo kutoka Benki ya Dunia. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kulihangaikia Taifa letu kwa kutafuta fursa mbalimbali huko Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi inasikitisha matumizi yake. Tumeambiwa na Kamati hapa bilioni takribani 46.8 zinakwenda kwa ajili ya uratibu, uendeshaji na dharura, katika Taifa ambalo limepimwa kwa asilimia 25 tu, katika Taifa ambalo lina vijiji takribani 12,318, vilivyopimwa ni viijiji 2,868 tu. Katika Taifa ambalo vijiji ambavyo havina mpango wa matumizi bora ya ardhi ni takribani 9,541, katika Taifa ambalo wananchi wamekuwa wakifa kila siku, watu wanakufa kutokana na migogoro ya ardhi, inasikitisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa dhati maana ukichangia hapa kuna minong’ono huku wanasema huyu

anataka uwaziri kama uwaziri unakuja kwa ajili ya kuchangia acha uje tu! Kama kwa *style* hii acha uje tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *I am not speaking out of nothing, I am speaking on something that I know,* nazungumza jambo ambalo nalifahamu sekta ambayo naifahamu vizuri sana na nime–*practice* sibahatishi kwenye ardhi na nimeweka matokeo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze katika fedha hizi matumizi yake vijiji 500 tu vinakwenda kupimwa na thamani ya kupima kijiji, gharama ya kupima kijiji kimoja ni milioni 12 mpaka Milioni 15, kwa hiyo kwa vijiji hivi vilivyotajwa 500 itatumika fedha bilioni 5.5 tu katika mpango wa fedha bilioni 345 *are we serious? are genuine?* ni kweli tunamsaidia Mheshimiwa Rais? ni kweli *are genuine?* au tunasema tu mdomoni mioyo yetu inakataa, hapana mi bado ni kijana mdogo nategemea kutumikia Taifa langu kwa miaka ijayo. Kwa hiyo *no matter what will happening to me* lakini leo tasema ukweli daima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza hapa nilijaribu kufanya tafiti kidogo nikajiuliza maswali asubuhi…

**MHE. SOUD MOHAMMED. JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. SOUD MOHAMMED. JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu kumpa taarifa Mheshimiwa Kunambi kwamba upimaji wa ardhi ni *process,* siyo kama labda ni upimaji wa ardhi utapima tu mara moja. Kwa hiyo nilikuwa naomba tu kumwambia kwamba upimaji huu ile miundombinu ambayo inakwenda kutengenezwa ina saidia kuweza…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane.

**MHE. SOUD MOHAMMED. JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu kumfahamisha Mheshimiwa Kunambi kwamba ile miundombinu kwamba ambayo itakwenda kutengenezwa katika mradi huu wa uwishaji usalama na rasilimali za ardhi ndiyo utakwenda kusaidia kuweza kuipima ardhi kwa haraka baada ya kwisha kuitaarisha ile miundombinu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godwin Kunambi unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua unapoteza muda kwa mtu ambaye *any way* siipokei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mzaha hapa! Nimefanya hesabu ndogo tu ya kujumlisha na kutoa ambayo kila Mtanzania anaweza kuifanya. Ukipima vijiji 2,000 katika mradi huu fedha hii ya mkopo ambayo kila Mtanzania analipa, vijiji 2,000 thamani yake ni bilioni 30 tu. Ukipeleka bilioni 30 tu, na mimi nakutaarifu Mheshimiwa Waziri nakuja kushika shilingi nataka kuona bilioni 30 inakwenda Tume ya Taifa ya Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijaribu kuangalia Ilani nimesema nimekuja na Ilani naomba niisome, naomba ninukuu Ilani ya Chama cha Mapinduzi Chama changu kwa ufupi Ibara ya 74 Ukarasa wa 120 mwenye Ilani arejee, naomba nisome Chama cha Mapinduzi kimeelekeza Serikali kwa miaka hii mitano kupanga na kupima vijiji takribani 4,131 na Wilaya 54.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fedha hizi unaenda kupima vijiji 500 huu ni mwaka gani huu? Mwaka 2023 bado miaka hii miwili, kutoka 2021 mpaka sasa Wizara wamepima vijiji 618 tutafika lengo hili la Chama? Ndiyo maana nauliza *are we serious? Are we genuine?*

**MBUNGE FULANI:** *No.*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Hapa tunacheza na changamoto za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikajiuliza kuhusu migogoro ya ardhi, nikauliza wenzetu wa jirani wa Uganda hivi kuna migogoro ya ardhi Uganda? Wakasema Hapana, nikauliza Rwanda kuna migogoro ya ardhi? Wakasema hapana. Nikauliza hapa Kenya kuna migogoro ya ardhi? Wakasema Hapana! Migogoro ya Ardhi ni matokeo ya kushindwa kwa sekta nchini, nataka nipigie mstari hapo, migogoro ya ardhi ni matokeo ya kufeli kwa sekta ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi naomba nijielekeze kuhusu wasimamizi wa sekta ya ardhi. Kama kuna eneo Wizara imekosea kuwachukua watumishi kutoka Halmashauri kuwapeleka wakawasimamie mfano, wanasema *TARURA,* wanasema *RUWASA, RUWASA* ni taasisi inayojitegemea ndiyo maana ina *perform, TARURA* ni taasisi inayojitegemea ndiyo maana ina-*perform,* sasa Wizara imechukua tu watumishi mi nadhani basi waanzishe taasisi na wenyewe basi ili wapime na kupanga, iwe mamlaka ya upangaji isiwe tena Halmashauri wanawaonea tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa ya pili dakika mbili, hamna zaidi ya hapo, Mheshimiwa Musukuma.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Utanisamehe sana rafiki yangu Kunambi maana Bunge hili tuko *live calculation* unazozipiga unalipotosha Bunge na Watanzania. Kwa hesabu unazozipiga hata tunatoka kwenye Halmashauri, tunaongoza Halmashauri zetu tunajua tunapima kwa *style* gani, kuna kupima kwa kudhulumu na kuna kupima kwa kulipa haki za watu. Sasa *calculation* unazolieleza Bunge hapa na bahati nzuri wewe ulikuwa Mkurugenzi hapa na mimi nimewekeza hapa nime-*deal* na wewe, nakufahamu na Wabunge wote wako hapa, kwa *style* ya wewe uliyoifanya hapa tukiruhusu hizo hesabu

zako Waziri akazichukua hii Tanzania tutachinjana kwa ajili ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunambi, unapokea hiyo taarifa?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa. Ninachosema ni kwamba kinachofanyika sasa unasema mamlaka ya nidhamu ni Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Mtumishi yuko Kakonko, mtumishi yuko Mlimba hivi utendaji kazi wake kule anajuaje? Anasema kuna Kamishna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamishna yuko ngazi ya Mkoa na niseme kuna mgomo Mheshimiwa Waziri kama hujui nakusaidia, kuna wale Watumishi mliyowashusha vyeo Wakuu wa Idara, mtu alikuwa na mshahara alikuwa na mshahara 3,400,000 leo hii anakuwa Afisa Ardhi wa kawaida, wamegoma kwenye Halmashauri huko. Ndiyo maana hilo nenda kafanye uchunguzi nakusaidia tu na uchukue tu *positive* mchango wangu, nakupa tu hiyo siri kuna mgomo unaoendelea, wale watumishi mliowashusha vyeo huko kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyewkiti naomba nihitimishe, nahitimisha kwa mahubiri. Ukisoma…

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba dakika moja tu.

**MWENYEKITI:** Nusu dakika.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Dakika mbili tatu. Mtume Paulo kwa Wakorintho aliwahi kusema habari hii kwa Wakorintho jamani tusikilizane kidogo "Nikiitazama Dunia ni ubatili mtupu" lakini ndugu zangu kizazi chetu ni cha nne, uhai wetu ni miaka 70 jamani tafuteni kwanza ufalme wa mbingu mengine mtazidishiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Quran tukufu inasema maneno haya; *"Quburwa Twanii'h ninal manii"* kuipenda nchi yako ni sehemu ya imani Watanzania tuwe wazalendo kwa Taifa letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godwin Kunambi, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Mohamed Monni, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtumvu ajiandae.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara muhimu sana ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujalia afya njema na ametujalia uhai tupo hapa leo. Jambo la pili namshukuru Mheshimiwa Rais kwa hakika anayo dhamira njema, ana nia njema. Sisi ambao tunatoka maeneo ambayo yana migogoro wanafahamu kwamba iliteuliwa Kamati ambayo ina Mawaziri Nane ambao wanashuhulikia huu mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kidogo sana kuhusu mgogoro na watu Chemba nisiposimama kuongea kwenye Wizara hii watanishangaa sana na inawezekana nikapoteza kabisa asilimia 40 ya kura zote. Kwangu kuna changamoto moja ndogo sana lakini shida kubwa ya changamoto hii ni utashi wa Viongozi tuliyonao. Hii naomba niseme wazi kama kumsema hivyo nakosea potelea mbali lakini nataka niseme ukweli. Tuna mgogoro ambao umeanza mwaka 2014, mgogoro huu umeacha wakulima wananchi wangu 1,168 bila mashamba. Ni jambo la ajabu sana kwamba unakuta watu wana mashamba alafu unawaondoa tangu mwaka 2014 mpaka leo wanaendelea kuzurura haujui wanaishi vipi? Ni jambo la ajabu na haliwezi kutokea sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha mgogoro huu ndiyo maana nasema shida ni viongozi. Chanzo cha mgogoro huu ilikuwa ni ku–*review* mipaka, wakati wana – *review* mpaka kati ya Chemba na Kiteto maeneo ambayo yalikuwa ya Kiteto yalirudi

Kondoa wakati huo, sasa hivi ni Chemba. Baada ya kurudi Kondoa ambaye ni Chemba mashamba yao yakabaki Kiteto maana yake ni nini? maana yake kiijiji baada ya kuweka mipaka mipya wananchi wangu wamebaki na kijiji lakini mashamba yao yamebaki Kiteto na sisi wote tunafahamu, kwamba mipaka ya utawala haikufanyi upoteze haki yako ya shamba lako. Hii inafahamika lakini cha ajabu wananchi wale walilazimishwa na kunyang'anywa mashamba yao kwa sababu tu sasa mipaka ya kiutawala wamerudi huku Chemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la ajabu sana. Ninayo hukumu ya Mahakama hapa, wameenda Mahamani wameshinda, tena Mahakama ya Wilaya ya Kiteto kule kule lakini mpaka leo bado watu wamebaki hawana mashamba. Sasa mimi namuomba Waziri kama kuliko nibaki na watu ambao hawana mashamba naombeni kile Kijiji cha Oruboroti kichukeni kiwe Kiteto ili mashamba yao wabaki nayo, kuliko kubaki na watu 1,168 hawana mashamba maana yake wamekuwa tegemezi kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nimekuwa nikipata ushirikiano sana wa Viongozi wa kutoka Kiteto wenyewe, ninayo barua ya Waziri wa TAMISEMI wakati huo, ambayo inamuelekeza Mkuu wa Mkoa wa Manyara na Dodoma kwamba kwa sababu ya ku– *review* mipaka hiyo isiwe sababu ya wananchi wa Oruboroti kupokonywa mashamba yao, mipaka hiyo ni ya kiutawala tu. Barua hiyo haijawahi kufanyiwa kazi ninayo hapa Mheshimiwa Waziri, matokeo yake watu wangu wakienda kulima wanashikwa, wengine wanapelekwa, *imagine* mtu anachukuliwa Kiteto anapelekwa kufunguliwa kesi Arusha badala ya Manyara, huko anabambikiwa kesi ya nyara za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimuombe sana mimi nina uhakika yeye anaweza kutusadia, jambo hili limekuwa linaumiza sana hasa kwa watu wa Chemba. Siyo hivyo tu, nataka nikuonyeshe jambo la ajabu sana, baada ya hukumu ya Mahakama kutoka Mkuu wa Wilaya ya Kiteto ninayo barua hapa, alimwandikia Afisa Tarafa wa Makame ambapo ndiyo mashamba yapo. Kwa sababu wananchi hao wameshinda

kwenye kesi yao Mahakamani, warudishiwe mashamba hayo ndani ya wiki saba. Mkuu wa Wilaya anamwagiza Afisa Tarafa wake na hakuwahi kutekeleza mpaka leo, sasa hii ndiyo nchi ya namna gani? Hii ndiyo nchi ya namna gani? wakati alikuwa ana uwezo tu wa kumpigia simu tekeleza hilo mara moja, tafsiri yake ni kwamba, yawezekana haya maandishi lakini utashi wao wa kutatua changamoto hii haipo, kwa hiyo nikuombe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana pia tulikuwa na Mkuu wa Mkoa, Mbunge mwenzetu hapa anaitwa Mnyeti na wakati huo Mkuu wa Wilaya pia alikuwa Mbunge hapa, nakumbuka majibu waliomjibu maana Mnyeti alimwambia kwa nini unachukua mashamba ya watu wa Chemba? Mkuu wake wa Wilaya ambaye ni Mbunge sasa hivi ananisikiliza kasema hao watu ni wa Chemba lakini, akamwambia Chemba ni Rwanda? Wewe una akili gani? Nakumbuka nilikuwepo, nakushukuru sana Mheshimiwa Mnyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo unaweza ukaona sababu ya migogoro hii ni sisi viongozi wenyewe. Mimi nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, juzi kama siku tatu, nne zilizopita wameenda tena kubandika maeneo ya Chemba. Kuna changamoto nyingine ni ya ajabu sana, vipo vijiji ambavyo viko Wilaya ya Chemba lakini vinaitika Kiteto kwa sababu tu wao ni Wamasai kwamba wako tayari kwenda kwa Wamasai wenzao. Kitongoji kipo Chemba lakini wao michango yote kila kitu wanafanya kwenye Wilaya ya Kiteto na ukienda kuwagusa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niombe sana, kwa sababu kama ni suala la ku– *review* mipaka na *beacon* tayari limefanyika, sasa sijui tutumie maarifa gani? mimi nikuombe sana Mheshimiwa Waziri hebu upate fursa na wewe ukatembee, safari hii Mheshimiwa Waziri eneo lile watu wamekufa mara kadhaa, naiona hali, naliona joto lilivyo, ninaona kabisa hali ilivyo kwamba mvua zikinyesha mwaka huu hali itakuwa tete sana. Sasa niwaombe sana, niwaombe sana hebu ifikie mwisho wa mgogoro huu kwa sababu kama ni Mahakamani tumeenda tumeshinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo limekuja pale Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri kuna watu wanaitwa *WMA, WMA* wamekuja wamekuta watu wana mashamba, wameongea na kijiji, kijiji hakikuwahi kulipa fidia wala hiyo *WMA* hawajawahi kulipwa fidia wanawaondoa wananchi wangu na sasa hivi wameendelea kujitanua kwenye maeneo mengine kumekuwa na mgogoro mkubwa sana. Migogoro hii ya ardhi inamaliza ndugu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wiki mbili zilizopita amekufa Mwenyekiti wangu wa kitongoji, kwa sababu ya mgogoro wa ardhi, wamemuua kuna mgogoro wa ardhi pale wameenda wakamuua na sasa hivi kesi inaendelea Mahakamani. Kwa hiyo unaweza ukaona namna ambavyo kuna changamoto kubwa hii. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri nimesimama hapa kwa ajili ya kuongea hili tu, na nimesema kwamba kama kuna sababu yoyote au kama ni lazima wale wananchi wa kijiji cha Oruboroti kurudi Kiteto ili mashamba yao yabaki naomba wawachukue, ili mradi warekebishe beacon kuliko kukaa na watu ambao hawana mashamba na kila siku wanatuletea shida. Mimi nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, mimi mchango wangu leo ulikuwa huo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo wanashukuruni sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Monni, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi leo nitajikita Jimbo la Kawe zaidi, kwa sababu naona kama Kawe kuna kaombwe hivi, sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri unisikilize kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika ukurasa wako wa 78 umezungumzia miradi ya 711 na umesema kwamba utakamilisha miradi mikubwa iliyosimama ya Kawe 711 na *Golden*

*Premium Residence*. Vilevile wataendeleza mradi wa *Samia Housing Scheme* Kawe. Sasa nilitaka unipe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu *seven eleven one* ilikuwa na thamani ya Shilingi bilioni 142, na *Seven eleven two* Shilingi bilioni 103. Nilitaka kufahamu ukamilishaji una lengo la kukamilisha asilimia 100 ama kiwango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka ulioishia Juni, 2018, alisema wazi kabisa kwamba kutokana na miradi hii kukwama *likelihood* 2018 nazungumza; *likelihood* ya Serikali kupata hasara ya Shilingi bilioni 99.9 kipindi kile, lakini kuna hasara nyingine ya Shilingi bilioni 2.6 kwa sababu kuna wananchi ambao tayari walikuwa wameshalipia yale majengo lakini hakuna kilichoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri akija naomba anijibu kwa ufanisi kabisa ili tuweze kujua ni hasara kiasi gani ambayo nchi na Serikali imepata kutokana na mradi huu kukwama toka mwaka 2017 mpaka sasa na hasa ukizingatia kwamba Shirika la Nyumba la Taifa lilikuwa linatumia mikopo ya kibiashara kwenda kukopa ili kufanya hii kazi. Uzembe huu na hasara hii kwa nchi imetokana na Serikali kuinyima kibali kwa miaka zaidi ya saba kwenda kukopa wakati ikijua hili jambio ni la kibiashara. Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni migogoro ya ardhi. Nashukuru leo amezungumza Mwenyekiti wa Kamati, naunga mkono hoja yake. Mwaka jana 2022 nilisema hapa, migogoro ya ardhi nchi hii, Mawaziri na watendaji wa Serikali, kwenu ninyi mnatuimia kama dili la kuzunguka kufanya ziara. Hamna dhamira hata kidogo ya kuhakikisha nchi yetu inapangiwa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili ifike kipindi tuachane na migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022 tuliambiwa kuna mkopo tukajinasibu sana. Leo Kamati inatuambia eti katika ule mkopo shilingi bilioni 47 ni ya posho na uratibu na kuzurura zurura

huko, halafu Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, wanapewa chini ya shilingi bilioni 10!

*This is nonsense! (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, *this is lack of seriousness*. Haya mambo yanauma. Jimbo la Kawe Mheshimiwa ninakuomba sana, tuitatue migogoro ya ardhi kwa Mwenyekiti wa lile Jimbo. Nimeondoka siku mbili tatu, kunalipuka. Kata ya Mabwepande, Mtaa wa Mbopo, kwa ndugu yangu kule wa Kibamba, Tegeta A, Isumi, eneo lingine la Madale Jimbo la Kawe, kuna mgogoro unaofukuta wa huyu *mdudu* anaitwa *DDC*. **[Neno "mdudu" Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina nyaraka hapa Mheshimiwa Waziri toka mwaka 1980 eneo ambalo *DDC* inadai ni la kwake lilikuwa ni eneo la Kijiji, nyaraka zote ziko hapa. Kijiji kiliwaambia kitawapa hekta 500 kwa masharti kadhaa. *DDC* wakaenda wakakaa kikao na Wizara ya Ardhi, wakatengenezea hati mezani, wakaja na hati ya hekta 5,000. Ndiyo maana leo tunatoka kwenye Kijiji cha Jimbo la Kawe cha Mabwepande, tunaenda kwenye mtaa mwingine wa Mabwepande wa Kata ya Kawe ambao…

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, napata mzuka yaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda kwenye kata nyingine ya Jimbo la Kawe inaitwa Kata ya Wazo Mtaa wa Madale. Mabwepande ilipo ni kata tofauti, Wazo ilipo ni kata tofauti. Tunaenda kwenye Jimbo la Kibamba la ndugu yangu kata ya Goba. Taasisi za Serikali, hiki *kimdudu* kinaitwa *DDC* toka mwaka 1980 waliambiwa tufanyieni hawa mje mlipe wananchi fidia, hawajaja. **[Neno "kimdudu" Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2004 wakaja wakapiga *sound*. Wananchi wakawaambia makubaliano yetu yako wapi?

Juzi bahati mbaya sana wamekwenda na Mkuu wa Mkoa. Nina barua za toka mwaka 1980 hapa. Wameenda na Mkuu wa Mkoa Makala na maaskari Polisi na mitutu ya bunduki, wanatisha wananchi wa Jimbo la Kawe eti na kuwaambia tunawapora, tuwapimie ardhi upya. Yaani mimi nimeshanunua ardhi, nimejenga, unakuja kuniambia unipimie nyumba yangu nikulipe tena!

*That is nonsense, that is nonsense*. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge].**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, jaribu kutumia maneno ya Kibunge ambayo ni ya heshima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yanauma. Haya nafuta.

**MWENYEKITI:** Hata kama yanauma. Haya.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vitu vinauma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa kaenda na jeshi lake, analazimisha wananchi, anaongea na wananchi lugha za kejeli, dharau na kiburi. Sasa nakuomba Mheshimiwa Waziri, kwanza kaa ukijua wananchi pale tumeshajipanga, hakilipwi kitu.

Pili, tunazungumza kwa eneo la Mabwepande peke yake, ni kaya zisizopungua watu 39,000. Hako kaeneo kamoja, sijamzungumzia ndugu yangu wa Kibamba, sijamzungumzia suala la kata ya Wazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule za Umma ziko pale, kuna hospitali za Umma ziko pale, kuna miradi ya maji eneo la Tegeta A, limejengwa tanki kubwa la Umma linalohudumia Jimbo la Kibamba na Jimbo la Kawe. Leo kuna kajitu kamoja kalikuja kuomba shamba la mifugo, hajawahi kutuletea hata mbuzi, hajawahi kuleta hata kuku, miaka 40 baadaye mmempiga nyie

sijui bili ya ardhi ya Shilingi milioni 4.5 anafikiria atakuja kuponea kwa wananchi? *Over my dead body,* hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Bunda Mjini; Nyatwali. Ni hivi, sheria za nchi zinasema hivi, ukitaka kuchukua ardhi ya mwananchi, lazima ufidie kikamilifu na usimwache kwenye ufukara, umpeleke katika hatua aliyokuwanayo ama hatua ya juu ya zaidi. Ukisoma Katiba hiyo hapo, ibara ya 24(2) imesema, ukisoma Sheria ya Ardhi hapa *part two* imesema, ukija Sheria ya Utwaaji wa Ardhi imesema. Hivi kweli ni akili leo, wananchi wa Nyatwali wako pale zaidi ya miaka 700, Serikali mnakuja mnataka kutengeneza njia ya Wanyama, yaani jinsi ambavyo mnapenda wanyama kuliko watu. Mnahamisha kata nzima ya watu 13,000 unaenda unamwambia mwananchi ninakulipa fidia *square meter* moja shilingi 495! Halafu unasema kama una hati ninakulipa *square meter* moja shilingi 704! Halafu mbaya zaidi unatoa hayo makadirio yako…

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba mchakato wa Nyatwali tunaenda kunusuru maisha ya wananchi ambapo kumekuwa na changamoto kubwa sana ya wanyama wakali na waharibifu. Kwa hiyo, wananchi wanaoondolewa pale, siyo kwa sababu eneo lile Serikali inalitaka, ni kwa sababu tunaokoa maisha ya Watanzania.

**MWENYEKITI:** Unapokea taarifa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema hivi, kwanza wananchi wa Nyatwali ni wastaarabu sana. Wamekaa pale miaka 700…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, umeipokea hiyo taarifa kwanza? Subiri kwanza. Mheshimiwa Halima umeipokea taarifa ya Mheshimiwa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja kwanza, dakika zangu zinahesabiwa kwake sasa.

**MWENYEKITI:** Najua. Umeipokea hiyo taarifa ya kwanza au hujaipokea?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa ya kwanza nimeipokea na *reservations.* Kwa nini nimeipokea? Nimeipokea kwa sababu kwa maelezo yao hao wenye meno, wananchi wanatakiwa wahame. Wananchi wamesema sawa, tumekaa hapa miaka 700, tutahama, lakini lipeni fidia kwa matakwa ya sheria za nchi yanavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Nyatwali ni Bunda Mjini, halmashauri hiyo hiyo watu wanalipwa *square meter* kwa vipimo ni shilingi 6,000, halmashauri hiyo hiyo Kata ya jirani basi, tufanye sawa, kata nzima inaondoka. Huyu mwananchi hawezi kubaki kata hiyo, lazima anunue ardhi eneo la jirani. Eneo la jirani *square meter* moja ya ardhi ni shilingi 2,000 kwenda juu mpaka shilingi 3,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni hivi, ni bahati mbaya, halafu nasikia kuna jamaa mmoja sijui anaitwa mtathmini huyu; mtathmini mmoja anaitwa Sanga. *Chief Valuer* anapambana na wananchi wanafurahia sana *Chief Valuer* anavyopambana nao, lakini kuna haka kajitu huko kanaitwa Sanga, kanawapeleka wananchi mpera mpera. Sio Sanga wewe, siyo Sanga wewe, tulia. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, muda wako umeisha. Malizia dakika moja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa usahihi na kumalizia na kwa msisitizo, mmepewa dhamana. Ninarudia, ardhi ni mali ya Watanzania. Rais amepewa dhamana yaani ni *trustee* kwa niaba yetu. Sheria zizingatiwe, haki itendeke. Sitaki mjibu hili suala *emotional. Don't personalize matters. Don't personalize issues*. Jibuni kwa mustakabali mpana wa wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na machungu mliyonayo ya wananchi huko kwenye majimbo, lakini naomba humu ndani tukizungumza, tuzungumze kwa lugha za staha za kibunge kwa mujibu wa kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Halima katika mazungumzo yake ametaja mdudu. Binadamu hatushirikiani na wadudu katika kufanya kazi. Naomba na hilo neno la "mdudu" liondolewe kwenye *Hansard.*

Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga na Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo, ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia fungu 48 - Wizara ya yetu hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kwa nafasi hii naweza kuchangia maeneo kama mawili na nikipata muda zaidi nitakuwa na eneo la tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze hapa ambapo ameishia Mheshimiwa Halima kwenye eneo la mgogoro. Kwanza, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyoendelea kuwaaminisha Watanzania kwamba gurudumu linaendelea bila kusimama, wazi kabisa. Nitatoa uthibitisho katika maeneo mengi haya ambayo nitachangia. Pia nawapongeza sana Wizara; Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mabula na kaka yangu Mheshimiwa Pinda, pamoja na Katibu Mkuu na timu

yake ya watendaji, wananendelea kufanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza hapa alivyosimama Mheshimiwa Halima juu ya mgogoro wa kule Dar es Salaam, eneo ambalo linaingiliana katika majimbo mawili. Hili linaitwa Shamba la Malolo *(Malolo Farm)*. Kwenye historia, ni kweli shamba hili lilikuwa linamilikiwa na Shirika la Maendeleo Dar es Salaam (*DDC)* kwa hati Na. 30 (163) iliyotolewa Tarehe 01 mwezi wa Nne mwaka 1983 ya miaka 99 na eneo hilo lilikuwa kwa ajili ya kilimo na ufugaji kwa hekta au ekari 4,743.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza tukubaliane, ni kweli shamba lilikuwa la *DDC,* hilo lazima tukubali, lakini kwa kupumzika na wakawa wamelala, hili Shirika la Maendeleo Dar es Salaam, wananchi wakaingia. Sasa wananchi hawa ni takribani zaidi ya 70,000. Upande mmoja wa Kinondoni zaidi ya 39,000, maana wengi wapo Kibamba katika maeneo aliyoyasema Tegeta *A*, Goba maeneo ya Msumi yote, lakini na maeneo ya upande wa Kibesa Mabwepande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa upande mmoja watu wana uelewa kidogo hili jambo lililotembea upande wa Kinondoni. Nitumie nafasi hii sana kumpongeza Mkuu wa Mkoa aliyeondoka, Cyprian Amos Makala na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ndugu yangu Abas Zuberi Mwishehe Mwanga Mtemvu. Nisiache kumpongeza sana Mkuu ya Wilaya ya Kinondoni, wamefanya vikao zaidi ya vitatu juu ya hii sintofahamu. Mheshimiwa Waziri umesema, moja ya njia zako za kutatua migogoro ni viongozi kutembelea maeneo yale. Ulitamka kabisa, na hii ndipo ilipopatikana. Maana Mkuu wa Mkoa alipoenda kutembelea kule, ndiyo akaliona hili jambo na akatoa maelekezo ya vikao vianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa upande wa Kinondoni kwenye watu 35,000 Mheshimiwa Gwajima angekuwepo angesema, na ndiyo maana nampongeza sana. Amekaa vikao vitatu, wamefikia kwenye *solution,* kwamba walipe

fidia kuanzia shilingi 8,000 wakakatana, shilingi 6,500 wakakatana, wamefikia shilingi 4,000 kwa kiako cha juzi. Hiyo ni hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu mimi niseme, kwa sababu *engagement* haionekani wameingia watu wa Ubungo na wakati fulani niliwahi kumwuliza Mheshimiwa Kheri Denis James, *Comrade,* Mkuu wangu wa Wilaya akaenda Mbulu. Vipi hili jambo? Akasema anaendelea nalo, lakini nilipofuatilia hakuna vikao vya Ubungo ambavyo vimeingia kwenye ile *engagement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sana, wamefikia 4,000 sawa, lakini kama mtu namiliki kipande cha *square meter* 500 akalipwa shilingi 4,000 ni shilingi 2,000,000 kule kuna watu wana nyumba za udongo, anatoa wapi shilingi 2,000,000? Kwa hiyo, mimi kama Mbunge wa upande mmoja mwenye watu wengi, hapo mlipofikia kama Serikali ni jambo zuri, mmeangalia *consideration* ya wananchi wako pale, lakini shamba hilo, hili ni Shirika la Serikali tu. Kwanini isiwe bure?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani kwa nini shilingi 4,000? Anaenda kupewa nani? *DDC* aliyekaa miaka 40 na kuliacha! Hebu mwende mkaone, *engagement* ya Wilaya ya Ubungo; na hapa nitumie nafasi hii kumwomba sana *Comrade* Hashim Abdalla Komba, *DC* bora kabisa, yaani ni *DC* sijawahi kuona. *DC* bora kabisa aingie kwenye jambo hili vizuri, tuweze kuona wananchi wa Jimbo la Kibamba upande wa Tegeta A, Goba, upande wa Msumi nzima na upande wa Kibesa, nusu ya Mabwepande. Kwa hiyo, kwa sisi shilingi 4,000 bado ni kubwa, tupunguze au twende na bure kabisa. Hayo ni maoni yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nafikiri hapo utakuwa umenielewa, kazi mmeinza, mmefanya vizuri. Siyo tu ya kulaumiwa, kweli wananchi waliingilia eneo hilo la ekari 4,700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu urasimishaji. Kila nikisimama hapa, lazima niseme hili, na huwa nasema kidogo kwa ukali, lakini leo nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri. Tumekaa vikao vingi Dar es Salaam. Sana. Tumekaa vikao vingi

Jimboni, umekuwa ukitafuta jinsi ya kutatua jambo la urasimishaji. Urasimishaji limefeli Dar es Salaam. Kweli, lakini nilisikia sehemu tunazungumza, kama huyu, mpeni mpango mmoja wa miaka 10. Kama umefika mwisho, Desemba mwaka huu wa 2023, twende kwenye *masterplan.* Nikakwambia, hapana, *masterplan* ina gharama kubwa na ni ngumu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ile tuliyokuwa ya kuwapatia hati kwa gharama nafuu, tuendelee kuwa nayo. Leo umeniambia kwenye *page* 59, unao mradi wa uboreshaji wa miliki za ardhi *(LTIP),* Dola 150,000,000 takribani Shilingi bilioni 345, hongera sana, lakini moja na vipaumbele vyako vingi vya kujenga maofisi na kadhalika, namba moja ni kutatua changamoto ya urasimishaji katika maeneo mengi nchini na hasa Dar es Salaam. Nakupongeza sana. Umeenda mbali, unatatuaje? Unasema utaenda kuanza na mitaa 559. Mimi nina mitaa 42 tu. Naamini ndani ya mitaa yako 559, mitaa 42 yote, najua mmeambiana *sample* na Benki ya Dunia, lakini mpeleke yote 42 ili tutatue tatizo la wananchi wa Jimbo la Kibamba kwenye urasimishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi wangu naomba niwaambie, utafiti umepatikana, Mheshimiwa Waziri anaenda nalo vizuri na timu yake ya Wizara, na anawaondoa hofu wananchi wa Kibamba, yale mambo yangu matatu makubwa; maji, barabara na urasimishaji, yote yanapata majibu mwaka huu. Mambo yanaenda vizuri bambam, mambo yanakwenda vizuri Kibamba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Jambo lingine ni uboreshaji wa makazi, ndiyo jambo la tatu nilisema kama muda upo. Naona upo. Nimekuwa nikisema hapa pia kuhusu uboreshaji wa makazi. Nimeangalia taarifa za mapato na maduhuli, bado yako chini, 42% ni chini sana. Waheshimiwa Wabunge wengi waliotangulia kusema, wanne au watano mbele yangu, wameendelea kusisitiza kwamba Mheshimiwa Waziri ongeza mikakati ya kukusanya mapato. Pia ongeza ubunifu wa kuona vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisema na juzi kwenye semina yako nilisema lakini nilipata majibu kwa wataalamu ambayo yanaleta moyo. Nitumie nafasi hii tena kumpongeza Mheshimiwa Rais na nilikuwa nasema, nitaendelea kusema, nampongeza kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi wa *Samia Housing Scheme,* nyumba 5,000 ni jambo kubwa sana, kwa sababu dhamira au dhima ya mpango wetu wa maendeleo wa miaka mitano, ulikuwa ni kuona tunaboresha makazi ya wananchi wetu ili wajiinue kiuchumi. Mama ameionesha wazi, tunabishana wapi hapo? Nyumba 5,000, asilimia 50 zinakaa Dar es Salaam, asilimia 20 zinaenda Dodoma, asilimia 30 katika mikoa mingine. Ndivyo tulivyoambiwa. Jambo la kupongeza sana hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba, hilo mmepeleka pale Kawe, kwenye eneo moja tu, makazi mapya na wananchi wengi watapata, lakini vipi yale makazi holela, makazi ya chini sana ya wakazi wa Tandale? Nimeendelea kusema, mwaka wa tatu nasema hapa; Manzese ni wachache. Ndugu zangu Wakinga pale akina Sanga wanachukua chukua tu pale wanajenga magorofa Manzese. Kuna Vingunguti na majiji mengine, maeneo ambayo kwa kweli yana hali mbaya, kwa nini tusiende tukatengeneza *engagement* pale ya kutengeneza *MoU,* mkubaliane na wananchi wanaomiliki vile vinyumba vya urithi, mkachukua mkawaachia chini ya *floor* ya kwanza ya pili, Serikali ikachukua ya tatu mpaka ya kumi mkaingiza wananchi wengine? Maana yake wananchi sasa watakuwa wanalipa kodi ya majengo, wananchi watakuwa wanalipa mambo mengine, na maisha yao na afya zao zitakuwa zimeboreka na pia miundombinu ya miji itakuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la msingi. Nilisema juzi, mfano kule Lang'ata *constituency,* Jiji la Nairobi; hili ni Jimbo ambalo alikuwa anaongonza Mheshimiwa Raila Odinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli kulikuwa kuna eneo linaitwa Kibera, nyie wengine mnajua, lilikuwa lina mabati-mabati, hivyo kuliko hata Tandale, leo liko vizuri, twende tuige hivyo. Misri kule,

*South Africa* haya mambo yapo ni gharama ni kweli. Juzi nilijibu, hebu endeleeni ingieni tufanye uchumi wa hewani, nyumba ina miaka 30/40 ndiko kwetu sisi, Magomeni, Manzese, Kariakoo, ndiko kwetu, ndiko kwa wazee wetu. Tuko tayari, njooni mtupe uchumi wa chini wa maduka na *floor* ya kwanza ya pili, chukueni ya tatu hadi ya kumi, mbona tayari hapo utaongeza mapato Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niliona mwaka huu wa tatu nimesema na ninashauri anza kufanya...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** ...kwa hiyo...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, muda wako umeisha Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naunga mkono hoja ya Wizara hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa sana niende kwenye kipengele hiki cha migogoro. Si kizuri, lakini sasa inabidi tu tukisemee, ilipaswa tuje hapa tuchangie maeneo mengine ya kuboresha zaidi, lakini sasa inabidi turudi nyuma tusemee migogoro. Wamesema wenzangu hapa, na tayari wamesema chanzo cha migogoro ni sisi kutopima maeneo yetu kwa ukubwa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliongea hili jambo leo hapa kwa mara ya tatu; ni mgogoro wa mashamba ya wakulima Ndika. Wako wananchi Kijiji cha Mkuani, Makuka pamoja na sasa mgogoro unakua unaenda mpaka Kata nyingine ya Kipapa. Mkuani iko Kata ya Maguu, wananchi hawa tangu mwaka 2017 walichukuliwa mashamba yao na mradi unaoitwa Panda Miti Kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapa mimi niombe sana Serikali msomane. Maana tunaisema Wizara ya Ardhi lakini kumbe ndani yake kuna watu wengine Wizara ya Maliasili na Utalii na wengine wako humo ndani lakinimambo yanaenda Wizara ya Ardhi tu. Niombe sana Wizara hizi zisomane na mambo haya muyapange kwa pamoja, ili tuwe na amani katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Panda Miti Kibiashara sidhani kama Waziri wangu wa Ardhi anahusika nao hivyohivyo, huu uko upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii; lakini ardhi ile imechukuliwa ni ya wananchi waliokuwa wanaimiliki kwa halali kabisa. Wananchi wale wamekaa pale tangu kupata uhuru nchi hii, lakini kwa bahati mbaya sana anakuja mtu mmoja leo anasema anataka kuanzisha hili shamba ninyi ondokeni, lakini la pili kwa sababu, sijui umepatikana wilaya nyingine, zamani tulikuwa wilaya moja, sasa ninyi ni wilaya nyingine ondokeni, mkitaka mkaombe kule. Nani anasema tukigawa mipaka hii ya kiutawala inanyima uhuru na umiliki wa ardhi wa mtu Mtanzania huyu, ni nani anasema hivyo? Si sawa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi wale wanapata shida kuanzia mwaka 2017 mpaka leo. Wanakufa njaa ilhali wana mashamba yao pale kwa sababu tu ya mambo haya, mtu anakuja analianzisha hili jambo kirahisi tu hivi. Sasa niombe Waziri, wakati fulani Mheshimiwa Waziri Lukuvi alianza kulishughulikia hili na pakawa na amani, lakini ilifikia hatua pale maeneo yale, sisi hatujazoea, sisi Wamatengo kule mambo ya vita haya hatujazoea, lakini watu wametupiga risasi pale. Mgogoro, unapiga mtu risasi. Wanapigwa mapanga pale, kwa nini iwe hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Waziri, tutatue huu mgogoro kwa sababu mashamba yale ni ya watu walikuwa wanaishi pale miaka yote. Kuanzisha huu mradi kama kweli wanataka hawa watu kuchukua yale mashamba, mbona sheria ziko wazi, walipe fidia. Walipe fidia ili wananchi wale waondoke pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Aziza Mangosongo. Amefika anajitahidi kupambana na huu mgogoro, ili ufike mahali, lakini sasa kwa sababu uko na wilaya nyingine anashindwa. Sasa niwaombe, Mheshimiwa Rais wa nchi hii anafanya kazi nzuri ya kumaliza migogoro, siyo mpaka mgogoro huu wa Ndika tumsubiri Rais aje kutamka maneno pale, Waziri upo na viongozi wengine wapo, njooni mmalize huu mgogoro, tusimsubiri Mheshimiwa Rais, tunampa mzigo mkubwa, ana mambo mengine ya kutuletea fedha na maendeleo mengine ndani ya nchi hii. Hii migogoro ndiyo maana mpo nyie mtusaidie uishe, pale mahali wala si mahali pakuchukua muda mrefu; ukifika Waziri kwa sababu, maeneo ni ya watu utatamka tu neno, wananchi wale watasherehekea na ng'ombe watakupa, si rushwa, lakini ni sadaka kwa ajili ya shukrani; sisi wamatengo tunatoa shukrani. Uje ututamkie ili wananchi wa Ndika, wananchi wale kutoka Kipapa wawe na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kijiji kingine kipo pale, Kijiji cha Kata ile ya Burma, Kata ile ya Mpapa. Na kwenyewe tuna kijiji muda mrefu, kiko pale, lakini wamekuja watu sasahivi eneo lile lote wamelihamisha. Tumejenga mpaka shule, mpaka sasahivi wanafunzi wanatoka maeneo mengine mbali wanakuja kusoma kwenye shule ile ambayo ilikuwepo pale na kijiji kilikuwepo. Lakini ni kama nilivyosema suala hili si lako peke yako, zungumza na Wizara hii ya Maliasili na Utalii, mipango hii wanapofanya basi waifanye vizuri, ili kwamba mwisho wa siku tusilete hii mivutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu wa Ndika sasahivi wananchi wameamua kwenda kulima wenyewe. Wanasema hivi, kule kulikuwa ni kwetu, tuliondoshwa, sasa mtu kurudi kwao nani atakayemfukuza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamerudi pale, lakini kilichofanyika pale ni kama wametengeneza, yaani mgogoro wenyewe sasa ndio unaenda kuwa mkubwa. Kwa sababu wananchi wamesema sisi tunarudi kwetu. Tumeisubiri Serikali itoe maamuzi haijatoa, sasa sisi tunarudi kwetu kwenye mashamba yetu. Kwa hiyo hofu yangu tunakoenda huku kutakuwa kubaya zaidi kuliko huku tulikotoka. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri twende tukalimalize hili suala pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili. Nikushukuru sana kwa huu mpango wa hii fedha ya mkopo maana na mimi Mbinga ni mnufaika. Wananchi wetu katika vijiji vya Mbinga tutapata, japo ni vichache, tutapata na sisi kupimiwa viwanja vyetu. Ombi langu sasa, kama si kitu kibaya, Kamati hapa imeshauri kwa nini zile fedha nyingi zile bilioni 47 zikatumike kwa matumizi mengineyo na si kupima ardhi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama si kuvunja sheria, basi Mheshimiwa Waziri chukua huu ushauri wa Kamati. Kwamba, zile fedha nyingi tukapime vijiji vingi. Na hesabu zimetolewa hapa na Mheshimiwa Komredi Kunambi hapa, ametoa hesabu vizuri sana. Ametoa hesabu kwamba, tukipima vizuri fedha hizi tunaweza kupima vijiji vingi zaidi, ili kuvifikia hivi vijiji na lengo likiwa kupunguza hii migogoro. Maeneo haya yakipimwa mengi maana yake migogoro itapungua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine nilikuwa napendekeza; maeneo yetu haya, ardhi yetu hii kwa sababu hatujaipanga wananchi wanajichukulia hatua ya kwenda kukaa kila eneo. Kila eneo wanaenda kukaa, kila eneo wanaanzisha kijiji, kila eneo wanaanzisha mji, suala ambalo linasababisha hata Serikali kupata ugumu wa kupeleka huduma kwenye hayo maeneo. Sasa tukipanga, utoaji wa huduma na kupeleka huduma nyingine kwenye maeneo haya utakuwa ni rahisi sana, lakini pia tutaitunza ardhi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke tulipopata uhuru tulikuwa wangapi? Na mwaka huu tuko wangapi? Na miaka ijayo inayokuja tutakuwa wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ardhi yetu imebaki ni ileile. Kwa hiyo, tukiipanga hii, kama wananchi watakaa maeneo fulani na maeneo mengine yatakuwa kwa shughuli nyingine itakuwa ni jambo jema zaidi na ardhi yetu itakuwa nyingi na kubwa kuliko, hiataisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niseme haya kwa nafasi hii. Nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. Asante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga. Nilimtaja Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuchangia Wizara ya Ardhi. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai tunachangia hii Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, hususan kwa jinsi alivyoanza kushughulikia matatizo ya Wizara ya Ardhi, kwanza kwa kuunda ile Kamati ya Mawaziri Nane ili waende kushughulikia migogoro ya ardhi, lakini pili hapa juzi juzi aliweza kutoa msamaha wa riba kwenye pango la ardhi ili wananchi waweze kulipa pango lao la ardhi. Napenda pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa hilo, lakini niombe ikiwezekana atuongezee muda, awaongezee wananchi ili waendelee kulipa pango la ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Angelina Mabula na Naibu wake kwa kutuletea watendaji wa Wizara ya Ardhi hapa Bungeni na sasa tunaweza kushughulikia masuala yetu ya ardhi kwa wepesi zaidi. Napenda niwapongeze watendaji wote wa Wizara ya Ardhi na hususan nitaanza na Kamishna wao Mheshimiwa Mathew kwa uwajibikaji wake wa kupokea simu haraka na kujibu *message*. Nampongeza pia, Mkurugenzi wa *National Housing* Mheshimiwa Hamad Abdallah kwa kasi mpya aliyokujanayo kwenye sekta ya *national housing*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hizo pongezi ninayo masuala ya kuchangia kwenye Wizara hii. Kwanza kabisa naunga mkono hoja ya Kamati ya Ardhi, nikiwa kama Mjumbe naunga mkono mambo yote yaliyosomwa na Mwenyekiti wa Kamati yetu. Sisi kama kamati tuliona kwamba, Wizara ya Ardhi ina wajibu wa kupima ardhi na kusimamia ardhi ya Tanzania inapimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Tume ya Mipango ya Ardhi. Tume ya Mipango ya Ardhi imekuwa ikipewa pesa ndogo sana za kupima ardhi na matokeo yake imekuwa ikishindwa kutimiza wajibu wake wa kupima ardhi na hatima yake ni uzalishaji wa migogoro kwenye masuala ya ardhi kwa wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati tunapitisha bajeti hapa tuliomba tume iongezewe pesa shilingi bilioni nne, lakini suala hilo limechelewa kutekelezwa mpaka tumekuja kuingia kwenye bajeti nyingine. Tukiwa kama wajumbe wa Kamati tunaona kwamba, hii inaidhoofisha Tume ya Mipango ya Kupima Ardhi kuweza kutimiza wajibu wake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiona migogoro ya mipaka ikiendelea, lakini pia tumeona wakulima hawajui mipaka yao ni eneo gani la kulima, pia tumekuwa tukiona wafugaji hawajui maeneo yao ya ufugaji na hii kusababisha migongano kati ya wakulima na wafugaji. Ombi langu kwenye Wizara ya Ardhi ni kuiongezea Tume ya Mipango ya Kupima Ardhi Nchini ili iweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ninaomba kuzungumzia suala la pesa za mkopo ambazo Serikali yetu ya Tanzania imekopa mkopo huu ambao unaitwa *Land Tenure Improvement Program*. Pesa hizi ni dola 150, sawa na shilingi bilioni 350 za Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati tuliona kwamba, fedha hizi zingeelekezwa zaidi kwenye upimaji wa ardhi. Kwa maana kwamba, tukiwa kama Kamati tulipendekeza zaidi pesa

hizi ingepewa Tume ya Mipango ya Kupima Ardhi ili iweze kwenda kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango ya Kupima Ardhi ina uwezo wa kupima vijiji 826 kwa mwaka, lakini mradi huu unakwenda kupima vijiji 500 kwa muda wa miaka mitano. Ukiangalia uwiano ni kwamba, kutakuwa na uwiano wa vijiji 100 kupimwa kwa mwaka mmoja. Kitu ambacho tunaona kwamba, kwa mfano kama hii fedha Tume ya Mipango ingepewa ingeweza kupima vijiji 826 kwa mwaka, na matokeo yake kwa muda wa miaka mitano ingeweza kupima zaidi ya vijiji 4,131. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia unakuta kwamba, uwiano wa vijiji 500 kwa miaka mitano ni tofauti kubwa na uwiano wa vijiji 4,131 ambavyo vingeweza kupimwa na Tume ya Mipango ya Kupima Ardhi nchini Tanzania. Ombi langu kwa Serikali, ninaomba fedha hizi waweze kufanya utaratibu; Tume ya Mipango ya Kupima Ardhi ipewe fedha hizo ili iweze kupima hivi vijiji na ili iweze kuendana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo imesema kwamba, kwa muda wa miaka mitano tungeweza kupima vijiji zaidi ya 4,131. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ambalo ningependa kulizungumzia hapa kwenye huo huo mradi; tunaomba ile mikoa ambayo inakwenda kujenga hizi ofisi kutokana na hizi fedha, kwanza tungeomba ofisi zijengwe kwa uwiano wa kufanana. Yaani kwamba, mikoa yote gharama ya ujenzi ilingane; kwa maana ya kwamba, hata kule Katavi waweze kupata ofisi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ambalo ningependa kulizungumzia hap ani suala la mipaka yetu ya nchi yetu ya Tanzania. Suala la mipaka ni tata kwa sababu gani, tumeona sehemu nyingine hazijawekewa mipaka, lakini pia sehemu ambazo zimewekewa mipaka ni wanajenga vi-*box* vidogo sana ambavyo ni kama mita moja. Mfano, tulikwenda pale Tunduma tukakuta mpaka, ni kitu kimetoka chini urefu wa mita moja mpaka hapa, ndio unaitwa mpaka wa Tanzania na zamabia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka kuboresha mipaka ya nchini kwetu Tanzania ninaomba Serikali iweke utaratibu, hususan Wizara ya Ardhi ambayo inaratibu hili jambo, ijenge mipaka ya kuonekana ambayo itakuwepo sasa na miaka 100 ijayo. Ujenzi wa mipaka ambao unaendelea sasahivi, mipaka ile ni midogo na sehemu nyingine hazionekani, haijulikani mpaka uko wapi, umeishia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, fedha ambazo zinatolewa kwa ajili ya ujenzi wa mipaka ya nchi yetu ya Tanzania ni fedha chache. Hii inasababisha kwamba, huko baadaye sisi tutaishi na tutapotea, lakini tunataka kizazi kinachokuja kikute mipaka ya nchi yetu imeratibiwa vizuri na inaonekana. Kwa maana kwamba, kama unajenga urefu wa mita moja kutoka chini na unasema kwamba, huu ndio mpaka ina maana unahitaji baada ya muda labda miaka kama 20 utahitaji kujenga tena, kurudia zoezi lilelile la kujenga mipaka upya, kitu ambacho naona kwamba ni utumiaji wa fedha mara mbili. Kama tunaboresha mipaka yetu basi tungeboresha mipaka yetu vizuri na tujenge mpaka wa kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ambalo ningependa kulizungumzia, wananchi wengi wanakaa kwenye vijiji hawaelewi kwamba wanapaswa kupima ardhi zao. Matokeo yake ni nini? Matokeo yake mwekezaji anafika pale anachukua ile ardhi kwa sababu, yeye amewekeza na yule mwananchi ambaye amekaa pale kwa takribani muda wa miaka mingi anaondoka pale kwa sababu tu, alikuwa ahajapima ile ardhi na kwa sababu alikuwa hana hati. Ombi langu kwa Serikali, ninaomba Wizara ya Ardhi iwaelimishe wananchi waweze kupima ardhi zao kama ni shamba, ni kitu chochote waweze kukipima, ili kutoa huu usumbufu wa kunyang'anywa ardhi zao ambazo wanakuwa wamekaa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mtu anakaa mahali takribani zaidi ya miaka 50 halafu unakuja kumwambia kwamba, hapa si nyumbani kwako kwa sababu huna hati. Kwa hiyo naomba wananchi waelimishwe waweze kupima ardhi zao, lakini

pia waweze kutumia hizo hati zao kwa ajili ya kupata mkopo benki na sehemu nyingine. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuwajibika ipasavyo kwa michango yenu yote tangu asubuhi. Waheshimiwa Wabunge tuna matangazo machache hapa: -

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Abeid Ighondo, ambaye anaitwa Rashid Habibu, ni mpiga kura wake kutoka huko Singida. Karibu sana mpiga kura wa Mheshimiwa Abeid Ighondo.

Lakini pia, kuna mgeni pale kwenye Jukwaa la Spika nilimtangaza, Ndugu Chifu Daudi Babu Mrindoko, ambaye yuko kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, lakini na huyo pia ni *campaign manager* wangu tokea mwaka 2015 katika Umoja wa Wazazi. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia, tuna tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Kilimo, ambaye anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wanaotoka kwenye maeneo yaliyoathirika na utekelezaji wa Mkataba wa Mauziano ya Matrekta ya Ursus kati ya *NDC* na wakulima, kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambapo kikao hicho kinatarajiwa kufanyika leo tarehe 25 Mei, saa 8.00 Mchana katika Ukumbi Namba 231 uliopo katika Jengo la Utawala. Kwa hiyo, waliohusika wote wanaombwa kufika huko.

Lakini pia, tuna tangazo kutoka kwa katibu wa Bunge, ambaye anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Bodi ya Mfuko wa Barabara ipo katika viwanja vya Bunge kuanzia leo tarehe 25 na kesho tarehe 26 Mei, mwaka huu wa 2023 kwa

ajili ya kutoa elimu kuhusu matumizi ya mfumo wa kidijitali wa ufuatiliaji wa hali ya barabara. Kwa hiyo, Waheshimiwa wote mnakaribishwa.

Lakini pia, tuna tangazo jingine, lile ambalo nilitangaza asubuhi. Waheshimiwa wote mnaombwa kuhudhuria kwenye semina ya wenzetu wa Wizara ya Nishati mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge.

Baada ya kusema hayo, nawatakia mchana mwema; na Ninasitisha Shughuli za Bunge Hadi Saa 11:00 Jioni.

Waheshimiwa, hivyohivyo hata kama mnasimama; wachangiaji wetu wa jioni ataanza Mheshimiwa George Nathan Malima, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Abubakar Damian Asenga na Mheshimiwa Jafari Wambura.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo)Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala ulio mbele yetu ambao ni Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Tutaanza na Mheshimiwa

George Natany Malima, atafuatiwa na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ajiandae.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza jioni ya leo. Kwanza nianze na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuipa msukumo mkubwa Wizara hii ya Ardhi. Kusema kweli ardhi ndiyo maisha ya wanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamesema kuanzia asubuhi tulipoanza kuchangia, wamezungumza suala la kumilikisha ardhi kwa wananchi wetu wa Tanzania. Napenda nimpongeze sana Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Mabula na Naibu Waziri, ndugu yangu, Mheshimiwa Pinda, wanafanya kazi nzuri katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni kati ya Wizara chache zenye changamoto nyingi. *Interest* kubwa ya wananchi iko kwenye ardhi na ndiyo maana kila anayesimama anazungumza habari ya wananchi kumilikishwa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kuhusu umuhimu wa kupima ardhi katika maeneo yote ya nchi yetu. Umuhimu wake uko hapa, mwananchi akipimiwa ardhi yake anaweza kupata hati, akipata hati ya kumiliki eneo lake anaweza kuitumia kupata mikopo katika vyombo vyetu vya fedha na hivyo kumwondolea umaskini. Wananchi wetu wengi ni maskini lakini wana maeneo ambayo hawana uhakika kwamba kesho wataishi pale au wataondolewa lini. Hiki ndicho kitu ambacho Wabunge wengi wamezungumza leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana wananchi wetu wakawa na uhakika na eneo wanapoishi. Kwamba akiwa na hati, eneo lake limepimwa, hata kama Serikali itataka kutwaa eneo hilo kwa ajili ya matumizi ya umma, lazima fidia itakuwa nzuri, kutakuwa na utaratibu wa kisheria ambao utamsaidia yule

anayeondoka eneo lile atakwenda kule anakokwenda akiwa amepata fidia nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ilivyo, mtu amekaa anaambiwa apishe labda bomba la mafuta au apishe nini, anaondoka hakuna cha fidia wala nini, anaendelea kuwa maskini kuliko aliokuwa nao wakati ule. Kwa hiyo nashauri sana Wizara hii ipime. Migogoro hii ya ardhi mnayoiona Waheshimiwa ni kwa sababu ardhi yetu haijapimwa, kwa hiyo wananchi kila siku wananyang'anyana ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika ofisi ya Mheshimiwa Waziri, bado katika idara nyingi, hasa kwenye halmashauri, kuna wafanyakazi wachache wasio waaminifu. Wanamilikisha ardhi kwa mtu zaidi ya mmoja, matokeo yake mtu anakaa anajua ana kiwanja mahali Fulani, kumbe kile kiwanja kina wamiliki zaidi ya mmoja au watatu. Matokeo yake kila siku wako mahakamani kwa ajili ya kesi ya kutafuta nani mwenye umiliki halali. Naomba Mheshimiwa Waziri jambo hili alichukulie kwa uzito sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wafanyakazi wanaofanya ubadhirifu wa namna hii wachukuliwe hatua kali, hata ikiwezekana waachishwe kazi. Huwezi kumilikisha ardhi watu wawili, watatu, ukatarajia kutakuwa na amani katika eneo hilo, haiwezekani kabisa. Kwa hiyo, hili jambo ni muhimu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mpwapwa tuna maeneo, tuna kata ambazo tayari zina sifa za kupimiwa ardhi. Katika hotuba ya Waziri, ukurasa wa 34, amezungumzia habari ya Sheria ya Mipango Miji, Sura ya 355, akatoa hata sifa za eneo kutangazwa kwamba linaweza kupimwa. Waziri amesema anaangalia uchumi wa eneo hilo, maendeleo ya eneo hilo, hata mazingira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mpwapwa tuna maeneo mengi ambayo yanakidhi hizi sifa alizokuwa amezisema Mheshimiwa Waziri. Kwa mfano, kuna Kata za Chitemo, Chunyu, Mlembule, Lupeta, Godegode, Berege, Miima; haya ni maeneo ambayo yangepaswa kupimwa kwa sababu yana sifa zote.

Namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo ili eneo letu lipimwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpwapwa Mjini pia hatujapima, yaani zoezi la kupima linasuasua sana. Tunaomba Mheshimiwa Waziri a-*push* maeneo haya yapimwe ili wananchi wetu waweze kuyatumia kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida nyingine ambayo pia inaweza kufanyika vizuri ni kwamba Waziri akipima maeneo, Serikali itakusanya kodi kwa sababu wale wote watakaokuwa wamepimiwa maeneo na kupata hati, watapaswa kulipa kodi ya kila mwaka ya pango la ardhi. Ingawa utaratibu wa sasa Mheshimiwa Waziri, bado hauleti matumaini ya kukusanya fedha za kutosha, bado wananchi wetu hawajawa na hamasa ya kulipa kodi, walio wengi hawalipi kodi, lakini ni kwa sababu ya utaratibu ulioko sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ulioko sasa unamsubiri mlipakodi aende mwenyewe kulipa kwenye mamlaka inayohusika, lakini tungetumia utaratibu mwingine, hata wa kulipa kupitia simu, ili mtu apate unafuu wa kulipa. Leo tunakusanya kodi chache sana za pango la ardhi kwa sababu ya utaratibu ulioko sasa. Kwa hiyo naomba pia Mheshimiwa Waziri waliangalie sana hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuchangia leo ni juu ya utoaji wa hati. Hili nalo ni tatizo lingine katika Wizara hii. Mtu akishapimiwa na kulipa kila kitu, hati inachukua muda mrefu sana kupatikana. Hii ndiyo inasababisha hata viwanja vinavamiwa, kwa sababu mtu amelipa anakaa mwaka au miaka miwili hajapewa hati yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kuna tatizo gani, kwa nini hati hazitoki? Kama mtu amekamilisha kila kitu kinachotakiwa kwa nini hapewi hati yake haraka ili aweze kufanya maendeleo, aweze kuendeleza, aweze kupata mikopo katika mabenki ili aendeleze maisha yake? Hati zinachelewa sana, naomba sana suala la hati

waliangalie kwa ukaribu ili wananchi wetu waweze kujikwamua katika maisha haya ya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha kwa ajili ya ule mradi wa upimaji. Wamesema sana wenzangu, nami naomba sana fedha hizi nyingi zitumike kwenye mambo ya upimaji wa ardhi. Tumeona katika ripoti ya Waziri, fedha kidogo sana ndiyo inakwenda kwenye ile mamlaka ya kupima, lakini fedha nyingi zinatumika katika kazi ambazo kwa kweli hazina tija kwa wananchi wetu. Kwa hiyo kwa kauli za Wabunge wengi waliosema, naamini Mheshimiwa Waziri atakwenda kuangalia upya, fedha zile zifanye kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini akitumia fedha hizo kwa ajili ya kupima, kwanza kasi ya upimaji itakuwa kubwa, lakini mwakani hatakuja akasema tuna asilimia 25 ya upimaji mpaka sasa hivi. Ndiyo maana migogoro ni mingi, asilimia 25 ni sehemu ndogo sana iliyopimwa. Migogoro hii haitaisha ndugu zangu kama hatutapima maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninakushauri sana Mheshimiwa Waziri, fedha hizi zitumike vizuri, zipime maeneo mengi katika nchi yetu ili mwakani anaporudi hapa atuambie tumepima asilimia 75 na hiyo 75 itatuonesha kwa sababu tutaona migogoro ya ardhi imepungua, hasa ndilo lengo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasemaji wamesema hata nchi za wenzetu majirani migogoro yao ya ardhi siyo mingi kama ya kwetu, lakini ni kwa sababu hatujapima. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, anafanya kazi nzuri sana katika Wizara yake, nampongeza sana, lakini kwenye eneo hili la kupima, naomba sana alichukue kwa uzito wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, basi naomba niunge mkono hoja; ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege ajiandae.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii adhimu ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya na ya kupigiwa mfano ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa taasisi hii ambao wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba sekta hii ya ardhi inapata mapato ya kutosha na kuweza kuwatatulia wananchi kero zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika makusanyo ya maduhuli. Wizara katika kipindi cha mwaka 2022/2023 ilijipangia kukusanya shilingi bilioni 250 kutokana na vyanzo vyake vya mapato. Uhalisia wa mapato hayo waliweza kukusanya asilimia 42.55 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha mwaka 2023/2024, Wizara pia imeweza kujipangia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 300. Naomba niulize Wizara kupitia Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji; changamoto ambazo hazikuweza kushughulikiwa katika kipindi cha mwaka 2022/2023, je, tutaweza kuzishughulikia changamoto hizo katika kipindi hiki cha 2023/2024?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ni nyingi, moja ikiwa ni migogoro mikubwa ya ardhi inayolikumba Taifa letu. Nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kuweka nia ya dhati kabisa ya kuwasaidia wananchi wa nchi hii kupitia migogoro hii ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la Mradi wa KKK, Wizara imeweza kutoa fedha za mikopo katika halmashauri mbalimbali, lakini kuna halmashauri ambazo zimeweza kufanya vizuri na kuweza kukusanya mapato na kurudisha mikopo hiyo. Hata hivyo, zipo halmashauri kadhaa ambazo zimeweza kuchukua mikopo lakini hazikuweza kurejesha mikopo hadi hivi sasa, lakini pia wanaendelea kutekeleza miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zile zinatakiwa zirejeshwe ili baadaye halmashauri nyingine ziweze kutumia fedha hizo ambazo zinasubiri. Hiyo ni changamoto kubwa ambayo Wizara wanatakiwa kutuhakikishia kwamba fedha hizi zinarejeshwa haraka ili ziweze kuwasaidia halmashauri nyingine ambazo zinasubiri fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la migogoro ya ardhi; migogoro hii kama walivyosema Waheshimiwa wenzangu, ni mikubwa na ni mingi sana. Kwanza, niipongeze Wizara kwa kuweza kupata Shilingi Bilioni 350 ambazo ni sawa na Dola za Kimarekani milioni 150 ambazo zitaweza kusaidia kwa kiwango kikubwa kuondoshwa migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha ni kwamba Wizara katika mradi huu imeweza kujielekeza katika halmashauri 41 tu katika kutatua na kutekeleza miradi hii ambayo ni pamoja na kupanga na kupima katika maeneo ya halmashauri hizo. Migogoro ya ardhi iko nchi nzima, kwa nini Wizara ijielekeze katika halmashauri 41 tu? Katika halmashauri hizo 41 katika fedha hizi imejipangia kutatua migogoro ya ardhi, kwa kushughulikia vijiji 500 tu ambavyo kila mwaka watakuwa wanashughulikia vijiji 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini, kwa vile tunayo Tume yetu ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na ina ukwasi mkubwa katika kupata fedha za kuendeleza miradi ya maendeleo ambao ni ule Mradi wa Kupanga na Kupima Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wizara isitenge bilioni 62 tukafuata maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu

ambayo imeelekeza mpaka ifikapo mwaka 2025 vijiji vipya 4,131 viwe tayari vimeshapimwa. Kwa nini Wizara kupitia fedha hizi tusitenge shilingi bilioni 62, tukazielekeza katika tume hii na kuanza kutekeleza Mradi huu wa KKK katika vijiji vyote na tukahakikisha kwamba mwaka 2025 vijiji vyote viwe tayari vimeshapimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, 2025 haiko mbali, Chama Cha Mapinduzi kiliingia mkataba na wananchi na kikawahakikishia kwamba ifikapo mwaka 2025 vijiji vyote vitakuwa vimepimwa. Kwa nini tusitenge fedha, shilingi bilioni 62, tukaenda tukatatua migogoro ya ardhi kwa kuangalia suala la kupanga na tukaweza kupata mapato makubwa kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote tukae tuupitie tena mradi, tuangalie namna ya kutenga shilingi bilioni 62 ili tuzielekeze katika mradi huu wa kupanga ili kuhakikisha kwamba tumekwenda na maelekezo ya Ilani, ifikapo mwaka 2025 vijiji vyote 4,131 viwe tayari vimeshapimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna jumla ya vijiji 12,318, lakini vijiji vilivyopimwa ni 2,818 tu ambayo ni sawa na asilimia 23. Tutakapoingia katika mradi huo na kuweza kutenga fedha ya kutosha tutaweza kupima vijiji 826 kila mwaka. Tutaweza kuondosha migogoro ya ardhi kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kuhusu asilimia 30 ya mapato ya halmashauri ambayo fedha hizi zilikuwa zinabaki ndani ya halmashauri na kuweza kuwanufaisha na kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, karibuni tu tutakuwa na bajeti hapa na kupitia sheria mbalimbali, naomba sana Serikali tuweze kurekebisha sheria hii na kuelekea kwenye kanuni na miongozo mbalimbali ili fedha hizi asilimia 30 ziendelee kubaki halmashauri ili ziendelee kuzisaidia halmashauri katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niunge mkono taarifa ya Kamati, lakini pia niendelee kuunga mkono hoja ya Wizara lakini kwa kuona kwamba changamoto zote ambazo tumezieleza, ziweza kufanyiwa kazi, ahsante.. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii na mimi kuchangia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hapa leo nachangia, pamoja na ushauri mwingine, lakini jambo langu kubwa ni moja tu la mgogoro wangu wa ardhi kule Ifakara, Kata ya Mlabani ambao unahusisha eneo la Baba Askofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kabla ya kwenda huko, naomba nikishukuru Chama cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sera nzuri tunazoendelea nazo kuhusu ardhi. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri waendelee kusimamia sera hizi kwa sababu tunavyotembea katika nchi jirani tunaona huko mabalaa, kwamba ardhi huko katika nchi za jirani ni ardhi za watu, lakini sisi Tanzania ardhi bado ni mali ya umma na ni mali ya Serikali. Hili ni jambo la kijamaa kabisa na kwa sisi wajamaa tunataka liendelee kuwa hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Rombo kule kama *DAS,* nilikuwa navuka jirani pale Kenya, unaona kwamba mwenye kipande cha ardhi anakuwa kama Mungumtu, kwa hiyo sisi Tanzania ni muhimu sana tukaendelea nalo hili kuliweka katika misingi kabisa kwamba litakuwepo miaka dumu daima dumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa Jimbo la Kilombero, Wilaya ya Kilombero, Halmashauri ya Mji wa Ifakara, kwa mkakati wa Serikali wa hatimiliki. Katika jimbo langu sehemu kubwa sana za vijijini wamepewa hatimiliki

na baada ya kupewa tu zile hatimiliki za kimila, ardhi imepanda thamani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo tunayo ni kwamba wananchi hawakupewa elimu ya kutosha kwamba wanavyouziana zile ardhi kuna utaratibu wa kisheria wa kufuata ili umiliki utoke katika kaya au mila kwenda kwa mtu mwingine. Kwa hiyo ombi langu kubwa kwenye jambo hili ni kwamba, lazima elimu ya kutosha itolewe kuhakikisha kwamba wanaambiwa maana ya hati ya kimila ni nini na wanavyotaka kuuziana wanauziana kwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunakushukuru Mheshimiwa Waziri, tunaishukuru Wizara kwa mikopo ya Halmashauri. Halmashauri ya Mji wa Ifakara ilipata fedha milioni 250 ambazo kwa kweli tunashukuru sana Wizara yako kutupatia fedha hizi angalau mmethubutu na mmeanza kuonesha. Changamoto kubwa katika jambo hili ni kwamba upimaji wa viwanja katika Halmashauri zetu malengo yake ni nini, pamoja na kupanga Miji lakini kitu kingine ni kwamba inasaidia watu wasio na uwezo vijana kupata viwanja vya kujenga. Sasa lazima Halmashauri ifikie kuongeza mapato lakini inaongeza mapato kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona wananachi wangu hasa vijana wakilalamika fedha gharama ya mauzo ya viwanja ni kubwa, nimekusikia kwenye *speech* yako Mheshimiwa umezungumza umesema hapa gharama hizi ni kubwa. Vijana wetu wadogo, vijana wetu ambao wanafanya biashara kama watoto wa fundi cherehani, nywele zao za kipilipili, kiwanja cha milioni tatu atanunua wapi? Kiwanja cha milioni mbili atanunua wapi? kwa hiyo lazima kuna maeneo na kule kwetu kuna mashamba makubwa ya bei rahisi vipimwe viwanja vya laki tano, milioni na muda wa kulipa uwe mrefu hata kama ni mwaka miezi sita. Mtu anapewa siku 90 alipe milioni mbili, milioni mbili na nusu watu hawawezi wanaacha viwanja na viwanja vinabaki kwa akina Asenga tuna watu wengine. Wale vijana wadogo kwa mfano Hansi wa Kidatu, Maisha wa Lumemeo, Sande, Mijije, wakina Kalyoma, wakina Mido hawa ni vijana wadogo *sample* ya

Jimbo la Kilombero vijana maarufu ambao wanajulikana hawawezi hata siku moja kumiliki maeneo hayo kutokana na bei hiyo kuwa milioni tatu ama milioni nne.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusisitiza pia kwamba wekeni wazi, nimeona maoni ya watu hapa, ninachofahamu Mheshimiwa Waziri ni kwamba Tume hii haina mamlaka ya kupima, mamlaka ya kupima yapo kwenye Halmashauri zetu, kwa hiyo ufafanuzi huo uwekwe wazi ili muweze kuziwezesha Halmashauri kama Wabunge wengine walivyoshauri hapa. Halmashauri ndiyo ziwezeshwe zipime na ziangalie *level* na maeneo na watu wenye uwezo kama nilivyosema awali vipatikane viwanja, nchi hii viwanja vya laki tano vinaweza vikapatikana vijijini. Ifakara kule pimeni viwanja vya laki tano, tano, milioni, vijana na wakulima wale waweze kumiliki viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anapata gunia zake tano akiuza alipe kiwanja, sasa mtu anauza gunia kumi bado haitoshi kulipa kiwanja, gunia kumi za mpunga. Sasa hii kwa kweli inakuwa ngumu matokeo yake wageni wanamiliki ardhi na wananchi wetu wa kawaida wanakosa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili ni kubwa Mheshimiwa Waziri, kuna mgogoro pale ambao mimi niliusikia tangu 2015, Kanisa la Roma chini ya Baba Askofu Libena, Baba Askofu Salutaris Libena tunavyozungumza hivi yuko Roma anapiga goti kuombea nchi yetu, anaombea Jimbo letu wako Roma huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro tangu 2015 Rais alipokuja pale wakati ule aliambiwa mbele ya umati, kuna eneo kubwa la kanisa liko Ifakara Mjini karibu heka 1,000, kuna hekari kama 200 sikumbuki vizuri zimevamiwa na wananchi wamejenga, hawa ni wananchi wetu. Mwanzoni kanisa lilikuwa na msimamo wa kutaka watu wale wahamishwe, lakini mimi mwenyewe nimeenda kuzungumza na Baba Askofu. Baba Askofu Libena amekubali wananchi wale wapimiwe wamilikishwe apewe ardhi mbadala, ni jambo kubwa na ni jambo zuri na nimeenda Kata ya Mnadani nimekaa na wananchi wako tayari kupimiwa kulipa hati zao ile fedha ikatafutie Baba Askofu ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri fedha za kupima tu zinakosekanaje, sasa wewe ni Mama yangu, wewe msikivu, mimi hapa kweli nilete ukorofi wa kushika shilingi kwenye jambo hili, hata wananchi wangu watasema tena kwa Mama Mabula kweli mbona umekosa adabu. Nisaidie Kamishna Frank ni mtu mzuri, Kamishina wetu wa Ardhi Mkoa wa Morogoro mtu mzuri, ukimsaidia kwenye barua yake na barua yake nimekuletea mezani hapo ili Baba Askofu akirudi huko aliombee Taifa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asenga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ndulane.

**TAARIFA**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huo anaozungumza Mheshimiwa Abubakari Asenga ni wa kweli kabisa na ulianza wakati nilipokuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Ifakara. *Just imagine,* Kata Tano ya Mji wa Ifakara ziko ndani ya eneo la Kanisa Katoliki Jimbo la Ifakara, kwa hiyo ni mpango muhimu naomba asaidiwe.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga taarifa unaipokea.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kabisa Kaka Ndulane nakushukuru sana Mkurugenzi wangu na ikimpendeza Mungu urudi tena pale kwa mara nyingine kuwa Mkurugenzi! Hiyo nimechomekea tu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kwa kweli alikuwa Mkurugenzi wetu wa Halmashauri yetu ya Mji wa Ifakara, yeye na Mbunge wa Mikumi Mheshimiwa Dennis Londo naye alikuwa Mkurugenzi pale wanajua mgogoro huu, nasi Wakurugenzi wetu wana bahati ya kuwa Wabunge. Kwa hiyo hawa wawili walikuwa Wakurugenzi na sasa hivi ni Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kusema ukweli kwamba hili jambo ni *very serious* kabisa na tunashukuru Baba Askofu asije akabadilika kama amekubali kutoa ardhi hii kwa wananchi wale waliovamia na ameweka mpaka kabisa hawaruhusiwi kuendelea kuvamia tena maana pale kuna hospitali kubwa ya kansa amejenga, *Good Samaritan*, kuna hospitali ya St. Francis katika hilo eneo ya Rufaa ya Kanda, sasa wananchi wale hawawezi kuendeleza, hawawezi kupata mikopo, kwa sababu ardhi ile siyo ya kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo Mbunge mwenyewe nimetafuta hela nimepeleka katika Kata ya Mnadani fedha za zahanati, hatuna eneo la kujenga zahanati Baba Askofu anasema mpaka mmalize mgogoro wangu ndiyo nitawakatia eneo la kujenga zahanati. Kwa hiyo, maendeleo katika Kata ya Mnadani na Ifakara kwa ujumla yanakwama kutokana na mgogoro huu, viwanja hivi ni takribani elfu kumi tu, wananchi wale wapimiwe wapate hati zao waweze kwenda kukopa huko waweze kufanya maisha yao vizuri, tupate baraka za Baba Askofu, maana Baba Askofu unajua akishavaa madude yake yale anatisha Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, tunakuomba sana utusaidie jambo hili liishe na mimi sitaki kukukera hapa wala kuongea sana muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechangia ardhi kwa sababu ya agenda hiyo moja kubwa na Baba Askofu aliniambia sijui kama mlisoma wote anakufahamu vizuri, sasa mimi napata mashaka wewe Waziri huwezi kumsaidia Baba Askofu kwenye jambo la haki kama hili, mimi nataka kusikiliza majibu hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jafari Wambura Chege atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipatia nafasi na mimi kutoa mchango wangu kwenye Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimekuwa nikisema awali, mimi ni mdau lakini nimekuwa mtumishi zaidi ya miaka kumi kwenye Wizara hii. Kwa hiyo, nikisimama huwa napenda ni-*declare interest* kwa maana kwamba Wizara hii ndiyo imenilea, maoni yangu na ushauri wangu nitatoa kulingana na taaluma yangu niliyonayo kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo anapambana. Anatusaidia Wabunge lakini lengo lake ni jema kuhakikisha angalau kunakuwa kuna ustawi kwenye sekta ya ardhi kupunguza migogoro, angalau ardhi sasa iwe katika sehemu, itumike kama sehemu ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya, natambua changamoto zipo nyingi lakini kwa kuwa Wizara ndiyo Wizara Mama na inabeba sekta nyingi lazima mkutane nayo na nichukue nafasi hii kuwapongeza sana namna mnavyopambana kuhakikisha mnayatatua yale ambayo yanapaswa na mnaweza kuyafanyia kazi. Niwapongeze Watumishi ndani ya Wizara hii kwa namna ambavyo na wao wanaendelea kuhakikisha angalau nia na dhamira ya Mheshimiwa Rais inatimia kwa wakati wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema naunga mkono hoja mapendekezo ya Kamati yale yote yaliyotolewa na ninaamini kabisa yanatoka kwa nia njema Wizara imesikia na Serikali imesikia itakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo mawili leo ya kuchangia, kwanza ningetamani sana nichangie kuhusu chanzo cha migogoro nchini. Kwa *study* yangu ya kawaida tu inaniambia kwamba moja ya sababu ambayo inaweza kuwa inasababisha migogoro kwa sasa kwenye Taifa letu Tanzania ni kupitwa kwa

sera ya ardhi na maendeleo ya makazi hilo ni la kwanza kabisa kwa sababu sera tunayoitumia ni ya mwaka 1995 haiendani na kasi ya uzalishaji na shughuli za kiuchumi za wananchi wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *population* iliyokuwa wakati sera inatungwa 1995 haiwezi kuwa sawa na *population* ya sasa na namna ya shughuli za uzalishaji zinavyofanyika. Kwa hiyo, kwa namna moja au nyingine lazima kutakuwa na mwingiliano wa namna moja kwenda sehemu moja na sehemu nyingine. Pili ni kukosekana kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye ngazi za vijiji. Hili na lenyewe linaweza likawa linachangia kwa kiasi kikubwa sana; na jambo la tatu ni muingiliano wa Wizara za Kisekta, muingiliano kati ya Wizara ya Ardhi, Maliasili na TAMISEMI. Haya yote ya muingiliano huu wa shughuli za kiuchumi zinazofanyika yanatokana na kutokuwa na sera iliyopitwa na wakati. Ndiyo maana mimi nimekuwa nikikuomba sana kwamba jitahidi sana kwa namna moja inayowezekana sera ya ardhi ndiyo chimbuko na *solution* kubwa inayoweza kutatua changamoto hizi ambazo zinajitokeza kati ya muingiliano wa Wizara na Wizara lakini pia na maeneo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo hapa kuhusiana na migogoro. Utakubaliana na mimi, migogoro mingi ya ardhi kwenye maeneo mengi kwanza inatugombanisha Wabunge na wananchi lakini mbili inaigombanisha Serikali na wananchi, tatu inagombanisha Chama na wananchi, pia inagombanisha kati ya jamii moja ya wananchi sehemu moja na sehemu nyingine. Sasa kwa namna tunavyokwenda na kutatua migogoro tumeona migogoro mingine pia inatugombanisha kati ya Wabunge na Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kutokana na maelekezo wanayopewa ya kusimamia na kutatua ile migogoro na wengine hatupendi haya yatokee, kwa hiyo hii Mheshimiwa Waziri lazima uitazame sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano kwangu Rorya nina mgogoro, siwezi kuita ni mgogoro ni sintofahamu ya eneo la Utegi kati ya Kitongoji cha Kiwandani na Begi. Siwezi kuita mgogoro kwa sababu katika vijiji 975 vilivyoainishwa vyenya mgogoro nchini

ambavyo Mawaziri wanapita hivi vitongoji havimo, lakini unaweza ukaona sasa hivi tumekwenda tumetengeneza taharuki pale, tunawaambia wale wananchi zaidi ya kaya 300, wananchi zaidi ya 1,200 wahame hawalipwi fidia wanalipwa uwezeshaji peke yake, sasa tunataka kutengeneza mgogoro ambao hauna tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nichukue nafasi kukuomba sana Mheshimiwa Waziri kwa kipekee kabisa naamini hili unaliweza, jambo la kwanza twende na maoni ya wananchi wanacho sema. Wananchi wanasema kabla hatujafika huko, kwanza tusimamie Sheria ya kushirikishwa kwenye mikutano waambiwe dhumuni ni nini la wananchi kuondoka eneo lile na hii ndiyo Sheria ya uthamini inavyotaka. Ningeomba sana hili lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili wananchi hawa wasingependa uendelee utaratibu wa kuitwa wao ni wavamizi, wana miaka zaidi ya 60 pale, wana miaka zaidi ya 70. Shule ya Msingi pale imejengwa toka mwaka 1959, tukiwaita wavamizi kwamba waondoke bila kuwalipa tunakwenda kutengeneza mgogoro mwingine na lengo la Wizara ni kupunguza na kuzuia mgogoro, mimi kama Mbunge nisingependa kwenye kipindi changu hiki nizalishe mgogoro kwenye Wilaya yangu ya Rorya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo manufaa mengi ambayo tumeyapata kupitia kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais, tumepata maji, tumepata miundombinu ya barabara, nisingetamani tena tuende tukatengeneze mgogoro mwingine ambao utanikwamisha mimi kama Mbunge kutimiza wajibu wangu. Mheshimiwa Waziri ndiyo maana naomba sana haya matatu ambayo wananchi wanaomba, moja kushirikishwa kwenye vikao, mbili kutokuitwa hili jina, lakini tatu ikibainika wanatakiwa kuhama walipwe fidia stahiki kwa mujibu wa Sheria. Wale wananchi hawajagoma lakini wanachogoma ni ushirikishwaji na wanavyoona namna wanavyotaka kupelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri utakubaliana na mimi kabla tunakwenda kutamka juzi hakuna kiongozi aliyewahi kwenda kukaa nao wale wananchi akawaambia *ABC*, kwa hiyo ukija ukitamka vile maana yake unakwenda kutengeneza mgogoro mwingine ambao hauna tija na hauna afya kabisa kwenye Wilaya yangu ya Rorya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, lipo jambo linazungumzwa hapa na mimi niombe sana Mheshimiwa Waziri chukulia hii changamoto siwezi kuita changamoto, chukulia haya maoni ya Waheshimiwa Wabunge yanayotoka ndani ya Bunge kama ni sehemu ya kukutakia mema na wanakupenda sana na mimi nitajenga hoja kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ukurasa wa 120, Ibara ya 74 inasema, kwa miaka mitano kwa maana ya 2020 mpaka 2025, vijiji vinavyotakiwa kupangiwa matumizi bora ya ardhi ni 4,131 Ilani inatamka. Mpango wa Tatu wa maendeleo unasema angalau kufika 2025/2026 tuwe tumepanga matumizi bora ya ardhi. Naomba hapo nieleweke, kupanga matumizi bora ya ardhi sizungumzii kupima. Kupanga matumizi bora ya ardhi angalau kufikia asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais hapa ndani alipokuwa anahutubia Bunge alikazia hili kwamba angalau kufika 2025 tuwe tumepanga matumizi bora ya ardhi ya asilimia 50 ya vijiji vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji tulivyonavyo sasa ni 12,318, tulivyopanga toka uhuru ni elfu mbili mia nane kumi na kitu, maana yake ni asilimia 23 peke yake, lakini kwa miaka mitatu ilikuendana na Ilani, ilikuendana na mpango, ili kuendana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwa miaka mitatu tumepanga vijiji 681 peke yake. Wabunge wanachosema Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa haya yote tunatambua ambao tumekuwa kwenye Wizara hii muda mrefu tunajua yote haya yamekuwa ni changamoto kwa sababu ya ukosefu wa fedha, tunashindwa kutimiza haya matatu ambayo ni maelekezo kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri sasa umepata fedha, tumepewa mkopo zaidi ya bilioni 345 tunachotakiwa pale ni kutenga bilioni 60 peke yake unakwenda kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kupanga vijiji vyote 4,131, unakwenda kutekeleza mpango wa tatu wa uchaguzi, unakwenda kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais lakini utakwenda kutengeneza *legacy* kubwa sana kwenye nchi hii kwa sababu kutoka uhuru wewe ndiyo utakuwa umepanga matumizi ya vijiji vingi kuliko wakati mwingine wowote, utakuwa umetengeneza *legacy* kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais. Kwa sababu kama toka uhuru tunazungumza vijiji 2,600 tukipeana miaka mitano sasa tukapanga vijiji elfu nne na kidogo maana yake Mheshimiwa Waziri unakwenda kutengeneza *legacy* na wataalam ambao tuko kwenye sekta ya ardhi hatutakusahau kwenye hili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ndiyo maana, mimi nikuombe maoni yote ya Waheshimiwa Wabunge yanayotolewa humu yachukue kama sehemu ya kuboresha ili angalau tuende tufike mahali fulani. Tunaamini uwezo wako, tunaamini unaliweza hili, kama utachukua haya yanayozungumzwa ukafanya *adjustment* ya ule mkopo, uka-*impose* fedha kwenye Tume ya Mipango, ukaipa maelekezo kuhakikisha wanapanga matumizi bora ya vijiji hivi kupunguza migogoro, utakuwa umefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuambie Mheshimwa Waziri migogoro hii haina tija kwetu kwanza kama nilivyosema inatugombanisha na wananchi lakini kutokupanga matumizi maana yake umepunguza thamani ya kile Kijiji chenye ardhi, lakini pili inatusumbua sana wanapokuja wawekezaji. Leo akija mwekezaji ambaye anataka kuwekeza Wilaya ya Roya hatuna *land bank*, hakuna mahali anapofika akaambiwa hili eneo ni kwa ajili ya viwanda ukienda Wilaya ya Rorya, hili ni kwa ajili ya kilimo, hili ni kwa ajili ya ufugaji, hili huwezi kwenda kwa sababu kuna hifadhi, kwa sababu eneo lote limepangwa matumizi halisi, hiyo *land bank* hakuna kwa hiyo Mheshimiwa Waziri mimi nikuombe sana kwa unyenyekevu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanayozungumzwa kwa sababu yamezungumzwa na Kamati, tumeyashauri mwaka jana tumeyashauri mwaka huu kama kuna uwezekano wa kufanya *adjustment* ya mkopo huu ili kuleta maslahai ya Taifa, ili kwenda kugusa maeneo mengi, kupunguza migogoro ya Wabunge wanayozungumza humu, ningetamani sana ulione hili na hili linkwenda kukubeba mimi nikutie moyo kwa namna yoyote hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na kama kuna mtu anakwambia hili litakuharibikia haliwezi, ndiyo maana nikasema unakwenda kutengeneza historia kwa kupunguza migogoro ya wananchi wanaumizana kule nje. Mheshimiwa Waziri mimi naamini sidhani kama unapendezwa leo tuko hapa ndani unasikia kati ya mkulima na mfugaji wanapigana, unasikia kati ya maeneo ya hifadhi wananchi wameingilia. Kuna maeneo ya vishoroba ambayo Tembo wanapita kwenye vishoroba wanaingia kwenye maeneo ya wananchi, wananchi wanakufa maeneo yale, kwa nini hakuna mpango bora wa matumizi ya ardhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza sekta ya maliasili wanakuambia *solution* hapa ni kupanga matumizi bora ya ardhi kwenye maeneo haya. Mheshimiwa Waziri nikuombe kwa haya ambayo nimeyasema mimi naamini kabisa kesho utakuja kuyatolea maelezo vizuri na niseme tu kweli kesho nisiporidhika nitakuwa miongoni mwa watu wa kushika shilingi kwenye hili ili angalau niweze kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro ajiandae.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya mimi kuwa mchangiaji katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii muhimu ya Ardhi ambayo kimsingi imeshika hatma ya Wabunge wengi ndani ya Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mtovu wa fadhila kama sitaanza mchango wangu kwa kumshukuru Rais wetu Mama yetu Samia Suluhu Hassan pamoja na Watendaji wake wa Wizara ya Ardhi kwa jitihada ambazo wanazionesha kuziwezesha Halmashauri zetu kupata fedha kwa ajili ya kupima maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya Halmashauri ambazo zimefaidika na fedha hizo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na Jimbo la Mikumi hasa pale Makao Makuu ya Jimbo la Mikumi, tumepata fedha za kutosha ambapo tumepima viwanja zaidi ya 2,000. Hatujawahi kupima tangu uhuru na zoezi hili linaashiria *commitment* ya Serikali katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba ifikapo 2025 asilimia 50 ya maeneo ya nchi yetu yatakuwa yamepimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo pale Ruaha kuna Miji ambayo inakua kwa kasi sana *peri urban,* Tanzania nzima ukienda ambazo watu wanawahi kujenga kabla ya Serikali kufika kupima, kupanga na kumilikisha. Matokeo yake ni nini? Tunaona *slams* zinatengenezwa halafu Serikali inakuja baadae kurasimisha, sasa ni mapendekezo yangu kwamba ni vema fedha ambazo tumezipata kama mkopo kuhakikisha kwamba tunaenda kupima maeneo yote ili wananchi wanapofika au wanapohitaji ardhi waende kwenye maeneo ambayo yamepimwa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mpango wa matumizi bora ya ardhi, Watanzania wanaongezeka na tunazaliana kweli, lakini ardhi ya Tanzania haiwezi kuongezeka na haitakuja kuongezeka. Namna tunavyoenenda ni kana kwamba tuna nafasi ya kuongeza ardhi ya Tanzania, namna ya ujenzi wa majengo yetu tunayojenga hata hapa Dodoma, tunaweza kuona wazee wetu miaka ya 1970 walivyotengeneza Mji wa *Area D,* pale kuna *Site One, Site Two,* kuna *Site Three* lakini unaanza kujiuliza *Site Four, Site Five, Site Six* ziko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona maeneo yamepimwa katika viwanja vidogovidogo vya *square meter* 200, 300, 400 hivi haturudi nyuma kujiuliza wale wazee wakati huo miaka ya 1970,

1980 wakati Dodoma sehemu kubwa ikiwa Jangwa ikiwa pori hawakuona sababu ya kujenga hivi vibanda ambavyo tunavijenga katika kila mtaa? Kwa nini walijenga magorofa pale *Area D*, ambayo yamekaa kimpango ambayo sasa hivi hayapatikana kila Mbunge anatamani kwenda kukaa pale na hawapati nafasi, lakini ni mawazo ya watu ambao walitutangulia. Kwa hiyo, suala la uendelezaji wa makazi ni muhimu kama lilivyo suala la kupima, kupanga na kuendeleza ardhi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili hatuwezi kulifikia kwa kutegemea fedha na bajeti ya Serikali. Ni vizuri Serikali ikakaa ikatafakari namna bora ya kushirikisha sekta binafsi, kuziwezesha, kuweka *incentive* wajenge majengo mengi kwa gharama nafuu ili iwe gharama kubwa kwa mtu kujenga nyumba yake binafsi badala ya kununua *apartment*, kwa kufanya hivyo Serikali itakuwa imepanga watu wake, inaweza ikakusanya mapato makubwa zaidi kwa sababu wanakaa katika maeneo ambayo yanaeleweka na kufahamika ambayo yamepimwa na yana hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu suala la migogoro. Sisi watu wa Kilosa tuna migogoro ya ardhi katika maeneo mawili. Moja, kati ya wafugaji na wakulima; na pili, kati ya hifadhi na wananchi. Tunashukuru kuna jitihada za Serikali ambazo zinaendelea kufanyika. Kipekee kabisa namshukuru Kamishna wa Ardhi wa Mkoa wa Morogoro, ndugu yangu Frank, amejitahidi na anajitahidi na hata wiki iliyopita alikuwa katika vijiji kwa ajili ya kuondoa changamoto kati ya wananchi na mipaka ya vijiji kule Ukwiva na Paulanga katika Kata ya Kisanga lakini pia Kata ya Ulaya na kule Kilangali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro hii iko katika kila sehemu ya Tanzania. Ziara ya Mawaziri nane walikuja Morogoro, kwa bahati mbaya hawakufika Mikumi, na sina hakika kama watakuwa na uwezo ama watakuja kuwa na nafasi ya kupita katika kila eneo la Tanzania. Ni vizuri tukaweka mifumo ambapo kila mmoja kwa nafasi yake aiheshimu. Wananchi pale wanalalamika kwamba mipaka ya *TFS*, mipaka ya hifadhi inahama. Kwa nini mipaka ya hifadhi ihame? Kwa nini kuwe na ramani zaidi ya tatu ambazo zinatafsiri mipaka tofauti? Kuna *GN*

ngapi kwenye hii nchi? Kuna Serikali ngapi ambazo zinaweza zikafanya maamuzi ya mipaka kati ya wananchi na hifadhi na kati ya wananchi na vijiji? Kwa hiyo, ni vizuri tukaangalia suala zima la *GN* na mipaka katika jitihada za kutatua migogoro kati ya wananchi na hifadhi na kati ya wafugaji na wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la matumizi bora ya ardhi. Kuna changamoto. Kuna Wabunge wamechangia suala hili, lakini mimi nina mfano. Pale Kata ya Zombo kwenye Jimbo la Mikumi, kuna Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi na wananchi wametengeneza utaratibu wao, lakini wanapochukua hatua hawapati *support* ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Kwa mfano, Machi, 2022 kulikuwa na wimbi la ng'ombe zaidi ya 2,000 zilivamia mashamba ya watu, wakatozwa kwa sababu hawakufuata Sheria ya matumizi bora ya ardhi. Polisi wakaingilia. Mpaka leo faini halali ambayo imetozwa na Kijiji haijalipwa, na hakuna jitihada ambazo zinaonesha kwamba kuna usimamizi wa Sheria ambayo imewekwa na wanakijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatuwezi kuheshimu sheria ambayo imewekwa na mamlaka ya Kijiji: Je, ni sheria zipi ambazo tunaweza kuziheshimu? Tutambue kwamba Serikali ya Kijiji ni Serikali kamili, ni Serikali ambayo iko kikatiba, ni Serikali ambayo ina kauli thabiti na lazima iheshimiwe na vyombo vyetu lazima visaidie Serikali za Vijiji katika utekelezaji wa maamuzi ya Serikali za Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni maeneo ya huduma za jamii, yanahangaikia kodi. Tunatoza kodi kubwa kwenye maeneo ya huduma za jamii kama hospitali, kama shule. Pale Mikumi kuna hospitali ya *St. Kizito* ambayo ni hospitali teule inayohudumia wananchi wa kipato cha chini pale katika Jimbo la Mikumi, Wilaya ya Kilosa na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi ya ardhi ambayo wanatozwa ambapo kimsingi anatozwa mgonjwa ni kubwa sana ambayo inakwenda kudumaza ubora wa huduma ambazo zinatolewa na hiyo hospitali. Ni vizuri Serikali ikaangalia maeneo ambayo yanatoa huduma kama siyo chanzo kikuu cha mapato kupitia

ardhi. Kwa sababu unapotoza kodi ya ardhi katika maeneo hayo, maana yake unamtoza mgonjwa ama mwanafunzi ambaye anahudumiwa ama anapata huduma kutoka kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Sheria Na. 7 ya Ardhi ambayo inatambua Serikali za Mitaa kama Msimamizi wa Kupima, Kupanga na Kumilikisha. Kwenye eneo hili tunaona *masterplan* mbalimbali na maeneo mengine hayana *masterplan,* lakini hata maeneo ambayo yana *masterplan* unaona kinachojengwa ama kinachoendelezwa ni *contrary* na *masterplan.* Sasa, hapa nani tumchune ngozi? Ni Wizara ya Ardhi ambayo ina dhamana ya kusimamia ama Wizara ya TAMISEMI ambayo ina wajibu wa kusimamia Sheria hii Na. 7?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili napenda nishauri suala zima la mawasiliano na mahusiano kati ya taasisi na Wizara za Serikali. Ni vizuri Wizara ya Ardhi, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Maliasili zikawa na mawasiliano ya karibu katika kusimamia na kuendeleza ardhi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuona hata ile asilimia 30 ya *retention fee* ambayo ilikuwa inarudi katika halmashauri kama *incentive* ya kuendelea kusimamia ardhi, hairudi tena. Matokeo yake yamekwenda kufubaza jitihada za halmashauri katika kusimamia suala la ardhi katika halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutazungumza kwamba Serikali ni moja, ni vizuri kukawa na uratibu hasa linapokuja suala la ardhi. Kinachoendelea katika maeneo mbalimbali ya halmashauri zetu hakiakisi ukweli kwamba tunaishi katika karne ya 21. Ukienda kwenye maeneo ya taasisi mbalimbali za Serikali, unaweza kuona nyumba ambazo zimejengwa miaka ya 50, 60, 70, zimejengwa siyo kwa gharama lakini zimejengwa kwa mpango na zinavutia. Ukiangalia kile ambacho kinafanyika sasa hivi, viwanja vinavyomegwa, viwanja vinavyogwanywa, haviakisi uhalisia kwamba ardhi hii tumepewa kizazi hiki kama dharama kwa ajili ya kurithisha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalize kwa kusema kwamba, ni vema tuka – *review* Sera ya Ardhi ya Mwaka 1995. Je, itatupeleka tunakotaka kwenda? Watanzania wanaongezeka na sensa tumeiona. Hii sensa ina-*reflect* vipi katika mikakati ya halmashauri kwenda kutimiza malengo yake, kupima maeneo yote na kuendeleza miji midogo midogo, kwa mfano, Mikumi, Ruaha, Kibodi, Ulaya na Masanze? Haya yote ni maeneo ambayo yanakua kwa kasi na tunahitaji Serikali kuona inachangia vipi katika kupima, kupanga na kumilikisha ili watu wasiende kujenga bila utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dennis. Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, ajiandae.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kupata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Ardhi. Kwanza kabisa, naungana na wenzangu kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais, kwa namna ambavyo anaendelea kulihudumia Taifa, lakini kwa maslahi mapana ya wanajimbo la Kibaha Vijijini, namshukuru yeye kwa kutenga pesa nyingi na kuendeleza Mji wa Kwala ambalo limewekwa kongani kubwa ya viwanda ambayo inakwenda kujengwa katika eneo lile na kuufanya Mji wa Kwala kuwa mji mkubwa kabisa katika Miji ya Tanzania. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo anaendelea kupambana na changamoto mbalimbali anazokabiliananazo ambazo zinaelezwa na Wabunge mbalimbali kutoka katika kila Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitakuwa na maeneo machache sana ya kuchangia kwenye eneo hili. Eneo langu la kwanza ambalo nitapenda kuchangia ni eneo la utawala wa ardhi. Tunafahamu sehemu ya utawala wa ardhi inahusisha mambo kadhaa ikiwemo masuala mazima ya migogoro ya ardhi, ugawaji wa ardhi, usimamizi wa masharti ya umilikishwaji pamoja na usajili wa hatimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwanza kwenye eneo hili la migogoro. Naomba nitumie hadhara hii kuwasilisha migogoro ambayo inapatikana jimboni Kibaha. Nimesukumwa kufanya hivi baada ya kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kugundua kuwa alitembea Mikoa yote ya Tanzania Bara na kwetu Pwani alifika, na alipofika Pwani katika taarifa yake inaonesha kwamba alishughulika na migogoro 83. Nikapata taabu sasa hii migogoro 83 ni ndani ya hii ambayo ninayo Kibaha Vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu sikuwa na kinachonionesha kwamba katika migogoro hii 83 iliyoshughulikiwa Mkoa wa Pwani, ya Kibaha Vijijini ni mingapi, basi nitumie nafasi hii kuwasilisha migogoro hii kwa Mheshimiwa Waziri ili aone namna bora ya kuishughulikia. Japo ipo migogoro mingine, ninaamini kabisa ilishashughulikiwa, lakini tatizo Wizara au Serikali haijarudi kwa wananchi kutoa msimamo au kauli ya Serikali kwamba mgogoro huo umemalizwa kwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuelezea migogoro ya mipaka ya maeneo ya kiutawala. Pale Kibaha Vijijini tuna migogoro ya kiutawala na mamlaka nyingine za halmashauri. Kwa mfano, tuna mgogoro mkubwa sana wa mpaka wa Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Morogoro, kule kwenye kipande cha Kata yangu ya Magindu. Ni mgogoro ambao una muda mrefu. Zipo hatua ambazo zinaonekana zimechukuliwa, lakini wananchi kule bado hawana uhakika na nini kimefanyika kwa sababu hawana majibu ya jambo lililofanyika. Kwa hiyo, napenda waufahamu mgogoro huo kama sehemu ya mgogoro mmojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro mwingine pale Kibaha tena mgogoro wa Kibaha *DC* pamoja Kisarawe. Kuna shida sana kwenye eneo la Kata ya Kikongo, kwenye upande ule kwa sababu kuna mgogoro mkubwa unaozungumzwa miaka nenda miaka rudi, lakini haupati ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro mwingine, tena mgogoro huu unachekesha sana. Kibaha vijijini ndiyo imeizaa Kibaha Mji, lakini cha kuchekesha leo, eti kuna mgogoro wa

mpaka kati ya Kibaha Mji na Kibaha Vijijini. Sasa unashangaa, wa kuulizwa ni Kibaha Vijijini, ulimkatia mwenzio mpaka wapi? Leo nashangaa mgogoro unakua tu, unaendelea tu, haupatiwi ufumbuzi wakati wa kuulizwa tupo na tungeweza kuwaambia hawa wanetu wakati wanazaliwa tuliwapa mpaka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna tatizo la kwenye kutoa maamuzi ya migogoro na sijui inasababishwa na nini? Kwa sababu kama hii migogoro ya mipaka ni kazi nyepesi tu, ni Serikali kutoa tamko kwamba kuanzia hapa sasa ndiyo kutakuwa kunaitwa mpaka, sasa tuone atakayebisha. Kwa sababu kila mmoja atakuwa hahami na kila mwananchi atakuwa anakaa kwenye eneo lake, anaendelea na shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama wananchi hawasikii nini kimetamkwa na Serikali, utabaki ugomvi unaoonekana kati ya Wabunge na Wabunge au Wabunge na Wakuu wa Wilaya kitu ambacho hakuna sababu ya kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, kuna migogoro ya wakulima na wafugaji. Kuna maeneo yametengwa kwa ajili ya wakulima na kuna maeneo yametengwa kwa ajili ya wafugaji. Sasa kuna maeneo yana migogoro ya mipaka; wafugaji na wakulima wanaambiana mimi naishia hapa na mimi naishia hapa. Kwangu pale katika Kata ya Gwata kuna Kijiji cha Kigoda na Kijiji cha Ndwati, wanagombana kitu ambacho kinahitaji majibu mepesi tu. Kwa hiyo, naiomba Wizara ingefanya hivi kwenye kutoa matamshi ilimradi kila mmoja ajue anaishia wapi na mambo mengine yaendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano pia kuna ndugu yangu wa Chalinze, bahati mbaya hayuko hapa, lakini ngoja niseme kidogo. Wapo wananchi wanatokea katika Jimbo la Kibaha Vijijini, walikuwa na maeneo yao ya urithi katika maeneo ya Mbala na hili jambo nilikwenda nalo mpaka kwa Naibu Waziri, nilijaribu kumhusisha, lakini inaonekana kwamba sasa hivi pale wanasema ni Kijiji cha wafugaji. Matokeo yake wale wafugaji wanawaondoa wananchi wa asili kwamba, sisi tulishapewa hapa ni kwetu, ninyi hamstahili kufanya shughuli katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia, yanatokea masuala ya sintofahamu, wananchi hawa waende wapi? Kama wao walizaliwa pale, wenzao wamekuja wameoneshwa sehemu ya kuishi, leo wanataka kuchukua kijiji kizima. Nafikiri ni vizuri jambo hili likazungumzwa. Nimeamua niseme hapa kwa sababu ni sehemu ya watu wanaoathirika katika Jimbo la Kibaha Vijijini pamoja na eneo la Chalinze kwenye eneo la Mbala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, upo mgogoro kwenye Kijiji cha Mwembengozi. Wizara ya Ardhi, kupitia pia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, pale Kwala ambapo ndiyo tumejenga bandari kavu, ambapo ndiyo imetengwa kongani ya viwanda, eneo kubwa lilikuwa linamilikiwa na Serikali, lakini kwa umuhimu wa kuwekeza bandari kavu, kwa umuhimu wa kuwekeza kongani ya viwanda, waliamua kupunguza eneo na kuliweka katika mazingira haya ambayo yanatumika kwa shughuli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lipo tatizo pale Mwembengozi. Sote tunafahamu kwamba Sheria ya Ardhi inaruhusu Serikali za Vijiji kwa mamlaka walizonazo kisheria kugawa ardhi na wamegawa baadhi ya ardhi kwa wawekezaji. Leo pale Mwembengozi walipokuja na hili suala la kongani ya viwanda, Serikali imekwenda pale Mwembengozi, wanawaambia wale wote waliopewa na Serikali za Vijiji hawawatambui. Hawawatambu eti kwa sababu eneo hili lilikuwa ni la kilimo. Wananchi wanashangaa, ni eneo la kilimo tangu lini? Kijiji kile kipo pale miaka mingi, na mihtasari ya kuwapa wawekezaji hawa Kijiji wameitoa kwa mujibu wa sheria, na imepitishwa kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumeamua kubadilisha matumizi, tunawapora mamlaka ya ugawaji wa ardhi na kuwaona kwamba hawana mamlaka ya ugawaji ardhi. Sasa jambo hili limeleta mgogoro mkubwa, kesi hizi haziishi. Mkuu wa Mkoa amekwenda pale, ameunda tume, lakini watu hawaelewani. Kwa hiyo, namwomba Waziri, kupitia viongozi wa ardhi, hasa wale makamishina wa ardhi, hebu hii migogoro midogo midogo waende wakaitolee tamko ili ionekane imekwisha na mambo haya yaende kwa utaratibu unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema leo nitajielekeza sana kwenye migogoro, kwa sababu sina hakika kama ni hii migogoro 83 ya Mkoa wa Pwani imezungumzwa. Ukienda kwenye Kata ya Kikongo na Mheshimiwa Waziri anafahamu kwa sababu kabla hajawa Waziri jambo hili lilifikishwa kwake kwa muda mrefu sana. Pale Kikongo tulikuwa na shamba la *UFC*. Wananchi wanafahamu Shamba la *UFC* linaishia wapi, na lipo eneo ambalo lilibaki kwa ajili ya wananchi wanaendelea na maisha yao. Pia kulikuwa na maeneo ya kijiji ambayo kuna mtu anaitwa *Transcontinental, anadai* kwamba yeye amenunua. Vikao vyote vya ngazi ya Wilaya na Mkoa vimeenda. *Transcontinental* anaambiwa alete nyaraka za kuonesha amepataje maeneo hayo? Hana nyaraka. Leo anasumbua wananchi katika eneo lile, anataka wananchi wale watoke, wampishe eneo lile amiliki yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna taabu na maswali ya kawaida wananchi kule wanajiuliza, huyu *Transcontinental* kama anakiri yeye alinunua, nyaraka zake za kununua kutoka kwa wananchi ziko wapi? Kama anakiri alipewa hati, nani alimfanya athibitishwe apewe hati wakati vijiji vinakataa havimtambui? Kwa hiyo, kuna migogoro mingine hii inakuzwa na namna ya watendaji wetu wanavyofanya kazi. Wanashindwa kutoa majibu ya moja kwa moja ili mambo haya yaishe na mambo mengine yaendelee. Kutofanya hivyo, wananchi hawa wanaingia kwenye mgongano mkubwa sana na sisi viongozi tuliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo naomba niliseme hapa pasipo uwoga kwamba, jamani tuko wote hapa tumeingia kwa utaratibu wa siasa, na kila mmoja anacho chama ambacho anajua kabisa kinaweza kikatetea masilahi yake. Chama cha Mapinduzi ambacho wananchi wamekiamini kwa asilimia kubwa na wananchi wanaamini hakishindwi kumaliza migogoro hii, nimekwenda pale mpaka na Mwenyekiti wa Mkoa wa Chama cha Mapinduzi, amemwomba Kamishina wa Mkoa asaidie kumaliza tatizo hili, mpaka leo majibu hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba ndugu zangu, naiomba Wizara iende ikachukue hatua pale tumalize hii migogoro ambayo ipo. Kwa sababu ya muda nitaiweka vizuri

kwenye maandishi na nitaikabidhi pale Wizarani ili waone namna bora ya kuishughulikia migogoro hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, nimesema nimempongeza Mheshimiwa Rais, kwa namna ambavyo ametutengea lile eneo la Kwala kuwa eneo la kongani ya viwanda lakini pia kuufanya kuwa mji mkubwa wa uwekezaji. Hata hivyo, nataka niende sambamba na jambo zima la kutengeneza makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kongani pale Kwala, tuna heka 1,000 pale Bisunyala na ndani ya eneo kubwa ambalo Serikali wamepima, lakini sina hakika kama uwekezaji huu wa viwanda unaoendelea pale, unakwenda sambamba na sisi kujenga majengo ya kuweza kuwapokea watumishi wanaokuja pale. Kwa sababu maeneo yote yale ya karibu yamepimwa kwa ajili ya viwanda. Je, wananchi watakaokuja kufanya kazi pale, wanaweza kufanya kazi wakiwa wanaishi kwenye maeneo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba kwa sababu tuna shirika letu la ujenzi wa majumba, ni vizuri wangeenda pale wakatengewa na wao maeneo sasa hivi. Wakati viwanda vinaendelea kujengwa, na wao wajenge maeneo hayo ili wananchi waweze kuishi kwenye maeneo hayo, na kwa kufanya hivyo mji ndiyo unaweza ukawa vizuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona unanitazama kwa ajili ya muda, basi niungane na Wabunge wote ambao wameipongeza Serikali, nami naunga mkono hoja. Naomba tu Waziri aje kunisaidia kumaliza ile migogoro ambayo iko pale jimboni kwangu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga na Mheshimiwa Deus Clement Sangu ajiandae.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa. Kwanza nianze kwa kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuonesha mapenzi makubwa sana kwa Watanzania hasa pale alipoagiza migogoro yote ya ardhi nchini iende ikatatuliwe. Rais ameonesha mapenzi makubwa sana kwa Watanzania. Sisi Wabunge tunamuunga mkono, Watanzania wote wanamuunga mkono, wanasubiria kuona hatua za Serikali za kutatua migogoro hiyo mmoja baada ya mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ngara walioniamini mwaka 2020 wakanituma nije hapa Bungeni kuweza kuwatetea na kuwasemea kuhakikisha kwamba Serikali inatatua changamoto mbambali zinazowakabili. Nitaendelea kuwa mwaminifu kwa wananchi wa Jimbo la Ngara, nitaendelea kuwasemea na kuwatetea kwa kadri Mwenyezi Mungu anavyoniwezesha. Niendelee kuwaomba waendelee kuwa na imani kubwa juu yangu, mambo yao ninayashughulikia moja baada ya lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la kwanza ambalo nachangia hapa ni mgogoro wa ardhi baina ya Kijiji cha Rusumo na Gereza la Rusumo, mgogoro ulioletwa na Afisa wa Ardhi ambaye mamlaka yake ya kinidhamu iko chini ya Wizara ya Ardhi. Afisa huyu kwa kushirikiana na viongozi wa Gereza la Rusumo walikwenda wakajifungia kwenye chumba wakachukua *laptop* na *mouse* wakaweka pale, wakaweka na *software* wakaanza ku-*generate coordinates,* wakapima eneo kwamba eneo linalomilikiwa na Gereza la Rusumo ni hili, wakapima kwa kutumia *Computer.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya jambo hili walilofanya ni kwamba *coordinates* ya kwanza (majira ya nukta) yaliangukia *kwenye noman's land* kwenye mto ambao tunaumiliki Tanzania na Taifa lingine. Hapa nimetumia neno la kidiplomasia kidogo. *Coordinate* nyingine ambayo walii-*generate* kwenye *laptop*, inanonekana sasa magereza wanamiliki eneo ambalo linamilikiwa pia na *TANAPA*. Wakati huo huo, *coordinates* nyingine wame-

*generate,* Magereza wanamiliki barabara ya kimataifa ambayo ilikuwepo hata kabla ya gereza lenyewe kwenda pale. Sasa matokeo yake wametuletea matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Wilaya ya Ngara Kanali Mathias Kahabi, aliunda tume ya kwenda kuchunguza, nami nilishiriki tukatumia kifaa kinaitwa *real time kinematics (RTK)* kwa ajili ya ku-*verify,* tukakutana na madudu makubwa. Sasa wakati nawasubiria kwa hamu Wizara ya Mamabo ya Ndani, na kwa sababu wanajua walichokifanya mwaka 2022, Mheshimiwa Jenista Mhagama unakumbuka, lile swali langu la mgogoro wa Rusumo ulivyokuja hapa Bungeni, Magereza wakaidanganya Serikali kwamba hakujawahi kutokea mgogoro. Nikasema Mheshimiwa Jenista Mhagama tupilia mbali hilo, hayo majibu siyahitaji. Ukayatupilia mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati nawasubiria kwa hamu Wizara ya Mambo ya Ndani, na nimemwambia Mheshimiwa Masauni mara nyingi kwamba, wanampotosha Magereza. Naomba Wizara ya Ardhi mshughulike na huyu Afisa wa Ardhi ambaye ametuletea matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshazungumza na Katibu Mkuu, ninasubiria utendaji. Wananchi wa Rusumo wanasubiria kuona mnachokifanya, namna mnavyo mshughulikia huyo Afisa wa Ardhi ambaye ametuletea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la 2025 limeshakaa vizuri maeneo mengi, naomba msiniharibie, naomba huu mgogoro muende muuondoe mara moja kwa sababu kitu kimeshakaa kibra 2025, nataka nipite kwa kuogelea. Sasa, nataka nikuombe Mheshimiwa Waziri, nenda kamalize ule mgogoro, shughulika na yule mtu wako, na mimi nitaendelea kuhangaika na watu wa Wizara ya Mambo ya Ndani nao waweze kufanya kwa upande wao. Ndiyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nichangie ni namna ambavyo Wizara ya Ardhi inafanya utafiti wa kujua viwango vya fidia kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini.

kule Ngara kuna mchakato wa *disclosure* unaoendelea ambao Mthamini Mkuu wa Serikali ambaye yuko hapa Bungeni ameusimamia, mama mmoja Mrs. Zuhura Hiraly aliachiwa nyumba na baba yake mwaka 1943; hii nyumba wameenda kuifanyia uthamini wanataka kumlipa shilingi laki saba. Mama huyo pia aliachiwa nyumba na mme wake tena mwaka 1950 wanataka kumlipa shilingi milioni moja na laki mbili. Hiyo fedha haitoshi hata kujenga banda la kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule mama amesema nendeni mkabomoe lile eneo bomoeni majumba bomoeni kila kitu mkachukue hahitaji hiyo fedha kwa sababu haina uhalisia. Nimezungumza na Mthamini Mkuu wa Serikali, nikamwambia utaratibu huu wa kuibua viwango vya fidia vinavyo akisi thamani halisi ya majumba ya watu na ardhi za watu maeneo mbalimbali nchini vinatakiwa viangaliwe upya, viwe shirikishi na viweze kuakisi thamani halisi ya mali nyumba na viwanjanya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi viwango mnavyovitumia inawezekena na vyenyewe vime-*expire* kama ilivyo sera ambayo imepitwa na wakati, inawezekana vyote hivi vinatakiwa kwa pamoja viweze kupitiwa viangaliwe tuvi-*set* upya. Nimeambiwa wanamtafuta *consultant* anakwenda vijiini anakusanya mikataba anaandika ripoti anawasilisha kwa *valuer* wa Serikali. Sasa anayetaka kulipa hela ni Serikali anayefanya *valuation* ni Serikali katika ule mchakatohakuna *stakeholders' engagement* ili muweze kupata *second opinion* kwamba hiki siyo sawa hiki ni sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninataka niwaombe Wizara ya Ardhi, kwanza wananchi wangu wote wanaofidiwa kuanzia kule Mrusagamba kwenda Rurenge kwenda Tembonikeili kwenda Mrugarama kule mhakikishe mnatenda haki mmeenda kwa Diwani wa Kabanga Hafidhi Abdallah amechukua kiwanja amekinunua milioni tano mnataka kumpa laki saba, haiwezekani, haiwezekeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niwaombe mwende mkapitie ule mchakato upya ndugu yangu *government valuer*,

Waziri nendeni mkapitie mchakato upya, nendeni mkatende haki. Mtu anapewa shilingi 70,000 uliona wapi fidia ya mali ya shilingi 70,000? Naomba mwende mkapitie upya na mfanye haraka na msicheleweshe barabara yetu ya lami kwa sababu nyie ndio ambao mnaleta vitu ambavyo kwa kweli vinafikirisha. Kwa hiyo ninaomba eneo hili lifanyiwe kazi na wananchi wangu wote waweze kupata haki kwa wakati na barabara yetu isicheleweshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo nataka nichangie ni eneo la kuwezesha Wizara yenyewe ya Ardhi iweze kupima na kupanga maeneo mbalimbali ya kimkakati hapa nchini. Haiwezekani kwamba tunaongelea kwenda kupima vijiji tu badala ya kutafuta maeneo ya kimkakati, maeneo ya mpakani, miji inayokua, maeneo ambayo yanaweza yakarudisha fedha haraka haraka, maeneo yenye mzunguko wa hela ndiyo twende tukayapime ili Watanzania waweze kumiliki viwanja, waweze kupata hati, waweze kukopesheka na nchi yetu iweze kuendelea. Ifike mahali makusanyo yanayotokana na ardhi yaweze kutusaidia Watanzania kujiendesha kama Taifa. Eneo hilo halijatendewa haki vizuri

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika kuona kinachoendelea. Shilingi bilioni 80 zina uwezo wa kupima viwanja 368,000 kwa mika mitano. Narudia, shilingi bilioni 51 zina uwezo wa kupima viwanja 368, 000 kwa mika mitano. Hii shilingi bilioni 51 ikitengwa itarejesha shilingi bilioni 80 katika kipindi kile, kwa sababu ardhi moja itakayopimwa, yaani kiwanja kimoja, *average* ya malipo ambayo mwananchi wa kawaida anatakiwa kulipa ni shilingi laki mbili hadi shilingi elfu ishirini. Ukizidisha fedha hizi utakuta kwamba upimaji wa ardhi unalipa kuliko kitu chochote kile. Unatumia bilioni 51.5 unarudisha bilioni 80. Ni kwa nini tusitenge fedha tukaenda kupima ardhi ya Watanzania? Ni sababu gani inasababisha tuwe na kigugumizi kutenga fedha? Tumetoa fedha kwa ajili ya kupunguza bei ya mafuta nchini ili iweze kushuka. Sasa, kule tulikokuwa tunatoa fedha zile tuchukue fedha nyingine tuweke kwenye ardhi tuwasaidie Watanzania kupima ardhi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu asubuhi watu wamesema, kwamba wale watu wa ardhi wanapima ardhi kule na fedha yote inakwenda Serikali Kuu, matokeo yake watu wanatembea hata mafuta ya kuweza kutoka eneo moja kwenda jingine hawana. Ofisi zile za ardhi zilizoko Serikali za Mitaa ambazo pia nyie mnawajibika hazina kabisa fedha kwa ajili ya kuendeshea shughuli za upimaji, matokeo yake hakuna kazi kule inayofanyika. Zile Ofisi zimegeuka kutegemea wapimaji binafsi ambao wanakwenda kupima maeneo madogo yasiyo tosheleza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa muda wako umekwisha

**MHE. NDAISABA G. RUHORO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumalizia, ninaomba Serikali iwaachie asilimia 30 ya makusanyo yote yanayotokana na ardhi ili Ofisi zile ziweze kujiendesha na zifanye upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** ahsante sana, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Clement Sangu Mheshimiwa Ally Juma Makoa, ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niungane na Wabunge wenzangu wote waliompongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa kipaumbele kwenye sekta hii ya ardhi. Hali kadhalika nimpongeze sana Mheshimiwa Angeline Mabula, Waziri wa Ardhi na mlezi wangu, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalamu wote wa sekta hii ya ardhi. Nitakuwa pia mchoyo wa fadhila nisipo mpongeza Mthamini Mkuu, mthamini amesimamia zoezi la uthamini wa fidia vizuri kule Rudewa; aliitwa kwenda kuhakiki

akaenda na wataalamu wake, na hivi sasa ninavyozungumza wananchi wanalipwa fidia ya bilioni 15.4. Kwa hiyo niipongeze sana Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi niombe pia waweze kushirikiana na watu wa *NDC* na Wizara ya Viwanda na Biashara. Upimaji ule uliofanyika kule Liganga na Mchuchuma kulikuwa na haki mbili. Kulikuwa na *mineral right* yaani zile leseni za madini na kulikuwa na *land right,* hati za umiliki wa ardhi. Sasa, mwekezaji alimiliki eneo kubwa la ardhi lakini ulipaji wa fidia alipunguza eneo lake atakalofanya uwekezaji, na lile eneo jingine ambalo halijalipiwa fidia tulitaka tulipange tutoe hati kwa wananchi ili nao waweze kunufaika na mradi. Kwa hiyo naomba sana Mheshimiwa Waziri ili kuepusha mgongano na wananchi wataalam wawahi mapema sana, nina imani sana wanaweza wakafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua mpira mtu anaweza akaucheza vizuri akiwa nje ya uwanja, ukiwa nje unaweza kuwa na mawazo mazuri zaidi kuliko wachezaji walioko ndani; lakini na wewe ukipewa nafasi uende kucheza utaona pale unakuwa kituko. Sekta ya ardhi ni tofauti sana na tunavyo ichukulia. Sekta hii ina sheria nyingi sana, na zote za muhimu. Lakini mpaka hati ije kutengenezwa kuna hatua nyingi za kupitia na kuna wataalamu wengi wanahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru nimebahatika kufanya kazi kwenye sekta hii ya ardhi kwenye Wizara ya Ardhi kwa muda usiopungua miaka kumi. Katika kipindi hicho nimesimamiwa na kufundishwa kazi na wengi na mimi nimesimamia na kufundisha kazi wengi; kwa hiyo nina ufahamu mkubwa wa sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kazi zile za kuandaa mpango kabambe *(master plan)* ikishaandaliwa ile waje wale watu wa mipango miji. Na *master plan* ile inakuwa ni shirikishi, inahusisha watu wengi zaidi. Wanakuja watu wa mipango miji, anachokifanya Afisa Mipango Miji, mpima ardhi hawezi kukifahamu na hawezi kufanya. Ni taalum mbili tofauti wote

wanakaa darasani miaka miwili mitatu minne wanafundishwa, na anachokifanya Afisa Ardhi ni kazi tofauti. Ndiyo maana kuanzia ukurasa wa 30 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nilikuwa naisoma, ameainisha pale eneo la uandaaji wa mpango kabambe *(master plan)*, uandaaji wa mipango kina, upimaji wa ardhi, umilikishaji, na mambo ya utatuzi wa migogoro. Kwa hiyo kuna vipengele vingi ambavyo ni muhimu sana ningeomba ikiwezekana wizara iweze kutoa mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuna kitu pia nimekibaini, tunachanganya sana upimaji wa vijiji na upimaji wa mashamba ya wananchi na utoaji wa hati milki za kimila. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge tunachukulia kwamba upimaji wa vijiji ndio huohuo upimaji wa mashamba ya wananchi na utoaji wa hati miliki za kimila. Kwa hiyo haya maeneo ningeomba Wizara iweze kukutupa semina za kutosha ili tuweze kuwa na uelewa ili tunavyoishauri tuweze kutoa ushauri ambao uko sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano. Kwenye upimaji wa mipaka ya vijiji hili linanyika sana wakati ule inavyokuja sensa labda ya watu na makazi au uchaguzi, wanapotaka kuzaliwa vijiji vipya; au wakati wowote Ofisi ya Rais TAMISEMI wanavyo kuwa wanaongeza vijiji. Sasa, inatakiwa wananchi wakae wakubaliane mipaka ndipo wataalamu waweze kwenda kuweka mipaka hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na eneo hili ningeiomba Wizara ipunguze kutumia mipaka ile ya asili kama mito na milima, kwa sababu mazingira ya kijiografia yanabadilika. Kuna mito inakauka, kuna mito inahama. Kwa hiyo ni vizuri wakaweka zile *bicorn* kubwa kama ambavyo mmeweka kwenye mipaka ile ya kule kwenye hifadhi, na kule kwenye mipaka ya nchi. Zile nguzo ni kubwa zimefyatuliwa pale, mwananchi yeyote anaweza kuona, kwa sababu tukitegemea mto kuna wakati mwingine mto unahama. Kwa hiyo ni muhimu sana tukafyatua nguzo kubwa za *bicorn* ili wananchi wasije wakaingia kwenye migogoro. Kila mwananchi akiona anajua kwamba hapa ni mpaka wa kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mipango ya matumizi bora ya ardhi niipongeze sana wizara imejitahidi kadri ya uwezo

wake, imejitahidi sana; na Tume ya Mipango ya Matumizi Mora ya Ardhi nayo imejitahidi kufanya kazi vizuri. Niishukuru Serikali, mwaka jana wakati wa bajeti mara ya kwanza tuliweka ile bilioni 205 lakini zikaongezwa zaidi ya hizo ili angalau waweze kupima vijiji vingi zaidi. Kwa hiyo naomba sasa wataalamu wetu waweze kwenda kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji ambavyo vimepangwa kutekelezewa mradi huo, wapime mashamba ya wananchi na kutoa hati miliki ya kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sijui tutatumia njia gani, bado baadhi ya maeneo hati miliki ya kimila haina uzito sana, mwananchi akienda benki kuomba mkopo wa trekta bado haitambuliki sana. Sasa sijui tutatumia njia gani kuweza kuelimisha taasisi zinazotoa mikopo kwa wananchi waweze kuitambua vyema hati ya haki miliki ya kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunavyopima maeneo mengi zaidi kwenye nchi yetu na kutunza kumbukumbu za wamiliki vizuri tunapunguza muda wa kutatua migogoro wa ardhi. Mwananchi akija kama kumbukumbu ziko vizuri za mwananchi ni rahisi kumpa majibu. Kwa hiyo ni muhimu sana, Waheshimiwa Wabunge wanavyoshauri maeneo mengi katika nchi hii yaweze kupimwa na kutolewa hati miliki ni ushauri ambao ni mzuri sana ambao wizara haina budi kuufuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Serikali iongeze zaidi fedha na itoe kibali kwa Wizara hii kuweza kuajiri watumishi wa kutosha, kwa sababu wizara hii ina upungufu mkubwa sana wa watumishi, haijaajiri muda mrefu. Kwa hiyo ni muhimu sana Serikali Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma wakawapa kibali waweze kuajiri; kwa sababu vyuo vipo vijana wako mtaani hawana ajira na wana uwezo na wana utayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia takwimu, inaonesha watumishi waliopo hawazidi asilimia 30, kwa hiyo upungufu ambao upo kwenye Wizara hii ni zaidi ya asilimia 70, kwa hiyo ni pengo kubwa sana, hivyo tusitarajie miujiza kwa idadi hii ya upungufu wa watumishi. Kwa hiyo naomba Serikali iweze

kuajiri watumishi wa kutosha. Na kwa eneo la Dodoma nimeona Mheshimiwa Waziri amejaribu kuelezea pale kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa hapa Dodoma. Dodoma inabidi ichukuliwe kwa namna nyingine tofauto, kwa sababu moja, tangu mwaka 1973 kulikuwa na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *CBA*. *CBA* walikuwa na sheria tofauti walikuwa hawatumii Sheria ya Ardhi Namba Nne. Walikuwa hawafuari sana Sera ya Taifa ya Ardhi, walikuwa na taratibu zao ziko tofauti. Kwa hiyo baada ya kuvunjwa ndipo sasa tuka-*switch,* na mimi ndiye niliyekuwa Afisa Ardhi wa kwanza kuja kubadilli mfumo. Changamoto kubwa niliyokuwa nakutana nayo moja ni kutofautiana kwa sheria. Kwa hiyo tuangalie namna ya kuziba *gap* katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile Dodoma baada ya Makao Makuu kuja ardhi ilipanda sana thamani. Mahitaji ya ardhi yakawa mengi, na upimaji wataalam wamejitahidi wana viwanja, najua saa hivi wanakwenda kwenye milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Wizara ikaaangalia uwezekano wa kuongeza Kamishna mwingine wa ardhi hapa Dodoma. Kamishna mmoja mtamuua kabla ya siku zake, atazeeka kabla ya wakati wake. Kwa hiyo ateuliwe Kamishna mwingine wa ardhi ili aweze kusaidiana majukumu na Kamishna aliyepo namna ya kugawa majukumu Kamishna wa hapa atajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa, Deus Clement Sangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata ajiandae.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii ili na mimi niwe kati ya wachangiaji kwenye bajeti hii ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa natoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya. Na kipekee nimpongeze hasa kwa kuijali Wizara hii ambayo kufikia mei 15 alikuwa maewapatia asilimia 84.2 ya bajeti yote tuliyowapitishia mwaka jana, ambayo ni bilioni 175; lakini pia kwa namna ambavyo mwaka jana alifuta malimbukizo ya riba ya pango kwa ajili ya wale wadaiwa sugu. Kwa hili amewasaidia sana Mheshimiwa Waziri kusafisha dawati lenu ili sasa mnapoanza kusimamia jambo la makusanyo ya kodi muweze kwenda vizuri kwa kuwa yale madeni sugu Mheshimiwa Rais amewarahisishia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze kwa bajeti yenu yenye mwelekeo mzuri, wewe Mheshimiwa Waziri na Naibu wako, na tunawatakia kheri, tutakapo wapitishia mkatende yale ambayo mmeyasema kwenye bajeti yenu. Lakini pia nimpongeze Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Rukwa, dada yangu Rehema, anafanya kazi nzuri. Kwa muda mfupi ananipa ushirikiano mzuri na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nina mambo mawili muhimu. Jambo la kwanza nitaongelea migogoro ya ardhi, na nitazungumzia *specifically* migogoro iliyopo ndani ya Jimbo langu la Kwera na pengine Mkoa wa Rukwa kwa ujumla. Mwaka jana katika bajeti hii tarehe 25 mei, nilisimama tena kwa uchungu mkubwa na nikaongea maneno makali sana juu ya mgogoro wa ardhi uliopo ndani ya Jimbo langu la Kwera, kwa maana ya mgogoro wa shamba lile la Malonje la Efatha. Lakini Mheshimiwa Waziri mama yangu, dada yangu, rafiki yangu jambo niliona mmelichukulia *very lightly*. Hamku-*take very serious note* kwa jambo lile kwa sababu hivi ninavyoongea hatujakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kwamba mimi napinga uwekezaji wala nina shida na mwekezaji, Hapana; lakini lazima tufike mwekezaji anapofanya kazi yeye afanye shughuli zake za uwekezaji kwa amani na wananchi wawe na amani. Sasa iliyopo jimboni kwangu ni shida kubwa, migogoro haiishi. Juzi nilikuepo jimboni wananchi wameandamana kwenye Ofisi za chama. Kwa

sababu mwekezaji amewaandikia barua kwamba mashamba yote yale waliyolima mahindi hawatakiwi kuvuna mpaka waende kwake yeye. Wakati wamepanda wamepalilia wameweka mbole, wakati wa kuvuna umefika ndipo sasa mwekezaji anakwenda wakamlipe fedha. Na shida ni kwamba ninyi wenyewe Serikali kupitia hii Ofisi ya Ardhi mlileta *confusion.* Vijiji vilikuwa na mipaka yao na hati yao, kabisa, mkaja kumpa Mwekezaji sehemu ya vijiji, na wanakijiji wana sehemu ileile ya kwao. Kwa hiyo kuna mgongano hapa. Wanakijiji wanadai eneo hili ni la kwetu na mwekezaji anasema hili ni la kwangu kihalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mgogoro unaenda miaka 13 dada yangu Mheshimiwa Waziri na mwishowe tunaonekana sasa kama wananchi ni wakorofi, wanatumia nguvu nyingi ya dola kuwapiga, kuwaumiza, *issue* sio kupiga mnaweza mkapiga sasa mgogoro huu ni vijiji 11. Kwangu kwenye Jimbo langu la Kwela ni vijiji vitatu kule kwa ndugu yangu Aeshi vijiji saba, vyote hivi kila muda wapo kwenye *movement,* maisha yao ya *movement.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nikashauri kwamba Waziri aunde tume tuje tukae, tumalize mgogoro, imetosha sasa mambo ya kufukuzana, mwekezaji na pia nilishauri hapa Bungeni, sisi uwekezaji tunaupenda, lakini namna ya shamba lile kuwa *idle* ekari 23,000 kwenda 25,000 hakuna shughuli inayoendelea, mwekezaji amelihodhi liko *idle* na pengine kwa sababu ya migogoro pia anaweza kuwa naye hataki kuendeleza chochote. Sasa Serikali *position* yao ni nini kwenye jambo hili, sisi pale ngano ndio wanaongea, kila siku Waziri Mheshimiwa Bashe naye nilimwambia, anapiga kelele suala la ngano kuna vitu vingine Serikali tumeshindwa tu kufanya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shamba la hekta 25,000 la mwekezaji wa Shamba la Malonje Efatha liko *arable*. Tukiwekeza tu pale tutapata tani 175,000 mpaka tani 100,000 za ngano, Waziri ataenda kupunguza *deficit* hiyo anayopiga kelele hapa, lakini kama halmashauri sisi tutaenda kukusanya mapato kutokana na huo uzalishaji milioni 600, 700 mpaka bilioni moja, lakini katika jambo hili nashangaa kwa nini tunasitasita, sisi hatuna ugomvi,

twendeni tukakae pale mezani, tukaondoe huu ugomvi unaoendelea wa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tu imetokea shida tena ugomvi umehama kwa wananchi umehamia tena kwa mwekezaji na Serikali kwa sababu wale wafanyakazi wamechukua trekta lenye *harrow* wameenda kulima barabara ya *TARURA* ya kilometa wakaivuruga tu wakailima vuruga. Kilometa 1.5 wanadaiwa wakatengeneze barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunatakiwa tukaweke *standard* kwamba wewe ni mwekezaji mipaka yako ni ipi, ulipewa shamba kwa madhumuni yapi, ndani ya muda gani utekeleze nini, wananchi mipaka yenu ni hii moja, mbili, tatu. Tuna-*close* jambo lile kila mtu anaishi kwa amani, kuliko kila mwaka nisimame Bungeni, nina *hansard* nilikuwa nasoma hapa, mpaka nasikitika walilichukulia *very lightly*. Madhara yake yanakuja, watauana, wananchi wataamua kum-*sabotage* mwekezaji na mwekezaji naye anatumia walinzi wake kuwapiga wananchi. Hatuwezi kuuishi kwenye nchi hii kwa namna hii ya kuviziana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri kesho anapohitimisha hili jambo nimeliongea sana, nimwombe alichukulie *very serious* ili chama nacho kwenye Mkutano Mkuu wa Chama, Mwenyekiti wetu wa Chama Mama Silafu Maufi amesimama pale mbele ya Mheshimiwa Rais akaongelea jambo hili. Kwa hiyo hata Chama kwa Mkoa wa Rukwa wao nao wanapiga kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Mbunge hata Mheshimiwa Aeshi nilikuwa naye hapa, japo yeye anaweza asipate nafasi ya kusema, wananchi wetu wanatutazama juu ya jambo hili. Twende tukakae *party* zote tulimalize ili tuje na *conclusion* mwekezaji abaki na amani yake na wananchi wabaki na salama yao ili tukajenge majimbo yetu, yakawe salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili kuna jambo ambalo lipo chini ya mikono ya Wizara, Gereza la Mollo, Gereza la Mollo nalo hivyo hivyo kama alivyokuwa anasema ndugu yangu Mheshimiwa

Ndaisaba, wamekuja pale wamewakuta wananchi kijiji kipo wametwaa eneo, wakasema haya tunapitisha mpaka humu tunachukua gereza. Sasa nao huo mgogoro umechukua miaka mingi sasa, inaenda miaka 15, wananchi wanasema ni eneo letu Gereza la Mollo linasema ni eneo letu. Alitumwa wakati ule Mheshimiwa Kangi Lugola akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, akawaambia wananchi tulieni tutarudisha, ikawa ndio jumla mpaka leo. Sasa nawaomba, wao ndiyo waliopewa dhamana ya kusimamia ardhi, waende wakamalize migogoro ya aina hii tusi-*entartain* migogoro itakuja kusababisha maafa watu wakauana pasipo sababu. Mheshimiwa Rais kama nilivyosema anajali, anawapa bajeti wanaenda huko, waende na mwaka huu hawajaja na waliniahidi watakuja tena alipokuwepo Naibu hapa Ndugu yangu Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete alisema hamna shaka nakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi kule wanasikia, wanasema mbona Mbunge ulidanganywa. Tumeona pia timu ya Mawaziri Nane kwenye mashamba haya yenye vijiji 11 hawajaja. Nimwombe mama yangu Mheshimiwa Waziri jambo hili mwaka jana aliona niliongea kwa uchungu mkubwa na leo narudia, waje tumalize mgogoro, sisi nasi tunataka tupate mapato kulingana na shamba lile na mwekezaji aendelee na maisha yake, lakini haki ya wananchi itazamwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza jambo la mgogoro, niende jambo la pili la muhimu la kumshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa kupandisha hadhi vijiji sita ndani ya jimbo langu kuwa Miji Midogo kwa maana ya Mpui, Kaengesa, Mtowisa, Muze, Ilemba na Kiliamatundu. Sasa vile vijiji vinahitaji kupangiliwa sawa viendane na *standard* ya kuwa miji midogo. Niombe waisaidie sasa Ofisi ya Ardhi Mkoa kuongeza vifaa vya upimaji, tuna kifaa tu ambacho seti ile ya upimaji pale mkoani tunatumia Kalambo, Nkasi na Sumbawanga *DC*. Watuongeze ili vijiji vyote hivi ambavyo vimeshakuwa ni miji midogo niliyoitaja waweze kupangilia miji yao na kupangiliwa kwa miji tu hakutakuwa kunaishia hapo, bali kutaingiza mapato ambayo yata-*boost* mapato ya halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sangu. Mheshimiwa Ally Juma Makoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na Mheshimiwa Ester Bulaya ajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili kuchangia Wizara hii ya Ardhi. Awali ya yote nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake nzuri juu ya Wizara hii. Kwanza kwa kuona umuhimu wa Wizara hii, Mheshimiwa Rais ameridhia kuunda Kamati kwa ajili ya kushughulika migogoro ya ardhi. Hili ni jambo kubwa ambalo kwa kweli likikamilika litaleta tija kwenye nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, utaona amefanya mabadiliko kwenye Wizara hivi karibuni na ametuletea Naibu Waziri huyo hapo, tunamwona lakini na Katibu Mkuu mpya. Yote hii ni kutaka kuendelea kuimarisha hii Wizara, lakini Mheshimiwa Waziri yuko pale dada yetu Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula anaimudu hii kazi na ndio maana Mheshimiwa Rais kaendelea kumwamini. Kwa maana hiyo tunajua kwa safu hii iliyopangwa sasa hivi, tunawapa muda ili kuweza kushughulikia haya majadiliano na michango ya Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha angalau tunakwenda kupunguza hii migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru, leo utaona asilimia kubwa ya Waheshimiwa Wabunge wanachangia kuhusiana na migogoro, itafikia mpaka kipindi tutashindwa kuona kazi nyingine ambazo zinafanywa kwenye Wizara hii. Mheshimiwa Rais amemtoa *Engineer* Sanga kule Wizara ya Maji akamleta huku na sisi tulikuwa na mawazo kwamba tunataka sasa Wizara ya Ardhi tuanze kulipa kodi ya ardhi kupitia simu. Tunawapongeza Wizara sasa hivi tunaona tukiwa majumbani tunapata meseji na zenye *control number* na tunaanza kulipa kwa urahisi. Kwa maana hiyo tunaona mwendelezo mzuri na tunawatia moyo waendelee kushughulika na jambo hili ili na hii Wizara ionyeshe mchango wake mkubwa kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia huu mkopo umekuwa ukizungumzwa hapa na Wabunge, *of course* mkopo una mambo mengi mazuri ambayo tukiyafanya italeta tija kwenye Taifa, michango ya Waheshimiwa Wabunge ni kuhusiana na matumizi hasa ya fedha hizo, lakini tunaamini viko vitu. Wakinunua mashine, mitambo wakatujengea ofisi hizo na vitu kama hivyo, vitaleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wanaona ni nanma gani kunakuwa na migogoro mingi na ndio maana wote tunatamani ardhi yetu yote ingepangiwa matumizi bora ya ardhi ili kuondoa migogoro. Sasa hapa Mheshimiwa Waziri aendelee kuchukua ushauri wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii na aendelee kuufanyia kazi. Nakumbuka mwanzo walikuja na vijiji 250, baada ya ushauri wa Kamati, leo wamekuja na vijiji 500, bado Kamati inaona ipo *room* ya kuendelea kuongeza idadi ya kuvipima vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hotuba ya Kamati ni nzuri na waendelee kuichukua kama Wizara na waendelee kuifanyia kazi. Waone namna bora ya kuweza kuongeza idadi ya vijiji. Katika ule mkopo nilikuwa naona fedha zile zilipangiwa Kamati nyingine tofauti ya kuendelea kushughulika na zile fedha. Nadhani tunaongelea Tume ya Mipango ya Ardhi kwa sababu tunaamini wale ukiwapa fedha leo, leo hii wanaingia *site* kwa haraka na kwa kutumia vifaa vyao hivyo hivyo wataendelea kuvipima vile vijiji hata kama hiyo Kamati nyingine itakuwa haipo. Kwa hiyo, waendelee kuuchukua ushauri wa Kamati, ushauri wa Wabunge, waone namna gani wanaweza kuboresha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi jimboni kwangu; tuna migogoro ya ardhi kama ilivyo katika majimbo mengine, lakini sasa kwangu kuna migogoro miwili, mgogoro kati ya wananchi wa Mongoroma na Pori la Swagaswaga ambalo Mheshimiwa Rais alilitolea maelekezo. Sasa Mheshimiwa Rais anatoa maelekezo, lakini kule kazi nyingine zinaendelea za kuweka vigingi. Sasa kabla Wizara ya Ardhi haijakwenda kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kazi nyingine zinaendelea. Hapa inaonekana sisi

kama Wizara ya Ardhi tunakuwa nyuma, tunachelewa kwenda kufanya maamuzi ambayo yangesaidia kuondoa hii migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wito wangu bado Mheshimiwa Waziri kuna maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba kufika kule ambapo Kamati ambayo yeye ndiye Mwenyekiti walielekezwa kufika, hawakufika kama Kamati, lakini hali iliyopo kule kwa kweli sio nzuri, wananchi wanashindwa kuendeleza maeneo yao. Kwa hiyo, ni lazima kwenda kuutatua ule mgogoro ili kuwaweka wananchi wetu vizuri, waweze kufanya kazi zao za maendeleo wakiwa na amani kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la King'ang'a na Wananchi wa Kingale, jambo hili wamelishughulikia vizuri, tunawashukuru sana na mgogoro ule umekwisha. Wizara ilikwenda, Waziri alimtuma Mpimaji na ramani Mkurugenzi, amefika kule kafanya kazi yake vizuri. Kachukua mapendekezo yamefika mpaka kwa Mheshimiwa Rais, kwa ukarimu wa Mheshimiwa Rais ameridhia yale mapendekezo na ni mapendekezo ya wananchi. Cha ajabu juzi anakwenda Mkuu wa Gereza anakamata ng'ombe wa wananchi anawapiga faini. Najiuliza hivi kila idara, kila mtu anaamua tu kukamata ng'ombe wa watu na kuwatoza faini, hawa wananchi fedha hizo wanatoa wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Bwana anaitwa Juma Kanene ametozwa faini ya 150,000; kuna Bwana anaitwa Hamis Mwiguu ametozwa 400,000; na kuna Bwana anaitwa Kiteto Kiteto ametozwa 200,000; Bwana John ng'ombe wake wawili wamezuiliwa gerezani na huyu Bwana Samweli ng'ombe amezuiliwa gerezani. Sasa tunajiuliza kila mmoja akijipa jukumu la kukamata ng'ombe wa wananchi na hali ya kuwa eneo hilo tayari limeshakwishatatuliwa mgogoro wake, imebaki Wizara ya Ardhi kwenda kutuonesha tu mipaka tuliokubaliana, hii inakuwa sio sawa na inakuwa ni uonevu kwa wananchi. Kwa hiyo, naomba mamlaka iliyopo hapa ikiwemo Waziri wa Mambo ya Ndani amwelekeze Mkuu wa Gereza awarudishie wananchi fedha alizochukua kwa sababu si halali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara sasa iende ikakamilishe jambo hili, lililobaki ni kuwaonyesha tu wananchi kwamba Mheshimiwa Rais katupa maelekezo kwamba ninyi mpaka wenu unaishia hapa na gereza unaishia hapa. Tuwasaidie kuweka vigingi ili kila mmoja aweze kujua mpaka wake ili wananchi wetu hawa waweze kufanya kazi zao kwa amani bila kutishiwatishiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikipata nafasi ya kuja kuchangia kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani nitashauri juu ya uendeshaji wa lile gereza kwa sababu tunaona halina tija kwa safari hii, inabidi tulifanyie mapinduzi ili liweze kuleta tija katika nchi na wananchi wa eneo lile waweze kunufaika na gereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kuna wageni waliopo Bungeni jioni hii kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi ambaye ni Makamu wa Rais wa Chama cha Wataalam wa Mipango Miji Tanzania, Ndugu Everist Mfinanga, Karibu. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Ngara Mkoa wa Kagera. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Denis Londo, ambao ni wanafunzi 90 na Walimu sita kutoka Shule ya *St. Peter Clever Primary School* ya Mikumi Mkoa wa Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, hawa ni wanafunzi 90 wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tangazo lingine, Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni Mkuu wa Shughuli wa Serikali Bungeni yuko nje ya Mkoa wa Dodoma hivyo Mheshimiwa *Captain* Mstaafu George Huruma Mkuchuchika ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, anakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli wa Serikali Bungeni. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo ili nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Naomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha mimi jioni hii kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kama ilivyo ada nami naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa yale yote ambayo ameyafanya katika Wizara hii. Sisi ni mashahidi hadi mwezi Mei Wizara hii imepata asilimia 82 ya makisio yake, lakini wote sisi ni mashahidi tumeona jinsi gani Mama Samia Suluhu Hassan alivyokuwa na uchungu na wananchi wake na kusamehe madeni yale ya nyuma ili wananchi waendelee kulipa katika muda unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Mheshimiwa Rais ameweza kutafuta fedha nyingi karibu bilioni 345 na kuwakabidhi Wizara ya Ardhi ili Wizara hii iweze kutenda yale ambayo wananchi wanayatarajia. Ni matarajio yangu kuwa watendaji watazitumia fedha hizi vizuri sana ili wananchi waweze kuona matokeo ya fedha zao. Sina shaka kabisa na Mtendaji Mkuu wa Wizara ndugu yangu Sanga, uaminifu wake, uadilifu wake unajulikana huko alikotoka na nina imani ataitendea haki Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa kuunda ile Kamati ya Mawaziri Nane wa

Kisekta ambao wamezunguka Tanzania nzima kutafuta majawabu ya matatizo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba nijielekeze katika mchango wangu. Mheshimiwa Rais aliunda Wizara ya Kisekta ya Mawaziri Nane, Mawaziri hawa walitembea *almost* katika nchi yote hii na bahati nzuri katika Mkoa wa Mtwara walifika. Mheshimiwa Waziri yeye ni shahidi tulikuwa naye pale Mtwara na tulikutana nae. Yeye ni shahidi aliona jinsi gani watendaji wake walivyofanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kushangaza sana sisi Wabunge ambao ndio wawakilishi wa wananchi hatukushirikishwa kabisa katika mchakato huu. Ndani ya wilaya yangu, Kata ya Mkonona Vitongoji vya Wanika, Kitongoji cha Nambunda na Malomba. Vitongoji hivi vimehusika kabisa katika mchakato mzima wa kuhakikisha kwamba wananchi walipo ndani ya eneo hili wanahamishwa na kutafutiwa makazi katika eneo lingine. Cha kushangaza halmashauri kwa maana ya Madiwani sisi hatukushirikishwa hata siku moja. Kwa hiyo, kila kitu kilifanyika siri na Mheshimiwa Waziri mwenyewe ni shahidi na alishangaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Mtwara alipogundua jambo hili alitumia hekima kubwa na kulimaliza jambo hili kwa busara sana na tukashiriki kikamilifu, tukaondoka sisi, Wabunge na Kamati nzima ya Waziri mpaka katika eneo la tukio na aliona jinsi wananchi wasiopungua 10,000 wako pale ndani ya eneo wakisubiri maamuzi ya Serikali. Sasa Serikali imeshafanya maamuzi na sisi hatuna tatizo na maamuzi na Waziri ameikabidhi Serikali ya Mkoa iandae mchakato mzima. Najiuliza Serikali ya mkoa wanazo nyezo za kufanyia kazi maamuzi ya Waziri. Serikali ya Mkoa wamefanya tathmini ya wananchi wahame, wamewatafutia maeneo wananchi waende, lakini mpaka sasa hivi wananchi wale wanasubiri fidia ambayo ndani ya ripoti ya wataalam wamezungumza bayana kwamba wananchi wapewe fidia ili wahamie maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri, Wizara ifanye maamuzi sasa na sina uhakika kama ndani ya bajeti hii wale wananchi wa Wanika na Malomba, Nambunda wametengewa fedha ili waondoke katika maeneo hayo na waende katika yale maeneo ambayo wamepangiwa. Kama eneo hili halitashughulikiwa kesho nitatoa shilingi. Sitakubali wananchi wale waendelee kukaa miaka saba wakisubiri maamuzi ya Serikali, tunawatia umaskini wananchi wale. Kwa hiyo kesho Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze wananchi wale lini watalipwa fedha zao ili waende eneo ambalo Serikali ya Mkoa imeshawapangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili ni suala la migogoro. Migogoro imekuwa karibu kila mahali katika nchi hii na ndani ya Wilaya yangu ya Nanyumbu migogoro ipo. Naishukuru sana Wizara katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameeleza jinsi gani ya kuweza kupunguza migogoro na ni kweli ndani ya wilaya yangu mimi nina masikitiko makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ile hatuna Baraza la Ardhi la Wilaya, matatizo yetu yanakwenda kilometa 100 *ups and down* mwananchi anapopata matatizo ndani ya Wilaya ya Nanyumbu inabidi aende Masasi ambapo ndipo kuna Baraza la Ardhi, jambo hili linakwamisha utoaji wa haki kwa wananchi, jambo hili pia linasababisha wale wenye fedha ndiyo wanapata haki, kwa sababu mgogoro uko Nanyumbu, kesi iko kilometa 50, huyu mwananchi maskini ataweza kwenda kilometa 50?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa kuamua kuunda Mabaraza ya Ardhi kwa kila Wilaya, wasiwasi wangu naomba kesho utakapokuja unithibitishie, Wilaya ya Nanyumbu Baraza la Ardhi litakuwepo katika mwaka ujao wa fedha? Vinginevyo kesho patakuwa matatizo makubwa Mheshimiwa Waziri, sitakubali tupite tena mwaka mwingine bila kuwa na Baraza la Ardhi la Wilaya ya Nanyumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasaema hivyo kwa sababu wananchi wanahangaika, leo unapigiwa Mbunge fedha

umsaidie kwenda kwenye kesi Masasi, hili jambo siyo sawa hata kidogo. Kwa hiyo, lazima tuwasaidie wananchi wetu katika kutafuta haki vinginevyo watakuwa wanapata haki wale watu ambao wana fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda sana kulizungumzia hapa ni haya makampuni yanayopewa kazi kuja kufanya shughuli za upimaji katika maeneo yetu. Tunayo kampuni ambayo ilikuja kufanya upimaji wa ardhi katika maeneo yetu ili wananchi baadae wapate hati, ile kampuni mpaka leo imefanya ile kazi, wananchi hawajapata hati na wananchi wanahangaika. Jambo hili nilishalifikisha ndani ya Wizara na Wizara ikaahidi, tena kampuni yenyewe ni ya Serikali, Chuo cha Ardhi Morogoro lakini cha kushangaza mpaka leo wananchi wale wanahangaika, wananchi wale nikifika tu kutoka Dodoma wanajaa ofisini kwangu kuomba kujua ufafanuzi wa hatma yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakuomba sana, naiomba sana Wizara haya ambayo Wabunge tunashauri wayafanyie kazi. Kampuni hii kama kweli ipo, basi ilete hati ambazo wananchi wale wamechanga fedha zao na wanahitaji sasa kupata hati ili mambo yao yaendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu hati za kimila; hati za kimila zinatolewa, Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba unaweza ukaitumia hati ya kimila kupata mikopo. Mimi naomba anithibitishie hili, kesho atakapokuja kuhitimisha anielezee tu wananchi japo wanne wa Wilaya ya Nanyumbu ambao wana hati za kimila, wamepata mikopo katika benki zetu, vinginevyo tutakuwa tunadanganyana, tuelezwe ukweli hati za kimila, dhamira yake ni nini? Ukipata hati ya kimila, unapata mkopo? Lakini siyo unanipa karatasi ambayo mimi haina manufaa yoyote, kwa hiyo naiomba sana Wizara kesho ituthibitishie hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naiunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Ester Bulaya atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie na ninachangia jioni ya leo huku Kaimu Waziri Mkuu Kapteni George Mkuchika akinisikiliza, Waziri *Senior* kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwa kuwa yeye ni Waziri *Senior* anajua migogoro ya ardhi katika nchi yetu ilivyokithiri, kwa hiyo naamini Kaimu Waziri Mkuu atamshauri Waziri husika na Naibu wake na hasa ukizingatia michango tangu asubuhi hii ya leo imeonesha ni namna gani migogoro ya ardhi katika nchi yetu bado haijapatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Nyatwali tu leo hii. Suala la Nyatwali lilikuwepo tangu enzi ya Rais Awamu ya Nne Baba yangu Jakaya Mrisho Kikwete, akalisitisha kwa sababu hakutaka kuingia kwenye historia ya dhuluma ya wananchi wa Nyatwali. Suala la Nyatwali, Mungu amlaze mahali pema Hayati John Pombe Magufuli alilisitisha. Mmekuja Mheshimiwa Waziri mnataka kumuingiza Rais Awamu ya Sita aingie kwenye mgogoro na wananchi kwa sababu mnataka kumshauri vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili haliwezekani, wananchi wa Nyatwali waligoma kuhama kabisa, kabisa kwa sababu ya wasiwasi wa kudhulumiwa. Mkatumia nguvu kwenda kuwatisha, kipindi changu mimi niligoma na nikawaambia kuhama siyo *issue, issue* mnawahamisha kwa fidia ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkumbuke eneo la Nyatwali ni lao wako pale zaidi ya miaka 700, leo kwa dhamira yao mnawatisha, mnawashurutisha, tena mpaka Viongozi wa CCM, viongozi wa vijiji, Diwani mnawaita Polisi kuwashurutisha wananchi wanyonge wale na ninyi mnasema ni Serikali sikivu. Kwa nini hamtaki kuwasikiliza wananchi wa Nyatwali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnawalazimisha kuhama, sawa wamekubali, kweli nchi hii eneo la Nyatwali, eneo la lango kuu la kuingilia Mbuga ya Serengeti, eneo *very prime,* muende mkawalipe fidia ya shilingi 400 kwa *square meter*? Yaani mnataka kutuambia thamani ya ardhi kwenye Mbuga ya Serengeti, Nyatwali thamani yake ni ndogo kwa *square meter* kuliko *Coca-cola*, *Coca-cola* shilingi 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnataka kutuambia wananchi wa Bunda Mjini, thamani ya ardhi kwenye lango kuu la kuingia Mbuga ya Serengeti, Mbuga namba moja inachukua tuzo kila siku, thamani yake kwa *square meter* ni shilingi 400, *Coca-Cola* shilingi 500, chipsi kavu buku (shilingi 1,000)? Hatuelewi watu wa Mara. Watu wa Mara hatutawaelewa na mnatujua. Hatuhitaji migogoro na ninyi, tunahitaji haki yetu. Hivi leo unampa shilingi 400 kwa *square meter,* jirani Kata ya Bariri viwanja vinapimwa *square meter* ni shilingi 3,000. Mnataka kuwatoa watu 13,000 mkawafukarishe siyo sawa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namsikia Mbunge anayetoka kwenye makaa ya mawe kule anashukuru watu wake wanalipwa, nataka nijue, hivi kule nako mnawalipa shilingi 400? Watu wa Mara tumewakosea nini? Shilingi 400! Pale Nyatwali kuna ng’ombe 42,000, kaya 1,300, kwa *square meter* shilingi 400 ataenda kununua ardhi wapi? Leo mtu ana ekari tano unamwambia umpe shilingi milioni mbili? Tuvaeni viatu vya hawa wananchi! Tuvaeni viatu vya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mabula Dada yangu nakuheshimu, kama kuna watumishi wanakuongopea, usiingie kwenye historia ya kwenda kuwadhulumu. Kuna wamama pale wanalima, wana imani na Rais mwanamke mwenzao, msiende kumuingiza kwenye migogoro. Haiwezekani ng’ombe 42,000, wafugaji 1,000 zaidi ya 300, wataenda kununua hekari ngapi? Mtawaweka wapi? Kwa nini mnaamua kuwahamisha watu kabla hamjajipanga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumbe macho, mtumie Jeshi la Polisi, mtishe watu kwenda kuwadhulumu watu, kwenda

kuwatisha, muwaondoe huku wakiwa wana kinyongo? Taifa letu haliwezi likabarikiwa. Taifa letu haliwezi kuingia katika historia ya kuwadhulumu wananchi maskini. Kuwadhulumu wafugaji, kuwadhulumu wamama wa Nyatwali. Mimi binti yao siko tayari. Mimi binti yao niliyetoka familia maskini ya Manyamanyama, niliyelelewa na wafugaji wale sitokubali! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Nyatwali wanasema walikubali kuhama, walikuwa wana imani na Serikali yao, leo mnataka kuwalipa shilingi 400 kwa *square meter* siyo sawa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Patrobass Katambi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna changamoto za migogoro ya ardhi na ndiyo maana kukaamriwa kuundwa timu ya Mawaziri wale wa Wizara Nane kwenda kushughulikia changamoto hizi, katika *procedure* za Sheria ya Ardhi zinavyoelekeza, lazima mfanye vikao vya *consultation* na wananchi husika. Vikao hivyo vilifanyika, Mawaziri hawa nane walikaa na wananchi na waliwasikiliza na katika utwaaji wa ardhi hao wanajua, tusipotoshe. Sheria ya Ardhi inaelekeza *procedure* za *acquisition of land,* kwenye Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema mwananchi unapotaka kuchukua ardhi kwa matumizi ya Serikali lazima ulipe *fair and adequate compensation.* Hizo *procedure* zinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo taarifa ya mwisho katika utaratibu ule ule hakuna mwananchi ambaye alionewa na bado katika uthamini mwananchi anayo haki ya kukubali malipo au kukataa malipo kabla ya kwenda kwa *Chief Land Valuer.* Kwa

hiyo, utaratibu huo upo ni suala ambalo linafanyiwa kazi na ripoti italetwa na Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester taarifa unaipokea?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei taarifa yake, lakini Sheria ya Ardhi inasema fidia ya haki, kwa tafsiri hiyo, shilingi 400 ndiyo fidia ya haki kwa Serikali?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo fidia ya haki kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi? Mawaziri Nane walienda pale hamkuwatisha wananchi? Hamkuwatisha wananchi? Mnawatisha Diwani, mnawatisha Wenyeviti wa Vijiji. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Nyatwali hatutahama mpaka tupate fidia inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester muda wako umeisha kwa hiyo tunashukuru sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipatia nafasi ya kuchangia. Pili, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dokta Samia Suluhu Hassan kwa

kazi nzuri anayoifanya na kwa kutenga fedha kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dokta Angeline Mabula, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Pinda, Katibu Mkuu Injinia Sanga, Naibu pamoja na Wizara nzima kwa ujumla kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni mali, ardhi ni vizuri tuitunze, ardhi tuithamini kwa sababu watu wanaongezeka lakini ardhi haiongezeki. Kila mmoja anaongelea migogoro, kila mmoja anatamani ardhi yake iweze kupimwa. Namuomba Mheshimiwa Waziri aangalie suala la upimaji wa ardhi ili kusudi tuweze kwenda vizuri kadri tunavyokwenda kwa sababu ardhi haiongezeki lakini binadamu wanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi katika Mkoa wa Morogoro. Nyote mnaamini kuwa Mkoa wa Morogoro unaongoza kwenye migogoro ya ardhi. Mheshimiwa Waziri wewe ni shahidi, naamini ulishafika Mkoa wa Morogoro, Mawaziri wengine wengine wamefika kwenye Mkoa wa Morogoro, Mkuu wa Mkoa ameweza kutatua migogoro ya Morogoro, Wakuu wa Wilaya wameweza kutatua migogoro na wataalam lakini migogoro bado iko hapo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hii migogoro hasa ninayoisema kwa Mkoa wa Morogoro hasa ni kwa upande wa wakulima na wafugaji. Ninaomba Mheshimiwa Waziri wa upande wa Ardhi uweze kushirikiana na upande wa Wizara ya Mifugo muweze kutatua tatizo hili ambalo limekuwa sugu kwenye Mkoa wetu wa Morogoro. Migogoro hii ya ardhi ambayo iko kwenye upande wa wakulima na wafugaji iko kwenye Wilaya zote za Mkoa wa Morogoro ikiwepo Malinyi, ikiwepo Kilombero, hasa Kilombero ni hatari sana kwa sababu iko kwenye Bonde la Kilombero. Kwenye Bonde hili la Kilombero ndiyo linatoa maji ambayo yanakwenda kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, kama litaharibika hatutaweza kupata maji ya kutosha na umeme hatutaweza kupata umeme wa kuzalisha umeme kwenye

bwawa hili. Kwa hiyo naomba muiangalie. Mvomero pamoja na Wilaya zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaacha kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa jitihada alizozifanya kwa Mkoa wetu wa Morogoro, licha ya matatizo hayo lakini angalau ameweza kupima maeneo machache kwenye Mkoa wetu wa Morogoro kwenye Wilaya mbalimbali ikiwepo Wilaya ya Malinyi, Kilombero, Ulanga na Kilosa pamoja na Mvomero lakini upimaji umesimama, ninaomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja kujibu pale tuweze kujua kuwa upimaji huu unaendelea lini? Kwa sababu migogoro bado inaendelea na kutatua migogoro hii ni kupima ardhi kwa sababu ukipima ardhi watu watajua watapata hati miliki yao na wataweza kuwa na ardhi yao na wataweza kuzitumia bila ya mgogoro. Wakulima watakuwa na ardhi yao na wafugaji watakuwa na ardhi yao, itakuwa hakuna kuingiliana. Kwa hiyo, ningeliomba kujua ni lini upimaji tena utaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikifuatia hapo pia naongelea kuhusu vyuo vyetu vya ardhi ikiwepo Chuo cha Tabora pamoja na Chuo cha Morogoro na Chuo Kikuu cha Ardhi cha Dar es Salaam. Naomba sana kwa sababu wataalam inaonekana kuwa wanahitimu na wataalamu hawatoshi. Naomba udahili hasa kwenye vyuo vya kati uweze kueleweka, uweze kudahiliwa wanafunzi wengi kwa sababu hawa wa vyuo vya kati hasa ndiyo wanafanya sana upimaji wa ardhi, kusudi waweze kuajiriwa na tuweze kupata wataalam kwa sababu matatizo haya ya ardhi yatakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema kuwa utafiti wa migogoro wala siyo utafiti, migogoro inayoeleweka, huu utafiti wa kubainisha hii ardhi uweze kufanyika kwa sababu ili tuende na sayansi na teknolojia lazima tufanye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kuongelea bajeti. Bajeti inatolewa lakini naomba bajeti ya maendeleo iweze kuangaliwa kwa sababu hii bajeti licha ya kuongeza fedha na kutupatia fedha ndiyo ikitolewa kwa wakati na fedha zote tunazoziidhinisha humu Bungeni zikatolewa kwa wakati na

zikatolewa zote miradi yote ya maendeleo ikiwepo upimaji wa ardhi itaweza kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema kuwa namsihi sana Mheshimiwa Waziri uliangalie hili suala la upimaji wa ardhi kwenye nchi yetu nzima, kusudi tuondokane na hii migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru na Mwenyezi Mungu akubariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ishengoma. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mheshimiwa Jonas Van Zeeland ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitangulie kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa namna ambavyo kwa haraka sana ameleta mabadiliko katika kuisimamia Wizara hii ambayo leo tunaijadili bajeti yake. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Dada yangu, Mheshimiwa Angeline Mabula kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kushirikiana na Naibu Waziri wake pamoja na watendaji katika Wizara yake pamoja na watendaji katika taasisi mbalimbali zilizo chini yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza na takwimu. Katika sensa ya nchi yetu mwaka 2012 tulikuwa na watu milioni 44.9. Miaka kumi baadaye, yaani mwaka 2022 wananchi wetu waliongezeka hadi kufikia milioni 61.9 na kwa mujibu wa *projection* iliyopo, tunatarajia ifikapo 2025 wananchi wetu watakuwa milioni 67.9 na mwaka 2050 tunatarajia idadi ya watu katika nchi yetu ya Tanzania itakuwa milioni 151.2. Katika watu hao milioni 151.2 inatarajiwa asilimia 48 watakuwa wanaishi katika miji mbalimbali hapa nchini, kutokana na watu wengi

wanaohamia katika miji lakini wanaozaliwa pia katika miji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Jiji letu la Dar es Salaam ndilo jiji ambalo linaongoza kwa sasa kwa kuwa na idadi kubwa ya watu, ikiwa na watu milioni 5.4 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022 na inachukua asilimia 8.7 ya wananchi wote wa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kwa kusema, kwa mujibu wa taarifa za kiuchunguzi za *UN* zinaonesha kwamba Jiji letu la Dar es Salaam ni la tatu kwa kuwa na ongezeko kubwa la wananchi kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2022. Pia kwa mujibu wa taarifa hizo hizo za *UN,* inaonesha kwamba nchi yetu ya Tanzania inakadiriwa ifikapo mwaka 2100 itakuwa ni nchi ya tisa yenye watu wengi hapa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimetoa takwimu hizi makusudi ili mwone kwa namna gani tunatakiwa kujipanga katika kuhakikisha wananchi wetu tunawapatia makazi muhimu na Madhubuti. Ni lazima tuwe na mpango madhubuti wa makazi kwa wananchi wetu hasa wananchi wa hali ya chini wakiwemo watumishi pamoja na wale ambao wanafanya shughuli nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi uliopita Kamati yetu ya *PIC* (Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma) ilitembelea miradi inayosimamiwa na Taasisi yetu ya *NHC*. Kwa kweli tuliona mambo mazuri. Mheshimiwa Rais wetu amefanya mambo mazuri, amepeleka fedha nyingi kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi wa mradi wa nyumba pale *Morocco Square* na pia pale Kawe *Seven Eleven,* miradi ambayo ilisimama kwa muda mrefu. Nampongeza Mheshimiwa Rais, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayoendelea katika ile miradi miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mradi mpya wa *Samia Housing Scheme* ambao unasimamiwa pia na watu wa *National Housing,* lakini ukiiangalia ile miradi na matarajio ya pesa zitakapouzwa zile *apartments,* kwa kweli ni fedha nyingi sana

watahitaji kulipa wale watu ambao watanunua zile nyumba. Kwa hiyo, sioni nafasi ambayo Serikali imetoa kwa ajili ya uwekezaji kwenye nyumba za watu wa kawaida au watu wa hali ya chini kama watumishi wenye vipato vidogo vidogo, wakulima wadogo wadogo, wafanyabiashara wadogo wadogo na watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya mwanzoni kabisa mwa Uhuru tulishuhudia viongozi wetu, waasisi wa Taifa letu akiwemo Mzee wetu Abeid Amani Karume pamoja na Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakiwekeza kwa kiasi kikubwa kwa wananchi wa vipato vya chini. Kwa hiyo, naiomba Serikali, turudi katika ule mwanzo mzuri ambao walituanzishia waasisi wetu. Pale Magomeni kulikuwa na sehemu ile ambayo sasa inaitwa Magomeni Mapipa, nyumba zilikuwa zikiezekwa kwa mapipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale *Magomeni Quarters* kulikuwa na nyumba zilikuwa zimeezekwa kwa makuti, lakini Hayati Baba wa Taifa akasema Hapana, ni lazima twende na mkakati wa kuanzisha nyumba ambazo wananchi watakodishwa au kukopeshwa kwa masharti nafuu. Watakuwa katika utumishi wao na mwisho wa utumishi wao watakuwa tayari wanajimilikia zile nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna hali inayojitokeza ambayo wananchi wetu hasa watumishi wa hali ya chini wamejikuta wakijenga nyumba baada ya kupata kipato chao cha kustaafu, wengine wanajikuta sasa wanatumia ile hela yote na kikokotoo kimebadilika sasa hivi, kwa hiyo, unajikuta wanatumia hela yote kujenga nyumba na hawamalizi, kwa hiyo mwisho wa siku wanabaki na *stress,* wanakufa mapema na mwisho siku ni lazima sasa tuone namna ambavyo tutatengeneza hii skimu mpya ambayo itawasaidia watu wa kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kule Zanzibar kulikuwa na magorofa ya Michenzani yalijengwa na Hayati Abeid Karume kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa kipato cha chini. Kwa hiyo, rai yangu kwa Wizara yetu, twende tukabuni *revolving fund*

ambayo itapelekwa kwenye taasisi zetu ambazo zimehusika na ujenzi kama *NHC, TBA* pamoja na Mwananchi *Housing* ili waweze kujenga nyumba za aina hiyo, wananchi waweze kukopeshwa kwa bei nafuu wakiwa ndani ya utumishi wao, wakiwa na nguvu zao ili wanapofika umri fulani, basi wanamilikishwa zile nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukatumia kwa mfano vifaa vya ujenzi tukaweka mle *charge* kidogo. Kwa mfano, kwenye *cement* kila mfuko wa *cement* tukiweka kwa mfano Shilingi mia moja, mia moja, mifuko mingapi ya *cement* inazalishwa hapa nchini kwenye viwanda vyetu? Tutajikuta tuna hela nyingi ya kuweza kuhudumia hao wananchi, na hiyo *population* ambayo tunatarajia ikue mpaka kufikia 2100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilifikiri kwamba kuna sheria nyingine za umilikaji wa ardhi zimepitwa na wakati pamoja na mali. Kwa mfano, sasa hivi mwananchi ambaye sio raia wa Tanzania haruhusiwi kumiliki ardhi katika nchi ya Tanzania. Sikusudii hapa kuzungumzia suala ya uraia pacha *(duo citizenship),* ninachoweza kuzungumza hapa ni kwamba, kama mtu anauwezo wa kuja kujenga *apartments* katika nchi yetu ambazo zitawasaidia wananchi wetu, zile nyumba hawezi kuondoka nazo, hata kama yeye sio raia wa nchi hii. Tuliona kule Dubai, ona leo Zanzibar, mambo haya yanaendelea, yanafanyika vizuri kabisa. Watu wanaruhusiwa kuwekeza, wanajenga majumba, na watu wanakodi, wengine wananunua, maisha yanaendelea, yanazidi kuboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuihudumia ile *population* ya mwaka 2001 ni lazima twende na hii mikakati…

**MHE. ALI JUMA. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndulane, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji. Kwa Hayati Mzee Karume, alizijenga nyumba hizi ambazo amezizungumza mchangiaji, mijini na vijijini zote zikiwa na hadhi moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndulane, taarifa unaipokea?

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru ndugu yangu hapa, Mheshimiwa Ali, kwa kweli naipokea taarifa yake kwa asilimia 100. Kwa hiyo, naomba tuliangalie hili jambo katika Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu matumizi bora ya ardhi katika Wilaya yangu ya Kilwa, maana yake usije ukasemea Taifa halafu mwisho wa siku ukajikuta wewe kwako hujisemei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa matumizi bora ardhi, mwaka uliopita tulipitisha bajeti ya Shilingi bilioni 205, ilisomwa hapa, lakini baadaye ilirekebishwa, ikaongezwa hadi kufikia Shilingi bilioni 300. Kwa kweli Serikali ilifanya jambo zuri, lakini nasikitika kusema, katika vijiji kumi na moja ambavyo Wilaya yetu ya Kilwa ilitakiwa kuvipima katika mpango huu wa matumizi bora ya ardhi kupitia fedha zile ambazo niliomba hapa kwa kilio, bahati mbaya sisi wengine hatuna uwezo wa kuruka sarakasi, wala kupiga magoti, wala kulia ndani ya Bunge, ni wavumilivu sana, lakini zile pesa hazijafika hadi kufikia wakati huu. Naiomba Wizara, katika huu mwezi mmoja uliobaki ituletee fedha, tuendelee na upimaji na kuboresha mpango wa matumizi bora ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kulikuwa na mgogoro katika Kijiji cha Mtepela na katika utatuzi wa huo mgogoro tulijitahidi mimi pamoja na Mheshimiwa Diwani wangu wa Kata ya Miguruwe kusuluhisha. Pia Kamati ya Mawaziri nane ilifika, lakini kikubwa walichosisitiza pale wale Mawaziri, ni suala la ulinzi wa maji katika chanzo cha Mto Matandu. Mambo mengine

hayakuzungumzwa, lakini juzi tumeona, wafugaji wanaambiwa ifikapo mwakani wawe wameondoka, wakulima ifikapo mwezi ujao, Julai tarehe 30 wawe wameondoka. Naomba, kabla ya utekelezaji wa kuwaondoa wale wananchi wa Kijiji cha Mtepela pale, basi uwepo mpango madhubuti wa kulipa fidia pamoja na kuzingatia mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas Van Zeeland.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu katika hii Wizara ya Ardhi. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, kwanza kwa kuondoa riba na kwa kuwaongezea wananchi muda wa kuweza kulipa. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Makatibu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache tu ambayo nataka nichangie yanayohusu jimboni kwangu. Kwanza kuna jambo moja ambalo linaendelea jimboni kwangu kuhusiana na urasimishaji. Mheshimiwa Waziri jambo la urasimishaji tunalipenda kwa sababu linawasaidia wananchi ili waweze kupata hati. Sasa jambo hili limekuwa kero. Tumefanya mikutano na hizi kampuni ambazo zinakuja kwa wananchi katika kata nyingi sana, ukianzia Kata ya Minazi Mirefu, Kata ya Tabata, Kinyerezi, Kiwalani, mpaka leo hawa wananchi hawajapata hati zao. Hizo kampuni ambazo zinakuja kwa ajili ya urasimishaji zinachukua muda mrefu sana, halafu tunapokuwa tunaenda kufanya mikutano yetu, kwa mfano, kama Diwani au Mbunge anafanya mkutano, basi kero kubwa za wananchi kwa Jimbo la Segerea ni kuhusiana na kampuni za urasimishaji. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba sana Mheshimiwa Waziri hili jambo ulifuatilie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linaendelea katika Jimbo la Segerea ni kuhusiana na uwanja. Mheshimiwa Waziri unajua na ninafikiri nilikwambia, tuna uwanja wetu ambao ulikuwa unaitwa kwa jina la maarufu Uwanja wa Sigara. Huu ni uwanja ambao uko Kata ya Liwiti. Huu uwanja umekuwa unatumiwa na wanafunzi na watu mbalimbali katika mambo mbalimbali ya michezo kufanya mazoezi na watu wengine ambao wana shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2020 kuna mtu alijitokeza akasema kwamba hili eneo ni lake, lakini kipindi kile tuliweza kuzuia na akaondoka, lakini sasa Mheshimiwa Waziri kwa kipindi hiki mwezi wa Nne ambapo tuko hapa Bungeni, nasikia tayari huyo mtu ameishajitokeza katika Uwanja wa Sigara, na hivi ninavyokwambia, ameshapeleka *grader* limesafisha kabisa ule uwanja. Kwa hiyo, sehemu ambazo zilikuwa zinatumika kwa ajili ya mambo ya michezo na mazoezi mbalimbali, huu uwanja sasa hivi haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kata ya Liwiti pamoja na Jimbo la Segerea walitaka wajue, hili eneo lilikuwa ni eneo la wazi, inakuaje mtu anajitokeza na anasema ni eneo lake na anapeleka *grader* linaanza kufanya kazi na vyombo na Serikali ipo tu inaangalia. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri utusaidie tuweze kupata majibu ili pia tuweze kuwaambia wananchi, ni jambo gani linaendelea katika Uwanja wa Sigara? Kwa sababu ni wengi ambao tunalalamika na huu uwanja una kazi nyingi za kiserikali zinafanyika hapo. Kwa sasa hivi hatuwezi kufanya kitu chochote kwa sababu tayari ameshaenda pale, amepeleka *grader,* ameshaanza kuziba, hakuna kitu chochote ambacho kinaendelea. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri ufuatilie jambo hilo, utakapokuja kufanya *wind-up* uweze kutuelezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye Kata hiyo hiyo ya Liwiti, kuna wananchi karibu 1,800 Mtaa wa Amani Ladwa. Hawa wananchi 1,800 Mheshimiwa Waziri wote wana leseni za makazi, lakini wote wamewekewa huduma za jamii kwa maana ya maji, umeme na vitu vingine ambavyo vinahusisha huduma ya

jamii. Jambo la kushangaza na la kusikitisha, ametokea mwananchi anasema kwamba lile eneo lote ni la kwake. Kwa hiyo, anahitaji wananchi wahame au wasipohama waweze kumlipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa wamekaa kwenye hiyo sehemu kwa miaka 40, kuna watu wapo wanasomesha watoto, kuna watu wanasomesha wajukuu, imekuwaje siku zote hizo huyo mtu asijitokeze, mpaka leo baada ya miaka 40 ndiyo aje kusema hilo ni eneo lake? Tulikuwa tunaomba Waziri uingilie huu mgogoro ili watu waweze kujua ni jambo gani linaendelea katika huu mtaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kusema kwamba hivi anavunja sheria, kwa sababu hatujajua. Kwa sababu huwezi kujua, watu wamekaa miaka 40 na wanalipa leseni, wana huduma zote za kijamii. Kama watu wangejua kwamba hili eneo siyo lao au Serikali ingekuwa inajua kwamba hili siyo eneo la hawa watu, ina maana hata hizo huduma za kijamii wasingewekewa, na ni watu 1,800 Mheshimiwa Waziri na huyu ni mtu mmoja. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iweze kuingilia kati, tuangalie ni jinsi gani mnaweza mkawakomboa hawa wananchi. Kwa sababu hakuna mtu ambaye anaweza kuwahamisha wananchi 1,800 yeye akiwa peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kwenye Jimbo la Segerea nina kata kama nne ambazo ndiyo zenye makazi holela. Amezungumzia hapo mjumbe aliyemaliza. Tuna Kata ya Vingunguti, tuna Kata ya Buguruni, na Kata ya Mnyamani. Kwa hiyo, tulikuwa tunasubiri huo mradi ambao mna-*plan* kwenye miji ili nasi tuweze kufaidika. Kama unavyojua, Vingunguti, Buguruni pamoja na Mnyamani ni karibu sana na mjini. Kwa hiyo, tunaomba katika huo mradi ambao mtauanza wa ku-*plan* miji, basi na hizi kata zetu tatu mweze kuziingiza ili wananchi hawa nao waweze kufaidika, kwa sababu wanakaa mjini, pamoja na kwamba sasa hivi hawana uwezo wa kujenga nyumba zao, lakini najua Serikali mnaweza mkatengeneza mradi pale, wananchi wakafaidika na Serikali ikafaidika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa hiyo, naomba masuala yangu matatu yaweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jonas Van Zeeland atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho jioni hii.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo. Nichukue fursa hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uzima, lakini pia nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anazozifanya. Nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa na nzuri ambazo mnazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi wenzangu wamezungumza, lakini mimi naomba nijikite kwenye eneo la migogoro ya ardhi, na kwa sababu ya umuhimu wake, nitajikita zaidi jimboni kwangu, kwa sababu tuna migogoro mingi. Moja ya wilaya ambazo bado zina migogoro ya ardhi ni Wilaya ya Mvomero. Pamoja na kazi kubwa na nzuri ambazo wanazifanya watalamu wetu, akiwepo Kamishna wetu wa Ardhi, Bwana Frank ambaye yuko Morogoro na watalamu wengine ambao wako katika wilaya yetu, lakini bado migogoro hii ni mingi, na ni kwa sababu ya eneo ambalo ni *potential* kwa kilimo lililopo katika wilaya yetu hii ya Mvomero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mwekezaji ambaye alipewa eneo lenye ukubwa wa ekari 100,000 mwaka 1985 kwa ajili ya shughuli za ufugaji na eneo hili alipotea. Eneo hili ni lile la Kipunguni Mheshimiwa Waziri nafikili unalijua, liko Tarafa ya Mlali. Huyu mwekezaji alipewa eneo kwa ajili ya ufugaji, lakini hajawahi kufanya shughuli zozote za ufugaji kwenye hili eneo zaidi ya watu wachache aliowaweka ambao wanafuga mbuzi zisizozidi 50. Yaani mwekezaji ana eneo la ekari 100,000, anafuga, badala ya kufuga kama eneo linavyomtaka afanye, yeye anakwenda kufuga mbuzi 50 kwenye eneo. Sasa amekuja sasa hivi, anapima lile eneo, anauza vipande vipande lakini wananchi ambao

wameishi na lile eneo kwa miaka mingi amewaambia atawapa eka elfu moja moja kwenye vijiji vitatu. Kijiji cha Mkata, Kijiji cha Merela Mlandizi na Kijiji cha Msongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulipewa ekari 100,000 umeshindwa kuliendeleza, leo unakuja kuwapiga saundi wananchi kwa kuwapa eka elfu moja moja! Hata kama kuna baadhi ya maeneo huku alishatoaga akawapa wananchi, lakini kwa ekari 1,000 bado ni ndogo, na wananchi hawana maeneo mengine ya kwenda kufanya shughuli zao za kilimo na ufugaji isipokuwa ni hili eneo la Kipunguni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pia tuna wafugaji na Mheshimiwa Waziri unajua Mvomero ni eneo pia linalofanya shughuli za ufugaji. Tunao wafugaji. Sasa tunaomba katika eneo la huyu bwana wa Kipunguni ambaye alipewa mwaka 1985, eneo hili pia lipimwe wapewe wafugaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba, kuna eneo ambalo tulipewa na watu wa *NARCO* pale Dakawa, hili eneo tumepewa ekari 10,000. Ekari 5,000zilikwenda Luhindo kwenye Kijiji cha Luhindo, 5,000 zilikwenda kuinzisha Halmashauri. Tulipima kwenye eneo la ekari 5,000 ambalo limeanzisha halmashauri, tumepima eneo la ekari 3,000 tu, eneo la ekari 2,000 liko wazi na linaendelea kuvamiwa siku hadi siku. Sasa sielewi tatizo ni nini? Tatizo ni fedha za upimaji hakuna ili tuweze kulipanga hili eneo ni kimpango mji, ama ni uvivu tu wa wataalam wetu, wanakaa pembeni wakisubiri migogoro pengine inawezekana itakuja kuwanufaisha baadaye? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna eneo la ekari 5,000 ambazo zilikwenda pale Luhindo. Mheshimiwa Waziri hili eneo tunaomba lipimwe ili watu wamilikishwe kishera. Eneo hili tunataka kulitumia kwenye skimu ya umwagiliaji. Eneo hili sasa hivi limeshaanza kuvamiwa na mbaya zaidi wanawavamia watu ambao wanatoka nje ya Dakawa, wanatoka nje ya Kijiji cha Luhindo, mnatengeneza migogoro ninyi wenyewe halafu baadaye mnashindwa kuitatua hii migogoro. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, kama watu wako hawana fedha ya kutatua

hii migogoro, wape fedha za kutosha migogoro iishe. Sehemu yenye migogoro hakuna maendeleo Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Rais; Mheshimiwa Hayati pamoja na Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia wamefuta mashamba pori tisa. Haya mashamba pori waliyoyafuta yana ukubwa wa ekari 13,000, lakini toka yamefutwa hayo mashamba Mheshimiwa Waziri pamoja na maelekezo ambayo yametolewa kwamba wapewe wakulima wadogo wadogo, wapewe wafugaji na litengwe eneo kwa ajili ya uwekezaji, mpaka leo tunavyozungumzwa hapa, hakuna kilichofanyika. Hakuna upimaji wowote. Sasa leo tunalia migogoro ya wakulima na wafugaji kwa kukosa maeneo, halafu kuna ekari 13,000 zimekaa, Rais ameshazifuta, kwenda kupima na kuwapa wananchi mnashindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Mvomero ni miongoni mwa wilaya ambazo watu walikuwa mpaka wanauana kwa sababu ya migogoro ya wakulima na wafugaji. Leo tuna ekari 13,000 mnashindwa kuwapa hao wananchi? Au mnataka waingie wenyewe wajimilikishe mle halafu baadaye mje kutumia tena nguvu za kuwatoa? Mtengeneze migogoro ambayo leo hapa tunazungumza kuitatua wakati migogoro mingine mnaitengeneza inaanza upya ambapo badaye mtashindwa tena kuja kuitatua. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kama utatenga kwenye bajeti zako, naomba uweke hili jambo ili mweze kwenda kuimaliza migogoro pale Mvomero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna eneo la Wamembiki. Hili ni eneo ambalo lina mgogoro wa muda mrefu sana. Hii mipaka inahamishwa hamishwa mara kwa mara. Wakija hawa wanasema hapa, wakija hawa wanapeleka hapa, mara tatu mipaka imehamishwa. Kuna mgogoro mkubwa sana pale kati ya hifadhi na wananchi. Naomba pia wapeni fedha watu wa Morogoro na Mvomero wakapime yale maeneo ili wananchi waweze kujua hatima ya huo mgogoro ni mgogoro wa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Kijiji cha Mkata. Kijiji hiki kilianzishwa mwaka 1965. Mwaka 1979 Serikali ilitoa tangazo la *GN* Na. 75 kuongeza mipaka ya hifadhi, lakini baadaye wananchi wakaambiwa, walikuwa wanalima kwenye bonde ambalo linaitwa Ngongoro. Wakaambiwa hili bonde liende kwenye Hifadhi ya Mikumi, wao watapewa bonde linaloitwa Kidaga ambalo lipo mpakani kabisa na Kilosa kule Mkata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu, ilikuwa ni hekta 814 na wananchi wakakubaliana kila mwananchi kwa kipindi kile apewe ekari mbili mbili kwa ajili ya kulima, lakini leo Mheshimiwa Waziri ninavyozungumza hapa, kuna wasanii wawili sijui wamepataje haya maeneo? Wamechukua haya maeneo na sasa wanawakodishia wananchi. Ni mgogoro ambao unawaumiza watu. Eneo walipewa miaka ya nyuma na walimilikishwa kisheria, lakini leo wamekuja watu wawili kwa ujanja ujanja wanaoujua wao, wamekwenda wamepewa haya maeneo na sasa hivi wanafanya biashara ya kukodisha, hawalimi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, timu yako ijue kuna mgogoro huo na tunaomba muende mkautatue. Ni mgogoro wa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna mgogoro ambao uko pale kwenye mizani, ambapo ukishatoka Dumila kuna mizani, pale ndiyo mpaka wa Kilosa na Mikumi. Mwaka 2014 kulitokea mafuriko Wilaya ya Kilosa, kipindi hicho Rais alikuwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, akatoa maelekezo kwamba wale wananchi ambao hawana maeneo ya kuishi baada ya mafuriko, waende pale kwenye lile eneo ambako sasa wamejenga mizani. Wale wananchi wameanza shughuli zao pale na wanazikana pale, lakini leo kuna watu wa Magereza wanataka kuwaondoa wale wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jambo hili pia Wizara ilichukue kwa uzito wa kipekee. Nchi hii ni yetu sote. Mbona kuna maeneo mengine watu wanajifanya wao ni wakubwa sana? Hivi wewe Askari Magereza, watu wamepewa na Mheshimiwa Rais wakae, wewe unakuja kuleta kitambi chako, unasema hawa waondoke, kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri hawa wananchi wabaki. Walipewa haya maeneo na Mheshimiwa Rais, kipindi hicho alikuwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, lazima hawa watu kama mnataka kuwatoa, mwafidie, lakini hawawezi kuondoka bila fidia yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tuna eneo ambalo pia lina mgogoro na eneo hili linashughulikiwa na watu wa halmashauri. Kama mgogoro huu ukishindikana kule wilayani, mimi nitakuja kwako. Eneo la mwekezaji mwenye Kiwanda cha Sukari Mtibwa na kuna eneo linaitwa *Newland,* hili ni eneo la muda mrefu sana lenye mgogoro wa zaidi ya miaka 30. Mimi pamoja na watalamu na watu wa Mtibwa na ninashukuru sana na kumpongeza huyu mwekezaji, ametoa ushirikiano katika kutaka kuutatua huu mgogoro na nina imani mgogoro utakwisha na kama hautakwisha kwa namna yoyote ile, Mheshimiwa Waziri nitakuja ofisini kwako ili uutatue huu mgogoro ni wa miaka 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimalize, Mvomero hatutaki wawekezaji feki. Mheshimiwa Waziri kuna watu, na wengine wako humu ndani wana maeneo kule Mvomero, jamani, Mvomero mkichukua maeneo mlime, ama mfuge. Hatutaki mje mwekeze kule majoka. Migogoro hii haitaisha na tunawakosesha watu fursa. Kama tukitoa ardhi na mkaitumia kwenye kilimo, ama kwenye ufugaji, kwanza mtatengeneza na ajira kwenye eneo letu, lakini maeneo ambayo yanatolewa Mvomero, watu wakishapewa, akishapewa hati, anasema hili ni eneo urithi wa watoto wangu. Sasa urithi wa watoto wako si waanze kulima sasa hivi. Hao watoto wenyewe, utakuta mtu ana mtoto wa miaka mitano, anategemea aje amrithishe hilo shamba. Kwa hiyo, likae pori miaka yote hiyo kwa sababu ya mtoto wake akue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, nami nakuamini sana uchapakaji kazi wako tunaujua, Naibu wako tunamfahamu ni mchapaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na nina imani migogoro itaenda kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge orodha ya wachangiaji jioni hii imekamilika. Hivyo tumefika mwisho wa shughuli yetu ya jioni ya leo.

Kuna tangazo moja kutoka kwa Katibu wa Bunge. Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na wadau wake wameandaa maonyesho ambayo yanaendelea kwa sasa katika viwanja vya Bunge. Maonyesho hayo yanahusu huduma zinazotolewa na Wizara pamoja na teknolojia ya kisasa katika sekta ya ardhi.

Waheshimiwa Wabunge, wote wanakaribishwa kutembelea hayo maonyesho ili kujionea kazi za Wizara pamoja na wadau wake.

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.25 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 26 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*